NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

BUNGE LA TANZANIA

_____

MAJADILIANO YA BUNGE

_____

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Thelathini – Tarehe 16 Mei, 2018

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua

MWENYEKITI: Tukae. Katibu.

NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (K.n.y. WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI):

Randama ya Maadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

MWENYEKITI: Ahsante. Katibu.

NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

Na. 251

Wabunge wa Viti Maalum Kutoingia katika Vikao Vya Kamati za Fedha za Halmashauri

MHE. TASKA R. MBOGO aliuliza:-

Wabunge wa Viti Maalum ni sawa na Wabunge wengine wa Majimbo kwa sababu hakuna tofauti ya kiapo cha Wabunge wa Majimbo na wale wa Viti Maalum.

Je, ni kwa nini Wabunge wa Viti Maalum hawaingii kwenye Vikao vya Kamati ya Fedha za Halmashauri zao?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango, imeundwa kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Sura ya 287, kifungu cha 75 na Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura ya 288 kifungu cha 47 pamoja na kifungu cha 40(2)(c) cha Kanuni za Kudumu za Halmashauri za mwaka 2014 na Kanuni za Kudumu za Mamlaka za Serikali za Mitaa kifungu 41(1) zinazotaja Wajumbe wa kuingia kwenye Kamati ya Fedha na Mipango kuwa ni Meya au Mwenyekiti wa Halmashauri ambaye atakuwa Mwenyekiti; Naibu Meya au Makamu Mwenyekiti, Mbunge au Wabunge wa Majimbo wanaowakilisha Majimbo katika Halmashauri hiyo; Wenyeviti wa Kamati za Kudumu katika Halmashauri; Wajumbe wengine wasiozidi wawili watakaopendekezwa na

Mwenyekiti au Meya na kupigiwa kura na Baraza la Madiwani la Halmashauri, mmoja kati yao akiwa mwanamke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wa Viti Maalum hawaingii kwenye vikao vya Kamati za Fedha za Halmashauri kwa sababu hawajatajwa kwenye orodha ya Wajumbe iliyoainishwa na kifungu cha 41(1) na kifungu cha 40(2) cha Kanuni za Kudumu za Mamlaka za Serikali za Mitaa za Mwaka 2014, zinazofafanua mahitaji ya Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Sura ya 287, kifungu cha 75 na Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) Sura ya 288 kifungu cha 47.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbogo.

MHE. TASKA R. MBOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa Wabunge wa Viti Maalum ni Wabunge sawa na Wabunge wa Majimbo, hivyo basi, Serikali haioni kwamba kuwanyima Wabunge wa Viti Maalum kuhudhuria kwenye Kamati za Fedha inawasababisha wasielewe mipango ya fedha kwenye Halmashauri zao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, ni kwa nini basi hii sheria isiletwe humu Bungeni ikabadilishwa ili kuweka usawa na kuondoa ubaguzi wa jinsia kwa sababu kutomruhusu Mbunge wa Viti Maalum kuingia kwenye Kamati za Fedha ni ubaguzi wa jinsia ya mwanamke na mwanaume ambayo inaanzia kwenye sheria zetu za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA): Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la kwanza, ni kweli kama alivyosema ni vigumu sana kujua kwa kina yale ambayo

yamejadiliwa na kikao husika kama wewe siyo Mjumbe. Hiyo ni kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la pili kuhusu kwa nini Serikali isilete Bungeni marekebisho ya sheria ili kusudi Wabunge wa Viti Maalum wawe Wajumbe, naomba tu nilipokee hili sasa kwa niaba ya Serikali ili tukalizungumze ndani ya Serikali kwa kuwa Vyama vya Siasa ambavyo viliwateua Wabunge wa Viti Maalum na kila Mbunge wa Viti Maalum amepangiwa Halmashauri fulani ya kuhudhuria vikao na kupiga kura. Basi nadhani hiyo inaweza ikawa ni mwanzo mzuri wa kuangalia ni namna gani tuweze kuleta marekebisho ya hiyo sheria. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Wanasema wanabaguliwa. Tutawapa wanawake watupu. Mheshimiwa Catherine halafu Mheshimiwa Sware.

MHE. CATHERINE V. MAGIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Wabunge wa Viti Maalum wamekuwa na majukumu makubwa sana ndani ya mikoa yao; je, ni lini sasa Serikali itaanza kuwapatia Wabunge wa Viti Maalum Mifuko ya Jimbo kama walivyo Wabunge wa Majimbo? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli mapendekezo yamekuwepo mengi nje na ndani ya Bunge kuhusu Wabunge wa Viti Maalum nao kupewa sehemu ya fedha kama Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa maelekezo yaliyoko kwenye sheria hiyo, mpaka sasa hivi bado Wabunge wa Viti Maalum hawajaingizwa kwenye huo mfumo. Sasa kwa sababu ni pendekezo ambalo linahitaji majadiliano ya awali ndani ya Serikali kwanza, naomba nalo nilichukue.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Sware.

MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Wabunge wa Viti Maalum uwakilishi wao uko kimkoa, lakini sasa Wabunge hawa wa Viti Maalum wamekuwa wakipata changamoto nyingi katika kutekeleza majukumu yao ya Kibunge hususan katika kufanya mikutano ya hadhara. Sasa ni nini kauli ya Serikali katika hili? Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la mikutano ya hadhara linahusisha idara nyingi, ikiwemo Idara ya Polisi ambayo iko chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie tu kwamba kama kuna mawasiliano mazuri kati ya Wabunge wa Viti Maalum na mamlaka zinazohusika, wakiwemo Wabunge wa Majimbo, hakuna matatizo yoyote. Inawezekana ukaandaliwa mkutano, hasa Mbunge wa Jimbo anaweza akaandaa mkutano ambao vilevile utahutubiwa na Mbunge wa Viti Maalum kwenye eneo lake. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Bupe Nelson.

Na. 252

Serikali Kuboresha Huduma za Kibenki Mikoa ya Pembezoni

MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA aliuliza:-

Wanawake ni nguzo muhimu katika kukuza uchumi na kusimamia nchi yetu na kwamba ukimwezesha mwanamke umeiwezesha familia na Taifa kwa ujumla.

Je, ni lini Serikali itafikiria kuboresha huduma za kibenki zitakazoweza kuwahudumia akina mama walio mikoa ya pembezoni?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua mchango wa mwanamke katika familia na Taifa kwa ujumla. Kwa kutambua hilo, Halmashauri zote nchini zinatakiwa kutenga asilimia 10 ya mapato yao kwa ajili ya mikopo ya wanawake na vijana. Suala hili lipo kisera na ni maamuzi ya Serikali katika kuhakikisha kuwa wanawake wanawezeshwa na kujengewa uwezo kiuchumi. Aidha, Serikali itaendelea kuibua programu wezeshi kwa wanawake kwa kadri itakavyoona inafaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudi za kisera za Serikali za kuwawezesha wanawake kiuchumi, jukumu la msingi la Serikali ni kuweka mazingira wezeshi ili watu binafsi, taasisi za umma na binafsi ziweze kuwekeza katika miradi mbalimbali ya kuzalisha mali pamoja na huduma zikiwemo huduma za kibenki. Badala ya Serikali kujiingiza moja kwa moja kusambaza huduma za kibenki hapa nchini, Serikali itaendelea kuimarisha miundombinu ya usafiri na usafirishaji, upatikanaji wa maji, umeme, mawasiliano na usalama wa watu na mali ili kuvutia wawekezaji kusambaza huduma za kibenki katika maeneo mbalimbali hapa nchini yakiwemo maeneo ya pembezoni mwa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya kuboresha mazingira ya kufanya biashara, hususan sera, miundombinu na usalama yamevutia wawekezaji binafsi wa ndani na nje kuwekeza hapa nchini na hivyo kuimarisha huduma jumuishi za kifedha kwa njia ya *simbanking,* wakala wa benki, *mobile money, NGO's, SACCOS* na benki za kijamii. Jitihada hizi

zimesaidia kuongeza matumizi ya huduma rasmi za fedha kutoka asilimia 58 mwaka 2013 hadi asilimia 65 mwaka 2017. Aidha, matumizi ya huduma zisizo rasmi za fedha zimepungua kutoka asilimia 16 mwaka 2013 hadi asilimia saba mwaka 2017. Hivyo basi, ni wajibu wetu kuendelea kuwashawishi wawekezaji binafsi kusogeza huduma za fedha karibu na wananchi badala ya kuitegemea Serikali.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Bupe.

MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa kuwa gharama za maisha zimepanda na asilimia 10 ni sawa na milioni moja, sasa je, Serikali haioni umuhimu wa kuongeza kutoka asilimia 10 kwenda asilimia 50? *(Makofi)*

Swali la pili, kwa kuwa Benki ya Wanawake iko Dar es Salaam tu, wanawake wa mikoa ya pembezoni wanaisikia tu hiyo benki. Je, ni lini Serikali sasa itafungua Tawi la Benki ya Wanawake Mkoa wa Rukwa? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Hongera sana kwa maswali mafupi na mazuri. Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi. *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, swai lake la kwanza kuhusu kuongeza asilimia 10 hadi 50, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, Serikali yetu inatambua mchango wa wanawake katika kujenga uchumi wa Taifa letu. Hili ni pendekezo, tunalichukua kama Serikali. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kufuatia kuwatambua wanawake kwenye uchumi wa Taifa letu, ndiyo maana tulipopitisha bajeti ya TAMISEMI tuliondoa riba ambayo ilikuwa inachajiwa katika hii asilimia 10 ya mikopo waliyokuwa wanakopeshwa wanawake, hii ikiwa ni hatua ya kwanza kuhakikisha kuwa akina mama na vijana wanaendelea kupata mitaji inayopatikana na bila kurejesha kwa gharama nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili, napenda kumwambia Mheshimiwa Bupe na Bunge lako tukufu kwamba Benki ya Wanawake Tanzania ilikumbwa na changamoto na sasa Serikali inaisimamia vizuri na tunatengeneza mfumo mzuri wa kuweza kufanya iweze kusimama. Moja ya mikakati ya kuiwezesha kusimama ni kupata mtaji wa kutosha, ndiyo maana kwa sasa kuna mapendekezo, wanafanya kazi kwa karibu na Benki yetu ya *TPB* na itakapoimarika ni nia ya Serikali kuona kwamba Benki ya Wanawake inaendelea kuwafikia wanawake kule walipo.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Ngonyani halafu Mheshimiwa Genzabuke na Mheshimiwa Chikambo watafuata.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa asilimia 10 inayotengwa kwa ajili ya wanawake, vijana na walemavu katika Halmashauri mbalimbali katika nchi yetu zimekuwa ni jambo ambalo halijatungiwa sheria, kwa hiyo, linatoa *loophole* kwa Wakurugenzi wa Halmashauri zetu ama kupeleka au kutopeleka.

Je, ni lini Serikali itatunga sheria au italeta marekebisho ya sheria hapa Bungeni ili jambo hili la asilimia 10 kwa makundi haya iwe ni lazima na isiwe kama vile ambavyo wanafanya Wakurugenzi kwenye maeneo mbalimbali kwamba wanafanya kwa hiari? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA): Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira kidogo kwa sababu mwezi wa sita wakati wa kupitisha Sheria ya Fedha ya mwaka 2018 kutakuwa na kipengele ambacho kitamruhusu Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa

kutunga Kanuni ambazo zitawalazimisha Wakurugenzi kuhakikisha kwamba wanatenga fedha hizo asilimia 10 kama alivyopendekeza.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Genzabuke na Mheshimiwa Chikambo ajiandae.

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika Mkoa wa Kigoma ipo *NGO* ambayo imezunguka kwa muda wa wiki mbili katika Wilaya zote saba ikiwatoza wanawake shilingi 10,000 na kuwapigisha picha kwa kuwaahidi kwamba Serikali itatoa mikopo kupitia Mfuko wa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu. Ninataka Serikali inieleze, je, mpango huo wa kutoa pesa kupitia Mfuko wa Mama Samia upo? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli zote za uwezeshaji wananchi kiuchumi katika nchi yetu ya Tanzania zinasimamiwa na Sera ya mwaka 2004 na Sheria ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004 ambayo inaruhusu uanzishwaji wa taasisi mbalimbali kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa kuhusu taasisi hiyo zilishapatikana ndani ya Serikali na Ofisi ya Makamu wa Rais ilishatoa tamko la kuikana taasisi hiyo kwamba haihusiki nayo. Ninaomba nichukue nafasi hii kuagiza uongozi wa mkoa wa Kigoma kuifuatilia taasisi hiyo na kuikana na kuipa maelekezo kwamba Ofisi ya Makamu wa Rais haihusiki na jambo hilo. Kama wanaendesha shughuli hizo kwa kutumia sheria na taratibu nyingine, wanapaswa kujieleza kwa kutumia sheria na taratibu nyingine walizozifuata, lakini siyo Ofisi ya Makamu wa Rais. Kama wataendelea kuwadanganya wananchi kwa kutumia Ofisi ya Makamu wa Rais, Serikali haitasita kuchukua hatua kali dhidi ya taasisi hiyo. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Chikambo.

MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Hii asilimia 10 ambayo tunaizungumza ni ile inayotokana na mapato ya ndani ya Halmashauri. Sote tutakuwa mashahidi kwamba ziko Halmashauri hazina uwezo wa kukusanya vyanzo vya mapato, wana vyanzo vidogo na vile vyanzo vingine vimechukuliwa na Serikali Kuu. Hii inasababisha kushindwa kutenga hii asilimia 10 kwa ajili ya wanawake, vijana na walemavu. Ni nini kauli ya Serikali katika kuhakikisha tunazipa uwezo Halmashauri ili ziweze kutenga hizi pesa kwa ajili ya kukopesha wanawake, vijana na walemavu? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tumetoa maelekezo kwamba Halmashauri zote zifanye mapitio ya vyanzo vyao vya mapato ili kuhakikisha kwamba wanaongeza wigo wa ukusanyaji wa mapato ya ndani na pili ni kwamba hata kama wamekusanya shilingi 10; asilimia 10 iko pale pale. Asitoe vigezo kwamba eti kwa sababu amekusanya mapato kidogo, basi atenge hiyo asilimia 10. Asilimia 10 ni ya kisheria na kwa mujibu wa maelekezo. Kwa hiyo, hata kama amekusanya 100 asilimia 10 iko pale pale.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara hiyo hiyo. Mheshimiwa Machano Othman Said, kwa niaba yake Mheshimiwa Khadija.

Na. 253

Fedha Kutoka *Basket Fund*

MHE. KHADIJA NASSIR ALI (K.n.y. MHE. MACHANO OTHMAN SAID) aliuliza:-

Katika utekelezaji wa bajeti ya 2017/2018 Serikali imekuwa ikitegemea msaada wa wafadhili *(Basket Fund)* ili

kutunisha Mfuko wa Hazina katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha kutoka *Basket Fund* kimepatikana katika mwaka 2017/2018?

(b) Je, kati ya fedha hizo ni kiasi gani kimepelekwa Zanzibar kusaidia bajeti?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango napenda kujibu swali la Mheshimiwa Machano Othman Said, Mbunge wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Machi, 2018 jumla ya kiasi cha shilingi bilioni 182.92 sawa na asilimia 32.89 ya makadirio ya shilingi bilioni 556.08 kimepokelewa kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa kifungu cha 15(1) cha Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada ya mwaka 1974 pamoja na marekebisho yake, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inapokea misaada ya mikopo ya kisekta moja kwa moja kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Hivyo, basi kiasi cha shilingi bilioni 182.92 kilichopokelewa kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ni kwa ajili ya Tanzania Bara tu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Khadija halafu Mheshimiwa Khatib ajiandae.

MHE. KHADIJA NASSIR ALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, lakini pia nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ieleweke kuwa Zanzibar hatupati gawio la *Yeared Budget Support.* Tunapata gawio

la *Annual Year Budget Support* ambayo ni 4.5% na imekuwa ikishuka kila leo, nafahamu pia kuna vikao vingi vya *harmonization* vinavyoendelea. Sasa nilikuwa napenda tu Serikali ituambie wamefikia wapi juu ya kuweka mambo haya yote sawa? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama swali lilivyojielekeza, liliuliza kuhusu *Basket Fund* ambao ndipo jibu langu la msingi lilipoeleza kulingana na sheria. *Basket Fund* ni kwa ajili ya Tanzania Bara kwa sababu na Zanzibar nao wanapata *Basket Fund.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ajili ya *General Budget Support,* kama alivyouliza Mheshimiwa Khadija Nassir, napenda kulieleza Bunge lako tukufu kwamba kwa mwaka 2016/2017 *General Budget Support* iliyopelekwa Zanzibar ilikuwa ni shilingi 5,656,500,000 lakini pia kwa mwaka huu hadi Machi tayari Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeshapeleka shilingi 3,153,111,187.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto alizozisema Mheshimiwa Mbunge tunaendelea kuzishughulikia kwa pamoja tukifahamu umuhimu wa mapato kwa maendeleo ya Taifa letu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Khatib.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Tunatambua baada ya Uchaguzi Mkuu uliopita baadhi ya nchi wafadhili zilizuia kutoa misaada yao kwa madai ya ukiukwaji wa uchaguzi wa Zanzibar na makosa ya mitandao hapa nchini. Serikali iliahidi kwamba mazungumzo yalikuwa yanaendelea ili kuhakikisha wafadhili wanaondoa vikwazo hivi. Nataka kujua je, mazungumzo yale yalifika wapi? Je, tumeanza kufaidika na misaada ile kutoka kwa nchi wafadhili? Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, mazungumzo niliyosema yanaendelea sio kati ya Tanzania na nchi wahisani, hapana. Ni mazungumzo kati ya Serikali zetu mbili kuhusu hili. Sina uhakika sana kama kuna nchi zilizositisha misaada yao kwa sababu ya uchaguzi wa Zanzibar, hiyo siyo sahihi hata kidogo. Kitu ambacho kilikuwa kinasababisha mapato haya ya *GBS* yapungue ilikuwa ni kumalizika kwa muda wa mwongozo wa ushirikiano kati ya nchi yetu na nchi wahisani, ambapo napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba mwongozo mpya tayari umeshapatikana tangu Agosti, 2017 na tumeanza kuutumia kuanzia mwaka huu wa fedha. Kwa hiyo, mapato haya yanaendelea kupatikana.

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Nje. Meshimiwa Ally Saleh Ally, Mbunge wa Malindi (Albeto). Kwa niaba yake, Mheshimiwa Mtolea.

Na. 254

Utungaji wa Sheria Katika Jumuiya ya Afrika Mashariki

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA (K.n.y. MHE. ALLY SALEH ALLY) aliuliza:-

Utaratibu wa kutunga Sheria wa Jumuiya ya Afrika Mashariki unahusisha maslahi ya nchi zote tano wanachama wa *EAC* kuelekea fungamano la kiuchumi na siasa.

(a) Je, hadi sasa ni sheria ngapi zimeshatungwa na kwa mgao wa maeneo yapi?

(b) Je, hatua gani huchukuliwa unapotokea mgongano baina ya sheria ya ndani na ile ya Jumuiya?

(c) Je, kuna utaratibu gani wa kutoa elimu ya umma kuhusu Sheria za Jumuiya?

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ally Saleh Ally, Mbunge wa Malindi, lenye vipengele (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu kuanzishwa kwa Bunge la Afrika Mashariki mwezi Novemba, 2001 hadi hivi sasa jumla ya sheria 78 zimeshatungwa. Kati ya hizo, sheria 20 zimesharidhiwa na Wakuu wa Nchi na Wanachama na nyingine zipo katika hatua mbalimbali za kusainiwa na kuridhiwa. Sheria zilizotungwa zimelenga katika kuimarisha biashara, kukuza uchumi baina ya nchi wanachama na Jumuiya ya Afrika Mashariki na kuwezesha taasisi na vyombo vya jumuiya kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya sheria hizi ni Sheria ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Usimamizi wa Forodha ya mwaka 2004, Sheria ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Kusimamia Uondoaji wa Vikwazo Visivyo vya Kiushuru ya mwaka 2017, Sheria ya Udhibiti wa Uzito wa Magari ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2013 na Sheria ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Uanzishwaji wa Vituo vya Utoaji Huduma kwa Pamoja Mipakani ya mwaka 2013.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Ibara ya 8(4) ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Sheria za Jumuiya zina nguvu kuliko za nchi wanachama. Hivyo basi, ikitokea mkingano baina ya Sheria za Jumuiya na zile za nchi wanachama, nchi wanachama hazina budi kuzifanyia marekebisho sheria hizo ili ziendane na Sheria za Jumuiya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Tanzania sheria mbalimbali za kodi zilifanyiwa marekebisho, ili ziendane na utekelezaji wa Sheria ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Usimamizi wa Forodha ya mwaka 2004 ambayo ndiyo sheria inayotumika kwa nchi zote wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ili kuendana na makubaliano yaliyofikiwa katika Itifaki ya Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki, Serikali ya Tanzania imefanya marekebisho katika Sheria ya Masoko na Mitaji na Dhamana, Sura ya 79; Sheria ya Kubadilisha Fedha za Kigeni Sura ya 271; pamoja na Kutunga Sheria ya Kuratibu Ajira za Wageni Nchini Na. 1 ya mwaka 2015. Vilevile Serikali inaendelea na mapitio ya sheria mbalimbali ili kuainisha na zile za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imekuwa na utaratibu wa kutoa elimu kwa umma lengo likiwa ni kuwawezesha wananchi kunufaika na fursa zinazotokana na mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, ikiwa ni pamoja na kuwapatia uelewa wa sheria zilizopitishwa na Bunge la Afrika ya Mashariki. Elimu hii hutolewa kupitia vyombo vya habari, tovuti ya Wizara, makongamano, vikao vya wadau, warsha, *blog* za kijamii na mitandao ya kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mathalani mwezi Julai Wizara iliratibu kampeni ya kuhamasisha vijana wa Kitanzania kutumia fursa za biashara zitokanazo na mtangamano wa Afrika Mashariki iliyojulikana kama Chungulia Fursa, iliyolenga kuwahamasisha vijana kufanya biashara za kuvuka mipaka ya Tanzania iliyofanyika katika mikoa ya Dodoma, Mwanza, Manyara na Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Wizara ilitoa elimu ya faida na fursa za mtangamano kwa wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu na Wajumbe wa Baraza la Vijana wa Zanzibar. Mafunzo hayo yalifanyika mwezi Machi, 2018 na yaliongozwa na kaulimbiu iliyosema Vijana na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Mtolea.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Njia zinazotumika kuzitangaza fursa zinazopatikana ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki

zimekuwa ni zile zile ambazo zinawafikia tu watu wanaoishi mijini na wachache waliopata shule ya kutosha, lakini elimu hiyo haiwafikii watu walio vijijini na hasa wanaoishi mipakani ambao wangependa sana kuzijua hizi fursa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka kujua Serikali ina mpango gani tofauti wa kuhakikisha fursa zinazopatikana ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki zinaelezwa kwa wazi na kwa kina na kuwafikia Watanzania wote?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nchi wanachama zinabadilisha sheria zao ili wananchi waweze ku-*enjoy* fursa zilizokuwa ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na wenyewe wana kaulimbiu yao wanasema Chungulia Fursa. Sasa Watanzania walichungulia fursa zilizopo ndani ya Afrika Mashariki wakalima mahindi kwa kiasi kikubwa ili waweze kufaidi Soko la Afrika Mashariki kwamba wauze mahindi ndani, lakini wauze mahindi nje ya nchi hii kwa maana kwenye nchi za Afrika ya Mashariki. Serikali ya Tanzania ikapiga marufuku mahindi kuuzwa nje ya nchi.

Je, Serikali haioni kwamba inawanyima Watanzania fursa za ku-*enjoy* Soko la Afrika ya Mashariki? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Tunawafikiaje wananchi walio katika vijiji? Hakuna tofauti ya kuwafikia wananchi walio katika vijiji kama tunavyowafikia katika kampeni zetu, katika kutangaza sera za Serikali kwa kutumia vyombo vilivyopo na njia zilizopo. La kwanza, ni kutumia redio na *television.* Wananchi wengi siku hizi wanazo redio na wengine wanatazama *television.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, njia ya pili ambayo tunaitumia kuwafikia wananchi wetu ni kufanya makongamano katika maeneo ya vijijini, hasa yale ambayo wananchi wamekuwa karibu na miji. Hili limekuwa na mafanikio mazuri sana kwa sababu, wananchi wengi

wamekuwa wakifuatilia kwa makini siyo tu redio, na warsha ambazo zinapelekwa kwao. Na hii tumeanza...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, swali la kwanza umejibu vizuri sana. Mjibu swali la pili.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili ni kwamba Serikali yetu ina mkakati wa kuhakikisha kwamba tunacho chakula cha kutosha katika nchi yetu. Baada ya hapo hakuna kizuizi cha kuweza kuuza mahindi nje ya nchi. Sasa hivi kuna utaratibu wa kutengeneza maghala na kufanya tathmini inayoeleweka kwamba chakula cha kila mkoa au kutoka mkoa hadi mkoa kinaweza kukidhi mahitaji ya wananchi. Baada ya hapo, hakuna kizuizi cha kuweza kuuza mahindi nje ya mipaka yetu.

MWENYEKITI: Ahsante kwa majibu mazuri sana. Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Mheshimiwa Lema kwa niaba yake Mheshimiwa Selasini.

Na. 255

Ujenzi wa Barabara ya Afrika Mashariki

MHE. JOSEPH R. SELASINI (K.n.y. MHE. GODBLESS J. LEMA) aliuliza:-

Barabara ya Mzunguko wa Afrika Mashariki *(by pass)* inayojengwa katika Jiji la Arusha na viunga vyake inaonekana kusuasua ingawa fedha za ujenzi zimeshapatikana.

Je, ni lini Serikali italipa fidia kwa wananchi walioacha maeneo yao kwa ajili ya mradi huo?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la

Mheshimiwa Godbless Jonathan Lema, Mbunge wa Arusha Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa mradi wa barabara ya mzunguko inayojengwa katika Jiji la Arusha na viunga vyake ni sehemu ya mradi wa Arusha – Holili yaani Taveta hadi Voi, ambayo ni mradi wa kikanda chini ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Tanzania Mradi wa Barabara ya Arusha – Holili unatekelezwa kwa awamu. Awamu ya kwanza inahusisha upanuzi wa Barabara ya Arusha kutoka Sakina hadi Tengeru yenye urefu wa kilometa 14.1 kutoka njia mbili za sasa hadi njia nne ambayo ujenzi wake umekamilika mnamo Julai, 2017 na sasa upo katika kipindi cha uangalizi *(Defects Liability Period).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu ya pili inahusisha ujenzi wa kiwango cha lami wa barabara ya mchepuo *(Arusha by pass)* yenye urefu wa kilometa 42.4 ambayo ujenzi wake ulianza tangu Februari, 2017 na unategemea kumalizika Juni, 2018. Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AfDB).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wa Serikali katika kutekeleza mradi huu ni pamoja na kulipa fidia kwa wananchi watakaoathirika na ujenzi wa barabara hii. Jumla ya shilingi bilioni 21.195 zimetumika kulipa fidia kwa wananchi walioathirika na barabara hiyo ya mchepuo. Zoezi la kulipa fidia lilianza tarehe 22 Machi, 2016 na hadi sasa jumla ya wananchi 742 walioathirika na mradi huo wamepokea malipo yao ya jumla ya shilingi bilioni 21.195 na hakuna mwananchi anayedai fidia tena kwenye mradi huu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Selasini.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwa mujibu wa sheria, uthamini ukishafanyika, ndani ya miezi sita waathirika wote wanapaswa wawe wameshalipwa fiidia zao. Wako wananchi wa Arusha na

wananchi wa Rombo, Lotima na Holili, ambao bado wana malalamiko ya kutolipwa fidia zao. Je, Serikali iko tayari kupokea majina ya wananchi hawa wanaolalamika na kuwalipa fidia zao?

Swali la pili, barabara kutoka Mamsera Jimboni Rombo mpaka *Mahida KNCU* na kwa Abiola ilichukuliwa na *TANROADS* mwaka 2014/2015 lakini *TANROADS* wameitelekeza hadi sasa, Halmashauri, *TARURA* na *TANROADS* hawaiangalii.

Naomba kauli ya Serikali, barabara ile imerudishwa *TARURA* ili waitengeneze au *TANROADS* wako tayari kuendelea kuihudumia hiyo barabara? Kwa sababu, imekuwa kero kubwa kwa wananchi wa Mahida, Chana na maeneo mengine ambayo hiyo barabara inapita? Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu. Jiandae Mheshimiwa Mabula na Mheshimiwa Issaay.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Selasini kwa kufuatilia na anajua kwamba ziko harakati na juhudi kubwa ambazo zinafanyika kuhakikisha tunaboresha miundombinu ya barabara katika maeneo mbalimbali ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza niseme tu kwamba suala hili la kulipa fidia ni kwa mujibu wa sheria. Mheshimiwa Mbunge anatambua kwamba sheria hii namba 13 ya 2007 inatoa mamlaka ya kufanya fidia kwa wananchi pale ambapo mradi wa barabara unapita na hususan ukiangalia *section 16* inasema pamoja na mambo mengine, Sheria ya Kutwaa Ardhi *(Land Acquisition Act),* pia iko *Land Act* na *Village Land Act* ambapo zinatumika sambamba na sheria hii ya barabara ili kufanya wananchi waweze kupata haki zao. Kwa hiyo, nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi kama wapo wachache kama

nilivyosema, wengi wamelipwa, basi tutatazama, lakini sambamba na sheria, haki zao watazipata kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili amezungumza juu ya hii barabara ambayo anasema inatoka Mamsera, kulikuwa na sintofahamu labda kuhamishwa kwenda *TARURA*. Cha muhimu ni kuhakikisha barabara inaboreshwa. Nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hizi zinavyojengwa, ziko kwenye mpango, kwa maana ya kwamba sisi upande wa *TANROADS* iko *strategic plan* ambayo ina-*monitor* ujenzi. Tutazama tu kuona kama inakwenda *TANROADS* au *TARURA* lakini lengo itaweza kutengenezwa kwa mujibu wa taratibu zilizokuwepo.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mabula halafu Mheshimiwa Issaay, Mheshimiwa Bonnah na Mheshimiwa Gekul mjiandae.

MHE. STANSLAUS S. MABULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba nitumie nafasi hii kwa ruhusa yako niwape pole sana wananchi wa Jimbo la Nyamagana kwa mafuriko makubwa sana kwa siku ya jana ambayo yalisababisha shughuli za kijamii kusimama takribani masaa saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu dogo, Jiji la Mwanza ni moja kati ya majiji yanayokuwa kwa kasi sana Barani Afrika ikiwemo Nyamagana. Sasa nataka kujua barabara kubwa ya Kenyatta ambayo inatoka *Mwanza Zero* kupita Kata za Mkuyuni, Butimba, Nyegezi kwenda mpaka Buhongwa ikiwemo na Mkolani ni barabara finyu sana kwa sasa. Serikali inao mkakati gani kuhakikisha barabara hii inapanuliwa angalau kwa njia nne ili ionekane taswira halisi ya Jiji la Mwanza na ukuaji wake kwa kasi?Nakushukuru sana.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa

Mwenyekiti, niseme tu kwa ujumla kwamba Jiji la Mwanza linakua kwa kasi lakini shughuli za maendeleo ziko nyingi, nasi kama Serikali tunatazama ili kwamba miundombinu hii tunayoweza kurekebisha iende sambamba na kasi ya ukuaji wa shughuli za maendeleo na ongezeko la watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mabula na tumeshazungumza kwamba nitakwenda kutembelea Mwanza, tutaitazama kwa sababu hii anayoizungumza ya Kenyatta kwenda Buhongwa ikipitia maeneo ya Makuyuni - Mkolani kwenda Nyegezi kama alivyozungumza, ni muhimu. Ni nia yetu kuhakikisha kwamba tunaboresha miundombinu ili iende sambamba na ukuaji wa uchumi wa nchi yetu.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Issaay, wajiandae Mheshimiwa Gekul na Mheshimiwa Bonnah.

MHE. ZACHARIA P. ISSAAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Moja ya changamoto inayokabili sana Mji mkongwe wa Mbulu ni pamoja na barabara ya Magara - Mbulu kupita katikati ya Mji Mkongwe wa Mbulu. Kwa kuwa jambo hili linaathiri uchumi wa wananchi, je, Serikali ina utaratibu gani sasa ikiwemo Mji wa Mbulu na miji mingine nchini namna ya kupata barabara ya mchepuo katika miji yetu ikiwa ni pamoja na athari za kiuchumi lakini pia na jiografia ya miji hiyo inavyokua kwa kasi?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge anatambua kwamba tunatazama sana maeneo haya kadri yanavyokua na anatambua ziko barabara ambazo zitakuja kuunganisha Mbulu Mjini. Nampongeza sana kwa kufuatilia, anajua tutatoka Mbulu Mjini kwenda Karatu, tutakwenda kutoka Mbulu kupitia Magara kama alivyosema na kuja Mbuyu wa Mjerumani. Vilevile ipo barabara kubwa ambayo itakuwa inakwenda Katesh – Dongobesh. Sasa barabara hizi

zinavyokuja kuunga Mbulu, tunazitazama pia ukuaji wake na kuweka barabara za mchepuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako maeneo mbalimbali katika miji kama alivyosema, tunayatazama yakiwemo maeneo ya Songea. Najua ndugu yangu alikuwa anafuatilia kilometa 11 zile, lakini maeneo mbalimbali ukienda Mwanza, tunayatazama ili kupunguza msongamano katikati ya mji. Zipo barabara ambazo zimekamilika kwa ajili ya mchepuo. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Gekul, ajiandae Mheshimiwa Bonnah.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

MWENYEKITI: Maswali mafupi na majibu yawe mafupi.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hili la *by-pass* la Mji wa Arusha linafanana kabisa na tatizo la *by-pass* Mji wa Babati ambako kuna *by-pass* ya Arusha – Singida na Arusha - Dodoma. Wananchi takribani miaka saba wanasubiri fidia hawajawahi kulipwa na hawajui ni lini watalipwa juu ya *by-pass* hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumwuliza Mheshimiwa Waziri, Babati ni karibu, yuko tayari kuambatana nami ili akawajibu wananchi hao ni lini wanalipwa fidia zao za *by-pass* hizi mbili? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri swali lake, uko tayari kwenda naye? Sasa usianze mengine hapa.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufupi kabisa niko tayari.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Bonnah.

MHE. BONNAH M. KALUWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nilitaka nimuulize Mheshimiwa Waziri, kutokana na mvua ambazo zinaendelea kunyesha Dar es Salaam na Mheshimiwa Waziri alishafanya ziara Jimbo la Segerea na kuona barabara nyingi ambazo zimekatika na nyingine zimekata kabisa mawasiliano.

Sasa Serikali ina mpango gani wa haraka kuhakikisha kwamba hizo barabara zinarudi kwenye matumizi ya kawaida hasa katika Jimbo la Segerea, Kata ya Kimanga, Segerea pamoja na Kinyerezi? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kweli kwamba tumekuwa na mvua nyingi na maeneo mengi nchini yameharibika. Kwa Jiji la Dar es Salaam kuna hali mbaya sana naye mwenyewe kwa sababu anatokea Jijini Dar es Salaam kwa kweli miundombinu ya barabara imeharibika sana na kwa sababu mvua ni nyingi na zimeendelea kunyesha na ile mito mikubwa inaendelea kumomonyoka na kufuata makazi ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufupi tu ni kwamba tunatazama kwa macho mawili Jiji la Dar es Salaam kwa maana kwamba mvua zitakapopungua tuweze kwenda kufanya marekebisho makubwa. Niseme tu na niendelee kurejea kwamba upande wa *TANROADS* na upande wa *TARURA* wamekuwa wakifanya uratibu wa kuangalia uharibifu mkubwa uliofanyika. Kwa sababu uharibifu unaendelea kutokea, nawaomba tu kila kukicha waendelee kuona kama kuna ongezeko la uharibifu, tufanye makadirio kuona namna gani tutafanya ili kurejesha miundombinu iliyoharibika kwa sababu bado mvua zinaendelea kunyesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nampongeza Mheshimiwa Bonnah Kaluwa, aendelee kufuatilia na tuendelee kupeana taarifa, Serikali iko macho kuangalia na kufanya marekebisho.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Flatei.

MHE. FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ametoa majibu yake kuhusiana na swali la msingi, je, ahadi hizi zinazotolewa kuhusu barabara hizi hasa ya *Mbulu by-pass* ambayo inakwenda mpaka Maswa, ni lini sasa Serikali itakuja na mpango wa kuzijenga kwa kiwango cha lami?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri kwa kifupi, ni lini tu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye bajeti tumeonesha na Mheshimiwa Mbunge anajua na namshukuru kwa kufuatilia kwa sababu anajua ziko barabara mbili, hii *by-pass* ya kupita Eyasi na hiyo inayopita kwenye Jimbo lako Katesh, Haydom kwenda Mbulu Mjini na unafahamu tuko kwenye hatua nzuri tunaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tutaendelea kupeana taarifa na Mheshimiwa Mbunge ili kuona hatua nzuri zinavyokwenda ili naye aendelee kuwapa taarifa wananchi katika Jimbo lake la Mbulu. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Utalii, Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha.

Na. 256

Kuboresha Vituo vya Kitalii - Bagamoyo

MHE. MARYAM SALUM MSABAHA aliuliza:-

Bagamoyo ni mji mkongwe wenye vivutio vya kitalii kama ilivyo miji mingine nchini kama vile Zanzibar, Kilwa na Mapango ya Amboni, Tanga.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuboresha vituo vya kitalii nchini ikiwemo Bagamoyo ili kupata wageni wengi zaidi na kukuza pato la Taifa?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

MWENYEKITI: Mheshimiwa swali namba 256 la Maryam Msabaha.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, *sorry!*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji wa Bagamoyo ni moja ya miji mikongwe katika historia ya utamaduni na maendeleo ya Tanzania ukiwa kando kando ya Bahari ya Hindi. Bagamoyo ni moja ya vituo vya Malikale ambavyo ni mojawapo ya vivutio vya utalii hususani wa utamaduni hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, vivutio hivyo havitumiki ipasavyo katika kukuza utalii kutokana na changamoto mbalimbali ambazo ni ufinyu wa bajeti, ukosefu wa huduma muhimu kwa watalii, kutofikika, kuchakaa kwa vioneshwa na kutotangazwa ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia changamoto hizo, Wizara imeandaa mkakati wa kuvitambua na kuvitangaza vivutio vyote nchini ukiwemo Mji wa Bagamoyo. Mpango huu unalenga kushirikisha mashirika yaliyo chini ya Wizara, yaani Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania *(TANAPA),* Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro *(NCAA),* Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania *(TAWA)* na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania *(TFS).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, vivutio vya malikale vilivyo Bagamoyo ni miongoni mwa maeneo yatakayoendelezwa kwa ushirikano na mashirika hayo. Aidha, vivutio vyote vya utalii nchini vitaendelea kutangazwa kupitia taasisi zinazohusika ikiwemo Bodi ya Utalii Tanzania *(TTB).* Kazi zitakazotekelezwa na mashirika hayo ni pamoja na kuweka huduma muhimu kwa watalii, kuboresha miundombinu ya vituo hususani majengo na barabara ili kuwezesha kufikika kwa urahisi na kuwa na mwonekano unaovutia; kujenga vituo vya kumbukumbu na taarifa pale ambapo vinahitajika, kuboresha vioneshwa na kuvitangaza na kuhamasisha wawekezaji wa hoteli, michezo na vivutio vingine vya watalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mkakati huu, Wizara itaendelea kusimamia majukumu yote ya uhifadhi, utafiti na kuandaa taarifa zitakazosaidia kuboresha na kutangaza vivutio vya utalii vilivyopo nchini, kwa kutoa elimu kwa umma juu ya uhifadhi na matumizi endelevu ya malikale na maliasili za nchi yetu. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Msabaha.

MHE. MARYAM SALUM MSABAHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa hali ya utalii kwa sasa hivi imeshuka kutoka asilimia 12.9 na kufika asilimia 3.3 na Mji wa Bagamoyo wanategemea uvuvi na utalii na kuonekanika mahoteli mengi ya kitalii ya Bagamoyo kukosa wageni, je, Serikali ina mikakati gani kuhakikisha inatangaza vituo vya utalii vya Bagamoyo na kuangalia ni tatizo gani lililofanya kushuka kwa asilimia hii ya utalii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa majengo ya kale ya mji mkongwe wa Bagamoyo yamekuwa yanabomolewa na ramani za majengo yale yanatoweka ambapo yalikuwa ni kivutio sana kwa utalii, lakini ramani zile za kale zinapotea na kujengwa katika miundombinu

mingine tofauti, je, Serikali ina mikakati gani kuhakikisha majengo yale yanaboreshwa kurudi katika hali ile ya mji mkongwe?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya utalii kwamba imeshuka kutoka asilimia 12 hadi asilimia tatu katika eneo la Bagamoyo, hii kwa kweli inahitaji labda nipitie takwimu vizuri. Kilichojitokeza zaidi ni kwamba katika hoteli nyingi za kitalii zile za Bagamoyo zilikuwa zinategemea sana uendeshwaji wake wa mikutano, yaani utalii ule wa mikutano ambao ulikuwa unaendeshwa sana Bagamoyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivi sasa mikutano mingi imepungua kutokana na mabadiliko ya hali ya uchumi. Hata hivyo, kutokana na hali hiyo, ndiyo maana Wizara imechukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuamua kuchukua mashirika yetu yaliyoko chini ya Wizara ili yaweze kukabidhiwa hii dhamana ya kutangaza maeneo yote yaliyoko Bagamoyo ikiwemo na ile Hifadhi nyingine ya Saadan kusudi iweze kuvutia watalii zaidi waendelee kuwepo na kuongezeka kule Bagamoyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili kuhusu majengo ambayo yamekuwa yakiharibiwa na kubomolewa ramani zao zile za awali, ni azma ya Serikali kuendelea kuwahamasisha wananchi wanayoyamiliki hayo majengo kuhakikisha kwamba wanafuata taratibu za kurudishia ujenzi uliokuwepo kabla. Kwa sababu katika eneo lile tunataka majengo yale yaendelee kuwa na ramani na sura iliyokuwa inaonekana toka awali ili iendelee kuwa kivutio kwa upande wa wageni.

MWENYEKITI: Waheshimiwa, maswali mwisho ni saa 4.00 na bado tuna maswali manne. Tunaendelea Mheshimiwa Leah Komanya kwa Wizara hiyo hiyo.

Na. 257

Mapato yatokanayo na Uwindaji wa Kitalii na Upigaji Picha

MHE. LEAH J. KOMANYA aliuliza:-

Serikali hupeleka katika Halmashauri zilizopo katika Hifadhi ya Wanyamapori asilimia 25 ya fedha zitokanazo na mapato ya uwindaji wa kitalii na upigaji picha pasipo Halmashauri husika kujua msingi wa tozo hizo.

(a) Je, ni lini Serikali itaanza kupeleka takwimu ya mapato yanayopatikana ili Halmashauri ziweze kujua stahiki zake?

(b) Je, ni kiasi gani cha mapato kimepatikana kutokana na *Maswa Game Reserve* na Hifadhi ya Makao na kiasi gani kilipelekwa katika Wilaya ya Meatu kila mwaka kuanzia mwaka 2015 hadi 2017?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imekuwa ikitoa mgao wa asilimia 25 ya mapato yatokanayo na ada za wanyamapori wanaowindwa kwenye vitalu vilivyopo kwenye maeneo ya Wilaya husika. Katika mwaka wa fedha 2015/2016 na 2016/2017 Wilaya ya Meatu ilipata mgao wa shilingi 40,017,158 na shilingi 41,696,616.43 sawia ikiwa ni asilimia 25 ya mapato yatokanayo na wanyamapori waliowindwa katika vitalu vya Mbono na Kimali katika Pori la Akiba la Maswa na Makao *WMA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu za mapato yanayotokana na wanyamapori waliowindwa na upigaji

picha katika vitalu vya uwindaji na utalii wa picha nchini huandaliwa na kutolewa taarifa mbalimbali. Aidha, Wizara ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha mfumo wa kielektroniki ujulikanao kama *MNRT Portal* ambapo taarifa zinazohusu Wizara ikiwa ni pamoja na mapato ya uwindaji wa kitalii zitapatikana humo. Mfumo huo unatarajiwa kuzinduliwa rasmi tarehe 1 Julai, 2018. Aidha, nakala ngumu zitatumwa kwenda Wilaya husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe wito kwa Halmashauri nchini zinazopata mgao huu kutumia asilimia 40 ya fedha hizo kwa ajili ya shughuli za uhifadhi ikiwa ni pamoja na ulinzi wa maisha ya wananchi na mali zao dhidi ya wanyamapori wakali kama ilivyokubalika.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Komanya.

MHE. LEAH J. KOMANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali kwamba asilimia 40 ifanye kazi ya uhifadhi. Vile vile kwa mujibu wa waraka asilimia 60 inatakiwa iende katika vijiji vinavyopakana na hifadhi ambavyo ni Mwambegwa, Mwanyaina, Mwagwila, Semu, Nyanza, Matale na vingine vingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2016/2017 vijiji vile havikupelekewa hela na asilimia 40 haikufanya kazi ya uhifadhi na hivyo kuipelekea Idara ya Wanyamapori kushindwa kununua silaha kwa ajili ya kukabiliana na wanyamapori. Je, Serikali haioni sasa ipo haja ya zile fedha zikapelekwa moja kwa moja katika vijiji na asilimia 40 ikapelekwa katika Pori la Akiba kuliko kupelekwa Akaunti ya Amana? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, asilimia 44 ya kilometa za mraba ya Wilaya ya Meatu ni hifadhi. Halmashauri imepata ugumu katika kukabiliana na ujangili, uhifadhi wa maliasili na uvamizi wa wanyamapori kwa sababu ina changamoto ya vitendea kazi. Je, Serikali iko tayari kuipatia gari Wilaya ya Meatu? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi sana, muda wetu umekwenda.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Leah kwa jinsi ambavyo amekuwa akifanya kazi na kufuatilia masuala mbalimbali yanayohusu Jimbo lake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali asilimia 60 zinazobaki kule kwenye Halmashauri kwamba ziende kwenye vijiji kama alivyosema, ni wajibu kila Halmashauri zinazopata mgao huu ile asilimia 60 inatakiwa iende katika vile vijiji vinavyozunguka hifadhi, kwa sababu zinatakiwa zitumike katika kuleta maendeleo ya vijiji vile vinavyohusika. Kwa hiyo, nitumie nafasi hii kuziomba Halmashauri zote nchini kutekeleza hilo agizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili kuhusu maombi ya gari, naomba nichukue nafasi hii kusema kwamba ni kweli kabisa kumekuwa na changamoto katika lile eneo na Wizara yangu inazo taarifa za kutosha. Tutalifanyia kazi maadam amelileta, tutaona pale hali itakaporuhusu kifedha tutawapelekea gari lile ambalo litawasaidia katika shughuli hizo. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Mheshimiwa Mchengerwa kwa niaba ya Mheshimiwa Ungando.

Na. 258

Wananchi wa Rufiji Kuzuiwa Kuvua Samaki – Hifadhi ya Selous

MHE. ALLY S. UGANDO (K.n.y. MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA) aliuliza:-

Wananchi wa Kata za Mwaseni, Mloka, Ngoroko na Kipungila Wilayani Rufiji waliruhusiwa kuingia ndani ya Hifadhi

ya Selous na kuvua samaki na hivyo kuinuka kiuchumi. Baada ya marekebisho ya mipaka ya hifadhi wamezuiwa kuingia kwenye hifadhi na wakati mwingine wanatendewa vitendo kinyume na sheria.

(a) Je, Serikali inachukua hatua gani kusaidia wananchi wa maeneo hayo ili waweze kupata kipato?

(b) Je, Serikali inachukua hatua gani kurejesha amani kati ya vijiji vinavyozunguka maeneo ya mipaka ya hifadhi na watumishi wa hifadhi?

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa, Mbunge wa Rufiji, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia mwaka 1990 Pori la Akiba la Selous lilianzisha Mpango wa Ushirikishwaji Jamii zinazozunguka pori hilo katika uhifadhi chini ya mradi ulioitwa *Selous Conservation Programme (SCP).* Katika kutekeleza mpango huo, wananchi wa jirani waliruhusiwa kuvua samaki ndani ya Pori la Akiba la Selous kwa ajili ya kitoweo baada ya kuombwa na wananchi wa Vijiji vya Kata za Mwaseni na Ngorongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kibali hicho kilisitishwa baada ya kuwepo ukiukwaji wa masharti yaliyotolewa ambapo baadhi ya wanavijiji waliingia ndani ya hifadhi bila kujisajili au kujiandikisha na kuvua samaki kwa ajili ya kufanya biashara kinyume na kusudio la kibali hicho. Aidha, baadhi ya wanavijiji walitumia fursa hiyo kufanya ujangili ndani ya pori kwa kuingia na silaha walizoficha ndani ya mitumbwi yao na kuua tembo, faru na wanyamapori wengine. Kutokana na sababu hizi, Serikali haina mpango wa kuruhusu uvuvi katika Pori la Akiba Selous. Nashauri Mheshimiwa Mbunge kushirikiana na Serikali kuelimisha wananchi kuvua katika mabwawa yaliyo nje ya hifadhi

pamoja na kuhamasisha ufugaji wa samaki kibiashara ili kujipatia kitoweo na kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali katika kuimarisha mahusiano mema kati ya wahifadhi na jamii inayozunguka maeneo yanayohifadhiwa itaendelea kuhakikisha inatoa elimu kwa jamii na kushirikiana nayo kwenye shughuli mbalimbali za kimaendeleo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ungando.

MHE. ALLY S. UNGANDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Wananchi wa Mwaseni na Ngorongo walipewa ahadi ya ujenzi wa mabwawa katika maeneo hayo, je, ni lini Serikali sasa itajenga mabwawa hayo ili wananchi hawa wafaidike katika maeneo hayo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Kibiti imeshindwa kukusanya mapato yake ya ndani kutokana na matatizo yaliyotokea. Je, ni lini sasa Serikali itawajengea mabwawa wananchi hao ili waongeze kipato chao katika Halmashauri ya Kibiti? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi sana.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa fursa hii ya kujibu maswali mawili ya nyongeza ya jirani na ndugu yangu Mheshimiwa Ally Seif Ungando na ninampongeza sana kwa jitihada kubwa anazozifanya za kuhakikisha kwamba maendeleo yanakwenda kule nyumbani kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza juu ya watu wa Mwaseni na Ngorongo kuahidiwa kupata mabwawa. Nataka nimwambie na niwaambie ndugu zangu wa Kibiti, Rufiji, Mkuranga, Kisarawe na Watanzania wote

kwa ujumla, Kata za Mwaseni, Ngorongo na kata nyingine katika Wilaya ya Rufiji zitakwenda kuwa wanufaikaji wakubwa sana wa mradi mkubwa wa uzalishaji wa umeme wa *Stiegler's Gorge,* mradi ambao utakuwa na matokeo chanya pia kwa sababu kutakuwa na eneo la ekari 140,000 kwa ajili ya kilimo. Vilevile katika bwawa lile tutakuwa na uwezo wa kuzalisha samaki wasiopungua tani 12,000 mpaka 20,000 kwa mwaka mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itakwenda kuwa na faida kubwa pia hata katika utalii kwa maana ya kwamba wapo watu watakaokuwa wanakuja kufanya kazi ya kuangalia bwawa lile kwa shughuli za utalii. Hivyo, niwaambie wananchi wa Kata hizi ya kwamba watakwenda kunufaika juu ya miradi hii ya mabwawa.

Kwa upande wa Kata za pale Kibiti pia kesho tunasoma bajeti yetu, namwomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira, asikilize mipango mikakati tuliyonayo katika suala zima la ufugaji wa samaki. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ya muda, tunaendelea na Wizara ya Nishati. Mheshimiwa Issa Ali Mangungu.

Na. 259

Ujenzi wa *Substation* ya Mbagala

MHE. ISSA A. MANGUNGU aliuliza:-

(a) Je, ni lini ujenzi wa kituo kidogo cha kupoza umeme *(substation)* ya Mbagala utakamilika?

(b) Je, makubaliano ya mkataba wa ujenzi wa kituo hicho ulikuwa wa muda gani?

(c) Je, mkandarasi wa mradi huo yupo ndani ya muda au amechelewesha kazi kwa mujibu wa mkataba na je ni hatua gani zimechukuliwa?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Issa Ali Mangungu, Mbunge wa Mbagala, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuimarisha hali ya upatikanaji wa umeme katika Jiji la Dar es Salaam hasa maeneo ya Mbagala, Shirika la Umeme nchini *(TANESCO)* mwezi Februari, 2018 kupitia Mradi wa *TEDAP (Tanzania Energy Development and Access Expansion Project)* lilikamilisha utekelezaji wa mradi wa uboreshaji wa njia za usafirishaji, usambazaji na vituo vya kupoza umeme katika Mikoa ya Dar es Salaam, Arusha na Kilimanjaro. Mradi huu ulitekelezwa kwa ufadhili wa Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukamilika kwa mradi huu kumeimarisha upatikanaji wa umeme katika eneo la Mbagala ikilinganishwa na kipindi cha nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme cha Mbagala ulikamilika na kuanza kufanya kazi rasmi kuanzia tarehe 25 Februari, 2018.

(b) Makubaliano ya awali ya mkataba wa ujenzi wa mradi mzima ikiwemo ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme cha Mbagala ulikuwa wa miezi 18 kutoka siku mkandarasi alipokabidhiwa maeneo ya ujenzi wa mradi.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, mkandarasi amekamilisha kazi hii nje ya mkataba wa awali kutokana na kuzuiwa kufanya kazi katika baadhi ya maeneo kutokana na baadhi ya wananchi kudai kwamba hawakuridhika na fidia na hivyo kumfanya mkandarasi asikamilishe utekelezaji wa mkataba huu kwa wakati. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa hali ya umeme imeimarika katika maeneo ya Mbagala na Wizara yangu itaendelea kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi kuhakikisha hali ya umeme Mbagala inaendelea kuwa ya uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mangungu.

MHE. ISSA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa ushirikiano walioutoa kwa wananchi wa Mbagala mpaka mradi huu kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kuwa baada ya kukamilika *substation* ya Mbagala, Mbagala ni eneo ambalo lina viwanda; je, wana mkakati gani sasa kuvishawishi viwanda vilivyopo Mbagala kutumia gesi asilia ili kupunguza *low voltage* ambayo tunaipata kutokana na matumizi ya viwanda vile?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini Serikali itafanya eneo la Mbagala *(District)* kuwa Mkoa kwa sababu ina wateja wengi na *TANESCO* imeelemewa kule Mbagala kiasi kwamba inashindwa kupaleka umeme katika maeneo ya Toangoma, Vigozi, Mponda na maeneo mengine?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri tumepokea pongezi zake, nasi kwa kweli tunamshukuru sana kwa ushirikiano alioufanya kwa kipindi chote cha utekelezaji wa mradi huu Jimboni kwake Mbagala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge ameeleza mkakati wa Serikali wa kuvishawishi viwanda kutumia gesi asilia. Naomba nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge Wizara yetu kupitia *TPDC* tuna mkakati wa kusambaza gesi asilia kwa matumizi ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kwa mwaka huu wa fedha ambao utaanza 2018/2019 *TPDC* imeshaingia makubaliano ya awali ya kusambaza gesi katika maeneo mbalimbali ya viwanda yaliyopo Mkuranga, kwa mfano

Kiwanda cha Bakhressa, *Loth Steel* cha Mkuranga na pia hata Kiwanda cha Biku na Cocacola Kwanza, Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wazo lake hilo linafanyiwa kazi na viwanda tunavihamasisha vitumie gesi kwa sababu gesi ipo na ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, ameuliza ni lini tutaifanya Mbagala kuwa Mkoa? Naomba nilichukue hili suala na linajadilika ndani ya Wizara, tunaweza tukalifanyia kazi. Ni kweli Mbagala ina wateja na watumiaji wengi wa umeme. Naomba hili tulichukue. Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Justin Monko.

Na. 260

Kukamilika kwa Mradi wa *REA* II - Singida Kaskazini

MHE. JUSTIN J. MONKO aliuliza:-

Mradi wa *REA* Awamu ya Pili katika Jimbo la Singida Kaskazini ulisimama tangu mwaka 2016 na kukosesha huduma hiyo kwa vijiji vilivyokusudiwa mwaka 2017, utekelezaji wa *REA* Awamu ya Pili katika vijiji 30 kati ya 64 vilivyokusudiwa umeanza.

(a) Je, ni nini kauli ya Serikali juu ya ukamilishaji wa mradi wa *REA II?*

(b) Je, ni lini mkandarasi wa *REA II* awamu ya pili atapatikana na kuanza kazi?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati naomba kujibu swali la Mheshimiwa Justin Joseph Monko, Mbunge wa Singida Kaskazini, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Mradi wa *REA* Awamu ya Pili katika Mkoa wa Singida ulisimama kutekelezwa mwaka 2016 kutokana na mkandarasi *Spencon Ltd.* kushindwa kukamilisha kazi zake baada ya kufilisika. Hata hivyo, tayari vifaa vyote vya mradi vilikuwa vimenunuliwa na kuhifadhiwa. Wakala wa Nishati Vijijini wamesaini mkataba mpya na Kampuni ya *JV Emec Engineering Ltd. & Dynamic Engineering and System Co. Ltd.* wenye thamani ya shilingi milioni 991.6 kwa ajili ya kukamilisha kazi za *REA* Awamu ya Pili katika Wilaya ya Iramba, Mkalama na Singida Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Wakala wa Nishati Vijijini umesaini mkataba na Kampuni ya *JV East African Fossils Co. Ltd & CMG Construction Co. Ltd.* wenye thamani ya shilingi 459.23 kwa ajili ya kukamilisha kazi katika Wilaya ya Manyoni. Mikataba yote miwili imesainiwa mwezi Machi, 2018 kwa muda wa miezi sita. Kazi ya kusambaza umeme katika meneo yaliyotajwa zitakamilika mwezi Septemba, 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mradi wa *REA* Awamu ya Tatu mzunguko wa kwanza, kazi za mradi zinatekelezwa na Mkandarasi *M/S CC- Etern Consortium Ltd.* ya China, kazi za Mradi wa *REA III* mzunguko wa kwanza katika Mkoa wa Singida zinajumuisha kuvipatia umeme vijiji 150 ambapo Jimbo la Singida Kaskazini litaunganishiwa umeme jumla ya vijiji 30 na kuunganishia wateja wa awali 870. Mradi utakamilika mwezi Juni, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya kusambaza umeme katika Mkoa wa Singida kwa miradi ya *REA* awamu ya tatu mzunguko wa kwanza na wa pili zinajumuisha ujenzi wa kilometa 286.1 za njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 33, kilometa 568 za njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 0.4, ufungaji wa transfoma 284 na kuunganishia wateja wa awali 8,659. Kati ya wateja hao, wateja 7,795 wa njia moja na wateja 864 wa njia tatu. Gharama ya mradi ni shilingi bilioni 29.56 na dola za Kimarekani milioni 5.34.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Monko.

MHE. JUSTIN J. MONKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Singida Kaskazini lina Kata 21 na Vijiji 84. Kata za Muhunga, Ngimu, Itaja, Makulo na Ughandi hazina kijiji hata kimoja ambacho kimepitiwa na miradi ya umeme wa *REA II* na *REA III.* Je, ni lini wananchi hawa watapata fursa hiyo ya kupata umeme ambao ni muhimu sana katika shughuli za maendeleo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mradi wa *REA* Awamu ya Tatu ambao umeshaanza sasa yapo maeneo ya wananchi ambayo tayari wameshajiandaa pamoja na taasisi ambayo yanarukwa na umeme, katika mpango wa upatikanaji wa umeme huu ambao unaendelea sasa. Serikali ina kauli gani kwa wananchi katika maeneo hayo ambayo tayari wameusubiri umeme huu kwa muda mrefu na wako karibu na njia za umeme? Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Monko, ni Mbunge mgeni lakini kwa kipindi kifupi cha kuchaguliwa kwake amefanya kazi kubwa ya kufuatilia miradi ya nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kiti chako pia kimekuwa kikiagiza mara kwa mara kupitia Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wenyeviti na Naibu Spika, naomba niliarifu Bunge lako tukufu kwa miradi yote ya *REA* kwa ujumla yake, kulikuwa na agizo la kufuatilia ufunguaji wa *Letter of Credit.*

Naomba niliarifu Bunge lako tukufu na niishukuru Kamati ya Bajeti, Wizara ya Fedha na Benki Kuu na nikutaarifu kwamba mpaka sasa Wizara ya Nishati kupitia *REA*

tumefanikiwa kufungua *Letter of Credit* kwa makampuni 14 yenye jumla ya shilingi bilioni 220. Hii maana yake nini? Maana yake ni kwamba kuanzia sasa utekelezaji wa miradi ya *REA* Awamu ya Tatu itapata kasi kubwa. Niwathibitishie Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote kwamba wategemee sasa miradi kushika kasi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nijielekeze kwa maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, swali lake la kwanza ametaja Kata kadhaa ambazo amesema amesema hakuna hata Kijiji kimoja ambacho kina umeme katika *REA* zote zilizopita mpaka sasa. Nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa kweli kwa mradi huu unaoendelea wa *REA* awamu ya tatu, mzunguko wa kwanza na mzunguko wa pili yatafikiwa maeneo yote. Kwa hiyo, maeneo na kata ambazo amezitaja zitapatiwa umeme katika mzunguko wa pili utakaoanza Julai, 2019 na kukamilisha Juni, 2021. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, katika maeneo ambayo Mradi wa *REA* umeanza, Mheshimiwa Mbunge amesema zipo taasisi za umma zimerukwa na yapo maeneo ambayo wananchi wamepitiwa na umeme mkubwa lakini hawana dalili za kupata umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara ya Nishati imetoa maelekezo kwa wakandarasi wote nchi nzima. Hapa namwomba mkandarasi wa Mkoa wa Singida na wakandarasi wote; na kama nilivyosema sasa mambo ni mazuri, wahakikishe kazi inakwenda kwa mujibu wa *scope* na yale maeneo ambayo yameainishwa yapate huduma hii. Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umekwisha na tumekula muda wa ziada. Najua Waheshimiwa Wabunge mnakuwa na maswali mengi, lakini kwenye nishati tusubiri bajeti ya Nishati ambayo inakuja wiki ijayo. *(Makofi)*

Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii, wageni wawili wa Mheshimiwa Naibu Spika kutoka Kampuni ya *Cornwell*

Tanzania inayotoa huduma za matibabu katika Mikoa mbalimbali nchini ambao ni Dkt. Johnny Brinkman na mkewe Bi. Elizabeth Lema, karibuni Dodoma. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wageni 17 wa Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa, Naibu Waziri wa Kilimo ambao ni viongozi wa UWT Wilaya za Mkoa wa Mbeya wakiongozwa na Mwenyekiti wa UWT Mkoa wa Mbeya Ndugu Oliva Kibona. Mna Mbunge mzuri sana kwenu huyu, anaitwa Mary mashine hapa. *(Makofi)*

Wageni 13 wa Mheshimiwa Silafu Maufi ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Utekelezaji ya UWT Mkoa wa Rukwa na Wenyeviti wa UWT wa Wilaya zote za Mkoa wa Rukwa wakiongozwa na Mwenyekiti wa UWT Mkoa wa Rukwa Ndugu Maria Kalula, karibuni Dodoma. *(Makofi)*

Wenginei ni wageni watatu wa Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata ambao ni Madiwani wa Viti Maalum kutoka Sumbawanga, Mkoa wa Rukwa wakiongozwa na Mheshimiwa Khadija Maufi. *(Makofi)*

Wengine ni wageni watatu wa Mheshimiwa Jacqueline Msongozi ambao ni jamaa zake kutoka hapa Jijini Dodoma. Pia tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Josephine Genzabuke ambao ni jamaa zake kutoka Wilaya ya Kasulu, Mkoa wa Kigoma. *(Makofi)*

Wengine ni wageni wa Mheshimiwa Mussa Ntimizi ambao ni ndugu zake kutoka Wilaya ya Uyui, Mkoani Tabora, karibuni Dodoma. Vilevile tunao wageni 15 wa Waheshimiwa Wabunge wote wanaotoka Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ambao ni Mawakala wa Pembejeo za Kilimo wakiongozwa na Ndugu Joram Sokanyi. *(Makofi)*

Wenginei ni wageni 52 wa Mheshimiwa Lolesia Bukwimba ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, lakini pia tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Stanslaus Mabula akutoka *Tanzania Cassava Planters and Agribusiness Foundation* ya Jijini Mwanza, karibuni. *(Makofi)*

Wengine ni wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; wanafunzi 29 kutoka Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini cha Dodoma, karibuni. *(Makofi)*

Wengine ni wageni wawili kutoka Kituo cha Haki za Binadamu na Utawala Bora kilichopo Jijini Dar es Salaam.

MHE. SIXTUS R. MAPUNDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Spika.

MWENYEKITI: Waziri wa Nchi.

MHE. SULEIMAN A. SADDIQ: Mwongozo wa Mwenyekiti.

MWENYEKITI: Waziri wa Nchi.

HOJA YA KUTENGUA KANUNI

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kwa heshima ya Kiti chako, nitoe maelezo ya hoja ya Kutengua Kanuni za Bunge. Ninafanya hivi chini ya Kanuni ya 153(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa kuwa, kwa mujibu wa Kanuni ya 28(2) na (4), Bunge linakutana hadi saa 7.00 mchana na kusitishwa mpaka saa 11.00 jioni na baada ya hapo Bunge huendelea kukaa mpaka saa 1.45 usiku ambapo Spika husitisha shughuli na kuliahirisha hadi siku nyingine;

Na kwa kuwa, hivi karibuni ndani ya kipindi cha Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge unaoendelea, waumini wa dini ya Kiislamu wataanza Mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani ambapo katika kipindi hicho waumini wote wa Kiislamu watakaofunga hutakiwa kuswali na kufuturu kila siku ifikapo saa 12.45 jioni;

Na kwa kuwa, katika Kikao cha Kamati ya Uongozi kilichofanyika Jumanne, tarehe 15 Mei, 2018, Wajumbe waliohudhuria walikubaliana na umuhimu wa kutengua Kanuni husika kwa mujibu wa Kanuni ya 153(1) ili kuliwezesha Bunge kutekeleza shughuli zake zilizopangwa kikamilifu na kwa wakati huo huo kuwawezesha Waheshimiwa Wabunge ambao ni waumini wa dini ya Kiislamu waweze kuswali na kufuturu kwa wakati muafaka kwa mujibu wa taratibu za dini yao;

Hivyo basi, Bunge linaazimia kwamba Kanuni ya 28(2) na Kanuni ya 28(4) zitenguliwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 28(2) ambayo inaelekeza kwamba Bunge litakutana hadi saa 7.00 mchana ambapo Spika atasitisha shughuli yoyote itakayokuwa inafanyika hadi saa 11.00 jioni, itenguliwe na badala yake Bunge linapositishwa saa 7.00 mchana, liendelee na shughuli ifikapo saa 10.00 jioni badala ya saa 11.00 jioni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 28(4) ambayo inaelekeza kwamba Bunge litaendelea kuketi hadi saa 1.45 usiku ambapo Spika atasitisha shughuli na kuliahirisha hadi kesho yake, itenguliwe na badala yake Bunge liahirishwe ifikapo saa 12.00 jioni. Utaratibu huu utaanza kutumika mara tu Mfungo wa mwezi Mtukufu wa Ramadhani utakapoanza na baada ya mfungo huo kukamilika tutarejea katika utaratibu wetu wa kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Hoja imeungwa mkono, sasa nitawahoji.

(Hoja ilitolewa Iamuliwe)
(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)

MWENYEKITI: Walioafiki wameshinda. Kwa hiyo, Mwezi wa Ramadhani utakapoanza mabadiliko ya muda ni kama yalivyozungumzwa na Serikali.

MHE. SIXTUS R. MAPUNDA: Mwongozo wa Mwenyekiti.

MWENYEKITI: Mwongozo Mheshimiwa Sixtus, Mheshimiwa Murrad.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. SIXTUS R. MAPUNDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nasimama hapa kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7), kutokana na muda, naomba nisiisome.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa swali la leo namba 258 lilihusu Wizara ya Mifugo na Uvuvi na katika maudhui yake ya jumla yalikuwa ni mkakati wa Serikali kuongeza mapato kupitia sekta ya mifugo; na kwa kuwa zipo taarifa zinazagaa mitaani kwamba kuna nyama zinauzwa katika ma-*butchery* na machinjio ambazo zinaonekana kuwa siyo nyama bora na pia zipo taarifa kuwa kulikuwa na jaribio la kuuza nyama kibudu katika Machinjio ya Tegeta. Nini kauli ya Serikali kwenye hili?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Murrad.

MHE. SULEIMAN A. SADDIQ: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Na momi nasimama kwa Kanuni ya 68(7) naomba Mwongozo wako. Kamati yangu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira ilikuwa inasimamia suala la mafuta na kwa kuwa suala hili la mafuta sasa limeshapatiwa majibu na Serikali na vyombo vya habari vimeandika leo na jana Mheshimiwa Rais alifanya ziara bandarini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa kutumia nafasi hii kwanza kabisa nilishukuru Bunge kwa kuisimamia Serikali vizuri. Naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Spika kwa kulisimamia jambo hili kwa uwezo wake mkubwa, lakini pia

naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa kuwa msaada mkubwa kwa Kamati yangu, mara kwa mara wakati naonana naye amekuwa ni msaada mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Waziri Mkuu kwa kutoa taarifa Bungeni na maelekezo ya Serikali ndani ya Bunge. Pia kwa salamu za pekee kabisa naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa ziara yake aliyofanya bandarini jana. *(Makofi)*

MHE. PAULINE P. GEKUL: Huo siyo utaratibu.

MHE. SULEIMAN A. SADDIQ: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako, Kamati yangu ya Viwanda, Biashara na Mazingira ilitimiza wajibu wake, ilifanya kazi kwa mujibu wa Kanuni na hatimaye jambo hili likaanza kupata mijadala mbalimbali na sasa limeisha. Naomba Mwongozo wako, katika sakata hili Kamati yangu ilituhumiwa na sasa jambo limeisha salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, majibu ya Mwongozo wa kwanza wa Mheshimiwa Sixtus kuhusu mifugo. *(Makofi)*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima ya Kiti chako, naomba Waziri mwenye dhamana ya Sekta ya Mifugo na Uvuvi atupe maelezo kuhusu sakata hilo ambalo Mheshimiwa Sixtus amelieleza.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Mifugo.

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Vilevile namshukuru Mheshimiwa Sixtus Mapunda kwa kuomba Mwongozo huu ili kuweza kuondoa mkanganyiko ambao umejitokeza kwa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuujulisha Umma wa Watanzania kupitia Bunge lako hili tukufu kuhusiana na tukio la ng'ombe waliokufa na kukutwa wakichunwa ndani ya lori Wilayani Kinondoni eneo la Machinjio, Tegeta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo tarehe 13 Mei, 2018, majira ya saa 4.30 asubuhi, lori lenye usajili namba T 486 DHZ na trela lenye namba 584 *BJB* likitokea Morogoro lilikamatwa likiwa na ng'ombe 54, kati ya ng'ombe hawa 54, hao 42 walikuwa wazima na mizoga walikuwa 12. Katika hao 12 wanne walikuwa wamechunwa na wawili kati ya hao walikuwa wamekatwa vipande vipande. Tukio hili lilisababisha taharuki kubwa kwa jamii katika eneo hilo kuhusu usafi na usalama wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria ya Magonjwa ya Wanyama Na. 17 ya mwaka 2003 na kwa mujibu wa Sheria ya Nyama Na. 10 ya mwaka 2006 na kwa mujibu wa Sheria ya Chakula na Vipodozi na Dawa ya mwaka 2003, tukio hilo na jaribio hilo lilikuwa kinyume cha sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niweke wazi kwamba hili lilikuwa ni jaribio. Kwa hiyo tukio na jaribio hilo lilikuwa kinyume cha sheria. Kwa hiyo, baada ya kuona kwamba hili tukio ni kinyume cha sheria, Wizara yangu pamoja na Halmashauri ya Kinondoni tulichukua maamuzi yafuatayo:-

(i) Machinjio ya Tegeta tumeyafunga kwa muda usiojulikana. *(Makofi)*

(ii) Tuliamua kuteketeza mizoga hiyo 12 na kuifukia. *(Makofi)*

(iii) Nimeagiza mwenye machinjio ambaye mpaka sasa hivi amekimbia, anatafutwa, mwenye lori ameshakamatwa, lakini vilevile mmiliki wa machinjio anatafutwa ili aweze kufikishwa kwenye vyombo vya sheria kutokana na hilo jaribio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu magari haya yote huwa yanapita kwenye Kituo cha Ukaguzi pale Kibaha, nimeshamwagiza Katibu Mkuu kuwaondoa watumishi wote walioko kwenye kituo hicho na kubadilisha watumishi wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa *point* hapa ni nini? Nataka niwaambie Watanzania kwamba vyombo vyetu kwa maana ya Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo, Bodi ya Nyama, *TFDA* na Halmashauri, tunao usimamizi madhubuti katika ma-*butchery* yetu, katika machinjio yetu, katika kuhakikishia usalama walaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa *point* hiyo nataka niweke wazi kwamba wananchi wote wasipewe mashaka wala hofu na mtu yeyote. Nyama za Tanzania ni bora, zinatokana na malisho bora na kwamba wasijawe wala wasipewe hofu kwamba Watanzania wanaweza kula kwa namna yoyote vibudu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasimamia vizuri, Watanzania wale mifugo yao vizuri, vyombo vya dola vinawahakikishia usalama huo na tumejipanga vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hata huyu kwa jaribio tu, amefungiwa machinjio yake. Kwa hiyo, mko salama, msitiwe hofu na mtu yeyote. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tulikuwa na miongozo miwili. Mwongozo wa kwanza umeshapewa majibu, mwongozo wa pili wa Mheshimiwa Murrad, kwa kiwango kikubwa amelipongeza Bunge na Serikali kufanya kazi pamoja, na mimi naungana naye.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hatua hii ya kusema Kamati yako ilipewa tuhuma na tuhuma hukuzisema hapa Bungeni, sasa mwongozo wangu kwako, mwandikie Mheshimiwa Spika na ulieleze sakata zima lilivyotokea.

Katibu.

NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwakawa Fedha 2018/2018 – Wizara ya Kilimo

(Majadiliano yanaendelea)

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea. Tunaanza na Mheshimiwa Kaboyoka dakika tano, ajiandae Mheshimiwa Sabreena dakika tano.

MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii kuchangia katika hotuba hii ya Waziri wa Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa *scenarios* tatu ambazo zinanifanya niwe na mashaka kwamba Wizara hii ya Kilimo itaweza kusaidia kupatikana kwa malighafi za kuingia kwenye viwanda. Najua kwamba Wizara hii inategemea Wizara nyingine ili waweze kufanikiwa, matokeo yake ni kwamba Wizara hii hata ingewezeshwa kiasi gani, kama haya matatizo ambayo nitayazungumzia hapa hayakuangaliwa, sioni itakavyoweza kusaidia kwamba asilimia 65 ya malighafi iingie kwenye viwanda vyake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, wananchi tunajua kwamba sasa hivi miwa imekomaa sana, iko mashambani, lakini inashindikana kupelekwa kwenye viwanda kwa tatizo la kwamba barabara hazipitiki. Kwa maana hiyo, ni kwamba wakati Serikali inajenga viwanda, wakati Serikali inawekeza katika mashamba makubwa ya miwa, Wizara ya Ujenzi haina habari kwamba kunatakiwa kuwe na barabara ya kutoa malighafi mashambani kufika viwandani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi viwanda vya sukari ambapo sukari ingekuwa iko nyingi sasa hivi nchini, haiwezi

kutengenezwa kutokana na kwamba miwa hii inaozea shambani sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiuliza Serikali, kama hakuna jinsi ya kukaa pamoja na kuona tunawezaje kufanya *sustainability* ya hivi viwanda tunavyotaka kuanzisha, tutafanya nini ili basi tuweze kujikwamua? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie tunapopata ukame. Katika ukurasa wa namba saba, Mheshimiwa Waziri amesema mwaka 2016/2017 kumekuwa na ukame, kwa hiyo uzalishaji ukaanguka. Miaka yote tunazungumzia umwagiliaji, lakini ni wazi kwamba Idara ya Umwagiliaji iko Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Maji haina mpango wa kuona kwamba je, kuna mashamba gani makubwa ya uzalishaji ambayo yanatakiwa huu umwagiliaji ukafanywe kule? Imekuwa ni wimbo wa Taifa kila mwaka tunazungumzia Kilimo cha Umwagiliaji lakini matokeo yake, Wizara ya Kilimo inafanya vyake, Wizara ya Maji na Umwagiliaji inafanya vyake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukija *scenario* ya tatu, ni kwamba wakati hali ya hewa inakuwa nzuri, *production* inakuwa kubwa kama tulivyoona kwenye mahindi na mbaazi, yamevunwa mavuno mengi. Tatizo, hatuna soko, haturuhusiwi kuuza nje. Sasa swali langu ni kwamba kukiwa na mvua nyingi, kuna mafuriko, mazao hayawezi kutoka kwenda viwandani, kukiwa na ukame hakuna maji ya kumwagilia kuweza kuzalisha mazao, kukiwa na hali nzuri wananchi wakazalisha sana hakuna jinsi ya kupata masoko ya kuuza hizi *products.* Sasa nauliza hivi hapa tunafanya ngonjera, utani au tuko *really serious? (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napata shida sana kwamba ni lipi bora kwetu? Kwenye mafuriko hatuangalii kwamba siku moja kutakuwa na mafuriko, kwa hiyo, mashamba kama ya miwa yatengenezewe *structure* ambazo zinaweza kutoa miwa mashambani kwenda kwenye viwanda. Matokeo yake tuko tayari tutoe pesa ya nchi hii ikaingize sukari kutoka nchi

za nje kuliko kutengeneza miundombinu yetu. Sasa hapa *sustainability* na hivyo viwanda tunavijengaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, hii Idara ya Umwagiliaji, labda sijasoma vizuri, lakini sijaona mahali ambapo Mheshimiwa Waziri anapendekeza kwamba Idara hii ya Umwagiliaji kwa vile inakwenda kwenye kumwagilia mashamba, ihamishwe kutoka Wizara ya Maji iingie kwenye Wizara hii ya Kilimo ili wanapotengeneza mkakati wa kwamba ni mashamba gani yalimwe, basi ionekane kwamba maji yatakuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii *scenario* ipo hata kule kwangu Jimbo la Same Mashariki. Tunaweka kiwanda sasa hivi kikubwa cha tangawizi, barabara hakuna, maji hakuna, lakini tuna-*invest a lot of money* kwa ajili ya kutengeneza hiki kiwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kweli tutaweza kumsaidia Rais, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli afikie azma yake ya kuifanya nchi hii ya viwanda na uchumi wa kati kama kila Wizara inafanya *contrary?* Yaani hakuna *complementarity,* hakuna mawasiliano kwamba *priorities* ziende huku wakati wa kutengeneza barabara na wakati wa kutengeneza mashamba makubwa ya kumwagilia. Tunafanya kazi kwa *compartments,* kila mmoja anaangalia kwake na haangalii kwamba kweli huu uchumi tunaufikiaje kama tunataka kufikia uchumi wa viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niulize, hivi kwa mfano mbaazi, kwa nini tume-*rely* kwenye soko moja tu la India na tukasahau kwamba tunaweza...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Sabreena Sungura wajiandae Mheshimiwa Maftaha Nachuma na Mheshimiwa Magdalena Sakaya.

MHE. SABREENA H. SUNGURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru nami kwa kupata nafasi ya kuweza kuchangia katika sekta muhimu katika nchi yetu, lakini pia na duniani kwa ujumla. Napenda kusema kwamba sekta ya kilimo ni sekta ambayo inazalisha mara 11 zaidi ya sekta nyingine katika nchi za Afrika hususani zilizopo katika Ukanda wa Jangwa la Sahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuzungumzia vyama vya ushirika. Kumekuwa kuna migogoro mingi sana kwenye Vyama vya Ushirika. Vyama hivi vimeanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Ushirika ya Mwaka 2013 na mwenye mamlaka ya kushughulikia na kusimamia migogoro yoyote ndani ya Vyama vya Ushirika ni Ofisi ya Mrajisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakuu wetu wa Mikoa na Wilaya na viongozi wengine wamekuwa wana-*interfere* sana sekta hii ya Vyama vya Ushirika na hivyo kusababisha matatizo. Wamekuwa wana-*interfere* katika suala zima la masoko, lakini pia katika suala zima la uchaguzi, kwamba nani awe kiongozi wa ushirika? Wamekuwa na *interference* kubwa sana, kitu ambacho kinatuletea migogoro na vyama vyetu vya ushirika vinashindwa kujiendesha kama vyama binafsi na hivyo vinaonekana kama ni vyama ambavyo vinaingiliwa na siasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumwambia Mheshimiwa Waziri kwamba wananchi wa Kasulu katika Pori la Kagera Nkanda katika ziara ya Mheshimiwa Rais aliwaruhusu wananchi wale wafanye shughuli za kilimo pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara baada ya Mheshimiwa Rais kuondoka, wananchi walianza shughuli ile ya kilimo, lakini baadaye wananchi wale wamekuja kuingiliwa na kukatazwa na viongozi wa Mkoa na Wilaya. Kwa hiyo, tunataka kujua kwamba nchi hii nani mwenye mamlaka ya kupinga amri ambayo imetolewa na Mheshimiwa Rais? Tunaomba wananchi wetu wa Kasulu wa Pori la Kagera Nkanda wapewe fursa ya kuendelea na kilimo kwa sababu ni haki yao ya msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda pia kuchangia kuhusu suala zima la ardhi. Ardhi yetu imegawanyika katika maeneo mengi, hata ukiangalia kwenye sheria zake, kuna wenzetu hawa wa *Land Use Planning,* inaeleza kabisa kwamba tutakuwa na ardhi kwa ajili ya *agriculture,* tutakuwa na ardhi kwa ajili ya wafugaji, tutakuwa na ardhi kwa sababu ya *reserve,* tutakuwa na ardhi ya *forest*, tutakuwa na ardhi ambayo ni ya majanga *hazard*, lakini kwa nini ardhi ya wakulima mara nyingi inakuwa inaingiliwa na kusababisha migogoro?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii migogoro imekuwa haiishi wala haipungui, kumekuwa kuna *interference* kubwa sana, sasa kama tumetenga vitengo vya ardhi ambavyo vime-*categorize* ardhi kutokana na sekta mbalimbali, kwa nini wakulima katika suala zima la ukulima wanaingiliwa na wanashindwa kufanya kilimo chao kwa nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ni muhimu sana lingewasaidia wakulima wetu ni kuhusu kupata Hatimiliki ambazo ni za kisasa. Tunadanganywa hapa Bungeni kila siku kwamba Hatimiliki za Kimila na Hatimiliki za Kiserikali zina hadhi sawa katika mabenki yetu. Hili suala siyo kweli! Wakulima wanaoenda na Hatimiliki za Kimila katika mabenki hawapewi mikopo, mtu anaenda na Hatimiki ya Kiserikali anaonekana ana hadhi kuliko anayeenda na Hatimiliki ya Kimila. Wakulima wetu huko vijijini wanaenda kubalidishana mazao yao na chumvi, wanabasdilishana mazao yao na bodaboda, wanabadilishana mazao yao na nguo, wanabadilishana mazao yao na yeboyebo. Kwa nini Serikali isiweke mpango kabambe wa ardhi wa kuhakikisha kwamba hata ardhi za vijijini sina pata *granted right of occupancy* ili na wao waweze kuwa na hadhi sawa na watu wengine ambao wanapata mikopo na wasiendelee kubadilishana mazao zao na kuku na vitu vingine vinavyoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudi kwenye zao la mchikichi Mkoa wa Kigoma. Miaka ya 1970 Mkoa wa Kigoma tuliwapa zao hili mbegu nchi ya Malaysia na Malaysia

sasa hivi inafanya vizuri kwenye zao hili kuliko kitu chochote, kwa nini Serikali sasa isiunde Kituo cha Utafiti ili waweze kutafiti zao hili na kuweza kutusaidia wakazi wa Kigoma. Wenzetu Burundi ukifika mpakani pale mwa Kigoma ukianza Burundi mpaka unafika Makao Makuu ya Mji wa Burundi nchi yote imepandwa michikichi, kwa nini mnashinda kuendeleza zao la mchikichi katika Mkoa wa Kigoma? Ningependa kupata majibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika Wilaya yetu ya Kakonko tuna mazao ambayo tunalima, tuna mahindi, mihogo, mpunga, karanga lakini mazao ya biashara tuna tumbaku, kahawa na pamba. Serikali ina mkakati gani wa kuhakiksha kwamba mazao haya yanapatiwa ufanisi ili yaweze kusaidia katika sekta nzima ya Ardhi?*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta nzima ya kilimo inahusisha sekta nzima ya maji, huwezi kufanya kilimo bila kuwa na maji. Kwa hiyo basi, kwa sababu katika Wilaya yetu na Kakonko na maeneo mengine tumekuwa tukipokea Wakimbizi na kuna makambi mbalimbali ya wakimbizi hali ambayo inapelekea wakimbizi wale wakihitaji sekta ya nishati...*(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante muda wako umekwisha. Mheshimiwa Maftaha Nachuma kwa dakika tano na Mheshimiwa Magdalena Sakaya atafuatia kwa dakika tano.

MHE. MAFTAHA A. NACHUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhahuna Wataalah.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Waziri Mheshimiwa Dkt. Charles Tizeba aweze kunisikiliza kwa sababu haya ni maagizo ya wananchi wa Jimbo la Mtwara Mjini na Mikoa ya Kusini. Mwaka jana nilichangia Wizara hii kinatoa wasiwasi wangu juu ya suala la usambaji wa

magunia na *sulphur* bure nikaonyesha wasiwasi wangu na yametokea yale yale, kwamba mwaka huu Wizara imesema haitatoa tena *sulphur* bure na magunia bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka yote kulikuwa na pesa ambazo zilikuwa zinakusanywa ambapo hizi pesa zilikuwa zinapelekwa kwenye Mfuko wa Wakfu, lakini ule mfuko sasa hivi umefutwa na Serikali kwamba zile pesa za *export levy* taarifa tulizokuwa nazo za msimu wa mwaka jana tumeweza kukusanya zaidi ya shilingi bilioni 110 ambazo hizo pesa zilitakiwa ziende zikanunue *sulphur* kwa wananchi wa Mikoa hii ya Kusini, wananchi wanaolima korosho Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zile pesa wakulima wanauliza sana na wameniagiza nije kuzungumza ndani ya Bunge hili kwamba wamekuwa na matatizo makubwa ya *sulphur* mwaka jana, *sulphur* badala ya kuzwa shilingi 25,000 zikalanguliwa mpaka shilingi 110,000 kwa mfuko mmoja. Sasa tulikuwa tunaomba sana pesa za *service levy* ambazo zimekusanywa kupitia kwa wakulima hawa kila kilo moja ya korosho ziko zaidi ya shilingi bilioni 110, tunaomba zinunue pembejeo wakulima hawa, wananchi wa Kusini waweze kupata pembejeo kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hapa kuna wakulima ambao tayari mpaka leo ninavyozungumza wamepeleka pesa zao kwa vyama vya msingi ili waweze kupewa *sulphur* wengine wametoa shilingi 400,000 wengine shilingi 500,000 lakini mpaka *sulphur* maeneo mengi haijaenda. Mheshimiwa Waziri hapa amesema kwamba tayari wameagiza *sulphur* zipo zitaanza kugaiwa Mtwara na Lindi lakini maeneo mengi wananchi wametoa pesa *sulphur* mpaka leo bado haijafika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la msingi hapa ni kwamba kupulizia korosho wanaanza kuanzia mwezi wa Aprili maeneo mengine mwezi Mei huu, lakini mpaka mwezi wa Juni maeneo yote yanakuwa tayari yameshakamilika. Sasa unaposema *sulphur* iko njiani mpaka leo hawa wananchi wanaenda kupuliza muda gani. Kwa hiyo,

nilikuwa naomba sana Wizara pesa za *service levy*, pesa za *export levy* ambazo zimekusanywa ziende kununua *sulphur* ziweze kufika kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nimetumwa na wananchi wa Mikoa hii wakulima hawa wa korosho wanauliza suala la *CEO* ambaye alikuwa anafanya kazi nzuri sana Mheshimiwa Jarufo, tumepata taarifa ambazo siyo rasmi tu kwamba amesimamishwa kazi. Lakini ukaguzi unaonesha huyu jamaa alikuwa anafanya kazi vizuri, anashirikiana na wakulima vizuri, wakulima wanaolima zao hili la korosho, lakini tunaambia tu kwamba ametolewa. Sasa tunaomba majibu ya Mheshimiwa Waziri kwamba kumtoa huyu *CEO* ni kweli yanayosemwa na wakulima wa korosho kwamba katolewa kwa ajili ya ubaguzi. Tunaomba majibu utakapokuja kutueleza, utueleze kwamba utoaji wa *CEO* wakulima wa korosho wanasema katolewa kwa ubaguzi, lakini hajafanya jambo lolote baya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nilikuwa naomba kuzungumza hapa ni suala la malipo ya korosho. Maeneo mengi mpaka leo ziko zaidi ya shilingi bilioni nne wakulima wa korosho hawajalipwa. Wakulima wanapeleka kwenye vyama vya msingi korosho zao tangu tarehe 17 Novemba, 2017 na naomba ninukuu hapa baadhi ya maeneo tu, kuanzia pale Mtwara Mjini, Tandahimba na maeneo mengine kuna Kata ya Dinduma wananchi wanadai mnada wa tarehe 17 Novemba, 2017 mpaka leo hawajalipwa, wananchi wa Namnyanga, wananchi wa Mdimba, wananchi wa Tumbwe Tarafa ya Namikupa, Tarafa ya Mahuta, Litehu, maeneo haya yote hawajalipwa pesa zao za korosho tangu mwaka jana tarehe 17 Novemba. Jambo hili linaumiza sana kwa kweli wakulima wanajitahidi kulima kwa muda mrefu, wanalima wanapata changamoto nyingi, lakini pesa zao hawapewi kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala hili la *AMCOS*, wanaoteuliwa kuingia kwenye *AMCOS* hizi wanakuwa ni watu ambao hawana uwezo, ni watu ambao wanaenda pale kwa uwakilishi wa wananchi bila kufuata

vigezo na wahasibu ambao wanaingia kwenye hivi vyama vya msingi wanakuwa ni wajanja sana, wanapiga mabilioni ya pesa sana wahasibu kwa sababu viongozi wa *AMCOS* hawana elimu uwezo wao ni mdogo.

Naomba Mheshimiwa Waziri ulete muswada tubadilishe sheria hapa kwamba kila aneyeajiriwa kwenye *AMCOS* hizi, kila anayegombea kwenye *AMCOS* kuwe na sifa fulani angalau ya elimu wanapigwa sana, wakulima wanaibiwa sana Wahasibu wa hizi *AMCOS* zote kwa sababu uwezo wao ni mdogo. Kwa hiyo, naomba tulete Muswada wa Sheria kubadilisha hizi sheria waajiriwa waweze kuwa na uwezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine Mheshimiwa Waziri hapa wakati anazungumza ameleza kwamba kuna Tume ya kusimamia kilimo kule maeneo ya Kusini nami nilikuwa naomba sana kwa sababu maeneo ya Kusini ni asilimia 90 ya ardhi ni ardhi ambayo inarutuba sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, ajiandae Mheshimiwa Shangazi na Mheshimiwa Joseph Mhagama.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kidogo kwa dadika hizi nilizopewa kwenye Wizara hii muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema kwamba kama kweli tunataka kwenda kwenye uchumi wa viwanda ambapo asilimia kubwa inategemea mazao ya kilimo, lazima Serikali kujidhatiti kikamilifu kwenye suala la kilimo. Ukiangalia dhamira tuliyonayo na ukiangalia tunakokwenda havioani! Hatuwezi kuwa tunaenda kwenye

uchumi wa viwanda wakati huo huo kwenye kilimo tunawekeza kidogo, hatuwezi kwenda. Pia najiuliza swali pamoja na hicho kidogo tunachopa hiyo bajeti ndogo tu, Waziri umeweza kusimamia kipi kikaonekana kwa uhakika? Hicho kidogo tunachokipata, mimi naona tunalo tatizo la msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwenye utafiti, hatuwezi kwenda kwenye kilimo cha tija kama hatuna utafiti. Tulisema kwenye Bunge hili na imetengwa kwamba tuhakikishe kwenye bajeti ya Serikali tunatenga asilimia moja kwenda kwenye utafiti, leo ni karibu miaka kumi haiendi! Lini Serikali itafikia hatua ya kutoa *one percent* ya bajeti iende kwenye utafiti, hatuwezi kwenda huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna mazao mengi ndani ya nchi hii yana magonjwa sana kwa miaka zaidi ya 20 hayapatiwi ufumbuzi kwa sababu hatutoi fedha kwenda kwenye utafiti. Kuna mazao ya kilimo cha ndizi kule Bukoba hayaendi nje kwa sababa ya magonjwa hayaponi, tuna mazao ya mihogo, tuna machungwa yenye magonjwa, tuna maembe yenye magonjwa, tuna minazi hata vyuo vyetu vya utafiti hatuvipi uwezo viweze kutumia rasilimali zetu kwa ajili ya utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunazalisha, kama hatuna uwezo wa kusafirisha mazao hayo nje tunazalisha kwa ajili ya nini, ukiona maembe yetu wakati wa maembe yanaoza, yanadodoka chini, ukiangalia mengi yana wadudu, kwa nini kwa miaka 10/15 tushindwe kuja na *solution* ya magonjwa yanayosumbua mazao yetu hatuwekezi? Kwa hiyo, kwanza kabla hatujaamua kuingia kwenye utafiti hatuwezi kutoka, tutalima lakini bado hatutavuna vizuri kwa sababu nguvu zinatumika nyingi za wananchi lakini bado hatutoi kwa tija wala haturuhusiwi kusafirisha nje kwa sababu ya udhaifu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni upatikanaji wa mbegu. Kwa miaka yote mpaka leo tunapozungumzia habari ya uchumi wa viwanda, bado tunazalisha mbegu

ndani ya nchi kwa asilimia 20 peke yake, asilimia 80 tunatoa nje. Hii ni aibu kwa nchi ambayo asilimia 80 tunategemea kilimo ni aibu! Kwa hiyo, lazima Serikali ihakikishe kwamba inawekeza. Bahati mbaya hata mbegu hizi za nje bado siyo bora mimi mwenyewe nimejaribu mbegu za nje, lakini mbegu za ndani bado siyo nzuri watu tunaenda kwenye mbegu za nje sababu ndiyo zinazalisha vizuri. Kwa nini tunashindwa kujengea uwezo mamlaka zetu za ndani za mbegu zizalishe mbegu nzuri za kutosha na kwa bei nzuri, hili nalo ni tatizo kubwa sana.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Charles Tizeba, Waziri wa Kilimo ukija hapa utuambie umefanya kazi gani kwa miaka ambayo umewekwa kwenye hiyo Wizara kuweze kumsaidia Mheshimiwa Rais kwenda anakotaka, uje utuambie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kilimo ni suala la mzunguko, kilimo ni mashambani, kilimo ni maghala, kilimo ni usafirishaji na kilimo ni masoko. Kama kwenye mashamba hatuwekezi vizuri, Waziri anazungumzia juu ya uagizaji wa mbolea kwa *bulk* na kwa urahisi. Nikuambie mbolea hizi haziji kwa wakati, hata bei zake hazieleweki wanasema kwamba ni bei elekezi siyo kweli. Wilaya ya Kaliua mwaka jana tumenunua mbolea mpaka shilingi 140,000 wakati bei elekezi ni shilingi 75,000, wengine shilingi 90,000, mahali pengine shilingi 100,000, shilingi 120,000, shilingi 140,000, bahati mbaya sana mbolea ya Serikali iliyokuja imekuja wakati tunavuna wakati ni mbolea ya kupandia, leo iko kwenye maghala haina kazi, kwa hiyo, liko tatizo la msingi Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu amekuwa anafanya kazi kubwa sana kuisaidia Wizara hii. Kiukweli inapofika mahali panaonekana kitu, Mheshimiwa Waziri anafanya kazi kubwa hata kurekebisha zile *AMCOS* pamoja na ushirika wetu. Najiuliza swali kama Waziri Mkuu asingekuja Tabora kutusaidai *WETCO* leo angalau ina mabadiliko tungekuwa wapi na kwa nini Waziri Mkuu atoke alipo aje mpaka Tabora

akaangalie kuna shida gani wakati Waziri yupo? Pengine Waziri hatoshi hili ni tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni muwazi lazima tuseme, Wizara hii inahitaji mtu ambaye ni *very straight, very aggressive,* mchapa kazi anayeweza kutusaidia tunakokwenda tuweze kufika, lakini kwa Waziri aliyepo naona kama tunalo tatizo ambalo inabidi Mheshimiwa Rais aliangalie kwa karibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wa Mkoa wa Tabora tunalima tumbaku kwa kiasi kikubwa mwaka jana 2017 tumepa hasara ambayo haijawahi kutokea. Tumbaku yetu tani milioni tano imeuzwa kwa bei ya makinikia, bei ya makenikia kutoka bei elekezi dola mbili tumeuza dola 0.0... *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Rashid Shangazi atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Mhagama na Mheshimiwa Sikudhani Chikambo.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia katika bajeti iliyopo mbele ya Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku moja Mheshimiwa Rais aliwahi kusema kwamba anadhani kuna baadhi ya Mawaziri hawamuelewi, lakini mimi nataka niseme kwamba inawezekana Mheshimiwa Tizeba na Mheshimiwa Mwijage ni miongoni mwa Mawaziri ambao hawamuelewi Mheshimiwa Rais anataka nini. Hili nalizungumza katika Tanzania ya viwanda pamoja na mapinduzi ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nitajikita katika zao la mkonge. Jana sindano zilikuwa za pamba leo zihamie kidogo kwenye upande wa mkonge. Mkoa wa Tanga peke

yake una mashamba 27 ya mkonge, nchi nzima ya Tanzania inayo mashamba 53, mashamba 14 yapo katika Mikoa ya Pwani, Morogoro, Kilimanjaro na shamba moja liko Mkoa wa Arusha. Lakini mashamba haya mengi yametelekezwa na mpaka sasa ninavyozungumza hapa hata mkonge wa kusafirisha korosho na mazao mbalimbali tunaagiza *duty* kutoka nje ya nchi. Kwa hiyo, hapa utaona moja kwa moja kwamba kama tunakusudia kuwa na Tanzania ya viwanda bila kubainisha tunakusudia kuwa na viwanda vya namna gani, itakuwa hii ni hadithi ambayo itakwenda kukumbana na kifo muda si mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nchi hii ilipopata uhuru Mwalimu Nyerere alianzisha maeneo mbalimbali na mazao mbalimbali ya kimkakati ya kukuza viwanda vya ndani, miongoni mwa viwanda hivyo vilikuwa ni viwanda ambavyo vinachakata mazao ya mkonge ikiwemo *TANCORD*, ambayo wakati huo iko Tanga, kuna *Amboni Spinning*, kuna *Ubena Spinning* iko Morogoro na *TPM* ambacho kiko Morogoro na mpaka sasa hivi ndichoo kiwanda pekee ambacho kinazalisha magunia ya mkonge. Kiwanda kingine kiko Moshi, Kiwanda cha Magunia cha Moshi. Sasa utaona kwamba sasa hivi mkonge unaozalishwa nchini kwa mujibu wa takwimu za Wizara ni tani 26,495 na mwaka huu wanataraji kwamba tutazalisha mpaka tani 43,127, lakini viwanda hivi havipati malighafi za kutosha kwa singa nyingi zinasafirishwa kwenda nje kama malighafi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo viwanda vya ndani vinakosa *material* na miongoni mwa viwanda vinavyokosa ni pamoja hii *TPM* ya Morogoro, hawa wana uwezo wa kuzalisha magunia mpaka milioni 10 kwa mwaka, lakini sasa hivi uwezo wao ni kuzalisha maguni milioni moja peke yake, na soko la ndani peke yake lina uwezo wa kupata magunia milioni tatu ambayo tunaweza tukasafirisha mazao mbalimbali ikiwemo korosho. Hapa tatizo lipo wazi kwamba tatizo ni kwamba ni kwenye kodi, viwanda hivi vinavyozalisha ndani vina kodi mbalimbali *corporate tax*, kuna *VAT* na kadhalika. Wanaoagiza *duty* kutoka nje hawalipi

kodi kwa sababu hivi ni vifungashio ambavyo tumeridhia katika *Common Market Protocol* kwamba vifungashio vinavyokuja kufungasha mazao havitozwi kodi, matokeo yake ni kwamba tunakosa kodi kwa viwanda vya ndani kushindwa ku-*supply* bidhaa zao kupitia malighafi ambazo zinatoka na mazao ya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, ninakuomba sana Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana uliangalie hili kwa jicho la karibu sana kwamba ili kujenga uwezo wa viwanda vya ndani na kuelekea Tanzania ya viwanda ni lazima viwanda vinavyochakata mazao ya mkonge viweze kusimamiwa ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili nizungumzie suala la kilimo cha kahawa. Kahawa ilikuwa ni zao ambalo kule Kilimanjaro ni zao la wanaume, lakini sasa hivi wanaume wa Kilimanjaro wanashindana na wanawake kwenye ndizi, Baba Paroko pale ni shahidi kwamba hata wanawake wanaenda kutafuta *purchasing power* nje ya nchi kwa sababu wanaume wa Kilimanjaro pesa hazipo! Ni kwa sababu ya kilimo cha kahawa kimekufa na hapa tunahitaji tufanye utafiti, mabadiliko ya tabianchi sasa hivi yameikumba nchi yetu maeneo mengi kahawa haizalishwi tena. Kule Lushoto tulikuwa tunazalisha kahawa tani 300 mpaka tani 500 kwa mwaka, sasa imeshuka mpaka tani 150. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hesabu ziko sawa tu kwamba tulikuwa na shamba Kwehangala ambayo iko Jimbo la Bumbuli heka 450 sasa hivi shamba lile limekuwa ni viwanja vya kawaida tu watu wamerasimishiwa. Kwesimu heka 350 yote haya yalikuwa ni mashamba ya *Usambara Coffee Growers* sasa hivi hayatumiki tena kama mashamba ya kuzalisha kahawa. Kata sita Jimbo la Mlalo zinalima kahawa, Kata 14 Jimbo la Bumbuli zilikuwa zinalima kahawa, Kata nne Jimbo la Lushoto zilikuwa zinalima kahawa. Karibu Kata 25 ambazo zilikuwa zinalima kahawa sasa hivi hazilimi kahawa pia imeathiriwa na mabadiliko ya tabianchi. Kwa hiyo tunawaomba sana *TaCRI* wafanye utafiti ili kuweza

kuboresha zao hili liweze kurudi katika kama ilivyokuwa zamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo Lushoto peke yake hata maeneo mengine ya Tarime walikuwa wanalima kahawa, Mbozi walikuwa wanalima kahawa, Ileje - Mbeya kule walikuwa wanalima kahawa sasa hivi uzalishaji wa kahawa umeshuka sana ni lazima mazao haya yaweze kurejeshwa kama ilivyokuwa zamani na yatarejeshwaje? Ukurasa wa 69 hapa tumeona kwamba Wizara inazungumzia kwamba *TaCRI* watakuwa moja kwa moja wanawajibika kwenye Wizara na miongoni mwa majukumu yao itakuwa ni kufanya utafiti pia kugawa mbegu na kutoa elimu kupitia Maafisa Ugani, sasa hili la Maafisa Ugani ndiyo ambalo mimi ningeshauri muanze nalo. Maafisa ugani walioko huko hawaelewi kabisa hata huko Usambara kulikuwa kuna kahawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TaCRI* pia wafanye utafiti kutokana na mabadiliko ya tabianchi ni aina gani ya mbegu ambayo inaweza ikawa bora kwa hali ya hewa iliyopo sasa. Sambamba na hilo ni lazima sasa *AMCOS* za kahawa pia ziboreshwe. Vile vyama vyetu vya Ushirika vya zamani, *Usambara Cooperative, TARECU* na kadhalika vimekufa, kwa hiyo tunahitaji sasa kutoa elimu mpya ya ushirika kwa wakulima hawa wa kahawa kwa kule Usambara ili kuongeza tija lakini kuongeza uzalishaji na sisi tuweze kushiriki katika uchumi huu wa Tanzania ya viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika kwamba Waziri mwenye dhamana bado sijaona kama ana jitihada maksudi za kufufua zao la kahawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na semina mbalimbali zinazoendelea lakini tunahitaji sasa hizi semina ziweondoke maofisini, zihamie kwenye maeneo kahawa inakozalishwa. Kumekuwa na miaka miwili ya kuendesha semina maofisini, sasa naomba uanze kwenda *site*, acha kuvaa suti ni wakati wa kuvaa *gumboot* na kuingia *site* kuhakikisha kwamba wakulima huko wanazalisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni tozo kwenye nguo ambazo zinaingizwa nchini ili kunusuru viwanda vyetu vya nguo. Viwanda vya nguo...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mhagama, wajiandae Mheshimiwa Sikudhani na Mheshimiwa Sixtus.

MHE. JOSEPH K. MHAGAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi naomba nijielekeze moja kwa moja kwenye hoja na mchango wangu utajikita kwenye eneo la soko la mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kupata mapinduzi ya kilimo Tanzania kama hakutakuwa na mfumo madhubuti wa soko la mazao. Kinachomfanya mwananchi wa Madaba, mwananchi wa Njombe, Songea Mkoa wa Ruvuma, mwananchi wa Katavi, mwananchi wa Rukwa, mwananchi wa Sumbawanga, Songwe na Mbeya aamke asubuhi, aweke jembe begani akalime ni kwa sababu anataka kupata pesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkulima haendi kulima kwa ajili ya kutatua tatizo la *food security* ya nchi, ile ndiyo ofisi yake. Mwananchi wa Madaba, mwananchi wa Katavi anakwenda kulima mahindi kwa sababu anataka ajenge nyumba bora, kwa sababu anataka asomeshe mtoto wake katika shule zenye sifa, kwa sababu anataka amudu mahitaji ya afya katika hospitali zenye ubora, anataka kuishi maisha bora huyu Mtanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunaongelea asilimia 70 ya Watanzania ambao kipato chao kinatokana moja kwa moja na shughuli za kilimo, lakini tunaongelea asilimia karibu 90 ya Watanzania ambao kwa namna moja au nyingine wanategemea kilimo. Huwezi kupata mapinduzi ya kilimo bila mfumo madhubuti wa soko la mazao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Madaba wameumia sana na mfumo wa masoko, pia wananchi wa Mikoa yote niliyoitaja ukiwemo na Morogoro wameumia sana juu ya ukosefu wa soko la mahindi. Wakulima hawa kama ambavyo Wabunge tunataka tuwasomeshe watoto wetu katika shule zenye sifa, tujitibu vizuri, tujenge nyumba bora, tuvae nguo safi, nao pia wana ndoto hiyo. Hatuwezi kuipata Tanzania yenye mapinduzi ya kilimo kama hatutaki kuwekeza kwenye masoko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikupe ushahidi, ukuaji wa sekta ya kilimo mwaka 2014/2015 ulikuwa asilimia 3.4 na ukuaji wa sekta hiyo mwaka jana 2016/2017 ilikuwa asilimia 2.1, kwa nini? Kwa nini ukuaji umeshuka ni kwa sababu *incentive* ya mkulima ni soko. Hawezi kwenda kununua mbolea, hawezi kujikita kwenye mbegu bora, hawezi kutafuta mbinu bora za kilimo kama kilimo hakimlipi. Kwani ni nani ameenda kuwaambia vijana wanunue bodaboda, wafanye biashara Mjini, si kwa sababu inalipa? Hivi leo tunahitaji kuwambia wakulima wakalime? Tuwape soko wakulima watakwenda kulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkulima yeyote akishajua tangawizi inamlipa, mahindi yanamlipa, kahawa inamlipa huhitaji kwenda kumfundisha kulima atakutafuta mwenyewe, atakuambia nifundishe namna ya kulima mahindi, atakutafuta mwenyewe atakuuliza umwambie mbolea iko wapi. Leo tunawaweka wananchi wetu wakulima katika mazingira magumu sana, Madaba na maeneo mengine masikitiko ni makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea na hoja yangu nimshukuru sana Waziri na Ofisi yake Wizara ya Kilimo wamenisaidia sana, mwaka huu nilikuwa napoteza Ubunge Mabada kama suala la mbolea lisingezingatiwa. Ucheleweshaji ulikuwa mkubwa, wananchi wamelalamika lakini nakushukuru Waziri ulinisaidia na timu yako ya Katibu Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la soko la mahindi Serikali inajaribu kulitatua lakini bado halijapatiwa ufumbuzi. Mwaka 2015/2016 tulikuwa na ziada ya tani milioni 2.6 Serikali ilinunua tani 22,000 tu, mwaka uliofuata tani milioni tatu ziada Serikali ilinumnua tani 62,000 tu za mahindi. Mkoa wa Ruvuma hapa nina taarifa aliyopewa Waziri Mkuu alipokuja, tulizalisha ziada ya mahindi/nafaka tani milioni 1.4, ilinunuliwa tani 10,000 tu, tunakwenda wapi? Wakulima hawa wote mahindi haya wameyapeleka wapi? yameharibika, wameendelea kuwa maskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya kuzingatia muda nitakwenda moja kwa moja kwenye ushauri. Mheshimiwa Waziri azingatie mambo yafuatayo:-

Moja, sera ya kilimo inataka mambo manne nchi yoyote, nenda Marekani, nenda nchi zozote za Kusini mwa Afrika, Kenya na kokote sera yoyote ya kilimo ina mambo manne ambayo ni *safety, security, sufficiency* na *quality* ya maisha ya mkulima. Mheshimiwa Dkt. Tizeba hili naamini unalizingatia na tunaomba sana ulizingatie. *(Makofi)*

Pili, sera yoyote ya *agricultural trade,* sheria zote za mipakani zilenge kulinda maslahi na maendeleo ya wakulima ndani ya nchi yako ndipo utapata haya yote unayotaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaenda haraka haraka. Ilani ya Chama cha Mapinduzi imetoa mapendekezo juu ya ufumbuzi wa tatizo la soko la mahindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja imesema katika ukurasa wa 12, tuanzishe soko la mazao sasa *commodity exchange* kwa maana ya kwamba wakulima wetu wanapoingia shambani wawe na uhakika wa soko. Leo Sudan hawana chakula, Uganda na Tanzania tunapishana misimu ya kulima, Kenya wanahitaji mahindi ya Tanzania leo tunasema tunawanyima mahindi wakati mahindi yanaoza Madaba. Ilani ya Chama cha Mapinduzi imetoa muongozo kwenye eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili imependekeza *NFRA* iwe na kitengo cha kununua mahindi, inunue mahindi ya hifadhi lakini inunue mahindi ya kutosha kwa ajili ya kutafuta soko la nje. Kama tunataka ku-*control inflation,* kama tunataka tu-*control food security* basi *NFRA* apewe hayo majukumu, leo amepewa bilioni 15 badala ya kupewa shilingi bilioni 86, shilingi bilioni 15...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Sikudhani Chikambo wajiandae Mheshimiwa Sixtus Mapunda, Mheshimiwa Rashid Chuachua na Mheshimiwa Mama yetu Salma Kikwete.

MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote kwanza napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyenijaalia kusimama katika Bunge hili kuweza kutoa mchango wangu katika hii Wizara muhimu kama tunavyofahamu kwamba Wizara ya Kilimo ndiyo Wizara muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msimu wa mwaka 2016/2017 nilisimama kwenye Bunge hili, niliipongeza Serikali kupitia mfumo mzuri wa stakabadhi ghalani. Nilithubutu kusema kwamba mimi ni miongoni mwa waumini wa mfumo huu wa stakabadhi ghalani, ninaamini ni mfumo pekee ambao utaweza kumkomboa mkulima wa korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilieleza pia changamoto zilizopo kupitia mfumo huu wa stakabadhi ghalani. Mfumo huu wa stakabadhi ghalani, miongoni mwa changamoto zilizopo ni pamoja na wananchi kutokulipwa pesa zao kwa wakati. Waheshimiwa Wabunge wengi wamelizungumza jambo hili na katika vikao vilivyopita tulisema kwamba wananchi hawa wanapolima korosho na mazao mengine tumaini lao ni kutatua matatizo yao ikiwemo kusomesha

watoto wao na mambo mengine mengi hata ikiwezekana kwa wale wababa ambao wanakusudia kuongeza wake wengine kupitia pesa hizi, lakini kinyume chake kimekuwa sivyo, wananchi wengi wamekuwa wakipata misukosuko. Sheria inaeleza kwamba baada ya kuuza korosho ndani ya siku saba mkulima anatakiwa apate pesa zake, lakini imekuwa sivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka hivi tunavyozungumza wapo wakulima ambao wanaendelea kudai pesa zao. Sisi Wilaya yetu ya Tunduru zaidi ya shilingi milioni 200 wakulima wanadai, inawezekana pengine kupitia udhaifu wa makarani waliopo katika vyama vyetu vya msingi na ninapozungumza makarani waliopo kwenye vyama vya msingi naamini kwamba taasisi hii inahusika moja kwa moja na ushirika, lakini inahusika moja kwa moja na Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napata shida sana kwenye jambo hili kwa sababu mara nyingi tumelizungumza hapa kuona umuhimu wa wananchi kupata pesa zao. Sasa niombe Waziri atakapofika atueleze ni lini sasa wananchi wale watapata hizi pesa kwa sababu tumewahamasisha waweze kuuza mazao yao kupitia mfumo wa stakabadhi ghalani, lakini badala yake imekuwa matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na kutolipwa pesa na wakati, liko jambo lingine ambalo limejitokeza, wananchi kupata malipo yao kupitia benki, sina uhakika kama ni jambo la kisheria. Ninaweza nikazungumza upande wa korosho lakini baharti nzuri wako Wabunge wengine wamezungumza hata kupitia mazao mengine. Inaonekana kama ni jambo la lazima kwamba wananchi wapate pesa zao kupitia benki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana Serikali ilikuwa na nia njema katika kuona fedha za wananchi zinabaki katika mikono salama, lakini badala yake imekuwa sivyo. Wakati wa mauzo ya korosho ukija Wilaya ambazo zinahusika na mazao haya utawahurumia wananchi. Wanapanga foleni

kwenye mabenki, mtu anatoka kilometa 100 anakuja Makao Makuu ya Wilaya kufuata pesa yake, anakuja anaweza akakaa wiki nzima lakini anapofika dirishani anaambiwa pesa yako wewe haijaingizwa kwenye akaunti yako, mkulima yule anarudi kijijini, anarudi tena mjini imekuwa usumbufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya hilo basi tutofautishe kwa sababu siyo wakulima wote ambao wanapata mazao kwa kiwango kinachofanana, wako wakulima wengine wanauza mazao yao kwa uchache kadri ya Mwenyezi Mungu alivyomjalia kuvuna, sasa tunamtaka hata mtu wa kilo tano aende akapokelee pesa zake benki, mtu wa kilo 50 aende akapokelee pesa zake benki, mtu wa kilo 100 aende akapokelee pesa zake benki.

Mimi naomba kama ni jambo la kisheria basi ni vizuri tufanye marekebisho. Wananchi hawa wanakata tamaa na huu mfumo. Inafika mahali wanaona kwamba siyo mfumo mkombozi, kwa hiyo mimi niombe na nimuombe Mheshimiwa Waziri ni vizuri kama ni jambo la kisheria na sheria hiyo iwe imetungwa na Bunge hili walete tufanye mabadiliko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwamba dhamira kubwa ya hawa wakulima wanapolima ni kutatua matatizo yao. Mtu ameuza korosho toka mwezi Novemba mpaka leo hajapata pesa yake, naliongea jambo hili kwa masikitiko makubwa na mimi ni sehemu ya wakulima wa korosho inauma sana, naomba Serikali ilitilie mkazo jambo hili katika kufanya marekebisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nizungumzie suala la viuatilifu ikiwemo mbolea na *sulphur.* Wabunge wengi wamezungumza kuhusiana na suala la upatikanaji wa mbolea, tumekuwa tukisema sana, mbolea hizi haziji kwa wakati lakini leo tumepunguza ruzuku. Ukija kwenye *sulphur,* mwaka jana mimi nilisimama hapa kuchangia wakati tunasema kwamba Serikali itatoa *sulphur* bure, tuliipongeza Serikali, lakini tuliwaomba ni vizuri muweke mfumo sahihi ambao utaelekeza ni namna gani wananchi hawa

watapata *sulphur* bure, leo mmekuja na mabadiliko mengine, hivi kweli tuna nia ya kuliendeleza zao la korosho kama siyo nia ya kuliharibu zao la korosho? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nilizungumze hili kwa sababu sote tumehamasika sasa hivi na ndiyo maana Waziri husika amefika mahali amepeleka miche ya korosho maeneo ambayo ana uhakika hata korosho hazitaota Wabunge wamesema hapa, ni kwa kuona korosho zimeongeza pato la Taifa letu, ni jambo jema lakini kwa nini tusisimamie tukaona hivi viuatilifu vinapatikana kwa wakati? Hii *sulphur* tumeeleza kwenye kitabu cha Waziri katika ukurasa wa 30 kwamba *sulphur* wanetegemea kwamba Bodi ya Korosho itatangaza bei. Hivi tunavyozungumza tayari korosho zimeanza kuchipua lakini mpaka leo bado...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Sikudhani kwa mchango mzuri. Mheshimiwa Sixtus, Mheshimiwa Chuachua na Mheshimiwa Mama Salma Kikwete.

MHE. SIXTUS R. MAPUNDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa na mimi nafasi ya kuchangia kwenye hii Wizara ya Kilimo. Nianze mchango wangu kwa nukuu maarufu sana iliyopendwa kutumiwa na Marais wawili wa Marekani kwa nyakati tofauti, Ronald Reagan na Abraham Lincoln naomba niisome hiyo nukuu; *"You can not strengthening the weak by weakening the strong."* Kwa Kiswahili kisichokuwa rasmi ni kwamba "hauwezi ukamuimarisha mtu aliye dhaifu kwa kumdhoofisha aliye imara."

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya kilimo ndiyo sekta imara kuliko sekta zote kwenye nchi yetu. Ni sekta pekee inayoongoza kwenye pato la Taifa kwa ripoti sahihi na *statistics* zinatuambia inaongoza pato la Taifa kwa asilimia 26.1 ikifuatiwa na viwanda asilimia 7.3, sekta ya madini asilimia 4.1 na sekta ya utalii asilimia 3.1 kwenye kuzo la pato

la Taifa. Pia sekta hii ndiyo sekta inayoongoza kwa kuajiri Watanzania wengi zaidi ya asilimia 70, sekta hii ndiyo inayoongoza kwa *export* zaidi ya asilimia 85, sekta hii ndiyo inayoongoza kwa kutuhakikishia chakula kinapatikana nchini kwa asilimia 100. Pamoja na uimara wa sekta hii, tukaiangalia *report* ya Waziri mwanzo mpaka mwisho hatuoni sekta hii ikiimairishwa zaidi tukiona ikidhoofishwa kwa *expense* ya sekta nyingine, hii haiwezi ikawa sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wa Tanzania wanahitaji matumaini, wamefikishwa sehemu wamekata tamaa kabisa. Wamekata tamaa katika eneo la uzalishaji, wamekata tamaa katika bei, wamekata tamaa katika mfumo mzima wa kilimo kuanzia mazao ya chakula mpaka mazao ya biashara hakuna zao hata moja ambalo tunasema hili ni salama, kila zao lina tatizo. Tulitarajia leo hii angalau tupate njia ya kutokea, lakini hatuoni matumaini katika sekta ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Waziri inasema kwa makadirio mwaka huu tunaweza tukazalisha mahindi tani milioni nane, maana yake itakuwa imepanda kwa tani milioni mbili kutoka mwaka jana milioni sita sasa tunakwenda milioni nane lakini uwezo wa *NRFA* kununua mahindi, wana uwezo na wamepanga kutumia tani 28,200 tu. Tafsiri yake tutakuwa na tani zaidi ya milioni saba hazitanunuliwa na *NRFA,* maana yake ili kiwepo chakula wakulima wa mahindi, lakini sisi kule kwetu nenda ukaanzie Rukwa, Katavi, Iringa, Mbeya, Njombe na Ruvuma wote katika ujumla wetu hatulimi mahindi tu kama chakula, tunalima vilevile mpunga unakubali, viazi vinakubali, ndizi zinakubali na mihogo inakubali. Ukituambia tule mahindi tu tusiuze maana yake unataka tufe kwa kwashakoo, kitu ambacho si sawa! Lazima hii sehemu iliyobaki ya mahindi tani milioni saba Waziri uje hapa na mchanganuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati za hizi tani 2,220 zitakazonunuliwa na *NFRA* utuambie una mpango gani wa soko la nje, una mpango gani kwa kiwango gani pia kwa

kiwango kitakachobaki kitumike kama chakula ndani ya nchi yetu.Vinginevyo mimi sitakuunga mkono kwenye hoja hii na wakulima hawatanielewa nikikuunga mkono kwenye huo mchanganuo uliouweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao la kahawa bado tunaendelea kuumia, tunaumia katika maana ya uhakika wa soko, tunaumia kwa maana ya uhakika wa pembejeo, tumeomba kwa muda mrefu sana Serikali ijaribu kutazama pembejeo kwenye zao la kahawa, kwa sababu ni zao la muda mrefu lilikuwa linatuletea fedha za kigeni kwa kiwango kikubwa sana, lilipoanza kusuasua vyama vya ushirika vilivyokufa na Serikali ilipoondoa mikono na miguu ndipo tulipoharibikiwa. Leo hii tunashukuru sana Waziri Mkuu kwa ziara alizofanya kwenye maeneo ambayo tunalima kahawa kwa kweli tumeona dhamira ya dhati ya Waziri mkuu kurudisha vyama vya ushirika viende kwenye mazao ya biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliopo *site*, mashaka tunayoyaona kwenye vyama vya ushirika ni makubwa, leo hii hawa watendaji wa vyama vya ushirika ndiyo walioshiriki kuviua miaka hiyo ya nyuma. Tunakwenda mwezi ujao kwenye msimu ujao, wakulima wa pamba wanalalamika watalaam hawapo, wakulima wa kahawa tunalalamika wakulima wa korosho tunalalamika, watumbaku tunalalamika, tutakwendaje? Katika huu muda mfupi katika *crash program* tunaiomba Serikali ipeleke watalaam kama kweli tunataka tufufue ushirika. Vyama vya Ushirika haya mazao ambayo mwaka huu tumeyahamasisha tumezalisha kwa kiwango kikubwa tunayahifadhi wapi? Kwa mfano pamba, *consumption* ya pamba yetu ndani kabla ya uzalishaji ilikuwa *only 20%* viwanda vyetu vya ndani vinaweza kuchakata, asilimia 80 tulikuwa tuna-*export* tumehamasisha pamba imezalishwa kwa wingi, tutaiweka wapi? Lazima kuwe na mkakati wa dharura vinginevyo tutakuja mwakani hapa tena tutaanza kulalamika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho naomba niseme kuhusu pembejeo, tumelalamikiwa sana kuhusu

mawakala wa pembejeo wametiwa umaskini, wametoa huduma lakini hakuna tamko la Serikali linaloelezea haki yao watapataje? Kama hawajafanya kitu kizuri basi ieleweke, nani kakosea na nani kapatia, kuwaweka jumla tu kwa muda mwaka wa miaka miwili wakazika hela yao tunatengeneza umaskini uliokithiri, umaskini uliopitiliza. Lakini niseme neno moja Serikali ikiimarisha bei nzuri ya haya mazao hatutahiji mbolea ya rukuzu kwa sababu mbolea ya rukuzu inakuja kwa kuchelewa lakini muda mwingine inakuja hailingani na udongo wa eneo husika. Tungekuwa na utaratibu wa kununua mazao ya wananchi vizuri kwa bei nzuri tusingepata shida...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango mzuri. Mheshimiwa Chuachua, ajiandae Mheshimiwa Mama Salma.

MHE. RASHID M. CHUACHUA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kupata nafasi ya kuzungumza kidogo kuhusiana na Wizara hii muhimu kwa uchumi wa Taifa letu, Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuwapongeza sana Serikali pamoja na Mawaziri kwa kazi wanayoifanya kwa sababu changamoto katika kilimo zipo lakini yapo mambo ambayo hata wakulima wa korosho tunaona wameyafanya katika kupiga hatua mbele ya kutetea wakulima wetu. Changamoto zipo nasema lakini yapo mambo ambayo yamefanyika niwapongeze sana katika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia 80 ya chakula kinachozalishwa *Sub-Saharan African* pamoja na Asia kinazalishwa na wakulima wadogo wadogo ambao wanatengeneza ajira takribani kwa watu bilioni mbili. Sambamba na hilo asilimia zaidi ya 70 ya watu wanaoishi kwenye Bara la Afrika ni wakulima wadogo wadogo, Tanzania tuna asilimia zaidi ya 60 ya wakulima wadogo wadogo. Hakuna ubishi kwamba *this is the largest private*

sector on earth, lazima Serikali iangalie namna ya kutetea, kuwasimamia na kuwasaidia wakulima wadogo wadogo. Hata mjadala wetu katika Bunge kuanzia jana unawagusa wakulima wadogo wadogo. Ni muhimu Serikali sasa iangalie namna ambavyo inajikita sawasawa katika kupunguza au kuondoa kero zinazowakabili wakulima wadogo wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao utaratibu unaosemekana wa kuanzishwa kwa mabenki kwa ajili ya kuwakopesha wakulima wetu, ukweli unabaki pale pale kwamba wakulima hawa hawakopesheki. Inawezekana hawakopesheki kwa sababu miundombinu yetu ya kisera, kwenye sera ya kilimo au sera ya fedha lakini inawezekana hii inatokana na sababu ya miundombinu ya utaratibu mzima wa kuangalia namna gani mabenki haya yanaweza yakawa-*favor* wakulima wetu haijakaa sawa. Tunahitaji kubadilisha taratibu zetu za kifedha au sera zetu ili wakulima hawa waweze kukopesheka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, umefika wakati wa Serikali kuangalia kwa kina ni namna gani inaweza kusimamia matumizi bora ya ardhi zetu. Ukweli uko wazi kabisa kwamba Tanzania ina ardhi kubwa, lakini yapo maeneo ambayo yanakabili sawa wakulima wadogo wadogo kutokana na kuingiliana na wafugaji kwa ajili ya migogoro inayotokea hapa na pale. Migogoro ya ardhi pamoja na migogoro ya vyanzo vya maji haya ni maeneo ambayo Serikali inatakiwa ichukue hatua ili mkulima aweze kufanya kazi yake kwa tiza zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati sasa umekwishafika kwa ajili ya Serikali kuangalia namna ambavyo wakulima wanaweza wakawa na bima katika shughuli zake za kilimo, hili ni jambo la muhimu sana. Ni jambo muhimu kuanzia mkulima anakwenda kuandaa shamba mpaka anapeleka mazao yake sokoni. Kwa sababu tunapoweza kuangalia mnyonyoro mzima wa thamani ndivyo tunavyoweza kuboresha maisha ya mkulima kwa kupunguza athari au *risk* inayoweza kumpata katika shughuli zake za kilimo. Haya ni

mambo ambayo ni ya muhimu Serikali yetu ya Awamu ya Tano iangalie ili kuimarisha wakulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo pia eneo lingine, kilimo cha sasa lazima kiende sambamba na kisukumwe na haja ya soko la ndani na soko la nje. Ni lazima wakulima wetu wasimamiwe vizuri kabisa, namna gani wanaweza wakafanya kilimo chao kuwa biashara, wakati huo huo Serikali iangalie namna ya kupanua soko la ndani. Wabunge wengine wamekwishazungumza kwamba ili kutengeneza soko la ndani liwe na fursa ya kutosha ni lazima tuangalie namna ambavyo tunapanua uwekezaji katika viwanda vyetu ili Serikali iweze kuona namna gani wakulima wanaweza kuuza *raw materials* kwenye viwanda, wakati mnafikiria soko la nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, soko la nje ni muhimu kwa sababu tunahitaji fedha za kigeni, lakini soko la ndani ni muhimu zaidi kwa sababu tunahitaji wakulima hawa waweze kupata soko la uhakika. Leo hii tunauza asilimia zaidi 95 nje ya nchi. Leo hii tunauza pamba zaidi ya asilimia 80 nje ya nchi, hivi Wahindi ambao kwa mfano ambao ni wanunuzi wakubwa wa korosho pamoja Vietnam, wakisema sasa korosho ambazo wanalima huko zinawatosheleza tutauza wapi hizi korosho? Kwa hiyo, ni muhimu kuimarisha viwanda vyetu vya ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye masuala mengine ambayo Wabunge wameyazungumzia kwa kina. Mwaka huu Serikali kupitia Bodi ya Korosho ilifanya kazi ya kuingia mikataba na vikundi vya ujasiriamali pamoja na watu binafsi kwa ajili ya kuzalisha miche ya korosho. Katika mikataba ile Serikali iliwaahidi kuwalipa asilimia 30 kabla ya kuanza kufanya kazi na baadae kumalizia asilimia 70 ya malipo yao ili waweze kusambaza miche ya korosho. Ile *advance payment* haijalipwa, lakini kwa bahati mbaya sana mpaka leo hao waliosambaza miche kwa ajili ya mikorosho nao hawajalipwa. Hili ni jambo *serious* sana, kwa sababu ikiwa kila ambao wanajitolea na wanaonyesha uzalendo wa kusaidia sekta hii ya kilimo wanachelewa sana kulipwa

fedha zao, utafika wakati watu wataona Serikali yetu haiko *serious* katika kuhakikisha kwamba wakulima wanapata huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lipo jambo lingine la muhimu na wengine wamekuwa wakilisema, mwaka 2015/2016 walitokea watu ambao walikuwa wanasambaza pembejeo mawakala. Hili jambo kila Mbunge amekuwa akilisema na mimi nasema umefika wakati sasa unajua ukiwaona hawa mawakala wako *very loyal* na wanaonesha kabisa kwamba fedha ambazo wanaambiwa na Serikali ndizo zinadaiwa kama deni siyo fedha sahihi. Inaonekana kwamba ni bilioni 35 tu ambazo ziliidhinishwa lakini ukizungumza na mawakala wanaonyesha wazi kabisa kuna vocha zilibaki na zilirudishwa kutoka katika Mikoa hawajui vocha hizi ziko wapi? Deni linaonekana ni shilingi bilioni 64, ukweli ni kwamba madai ya mawakala wetu ni tofauti na fedha zilizoandikwa na watendaji waliosimamia zoezi hili.

Kwa hiyo, ni aibu sana miaka karibu miaka mitatu, minne tunazungumzia tunawahakiki, tunawahakiki kitu gani? Wale walioiba tunawafahamu tukamate tuweke ndani na hawa watu wengine walipwe. Hili ni jambo muhimu sana ambalo tunapaswa kuliangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine mpaka leo wananchi wangu wa Masasi wameniagiza sana niseme *sulphur* haijafika na ile ambayo inauzwa kwa bei ambazo siyo rasmi *na* siyo halali zinauzwa zaidi ya shilingi 70,000 kwa mfuko mmoja. Ni lazima sasa Serikali...*(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako mzuri. Mheshimiwa Salma Kikwete, ajiandae Mheshimiwa Anna Tibaijuka

MHE. SALMA R. KIKWETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu hatimaye

nikushukuru wewe kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia Wizara hii muhimu sana ya kilimo. Tukiamini kwamba kilimo ni uti wa mgongo wa Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ifikapo mwaka 2025 tunategemea kwamba nchi yetu ya Tanzania itakuwa ni nchi ya kipato cha kati ikiongozwa na kaulimbiu yetu ya Tanzania ya viwanda. Hili ni jambo jema sana kwa ustawi wa Taifa letu la Tanzania. Pamoja na hayo ili tuweze kufikia azma yetu ya 2025 kuwa Tanzania ya viwanda ni lazima kama nchi tuwekeze sana kwenye kilimo na hasa kilimo cha umwagiliaji ambacho kinatupa uhakika wa kile ambacho tunatarajia kukifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi nyingi duniani zilianzia kwenye kilimo hatimaye kukaja na mapinduzi ya viwanda, kwa mantiki hiyo tukiwekeza kwenye kilimo tutakuwa na uhakika wa kupata malighafi zitakazotusaidia kwenye viwanda vyetu hatimaye tutaweza kukua kwa kadri tulivyokuwa tunatarajia. Ushauri wangu kwenye jambo hili ni lazima tupange mikakati yetu vizuri ili azma yetu hii tunayoitarajia iweze kutekelezeka kama tulivyojipanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikizungumzia kwenye eneo la ufuta. Ufuta ni zao kubwa na ni zao muhimu. Sisi kama Tanzania tunalima ufuta lakini kama Afrika vilevile nchi yetu ni nchi ya pili ikiongozwa na Ethiopia, pia hatuko nyuma kwenye dunia. Katika nafasi ya dunia sisi Tanzania tuko kwenye kumi bora. Kwa mantiki hiyo ina maana kwamba tukiwekeza vizuri kwenye ufuta, nini kitakachoweza kujitokeza, tunaweza kuzalisha wenyewe mafuta ambayo sasa hivi ni changamoto kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumzia ufuta wakulima wetu tuliwahamasisha sana juu ya kilimo cha ufuta na mazao mengine mbalimbali. Tatizo linakuja baada ya wakulima kuweza kulima vizuri lakini hata hiyo pesa yenyewe waliyotumia kulima wamekopa kwenye mabenki, inafikia hatua uuzaji inakuwa ni changamoto kubwa kwao. Kwenye eneo hili vilevile ninafarijika. Nimesikia kwenye taarifa hapa

kwamba, kuanzia sasa kuelekea siku zijazo ufuta nao utakuwa ni kati ya mazao ambayo yatauzwa kwa stakabidhi ghalani, ninaipongeza sana Serikali kwa kuweka ufuta kwenye stakabadhi ghalani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nielekee...

T A A R I F A

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimpe msemaji taarifa kwamba kitendo cha ufuta kuingizwa kwenye stakabadhi ghalani kitasababisha hasara kubwa sana kwa wakulima kwa sababu unyaufu wa ufuta ni mkubwa sana kuliko unyaufu wa korosho. Kwa hiyo tusingependa ufuta uingie kwenye stakabadhi ghalani. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mama Salma.

MHE. SALMA R. KIKWETE: Ahsante sana kwa taarifa hiyo ambayo ameitoa, pamoja na kuitoa hiyo taarifa siipokei, kwa sababu kubwa za msingi yeye akiwa Mbunge anajua kwa nini hili limeingizwa kwenye stakabadhi ghalani. Naomba nilindie muda wangu niendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kuhusu korosho. Korosho tunaamini na zao kubwa na ni zao ambalo linachangia uchumi wa Taifa letu la Tanzania. Lakini sasa korosho hii imeingiliwa na mdudu na mdudu huyu ni unyaufu wa korosho. Katika taarifa sikusikia eneo lolote, ni mkakati gani wameupanga juu ya kuondoa tatizo hili la unyaufu wa korosho. Korosho hizi zinalimwa Lindi, Mtwara, Tanga, Pwani na Mikoa mingi ambayo iko kwenye Ukanda wa Pwani na sasa hivi korosho litakuwa ni zao la Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Lindi hakuna kiwanda hata kimoja, ina maana kwamba suala la korosho lisipowekewe mkakati wa kudumu wananchi wa Lindi watazidi kuwa maskini kwa sababu hawatakuwa na kipato chochote kile, kwa kuwa hakuna kiwanda hata kimoja.

Mheshimimwa Mwenyekiti, naomba nielekee kwenye zao la mbaazi. Mbaazi tuliwahamisha wakulima walime, wengi sana walilima kweli kweli. Lakini ikafikia wakati mbaazi zikakosa soko, Mkoa wa Lindi ni asilimia 20 tu kati ya mbaazi zote ambazo zimeweza kuuzwa nyingi zimeharibika na wananchi hawa ni maskini. Serikali tunaomba iwasaidie chochote ili waweze kuendelea na kilimo waweze kujipatia maslahi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo nakushukuru sana kwa kunipa fursa, lakini jambo lolote ni mchakato, naamini matatizo haya tukijipanga yataisha. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Salma Kikwete kwa mchango mzuri. Mheshimiwa Profesa Tibaijuka, ajiandae Mheshimiwa Nape Nnauye, ajiandea Mheshimiwa Pauline Gekul.

MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Wizara ya Kilimo kwa kujitahidi kutuletea mpango mzuri ambao kazi yetu sasa ni kujaribu kuonesha namna ya kuboresha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ibara ya 239 ukurasa wa 99 Mheshimiwa Waziri ameanza vizuri, ameanza kwa kuanza kwa kutupa mihimili minne ambayo sasa ataitumia katika kuendesha kilimo. Kwa umuhimu wake ninaomba ninukuu muhimili wa nne ukurasa wa 129 anasema anakwenda; “kuweka mfumo mpya wa usimamizi wa kilimo, kwa lengo la kuweka mazingira wezeshi kwa uendeshaji kibiashara na kuwezesha wakulima kuwa na sauti katika uendeshaji na biashara ya mazao yao.” Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina budi kumpongeza sana Waziri kwa mkakati huu na kwa wale waliokuwa wanasema Waziri hatoshi mimi naomba nitofautiane nao, anatosha

kabisa. Anatosha kwa sababu ametuonesha *principles* zake, sasa mimi naomba nioneshe matatizo ambayo nadhani yatakukwamisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu cha kwanza kabisa katika nchi hii labda wengi hatutambui kwamba mazao ya kimkakati kimsingi yanaendeshwa kwa sera za kikoloni ambapo mazao yale kimsingi sio mali ya wakulima, yanachukuliwa hususani kama mali ya Serikali. Jambo hili naomba litambulike na mimi nasimama hapa kwa niaba ya walionituma, wananchi wa Muleba Kusini na niseme kwamba Kagera kwa ujumla na Kanda ya Ziwa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya kilimo katika Jimbo langu la Muleba Kusini na kusema Ukanda wa Ziwa kwa ujumla ni taabani. Ni taabani kabisa ukweli ndio huo, hali si nzuri na tukiendelea hivi bila kumuunga mkono Mheshimiwa Waziri na kuleta mawazo ya kisasa, mawazo yanaweza kuleta mapinduzi katika kilimo tutaendelea kutaabika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapoona katika Ibara ya 178 wanazungumzia kwamba hatimaye watafikiria mpango wa mkakati kama wa *SAGCOT* kwa ajili ya Kanda ya Ziwa, mwaka jana nilisema na ninarudia kusema kwamba umechelewa Mheshimiwa Waziri, nataka kujua hiyo *LAPCOT (Lake Province Agricultural Growth Corridor)* inaanza lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu nchi yetu ilivyo ni vizuri kwamba *SAGCOT* iendelee na ni haki ni lazima tuipe nguvu lakini wakulima wa Kusini hawawalishi wakulima wa Kaskazini, hawawalishi Mikoa ya Ziwa, ninasimama hapa watu wamenituma hapa tena wananiamini kabisa neno mgomba hakuna neno mgomba katika kitabu hiki, jamani ndizi siyo chakula? tena sisi Wahaya tunasema kama ndizi haziko mezani na chakula hamna au siyo? Zao la ndizi/ mgomba umesahaulika kabisa *this is not serious,* hatuwezi kuwa na mpango wa kilimo ambao umesahau kabisa zao la mgomba! Hilo ni la kwanza naomba Mheshimiwa Waziri utakaposimama mimi ninaimani na wewe uje uniambie imekwendaje Mheshimiwa Tizeba imekuwa Tizijuka

umesahau kabisa? Maana yake majina haya yanashabihana kwa wale ambao hawajui lugha hizi, yaani tumekwendaje. Hiyo naomba Mheshimiwa Waziri lijibiwe tujue. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mnyauko tulikuwa tunahangaika hapa na mnyauko, *this is now forgotten completely* hakuna hata neno lolote la kusaidia wakulima wa migomba nchi nzima, *mind you* hata Mbeya *SAGCOT* wako, hilo ni la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili niongelee ushirika kwa haraka. Ushirika nilisema wakati tunajadili bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na nashukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu mambo mengine ambayo ameyafanyia kazi naona vijana wa *TRA* wanaanza kujipanga upya nashukuru sana, lakini suala la ushirika msiuchukulie kama tukio, sasa hivi Mheshimiwa Tizeba huna uwezo wa kuingia Muleba kununua kahawa yote. Ulikwenda kule nakushukuru lakini nilisikiliza ile *speech* yako uliyoyasema yale hayawezi kumsadia bibi kizee kama mimi ana magunia yake mawili pale mlangoni unamuambia abebe magunia apeleke kwenye chama cha msingi ambacho hakipo, ambacho kitafunguliwa kimechelewa, wakati ana uwezo wa kununua *direct farm gate price* kuuza kahawa yake kwa mteja wakapeleka . *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamani muangalie *implications* za vitu tunavyovipanga vingine havitekelezeki kwa mtu anayejua hali halisi ya kijijini, naomba Mheshimiwa Waziri unahitaji *time,* tukupe *time* ya mwaka huu uandae ushirika uje *next year* kutuambia *direct purchase, farm gate price* tunafunga na inayoeleweka kusudi tuweze kushiriki. Hii hii umeshtukiza mno *it can't work!* Lazima niwe mkweli kwako kwamba hapa tunapozungumza wenzangu wa Kigoma watasema, lakini kahawa imevuka. Kwa hiyo mambo haya Waziri anaenda vizuri tumuwezeshe na mwisho kabisa tumpe wataalam wa ugani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Kilimo hana watalaam, huyu Waziri *he is a general without an army!*

Maafisa Ugani wako chini ya Halmashauri, namshukuru sana Mheshimiwa Rais hatimaye Maafisa Ardhi wamerudishwa, Mabwana Shamba ni Wataalam wamesomea hizi fani, warudishwe kwenye Wizara mama waweze kuwajibika, sasa hivi wanafanya wanalotaka huko. Kwa hiyo, Maafisa Ugani hawapo nadhani tutakwama kwa mambo haya. Kwa hayo mambo matatu na utafiti ni muhimu sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mbegu hasa nimeona hapa *Agricultural Seed Agency* na wenyewe wanazo tani 700 wakati nyingine zote zinatoka nje, ninaomba uwezeshe *agricultural seed agency* kununua sasa mbegu kwa ajili ya *distribution* kwa wakulima, huo ni ushauri wangu, nafikiria kwamba Mheshimiwa Waziri anafanya kazi vizuri, lakini mfumo alionao hauwezi kumruhusu kwenda mbele. Kwa sababu kama wakulima wanamiliki mazao yao basi tuwape nafasi hawa watu wakulima ambao wako kwenye *fair trade* watu wa kahawa ambao wako kwenye *fair trade, organic trade* wale waruhusu hawana haja ya kuja kwenye mnada wa Moshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnada wa Moshi kile ni kituo cha mazao tu mnada huko London na New York, kama unataka kupata bei nzuri *auction* zipo London zipo New York pale Moshi tunafanya *coordination* tu na *coordination* inaweza ikafanyika pia kwa kutumia *farm records. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nafikiria kwamba wataalam wako Mheshimiwa Waziri wakupe *proper analysis* ya mambo yalivyo wengine humu tunayaelewa, tuko tayari hata kusaidia, lakini ukija na vitu ambavyo havitekelezeki, kwa mfano ukisema kwamba kwa dharura unazuia watu kuwasaidia wakulima itakuwa shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache atakaporudi naamini kwamba tutaelewana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Nape ajiandae Mheshimiwa Gekul, ajiandae Mheshimiwa Frank Mwakajoka.

MHE. NAPE M. NNAUYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie kwenye mapendekezo haya ya bajeti ya Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpa pole Kaka yangu *Engineer* Dkt. Tizeba nadhani hii kazi ni ngumu kidogo na pengine yako mambo yapo nje ya uwezo wake, naona toka jana shughuli imekuwa ngumu kidogo hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisikiliza mjadala huu toka jana kwa mara ya kwanza kuna dalili kwamba watu wengi hawaungi mkono haya mapendekezo, bila ya kujali pande zote na bahati nzuri kwa mfumo wetu wa bajeti tulionao iko *room* ya Serikali kwenda kuangalia upya, kwa sababu tunaanza na bajeti ndogo ndogo halafu tunakwenda kwenye bajeti kubwa. Kwa hiyo, ushauri wangu wa kwanza Mheshimiwa Waziri na Serikali tusione shida kukubali hali halisi kwamba ni vizuri tuende tukaangalie upya bajeti hii wala tusione taabu, ni jambo la kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mazingira tuliyonayo kama *trend* yenyewe ndiyo hii, nataka kusema huu ni mtihani mkubwa sana kwa Serikali ya Awamu ya Tano kwenye hii bajeti. Kwa sababu ni hapa ambapo tutatakiwa kujipambanua tunajikita kwenye maendeleao ya vitu au maendeleo ya watu. Kama ni maendeleo ya watu bajeti hii ndiyo inagusa zaidi ya asilimia 80 ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kelele unazozisikia Mheshimiwa Waziri kwenye pamba, kahawa, korosho na mbaazi ambayo mmetuambia tukale na maeneo mengine yote ni kwa sababu inagusa maisha ya watu. Sasa Serikali tunayo *choice* ya *message* tunayotaka kuipeleka kwenye umma. *Message* kwamba tunajali maendeleo ya vitu au tunajali maendeleo ya watu ambao ndiyo waliotuweka madarakani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia *trend* mwaka wa fedha 2016/2017 Serikali ilitenga asilimia 0.93 ya bajeti kwenye

Wizara ya Kilimo, mwaka 2017/2018 ikashuka ikaenda asilimia 0.85, mwaka 2018/2019 haya mapendekezo ya sasa hivi tumeshuka tena tumekwenda asilimia 0.52 ya bajeti. Maana yake moja tu ni kwamba kila mwaka tunashusha bajeti tunayoitenga kwenye sekta ambayo ndiyo inagusa watu wengi kuliko wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakumbukwa hapa tuliwahi kupendekeza wakati fulani na tukashambuliwa kama vile siyo wazalendo, kama vile tuna chuki hivi, tulisema Serikali ni vizuri ikakwepa kuwekeza fedha za ndani nyingi kwenye miradi mikubwa ambayo inaweza kujiendesha kibiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kuendelea kushuka kwa bajeti muhimu kama ya kilimo ni kwa sababu tumeamua kupeleka fedha zetu za ndani kwenye kuwekeza kwenye miradi mikubwa ambayo ingeweza kujiendesha kibiashara, kwa hiyo madhara yake tutayaona tu. Inawezekana kweli tukaonekana siyo wazalendo lakini hivi ukweli huu unahitaji elimu gani kujua kwamba tunaendelea kushuka na mimi naamini hili kaka yangu Mheshimiwa Tizeba siyo lako, tutakubebesha mzigo ambao siyo wako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana nimemsikia shemeji yangu Mbunge wa Ruvuma mpaka analia hapa, watu wanadai, watauziwa mali zao kwa sababu bajeti unayopewa ndogo huna namna. Hela inaenda wapi kama tumebana matumizi, hela inaenda wapi kama tunakusanya? Bahati mbaya rafiki zangu ushabiki unakuwa mwingi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu wa kwanza Serikali isione aibu kuipitia upya bajeti hii kwa sababu bajeti hii tukiipitisha kama ilivyo *message* kwa Watanzania ni mbaya sana kwa Serikali ya Awamu ya Tano kwamba tunataka kuwekeza zaidi kwenye vitu badala ya watu! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda ukaangalia hali halisi thamani ya mazao ambayo wananchi wetu

wanazalisha imeshuka sana. Nilikuwa naambiwa jana mahindi Ruvuma yamefika shilingi 15,000 kwa gunia, nenda kwenye maeneo yote kwenye mbaazi huko hata sitaki kusema, lakini bidhaa ambazo wananchi wanatakiwa kuuza bidhaa zao wakanunue bidhaa kama sukari, mafuta ya kula na vitu vingine vyote vimepanda sana, sasa uhalisia unakataa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tukikubali ni wananchi wangu nikikubali wakulima wa korosho watanishangaa, nikikubali wakulima wa mbaazi, ufuta na wakulima wengine wote katika nchi hii watanishangaa, wakulima wa pamba ambao tumewahasisha wamelima pamba kiasi kile watanishanagaa*! (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mazingira haya Mheshimiwa Waziri sijui, lakini nilikuwa naangalia Ilani ya Uchaguzi ambayo wengi hawataki tuinukuu, lakini ndiyo tuliyoiombea kura, ndiyo mkataba wetu na wananchi, bajeti hii ukipitia Ilani ya Uchaguzi zinakataana. Sasa kama zinakataana *simple logic* ndogo tu, tuishauri Serikali irudi mezani, muda upo bajeti kubwa tutakuja kuipitisha baadae, muda upo tuende tukaangalie upya tuweke vipaumbele ndicho tulichokubaliana na wananchi, humu tumekubaliana kwamba wananchi wetu Serikali tutakayoiunda itawasaidia kupata masoko ya nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kelele unazozisikia za mahindi na mazao mengine mgogoro wake uko hapo, kelele unazozisikia za mbaazi mgogoro wake upo hapo, ukimwambia mtu akale magunia 20 ya mbaazi si unamtukana huyu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Tanzania iliingia mkataba na Serikali ya China tupeleke muhogo, mkataba mmesaini mwezi Mei, 2017 tangazo kutoka Wizarani kwako ya kupeleka imetolewa Aprili...*(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Gekul, ajiandae Mheshimiwa Frank Mwakajoka.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee alikoishia mchangiaji aliyepita kwamba bajeti hii Serikali inyoongozwa na Chama cha Mapinduzi mmepoteana na llani ya Chama chenu lakini siyo tu kupoteana, mmepoteana na wapiga kura asilimia 80, waliowapigia kura ambao mnawaita ni wanyonge kila siku. Mheshimikwa Rais akisimama anasema Serikali ya Mheshimiwa Magufuli ni ya wanyonge. *(Makofi)*

Sasa kama ni ya wanyonge halafu bajeti ya wanyonge inapunguzwa kwa asilimia 34 bajeti ya *development* ya ajabu! Wanyonge gani wa nchi hii mnawaongoza wakati juzi tu kwenye maji mlipeleka asilimia 22, mkapitisha ile bajeti kwa *caucus* mkaitana mkaipitisha, lakini hii bajeti Mheshimiwa Waziri asilimia 18 tu ndiyo imepelekwa mpaka sasa, halafu mnajiita Serikali ya wanyonge, mlishapoteana zamani sana, siyo kupoteana na llani mpaka na wapiga kura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mbaazi amesema Mheshimiwa Nape, Waziri kwenye kitabu chako mbaazi hata kuongelea ujaongelea kabisa. *(Makofi)*

T A A R I F A

MHE. ALMAS A. MAIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna Bajeti ya Serikali inayopitishwa na *caucus* hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa hiyo anayeongea sasa hivi kwamba hakuna bajeti ya Serikali inayopitishwa na *caucus* ya chama chochote, bajeti inapitishwa na Bunge lako.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Gekul endelea taarifa hiyo.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, hata mtaitwa tu mtaenda *caucus* naomba niendelee kwa sababu hivi hivi haitapita hii bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali ya kawaida Mheshimiwa Waziri hata mbaazi hujaongelea kwenye kitabu chako, maana yake unatuambia watu wa Kanda hii yote tuliyolima mbaazi tukale na watoto wetu ndiyo Serikali ya wanyonge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa natafuta kwenye kamusi nini maana ya laana, lakini nikaona tu niipotezee kwa sababu wakulima wa nchi hii wanawalaani sana maana wamekaa mazao yao, wamekaa na mbaazi zao na mahindi yao ninyi hamuhangaiki, unakuja hata huongelei suala la mbaazi Mheshimiwa Waziri, sasa unasema ni Serikali ya wanyonge asilimia 80 ya Watanzania hata huhitaji kuongelea? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mahindi mmesema hivi mnataka muongeze *production* ifike tani milioni nane kutoka tani milioni sita iliyoko sasa, lakini Mheshimiwa Waziri unafahamu mliunda Bodi ya Mazao Mchanganyiko, ile bodi wanahangaika mmewakabidhi tu majengo ya *National Milling* mpaka leo Bodi ya Mazao Mchanganyiko wanaomba shilingi bilioni tisa kwenu hamjawahi kuwapatia hizo shilingi bilioni tisa, hao watu bodi ya mazao mchanganyiko wangetusaidia kununua mahindi yetu, mbaazi zetu wakachakata. Mnaita Tanzania ya viwanda mmeshindwa hata kufufua majengo ya *National Milling* mpaka leo. Bodi ya Mazao Mchanganyiko wanaomba shilingi bilioni tisa kwanye bajeti mnawanyima, wameomba mkopo *NSSF* shilingi bilioni tatu hata Serikali haitaki ku-*endorse* huo mkopo halafu mnasema mna mkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri kwenye kitabu chako umesema eti mmefungua mipaka mahindi yapelekwe nje ya nchi, huku mnasema kwamba ninyi ni Serikali ambayo inafufua viwanda na nchi ya viwanda hivi viwanda ndiyo kupeleka mazao nje ya nchi? Kwa nini

hamtaki kutoa hizi fedha shilingi bilioni tisa *National Milling* hawa na Bodi ya Mazao Mchanganyiko wakachukua mahindi yetu wakaweza kuyachakata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aibu zaidi katika Serikali yenu hii *NFRA* mliwapa fedha mwaka jana za kununua tani 18,000; mwaka huu mmewatengea fedha kununua tani 28,000 wakati mahindi tunazalisha tani milioni sita! Ninyi watu mmeshapoteana zamani sana, *you are in the middle of nowhere!* Hamjuani katika hili la wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaudhi mimi naomba niende kwenye *solution* naipongeza sana Kamati hii na hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani ambayo wameshauri *solution* mbalimbali... *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Frank Mwakajoka, ajiandae Mheshimiwa Qambalo Willy Qulwi na Mheshimiwa Grace Tendega.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na mimi kwa kupata nafasi hii niweze kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli kilichotokea kwenye nchi hii na kinachoendelea yako mambo ya ajabu sana, wakati Serikali hii ya Awamu ya Tano imeingia madarakani ilisema kwamba ni Serikali ya wanyonge, lakini huwezi kuamini kinachotokea, bajeti zinatengwa kila mwaka lakini utekelezaji wake haujawahi kuzidi asilimia 20. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka uliopita 2016/2017 ilitengwa bilioni mia moja na moja lakini fedha iliyokwenda kufanya shughuli za maendeleo ilipelekwa bilioni tatu. Mwaka 2017/2018 imetengwa bilioni 150 lakini fedha iliyokwenda kutekeleza majukumu ya maendeleo kwenye kilimo ni shilingi bilioni ishirini na saba ambayo ni sawa na asilimia 18.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposema kwamba hii ni Serikali ya wanyonge huu ni uhuni kwa Watanzania, Watanzania wanasikitika kupita kiasi, wanaona kama wamepata mkosi kwa sababu ya Serikali hii. Haiwezekani kabisa hii Serikali siyo Serikali ya wanyonge imekuwa ni Serikali ya watu asilimia tano wenye kipato cha chini na kipatao cha juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii asilimia tano ya Watanzania ambao wanauwezo wa kupanda ndege ndiyo ambao wamepewa kipaumbele katika nchi hii, leo hawa watu ambao wa wana uwezo wa kupanda ndege katika Taifa hili wanaendelea kununuliwa ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zimenunuliwa ndege tano kwa mkupuo na juzi wanasema wameongeza ndege ya sita kwa ajili ya kuhakikisha kwamba watu asilimia tano ambao wako katika Taifa hili wenye uwezo wa kununua magari, wenye uwezo wa kufanya kazi, wenye uwezo wa kujenga nyumba nzuri, lakini wale watu maskini wote wamesahauliwa kabisa. Jambo hili linasikitisha sana. *(Makofi)*

T A A R I F A

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu nimpe taarifa mchangiaji kwa mujibu wa Kanuni kwamba Serikali tunaposema ni Serikali ya wanyonge si kweli kwamba hatujadhihirisha hilo, wewe utakuwa ni shahidi Serikali hii ilivyobadilisha mtazamo mzima wa huduma za afya katika nchi yetu ya Tanzania na hao Watanzania anaowasema asilimia takribani 67 ambao ni wakulima, ndio hao ambao wameweza kupatiwa huduma za huduma za afya katika maeneo yao kwa kiasi kikubwa kwa mabadiliko ya Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, Serikali yetu pia imefanya kazi nzuri sana ya kutoa elimu bure kwa Watanzania wengi na hasa wanyonge. *(Makofi)*

MHE. PAULINE P. GEKUL: Anachangia, anachangia Mwenyekiti.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge hata kwenye suala la kilimo tunaelekea hukohuko kuwakomboa wanyonge. Kwa hiyo, hiyo ni taarifa na ni lazima aelewe kwamba tunaendelea.

MHE. FRANK J. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka nimjibu kwamba taarifa yake siipokei kwa sababu hata fedha za afya ambazo zinakuja kwenye bajeti yetu ni fedha ambazo zinatoka nje. Fedha za ndani hakuna fedha yoyote inayokwenda kwenye Wizara ya Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba Mawaziri wakae watulie, kazi yetu sisi kama Wabunge ni kuishauri Serikali. Sisi hapa hatugombani na Serikali bali tunaishauri iweze kufanya kazi vizuri lakini watu wanaomba taarifa ambazo hazitaweza kuisaidia nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema ni kwamba Serikali hii haijajipanga kuhakikisha kwamba maisha ya Watanzania yanakuwa bora. Watanzania asilimia 80 ambao ni maskini ambao ni wakulima na wafugaji wamesahaulika kabisa katika Serikali hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado naendelea kusisitiza Serikali hii ni Serikali ambayo imekuwa tofauti kabisa na Serikali zilizopita, ni Serikali ambayo haiwajali wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka kipindi cha Mheshimiwa Mkapa wakulima waliweza kuenziwa sana, walipelekewa pembejeo na walilima. Kipindi cha Mheshimiwa Jakaya Kikwete tumeona hali halisi ilivyokuwa kwenye bajeti ambazo zinaonekana kwenye taarifa za fedha mbalimbali kwa miaka ya nyuma lakini Serikali hii imekuwa Serikali ya vitu na siyo Serikali ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi hawa tunakoelekea watakwenda kuwauliza mwaka 2020 na kama mnafikiri wananchi wa miaka ya nyuma ndiyo wananchi wa sasa hivi, hawa wananchi wanaona na wanasikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna mawakala wetu walioweza kusambaza mbolea miaka iliyopita leo mnasema mnafanya uhakiki wa mawakala wetu kwamba wamedanganya, hivi mawakala wote nchi nzima ni wezi? Kwa nini tunaendelea kuishauri Serikali kwamba iendelee kuwaamini Watanzania, iendelee kuwaamini wananchi wake hamtaki kuelewa jambo hilo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda bado kwa sababu nimeibiwa muda. Nataka kusema mawakala wetu wapatiwe fedha zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine tumepata taarifa kwamba wanataka kutuletea mbolea ya Minjingu. Mbolea ya Minjingu kwenye Nyanda za Juu Kusini ni mbolea ambayo haikubaliki kabisa, imeshindikana. Tuliwahi kutumia mbolea hii lakini tulipata hasara kubwa. Tunaomba mbolea hii...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante, muda wako umekwisha.

MHE. FRANK J. MWAKAJOKA: Bado.

MWENYEKITI: Tulikuongezea dakika moja, si unaona sita na dakika moja hiyo? Kaa chini, Mheshimiwa Qambalo.

MHE. QAMBALO W. QULWI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii adhimu ambayo nimeipata ili na mimi niweze kuchangia Wizara hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma kitabu cha Mheshimiwa Waziri mwanzo mwisho, mara mbili, mara tatu.

Kama kweli haya yalioandikwa humu yatakwenda kutekelezwa nchi hii itakuwa *paradiso* nyingine. Hata hivyo, inaonyesha miaka yote mitatu iliyopita Waziri hakuwa na hela hivi atafanya maajabu gani ili yote haya mazuri aliyoandika humu yaende kutekelezwa? Sioni tofauti kubwa kati yake Waziri na Waziri Kivuli ambaye hana mafungu, sana sana Waziri anatembelea gari la Serikali. Kwa sababu miaka yote anapata chini ya asilimia 20, atakwendaje kutekeleza haya yote yameandikwa humu ndani? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii tulikuwa na historia ndefu ya ukulima uliotukuka wa mazao ya kahawa, mkonge, ngano na mazao mengine leo mazao hayo yameangukia pua. Sasa mahindi tunakwenda kuangukia pua, mbaazi tumekwishaangukia pua, ngano tunaangukia pua, hivi mkulima wa nchi hii alime nini ili awe salama? Sioni wapi yupo salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye masoko ya mazao. Mwaka jana mahindi tuliangukia pua, mbaazi tukaangukia pua, safari hii tunakwenda kuvuna, hivi mnatuambia nini sisi wakulima? Tunakwenda kuangukia pua au sasa tunaangukia mdomo ili meno yaishe? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge mwaka jana wakati Serikali imekuja kutoa kauli ya zuio la kupeleka mahindi nje, Waziri Mkuu alikuwa amekaa pale alipotoa kauli hii ni sisi wenyewe ambao tulimshangilia na upande huu ndiyo mlimshangilia zaidi, wale wanaojiita *the big five* ndiyo walishangilia kuliko wengine. Kweli wanasema mzigo mzito mbebeshe Mnyamwezi, leo Tizeba ataubeba mzigo huu kwa sababu haikuwa kauli yako. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wakulima tunalima ili tuzalishe chakula na tukauze ziada. Nimelima mahindi ya kutosha halafu unaniambia nisiuze, hivi unanizuia nisiuze nimekopa shamba niko mwenyewe, nimelima niko mwenyewe, nimenunua mbegu niko mwenyewe, palilia mwenyewe, navuna mwenyewe, halafu unakuja unasema

usiende kuuza kule. Sasa kama hutaki nikauze huko basi nunua wewe, sasa na wewe huna uwezo wa kununua si uniche huru nikauze? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani wakati mwingine huyu mkulima tumuache huru auze. Tuko kwenye utengamano wa Afrika Mashariki haya mambo ya kuuziana mazao ni ya kawaida. Mimi nikivuka Namanga naona soko zuri unaniambia nisiende, hasa nunua wewe basi unipe hela nzuri huwezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tumefika mahali wakulima wa mbaazi wameacha mbaazi shambani wanachungia ng'ombe, mahindi yanaoza kwenye maghala yetu, mnataka tupeleke watoto shule, mnataka tujenge madarasa, mnataka tuchangie hospitali, fedha hizi tunapata wapi? Mimi nadhani kwa kweli hatuwatendei haki wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi tulikuwa kwenye semina ya kilimo masula ya viwavijeshi vamizi. Wabunge tulipata semina lakini imekuja kwa kuchelewa sana, huko vijijini watu wanavuna halafu ndiyo mnatufanyia semina. Pia ilikuwa semina ya Wabunge na wakulima je? Wakulima wamehangaika mwaka mzima hakuna mtu anayewasaidia si Mkurugenzi na si Waziri ni mateso matupu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tishio la viwavijeshi huyu ni kubwa sana, hili kwa kweli ni janga la nchi. Bahati mbaya sana sijui kama nchi hii haina mfuko wa kuhangaika na majanga, kwa sababu hakukuwa na namna ya kumsaidia mkulima. Hata wale wa Maafisa Ugani hawana uhakika wa dawa ambayo inaweza kupambana na mdudu huyu, wakulima wameachwa tu. Kwa hiyo, tusipoangalia mwaka huu hata mavuno yatakuwa chini sana lakini pia ubora wa mahindi yatakayozalishwa utakuwa chini kwa sababu huyu mdudu ametusumbua sana. Kwa hiyo, nafikiri tuwe na mfuko imara ambapo likitokea janga kama hili wananchi waweze kusaidiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi Maafisa Ugani ndiyo wamekuwa Watendaji wa Kata na Vijiji. Nakubaliana kabisa na pendekezo...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Grace Tendega ajiandae Mheshimiwa Mtolea.

MHE. GRACE V. TENDEGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata fursa ya kuchangia katika Wizara hii ya Kilimo ambayo ni muhimu kwa zaidi ya asilimia 80 ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende moja kwa moja, kwanza kabisa ni bahati mbaya sana sekta hii ya kilimo imekuwa haipewi kipaumbele. Asilimia zaidi ya 80 ya Watanzania ni wakulima na napenda niseme katika taarifa ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha wakati akiwasilisha ukomo wa bajeti alisema kwamba katika bajeti ya mwaka 2018/2019 bajeti hii imetoa kipaumbele katika mambo yafuatayo, nitayasema machache. Alisema kwanza kulipa deni la Serikali; pili, kugharamia ujenzi wa miundombinu pamoja na reli na viwanja vya ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeweka kipaumbele katika vitu na si watu na ndiyo maana watu wanajiuliza, hivi mnavyosema uchumi umekua, umekua wapi? Mifukoni mwa watu hawana pesa, wakulima wanalima hawapati masoko ya mazao yao. Hawa wakulima sijui itakuwaje, mtawajibu nini mwaka 2020 kwa sababu mmewatelekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi katika Mkoa wangu wa Iringa wananchi wanalima mahindiambayo ndiyo zao lao la chakula na ndiyo zao lao kuu la biashara pamoja na mazao mengine yakiwemo alizeti, ngano, karanga, viazi na vitu vingine. Haya mahindi yalikuwa yanauzwa mpaka shilingi 80,000 kwa gunia mpaka shilingi 100,000 mwaka jana. Sasa

hivi gunia la mahindi ni shilingi 25,000, debe moja ni shilingi 5,000 mpaka shilingi 4,000. Huyu mkulima amenunua mbolea kwa gharama kubwa sana mwishoni anakuja kuuza gunia la mahindi kwa bei ambayo hata nusu ya mfuko wa mbolea haifikii, hii haikubaliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukijigamba hapa tunakwenda kununua ndege ili wananchi wapande, wananchi wangapi wanaopanda ndege? Katika Mkoa wangu wa Iringa ukitaka kuhesabu wanaopanda ndege asilimia zaidi ya 90 hawapandi ndege. Tunaomba mkae mliangalie suala hili ili wananchi hawa waweze kupata fedha kwa kuwapatia masoko ambayo yatakuwa yanawasaidia wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende katika suala la mbolea. Mbolea zimekuwa haziji kwa wakati, sisi kule kilimo chetu msimu wetu unaanza Novemba amabo ndiyo mvua za kupandia zinaanza lakini inapofika Februari au Machi ndiyo mbolea zinakuja, hii mbolea itamsaidia nani? Tumewatupa watu wetu na hatuwapi mambo yanayostahiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijawa Mbunge nilikuwa nasikia masuala haya ya kulalamikia bajeti ya Wizara ya Kilimo, ya kulalamikia jinsi ambavyo mawakala wanapata shida. Nimekuja nipo Bungeni mwaka 2015 hivyo hivyo, mwaka 2016/2017 hivyohivyo, naingia hii mwaka 2017/2018 bado suala la kulalamikia bajeti ndogo ya Wizara ya Kilimo iko vilevile. Tunaenda wapi na nchi hii? Tunakwenda wapi na Watanzania wanakwenda wapi? Mmesema tunataka tuwe na nchi ya viwanda, viwanda hivi vitapata malighafi kutoka wapi? Wakulima wamekata tamaa kabisa, hawana matumaini na Serikali yao... *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mtolea wajiandae Mheshimiwa Omary Mgumba na Mheshimiwa Jitu Soni.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, lakini pia nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na kuniwezesha kusimama mahali hapa ili tuweze kuishauri Serikali ya Chama cha Mapinduzi ili baadae iweze kufanya kazi vizuri na maendeleo yawafikie Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uchache sana, mimi nilikuwa na mapendekezo matatu tu ambayo nataka kuikabidhi Serikali ya Chama cha Mapinduzi ili wayafanyie kazi.

La kwanza, napendekeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi iangalie uwezekano wa kuiunganisha Wizara ya Kilimo na Wizara ya Biashara, Viwanda na Uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo la pili, nataka Serikali ikubali sasa ili tuelekee kwenye mapinduzi makubwa ya kilimo na kuijenga Tanzania ya viwanda basi tukubaliane kupiga marufuku uagizaji wa vyakula na malighafi zingine ambazo zinaweza kuzalishwa hapahapa nchini. *(Makofi)*

Pendekezo la tatu, ni kupendekeza Chama cha Mapinduzi ambao ndiyo *marketing manager* wa sera zinazotekelezwa na Serikali wabadilishe *logo* yao, wabadilishe nembo ya jembe na nyundo ambayo haihamasishi mapinduzi ya kilimo hapa nchini. Naomba niyajadili haya bila kufuata mpangilio wa namba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Serikali ya Chama cha Mapinduzi ilipoanza kusema wanataka kuitengeneza Tanzania ya viwanda, hatukuwa tunategemea kwamba tujenge viwanda ambavyo havitatumia malighafi zinazotoka shambani. Tuliamini kwamba Tanzania ya viwanda ni viwanda vile ambavyo vitatumia malighafi zinazozalishwa mashambani ili ziweze kuzalisha bidhaa ziweze kupandisha thamani mazao yetu na Mtanzania huyu ambaye anaitwa mnyonge ambaye kimsingi ametiwa unyonge na Serikali ya Chama cha Mapinduzi aweze kubadilisha maisha yake yale bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana tukasema ili haya yafanye kazi vizuri, ni lazima Wizara ya Kilimo na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ziwe zinafanya kazi kwa pamoja. Kitendo cha kutengana kwa Wizara hizi ndiyo unakuta anakuja Waziri wa Viwanda anakusomea hapa kwamba wamejenga viwanda vingi, lakini ni viwanda vya kutengeneza kandambili, viwanda vya kutengeneza mabeseni, viwanda vya kutengeneza mabanio ya nywele, viwanda vya maji, vitu ambavyo havitusaidii kuboresha mazao yanayotoka shambani. Kama wangekuwa wanafanya kazi kwa pamoja maana yake kwenye mafanikio ya Wizara ya Viwanda angekuja angesema kwamba tulikuwa tunazalisha mafuta ya kula asilimia 30 tu ndani sasa tumepandisha tunazalisha mafuta ya kula kwa asilimia 45.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungekuwa tunaona pia kwenye viwanda kwamba zao la chikichi limetengewa fedha kubwa ili uzalishaji wa malighafi za kutengeneza mafuta zipatikane ndani. Tusingekuwa tunaona kwenye kilimo wakulima wa ufuta wanalalamika kwamba hawana soko la uhakika, tusingekuwa tunalalamika kwamba eti kuna mafuta ghafi yamekwama bandarini yanataka kuingizwa huku ndani tunaanza kupiga kelele hapa inaharibu muda wetu wa kufanya mambo mengine kama malighafi hizo zingekuwa zinazalishwa ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna nchi imepiga hatua kwenye mapinduzi ya viwanda bila kupitia kipindi kigumu. Ukienda India watakuambia tulisimamisha kuagiza magari kutoka nje kwa sababu tulitaka tuzalishe ya ndani kwanza ili soko letu la ndani lote litumie magari ya ndani.

Ukienda China hivyo hivyo, sisi hapa bado tunaagiza sukari, mafuta, soya, mihogo mikavu kutoka nje, tunashindwa nini kulima hapa? Tupige marufuku uagizaji wa mazao haya kutoka nje, hata kama tunazalisha mafuta kwa asilimia 30 tuitumie hiyo hiyo, tutaona namna gani kumbe tunaweza tukaongeza, tunaweza tukatengeneza fursa kuzalisha hapa nchini. Hatuwezi kufa kwa kukosa mafuta ya kula, hatuwezi kufa kwa kukosa sukari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii sukari siyo kwamba tunashindwa kulima hapa ndani, ni ukiritimba tu wa kulinda viwanda vikubwa. Ukienda kule Kilombero kila mwaka miwa inalala shambani mnunuzi hakuna.

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Omary Mgumba ajiandae Mheshimiwa Jitu Soni.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nina dakika kumi.

MHE. OMARY T. MGUMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi...

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika zangu unazikataa.

MWENYEKITI: Ngoja tumsikilize dakika kumi zako ziko vipi?

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nina dakika kumi, tuna dakika 20 ameongea Mheshimiwa Maftaha dakika tano, Mheshimiwa Magdalena Sakaya dakika tano, Mheshimiwa Vedasto amejitoa sasa naingia mimi dakika kumi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa sikiliza, nafasi za CUF ni mbili, kwa maana hiyo mnachangia dakika 20 watu wanne.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Watatu.

MWENYEKITI: Wewe sasa hivi ni mtu wa ngapi kuchangia?

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mimi nachangia ni mtu wa tatu.

MWENYEKITI. Sasa si dakika 5?

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mimi napata dakika kumi.

MWENYEKITI: Dakika kumi kakupa nani na hapa majina yenu yamekuja manne? Wakati mwingine tukisema mnasema Kiti kinaleta umwamba, nafasi zetu ni watu wanne, dakika ni tano, tano. Amezungumza Mheshimiwa Maftaha, Mheshimiwa Sakaya na wewe ni wa tatu, sasa dakika kumi anatoka nani? Kuna nafasi nyingine moja ya mtu wa CUF, kama unaitaka...

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Vedasto amejitoa.

MWENYEKITI: Mimi sina taarifa, nataka mniandikie taarifa rasmi.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Amekuandikia.

MWENYEKITI: Mimi sijapata taarifa yoyote.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Sasa ukweli ndiyo huo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lulida umejitoa?

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Alikuwa Mheshimiwa Vedasto siyo Mheshimiwa Lulida.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lulida umejitoa?

MHE. RIZIKI SAID LULIDA: Ndiyo nimejitoa.

MWENYEKITI: Sasa mnatakiwa mnipe taarifa, wakati mwingine ni mawasiliano tu, haya endelea. *(Makofi)*

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Mwenyekiti...

MWENYEKITI: Hata malumbano na Kiti muda umechukuliwa vilevile, twende.

WABUNGE FULANI: Aaaa. *(Kicheko)*

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mkulima wa miwa kule Kilombero, tunalima miwa hatuwezi kupanga bei sisi anapanga bei anayekuja kununua. Yeye ndiye anapanga bei ya namna gani atautoa huo muwa wako kutoka shambani kuupeleka kiwandani kwake na namna ya kulipa pia anachangua yeye kwamba nakulipa kwanza asilimia kumi, hii asilimia kumi nyingine nitakulipa mwezi unaofuata yaani mkulima unakuwa kama unasaidiwa wakati unauza mazao yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yupo mfanyabiashara mmoja alijaribu kujenga kiwanda kidogo cha kutengeneza Sukari pale Sanje akapigwa vita mpaka akafunga kiwanda. Kwa hiyo, kuna mikakati ya makusudi kuhakikisha hakuna viwanda vidogo vidogo vya kutengeneza sukari vinajengwa ili wale ma-*giant* wakubwa ndiyo waendelee kuzalisha sukari hiyo kidogo ili mwisho wa siku Serikali itoe vibali vya kuagiza sukari kutoka nje wapewe wao ndiyo waingize wapate faida kubwa, hatuwezi kuitengeneza Tanzania ya namna hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni nembo ya Chama cha Mapinduzi, tunasema tunataka kwenda kwenye mapinduzi makubwa ya kilimo lakini wewe Mheshimiwa Waziri unasimama kunadi kwamba tunataka tuachane na jembe la mkono huku umezungukwa na watu waliovaa *t-shirt* ambazo zimebeba jembe la mkono na nyundo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara ni *brand,* namna ambavyo umeiweka *brand* yako ndiyo itasaidia kukutangaza kwamba wewe una malengo ya kuelekea wapi. Huwezi kubeba *brand* ya jembe na nyundo halafu utake ikupeleke kwenye kilimo cha kutumia matrekta. Hebu mkae, mnaweza kulichukua hili kama jambo la kisiasa, lakini hii siyo siasa, ndiyo ukweli, kilimo ni biashara. Watu wanataka kulima, wanataka wabadilike kutoka kwenye jembe la mkono watumie kilimo cha kisasa, unawapelekaje kwa kuvaa jembe la mkono?

Anzeni kubadilisha *mindset* zenu ndiyo mtaweza kulisimamia jambo ambalo mnataka kulitekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yawezekana mmeamini kwamba kila mambo mnayoyasema huwa hayatekelezeni, lakini *I assure you,* Tanzania ya viwanda inawezekana. Mpaka leo bado unapita hapo Dumila unakuta nyanya zinaoza, ni kwa sababu wenyewe hamuamini kwenye jambo ambalo mnalisimamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa anzeni kwanza kubadilisha mitazamo yenu kama Serikali muamini kwamba tunataka tujenge Tanzania ya viwanda lakini kwa kutumia malighafi zinazolimwa shambani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana watu wanapiga kelele leo, amesema hapa Mheshimiwa Qambalo kuwa Mheshimiwa Waziri ambaye uko ndani ya Serikali huna tofauti na mimi Waziri Kivuli, wote tunaongea maneno matupu ambayo hayaendi kwenye utekelezaji. Kama huna bajeti, bajeti inashuka kila siku, utatekeleza vipi hiyo mipango yako? Wanatushinda Rwanda, wametenga bajeti ya shilingi trilioni saba kwa ajili ya kilimo, nchi ndogo kama ile, sisi tunatenga shilingi bilioni 170, hiyo si nauli tu ya Waziri kutembelea mikoani, itatusaidia kitu gani? Bado Waziri unataka kudanganya watu hapa kwamba eti *NFRA* itanunua mazao yote ambayo yamesalia huko mikoani, hii haiwezekani. *(Makofi/Kicheko)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Omary Mgumba, atafuatiwa na Mheshimiwa Jitu Soni, ajiandae kwa dakika tano, tano Mheshimiwa Aeshi na Mheshimiwa Bashe.

MHE. OMARY T. MGUMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nitoe mchango kwenye Wizara hii muhimu inayogusa zaidi ya asilimia 70 ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niipongeze Serikali hasa kwa zuio la kuuza mahindi nje ya nchi. Nimesoma kitabu hiki kwenye ukurasa wa 61, nafikiri kilio cha Wabunge wengi mwaka jana, tuliolalamika kwamba Serikali isiingilie mfumo wa soko la mahindi, naona Serikali imesikia na mkatekeleze hili kama mlivyopanga. Isije sasa wakulima wanaanza linaanza tena zuio jipya la vibali watu wasiuze. Liacheni soko liwe huru, watu tukauze mahindi mahali popote panapohitajika. Naipongeza sana Serikali kwa ajili ya hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba kuishauri Serikali hasa kwenye soko la mbaazi. Soko la mbaazi ni gumu sana, wengi wamezungumza, mimi bahati nzuri nilikuwa kwenye kampuni ya wanunuzi wakubwa wa mazao hayo duniani kwa miaka 19 lakini tulifanya miaka mitatu tu, miaka 16 yote hatukununua hata kilo moja na ni kampuni ya Wahindi wenyewe. Changamoto kubwa ni soko lina hatari kubwa sana kwa sababu mnunuzi mkubwa ni mmoja peke yake. Kwa hiyo, siku yoyote akibadilisha sera zake au siku yoyote uzalishaji kwake ukiwa mkubwa ni tatizo kwenye mbaazi kama tulichokiona mwaka jana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu, mnunuzi mkubwa ni Serikali ya India ni vizuri sana, kwa sababu biashara ni diplomasia, Wizara ya Mambo ya Nje, Wizara ya Kilimo na Wizara ya Viwanda na Biashara mkae pamoja ili hawa watu wa diplomasia, Waziri wa Mambo ya Nje akae na Serikali ya India, tupate makubaliano ya awali ya kuwauzia mbaazi zetu kama walivyofanya Ethiopia na nchi zingine. Hata kukiwa na uzalishaji mkubwa hawawezi kubadilisha lazima watakuwa wanazingatia makubaliano, zaidi ya hapo, tutakuwa na soko la kubabaisha kwa sababu wao ndiyo wakulima wakubwa, wanunuzi wakubwa na walaji wakubwa wa mbaazi duniani. Lazima tukae na Serikali ya India, tupate ombi maalum la kuturuhusu kwamba mbaazi zetu tuuze kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni kuhusu viwanda vya kubangua korosho. Naomba sana kuishaui Serikali, suala la

viwanda vya kubangua korosho lilianza tangu mwaka 1978, Mwalimu Nyerere alifungua viwanda 11 na vyote havikubangua korosho na vilikuwa na uwezo wa kubangua zaidi ya tani 100,000. Kama mkikumbuka wakati ule uzalishaji wetu ulikuwa tani 174,000. Viwanda hivi havikununua hata kilo moja kwa sababu ya mabadiliko ya teknolojia, lakini ni kutokana na changamoto nyingi zilizokuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1994 tukafufua makampuni mengi ambayo yalikuja hapa kuwekeza kwa ajili ya ubanguaji wa korosho. *Olam Tanzania Limited* ilikuwa na uwezo wa kubangua tani zaidi ya 30,000, wamebangua kwa miaka 10 lakini tulipoanza tu stakabadhi ghalani wakahamisha kiwanda chao kwenda Mozambique. Kiwanda cha *Mohamed Enterprises* kilikuwa na uwezo wa kubangua zaidi ya tani 2,000 kimefungwa, Kiwanda cha *Premier Cashew* au Fidahussein kilikuwa na uwezo wa kubangua zaidi ya tani 3,000 kimefungwa; Kiwanda cha *Masasi Cashewnut* kilikuwa na uwezo wa kubangua tani 1,000 kimefungwa; na Kiwanda cha Buko Masasi nacho kimefungwa, hii ni miaka ya 1990 mpaka 2012. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa hivi tuna viwanda vitatu *Export Trading Group (ETG)* ana uwezo wa kuzalisha zaidi ya tani 5,000 lakini habangui hizo tani 5,000 kwa sababu *raw material* hapati, anasafirisha nje kama *raw material. Sunshine Group* pale Lindi kina uwezo wa kuzalisha tani zaidi ya 2,000 lakini *raw material* kwenye mnada anapata tani 200 tu; Haute ana uwezo wa kubangua tani 2,000 mwaka jana kapata tani 800. Kwa hiyo, unaona kuna shida ya upatikanaji wa *raw material* kwa viwanda vya ndani. Ni sababu sera zetu wakati mwingine haziruhusu au hazi-*favour* hawa wabanguaji wa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema hivyo? Hivi viwanda vya ubanguaji vinahitaji hela nyingi sana. Mtu anakuja, anawekeza hela zake anajua kwamba atarudisha baada ya miaka mitano au kumi baada ya miaka miwili sera zimebadilika. Kwa mfano, hapa Tanzania haturuhusiwi kufanya *importation* ya korosho kutoka nchi zingine. Wakati

dunia nzima ubanguaji wa korosho au soko la korosho ni la mzunguko yaani mwaka huu inakuwa miezi mitatu Tanzania, miezi mitatu India, miezi mitatu Nigeria na miezi mitatu Brazil. Kwa hiyo, mtu ananunua miezi mitatu, anabangua baada ya hapo anaenda sehemu nyingine. Kwa hiyo, jambo hilo sera inazuia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kwenye sera zetu tuliweka *export levy* kwa sababu ya kuzuia korosho yetu isiende nje. Ombi, hii ya asilimia 15 inatosha sana, aidha, ibaki hapo au kuwahakikishia wabanguaji iende juu zaidi ili kuzuia hizi korosho zisiende kule. Kwa sababu akija mtu mwingine kesho akishusha hii *export levy* maana yake mbanguaji wa ndani huyu hawezi kupata *raw material,* korosho yote itaenda India, itaendelea kwenda Vietnam kwa sababu wana bei kubwa na wana gharama nafuu ya uzalishaji kuliko sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya ushauri huo, naomba sasa niuombee sasa Mkoa wa Morogoro. Serikali ya Awamu ya Tatu iliamua wakati ule Waziri Mkuu akiwa Ndugu Sumaye na Rais Benjamin Mkapa kwamba Mkoa wa Morogoro ndiyo uwe Makao Makuu ya Nane Nane Tanzania na maonesho yote yafanyike pale kwa sababu ya hali ya kijiografia na uwepo wa Chuo cha Kilimo *(SUA)* pale Morogoro. Baada ya kuondoka, sera hiyo ikabadilishwa, sasa hivi Maonesho ya Nane Nane yanazunguka kila mkoa na kila kanda matokeo yake tunaongeza gharama kwa wadau, kujenga jengo kila mahali, hata yale majengo sehemu nyingi yamebaki magofu. Ombi langu, ni vizuri tuchague sehemu moja tuweke ndiyo Maonesho ya Nane Nane kwa nchi nzima kama tunavyofanya Sabasaba. Yako Maonesho ya Kibiashara Dar es Salaam, kila mtu anajua Dar es Salaam na Maonesho ya Nane Nane yawepo pale Morogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumzia kuhusu suala la ushirika. Mheshimiwa Waziri, hizi taarifa za kusema Morogoro tuko tayari kwa ajili ya stakabadhi ghalani mnazitoa wapi? Mimi natoka Morogoro Vijijini, hata kikao cha *RCC* hatujawahi kukaa Wabunge wa Morogoro, kikao

cha kisheria hatujawahi! Jana unaniambia kwamba Morogoro Mkoa tumekubali stakabadhi ghalani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumwambia Mheshimiwa Waziri aachane na taarifa hizi za kwenye maandishi. Morogoro Vijijini au Morogoro kwa ujumla hatuna vyama vya msingi, hatuna maghala, hatuko tayari na msimu unaanza mwezi ujao (wiki mbili zinazokuja), katika hali kama hiyo tunaanzaje? Huna ghala, huna wataalam, huna vyama, hujavitengeneza, sasa kwa sababu maamuzi yanatoka Serikalini, tunaweza tukakubali kwa sababu Serikali ni chombo kikubwa lakini mngetusikiliza sisi wawakilishi wa wananchi tunaotoka kwa wannachi tunawashauri kwa nia njema, mfumo huu tuanze mwakani badala ya mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kuhusu hizi *data* kwenye ukurasa wa 65, Mheshimiwa Waziri...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa mchango wako. Mheshimiwa Jitu ungesubiri kulikuwa na ombi la Mheshimiwa Dkt. Mponda alikuwa anakwenda hospitali. Muache Mheshimiwa Dkt. Mponda amalizie, nilikuwa sijakuona ulihama kwenye Kiti chako, muache Mheshimiwa Dkt. Mponda halafu utaingia Mheshimiwa Jitu.

MHE. DKT. HADJI H. MPONDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi kutoa mchango wa sekta muhimu sana katika maisha yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kutoa mchango wangu, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia sisi sote na mimi mwenyewe binafsi angalau leo natoa mchango katika sekta hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi wamezungumzia umuhimu wa sekta hii, ni kwamba asilimia 75 ya Watanzania

tuko vijijini na wengi walioko vijijini shughuli kubwa kule ni kilimo. Ukiangalia uchambuzi wa Kamati ya Kilimo, imebainisha wazi kabisa kwamba kasi ya sekta ya kilimo inazidi kuanguka mwaka hadi mwaka. Tunaiomba Serikali na maelekezo ambayo wametoa Wabunge waliotangulia, hebu muangalie changamoto hasa na baadaye mzipatie ufumbuzi wa kudumu katika kuendeleza hii sekta ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana mkono na Kamati ya Kilimo ambayo wameitaka Serikali kutambua fursa zilizoko na hizo fursa ambazo zinatambuliwa ndiyo mkakati hasa ufanyike. Mimi nitatoa mfano Mkoa wa Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi tunafahamu Mkoa wa Morogoro ni mkoa ambao tayari kuna miradi ambayo inaendelezwa pale. Naomba Serikali itupe mrejesho, kuna Mradi wa *SAGCOT,* kuna Mradi wa *Feed the Future* ambao unafadhiliwa na Wamarekani na vilevile kuna mkakati wa Fanya Mkoa wa Morogoro kuwa Ghala la Chakula lakini sii tunaotoka Mkoa wa Morogoro hatuoni jitihada za dhati kabisa juu ya miradi hiyo. Ukienda pale Morogoro, ukiuliza mtu wa kawaida tu *SAGCOT* unaijua, hawaelewi hali kadhalika hata huo mradi ambao unafadhiliwa na Marekani. Picha ya hapa ni nini? Kama kweli fursa zilizopo katika Mkoa wa Morogoro Serikali inawekeza pale, tunaweza tukatoa matokeo makubwa sana katika suala hili hasa la vyakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijikite zaidi ili unielewe, mfano nitautolea Wilaya ya Malinyi. Wilaya ya Malinyi kama itawezeshwa kilimo cha umwagiliaji tayari pale kuna mito zaidi ya 30 inamiminika kuanzia masika na kiangazi, lakini wilaya yote ile kuna banio moja tu liko Itete.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeeleza mara nyingi na kuishauri Serikali, mnaonaje sasa mito mingine kwa mfano, Rasesa, Furua na Sofi, kama itatumika na kuweka *scheme* za umwagiliaji, nina uhakika tatizo la chakula litakuwa limetoweka kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wa maeneo yale, wengi tunalima kilimo cha zao la mpunga na mahindi. Katika msimu wa mwaka uliopita tumechelewa kuanza kilimo cha mahindi kwa sababu ya shambulio la panya. Nilichogundua kwamba hakuna mawasiliano kati ya Wizara na watendaji walioko kule wilayani hawa Maafisa Ugani, vilevile kati ya Wizara na wananchi. Wadudu/panya hawa kumbe dawa yake ipo na dawa zinafanyiwa utafiti mara kwa mara kwenye Chuo cha *SUA, SUA* ndiyo *center* ya panya katika nchi hii. *SUA* iko Mkoa wa Morogoro, ni karibu sana na Malinyi, sasa kwa nini ndani ya miaka miwili mfululizo Wilaya za Kilombero, Ulanga na Malinyi tumekuwa na tatizo la panya lakini majibu hakuna! Kama mwenendo huu utaendelea, wananchi hawa wataendelea kuteseka zaidi na zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mbegu; wananchi Mkoa wa Morogoro pamoja na *SUA* tuna Kituo cha Utafiti cha KATRIN Ifakara, pale wanatengeneza mbegu ya kisasa ya *SARO 5* lakini usambazaji wake wananchi mpaka leo hawaelewi. Kwa hiyo, hoja yangu hapa, namshauri Waziri, hebu uweke mikakati ya mawasiliano, mnafanya kazi nzuri pamoja na vyuo vyenu vya utafiti, lakini hakuna mrejesho kwa wananchi. Wananchi mpaka leo hawajui ni mbegu gani bora ya kutumia katika zao la mpunga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara kadhaa nimeiomba Serikali kwamba wakulima wa mpunga wanasumbuliwa na ugonjwa ambao wa virusi. Ugonjwa huu kule tunaita *kimyanga* kwa lugha ya nyumbani, lakini lugha ya kitaalam unaitwa *rice yellow mottle virus.* Ugonjwa huu sio mgeni sana kwa nchi za Afrika, unapatikana sana *West Africa.* Niwaombe mara nyingine, kwa nini msipeleke wataalam waende wajifunze kule *West Africa,* wenzetu wameutatuaje ugonjwa huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa mwisho niongelee suala la masoko, wengi wameeleza, kama hatuna uhakika wa masoko kwa wakulima wetu kwa kweli tunapoteza nguvu za wakulima hawa. Niombe hasa soko la mpunga, mwaka wa fedha uliopita Serikali walitenga

angalau fedha za kuanza kununua karibuni tani 100,000 kupitia *NFRA* lakini naona kwenye bajeti hii wamesahau kabisa. Kwa hiyo, mtakapoweka soko hili la kupitia *NFRA* tayari itakuwa mmewatengenezea mazingira ya kuwa na soko la uhakika la zao la mpunga wananchi wale wa Malinyi, Kilombero na Ulanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie la mwisho na niendelee kusisitiza tu, kama tunataka tutoke na kilimo chenye tija, twende na kilimo cha kibiashara ambapo sifa kubwa ya kilimo cha biashara inahitaji maji. Maji yapo, ni utaratibu namna gani tunaweza tukayatengenezea skimu tukayapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine tunataka miundombinu, kwa mfano kule Malinyi inafikia wakati bei ya mpunga inateremka na wananchi wanaumia kwa sababu miundombinu hali siyo nzuri sana. Mtu utoe gunia la mpunga pale upeleke kwenye soko Ifakara toka Malinyi ni kilometa 150 lakini gunia lile linagharimu shilingi 10,000 kwa gunia moja la kilo 100. Kwa hiyo, hii linampunguzia mapato huyu mkulima na matokeo yake hata soko sasa linapungua kwa sababu ya bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu wengine wamekuwa wanaeleza hawana imani na Waziri, mimi binafsi Mheshimiwa Tizeba namfahamu, uwezo wake ni mkubwa, naomba tumuunge mkono, tumtengenezee mazingira hata sisi Wabunge, huu ndiyo wakati wetu kutengeneza bajeti hii, kama ina upungufu, Kamati ya Bajeti ikae...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Jitu Soni halafu atajiandaa Mheshimiwa Bashe dakika tano, Mheshimiwa Aeshi na Mtemi Chenge.

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nichukue fursa hii kwanza kumshukuru Mwenyezi

Mungu kwa siku ya leo. Mimi naomba nitoe ushauri kwa Serikali, kuna maeneo mengi tu lakini naomba nianze kwa kusema Mheshimiwa Spika kama alivyounda Kamati mbalimbali za kuangalia kwa mfano *Tanzanite,* makinikia na masuala ya uvuvi wa baharini, angeunda Kamati ya kukaa pamoja Wabunge ili tuweze kuona maoni mbalimbali na tuweze kuishauri Serikali nini cha kufanya kwenye sekta hii ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili ningeomba Serikali kwa kupitia Waziri wa Kilimo waangalie *Hansard* za miaka ya nyuma ushauri mbalimbali ambao ulikuwa unatolewa miaka nenda rudi, je, upi umefanyiwa kazi? Kwa sababu haya mambo Wabunge tunayasema kila mwaka lakini kwa sehemu kubwa unakuta ushauri huo hautiliwi maanani. Haya mawili yakifanyika, nina uhakika kuna mengi tutakuja kufaidi huko mbele ya safari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwanza kwa kusikitika kwamba bajeti ya sekta hii ya kilimo kila mwaka huwa inaendelea kushuka lakini bajeti kuu inaendelea kupanda na lengo lilikuwa bajeti iongezeke. Wizara ya Kilimo inafanya kazi yake vizuri sana ikiongozwa na Waziri, Naibu Waziri na wataalam wao, lakini hakuna uratibu au *coordination* baina ya Wizara ya Kilimo na Wizara zingine zote na ndiyo maana tunakwama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu tuangalie tunataka kuelekea wapi. Moja, naomba tuwe na mkakati kwamba bidhaa zile kuu ambazo tunaagiza kutoka nje kwa mfano mchele, sukari, mafuta, mbegu hata hizi *juice* zote za matunda hakuna tone la *juice* ambayo tunakunywa inazalishwa hapa nchini, yote ni *concentrates* zinazotoka nje ya nchi wakati bidhaa zote hizi tunaweza kuzalisha hapa nchini.

Ni vizuri tuje na mkakati kwamba ndani ya hii miaka miatatu au minne mchele, sukari, mafuta, mbegu na vitu hivi tutazalisha ndani ya nchi, uwezo tunao na namna ya kufanikiwa hivyo ni kuwekeza kwenye utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuweki fedha kwenye utafiti na hata hii leo tukisema tunataka kujitosheleza kwa mafuta hatuna mbegu. Hatuna mbegu nzuri ambayo tunaweza kujitosheleza lakini hivyohivyo kwenye maeneo yote inatakiwa tuwekeze zaidi kwenye utafiti. Tuna vituo 17 vizuri na bajeti yake sijaona kwamba kila kituo kitapatiwa shilingi bilioni ngapi ili vituo hivyo viweze kuboreshwa kwa kuwekewa vifaa vya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na hiyo narudia kusema kwamba hakuna *coordination* ndani ya Serikali. Leo hii vituo vya utafiti vinaomba msaada kutoka nje, vifaa vikija vinatozwa kodi, vifaa vinasaidia Mikocheni, Makutupora hapa kwenye umwagiliaji, vifaa vya umwagiliaji ambavyo havina kodi lakini wametozwa zaidi ya shilingi milioni 42. Sasa kama Serikali kwa Serikali inatozwa kodi, je, mwananchi na mkulima wa kawaida itakuwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkulima kitu anachohitaji ni uwezeshaji na mazingira mzuri ya kufanya kazi. Moja, Benki ya Kilimo ingepewa mtaji wa kutosha ile itoe mikopo wakulima waweze kununua vifaa vya kisasa kufanyia kazi na Mfuko wa Pembejeo uwezeshwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na hilo tufanye utafiti, ndiyo maana nasema hiyo tume au Kamati ya Bunge ikikaa iangalie masuala haya. Leo hii kodi na tozo tulizoainishiwa hapa nyingi tumeshangilia, lakini ipi yenye athari hata moja ambayo imemsaidia mkulima moja kwa moja, hakuna. Ukiangalia ushuru wa mazao iko palepale, ni ile tu kwamba waliokuwa wanakusanya 3% tumeshusha kwenye maandishi tu kutoka 5% kuja 3%, lakini mkulima wa kawaida hakuna mahali amefaidika na hilo. Zile kodi kumi na zaidi hakuna mahali mkulima zimemnufaisha moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kuwekeza zaidi kwenye ushirika na kutoa elimu vizuri hatutafika popote. Tumeanzisha *commodity exchange* leo mwaka wa tano hakuna maendeleo yoyote yanayofanyika pale. Stakabadhi ghalani pamoja na *commodity exchange* inaweza kuwa mkombozi

wa mkulima. Kwa hiyo, kwenye suala hilo pia, tuweke nguvu zadi, elimu itolewe, lakini Serikali iwe na nia njema, iwe na mkakati wa kuhakikisha kwamba haya yote tunaweza kufikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Wabunge wengi wamechangia masuala ya mbolea. Kwenye mbolea kuna upotoshaji mkubwa unatokea kwa sababu hatuelewi. Ni vizuri tukajua kwamba sawa na binadamu huendi hospitali ukapewa tu dawa, ukimueleza unaumwa kichwa, basi daktari anakupa dawa; hivyohivyo kwenye udongo unatakiwa ukapimwe. Pima udongo kujua mbolea inayotakiwa wataalam watakwambia tumia mbolea A, B, C, ndiyo utumie mbolea hiyo badala ya hii ya kwa ujumla tu. Watu wanapiga kelele kwamba Minjingu haifai, nini haifai, mkakati wa Minjingu ni kuzalisha mbolea ifikapo mwaka 2021 kiwanda kile kinachojengwa kule...

T A A R I F A

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa, kwanza Mheshimiwa Keissy.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, mbolea ya Minjingu Kahama na Tabora waliweka nje baada ya kushindwa kuuzika, wakawaambia wananchi wachukue bure, hakuna mwananchi alichukua bure. *(Kicheko)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Frank.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimia Mwenyekiti, napenda kumpa taarifa Mheshimiwa Jitu Soni, aliyekuwa anazungumza kwamba mbolea ya Minjingu kwenye Nyanda za Juu Kusini ukianzia Iringa, Ruvuma, Rukwa, Mbeya, imeletwa na tuliitumia tulipata hasara kubwa sana.

Kwa hiyo, baadhi ya Wabunge wanaozungumzia mbolea ya Minjingu waishauri pia Serikali iweke *guarantee* kwa wananchi ambao wataitumia mbolea hii.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Jitu.

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Wangekuwa kwanza wanaelewa kinachosemwa badala ya kurukia tu. Nimesema fanya utafiti kwenye udongo wako, ukifanya utafiti upate ushauri. Je, nyanda hizo zilifanya utafiti wa udongo wao wakaambiwa watumie aina gani ya mbolea? Kama utafiti huo upo ulete mimi niko tayari hapa kukulipa fidia wewe. Mimi niko tayari kulipa fidia kama ana utafiti wa udongo uliofanywa, nina uhakika hamjafanya.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: *Order please, order.*

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye masuala yote lazima twende kwa utafiti na ndiyo maana nasema tuwekeze kwenye utafiti badala ya kila siku hapa kupiga tu kelele kwamba tufanye A, B, C. Twende kisayansi, kilimo ni sayansi, kilimo ni biashara, kilimo tukiwekeza vizuri ndiyo kitakomboa watu wote. Watanzania 100% wanategemea kilimo cha humu ndani kwa sababu tunategemea chakula kinachozalishwa humu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo lingine muhimu sana inabidi Serikali ijipange kuhusu hili suala la *regulatory bodies.* Uzalishaji wa ndani ya nchi gharama inakuwa kubwa na ndiyo maana bidhaa hizi zinatoka nje ya nchi kutokana na hizi tozo, ushuru, ada na leseni mbalimbali ambazo tunatozwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote tungekuwa tumeyafanya vizuri nina uhakika kwamba gharama za uzalishaji zitapungua na viwanda vingi huku ndani vitapata malighafi kutokana na sekta hii ya kilimo, mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye yale mazao ambayo Wabunge wengi wameyazungumzia, leo hii Dodoma inaweza kuzalisha zabibu, lakini bado tunaagiza zabibu kutoka nje ya nchi wakati mvinyo na zabibu zingeweza kuzalishwa kwa wingi tukapata fedha hapa ndani lakini pia tukawa tuna-*export.* Tukiangalia upande wa migomba, Serikali ilikuwa na mpango mzuri wa kuzalisha miche ya *tissue culture* ipelekwe Kanda ya Ziwa. Suala lile lingefanyiwa kazi ungekuta ugonjwa ule ungepungua sana na wananchi wa kule wangekuwa wamepata chakula cha uhakika na ndizi za uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nishukuru kwamba mpango wa kuanzisha *LAPCOT* mmeusema. Naendelea kushauri kwamba mpango huu uanzishwe mapema ili kanda ile pia ambayo inaweza kuzalisha mambo mengi sana katika hii sekta ya kilimo kwa ujumla wake na wenyewe waweze wapate mafanikio kama *SAGCOT* ...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa, muda wako umekwisha. Tunaendelea na Mheshimiwa Aeshi dakika tano, Mheshimiwa Bashe dakika tano na tutamalizia na Mheshimiwa Mtemi Chenge.

MHE. KHALFAN H. AESHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi angalau dakika tano hizi niweze kuchangia kwa haraka haraka tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nimeamka tofauti kabisa, mara nyingi sana nilikuwa nafikiri Mheshimiwa Tizeba ni tatizo. Naomba nikiri leo ndani ya Bunge kwamba Mheshimiwa Waziri wa Kilimo hana tatizo lolote. Tatizo ninaloliona hapa ni Waziri wetu wa Fedha ndiyo kikwazo kwa kila jambo tunaloliongelea hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukilalamika sana kuhusiana na Wizara ya Kilimo, lakini leo naomba niseme

kwamba kwa 18% iliyotengwa kwa ajili ya bajeti ya maendeleo kwenye kilimo tumefanya makosa makubwa. Namuomba Mheshimiwa Waziri na Bunge lituunge mkono kwamba bajeti hii ikapitiwe upya ili tuje tuijadili kwa sababu muda bado tunao, lakini kwa asilimia 18 kwenye suala la maendeleo naomba niseme kimsingi tumeshindwa kutekeleza yale ambayo tulikuwa tumekubaliana toka mwanzo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwa harakaharaka tu, nikupongeze Mheshimiwa Waziri kwa kutoa kikwazo cha vibali kusafirisha mahindi yetu kwenda nje. Nikuombe tusifanye tena makosa haya. Kosa hili limetugharimu sana hasa sisi wakulima wa mahindi na mpunga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema hivyo kwa sababu, maeneo tunayotoka sisi ndiyo zao letu kubwa kama zao la chakula lakini ndiyo zao la biashara. Mnapofunga mipaka hii matokeo yake mnatufanya sisi tunaathirika zaidi. Sisi Wabunge wa maeneo hayo tuna kila sababu ya kuwatetea wakulima wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Sumbawanga gunia moja la mahindi ni shilingi 15,000 mpaka shilingi 20,000. Hebu niambie huyu mkulima leo hii unamwambia akalime tena mahindi ataweza kweli kulima? Kwa bahati mbaya mnambana kila kona na mkulima huyu hatumsaidii chochote. Narudia, hatumsaidii chochote. Nikuombe, kosa tumeshalifanya tusirudie tena kufanya kosa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi vibali unavyovisema Mheshimiwa Waziri vitatoka mikoani unaenda kukaribisha rushwa kule, kwa nini msifute moja kwa moja? Uwezo wa kununua hatuna, uwezo wa kuwasaidia wakulima hatuna, waachieni wafanye wanavyotaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala la kusema mkulima ndiyo wajibu wake kuhakikisha mwananchi hafi na njaa, tunakosea. Kama hoja ni hiyo, basi hata sisi watumishi na Wabunge, ikitokea kuna suala la njaa tuwe tunakatwa na

sisi mishahara yetu ili tukafidie kule ambako kuna tatizo la njaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme wakulima wetu hawa wanaonewa sana, ifike wakati sasa tuagalie jinsi gani ya kuwasaidia tuwaache wawe huru, walime wenyewe, wavune wenyewe na vilevile wakatafute masoko wakauze kokote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaenda haraka haraka, leo tuna mawakala wamekuja kututembelea hapa, mawakala hawa huu mwaka wa nne hawajawahi kulipwa hata senti moja. Tunaamini mmefanya uhakiki, mnaangalia madeni, mmechunguza, lakini Waziri wa Fedha aje atujibu hapa nini dhamira ya dhati ya hawa ambao walitusaidia wakati wa dhiki? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa mfano, juzi kule kwetu kuna mfanyabiashara mmoja ambaye ni wakala alikuwa anaitwa Mohamed, kwa jina maarufu alikuwa anaitwa Mohamed Msomali, kauziwa nyumba yake kapata *pressure* amefariki. Basi kama mmehakiki madeni yale ambayo ni halali walipeni kwanza wapunguze machungu wakati mengine mnayafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Mheshimiwa Waziri nikuombe sana, najua tatizo haliko kwako, Waziri wa Fedha akija hapa aje atujibu, lile ambalo mmeona ninyi ndiyo halali yao wapeni mengine wataendelea kudai baadaye ili wakapunguze machungu waliyokuwanayo. Leo hii hapo walipo wana wiki moja wako hapa Bungeni, kulala kwa shida, kula kwa shida, matokeo yake wamekuwa ombaomba hapa ndani ya Bunge, nafikiri na leo wapo hapa. Hebu angalieni jinsi gani ya kuwasaidia, kuweni binadamu, Waziri wa Fedha liangalieni hili, walipeni hawa watu kwa sababu walitusaidia wakati wa shida, tena wakati wa uchaguzi wa mwaka 2015. Kama hawadai, semeni hawadai ili wakaanzishe kazi nyingine waridhike kwamba sasa hivi hatudai, wasamehe hayo madeni. Mheshimiwa Waziri, hili sio la kwako, naomba Waziri wa Fedha aje atujibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaongelea kuhusu mbolea. Kila Mbunge ana haki ya kuchangia lolote lile ndani ya Bunge hili. Kila Mbunge ana wajibu wa kuchangia na wengine wachangie, siyo tusipingane, tupingane kwa hoja, sisi siyo wataalam lakini wataalam wanatuambia mbolea ya Minjingu inafaa. Mimi naona kuna shida hapa, shida ni jina, *brand* ile, wangeongeza neno moja 's' pale Minjingus ikawa la kizungu hapa tusingepiga kelele. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninavyojua kwa sababu kuna *DAP,* wameshazoea *DAP* kwa sababu ni la kiingereza. Leo hii hata shati...

T A A R I F A

MHE. AIDA J. KHENAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa.

MHE. AIDA J. KHENAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, mbolea ya Minjingu siyo kwa sababu ya jina. Kwenye Jimbo la Sumbawanga Mjini kata nne kulikuwa mashamba darasa mbolea ya Minjingu imeshindwa kufanya kazi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa endelea.

MHE. KHALFAN H. AESHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naongelea kuhusu wataalam, sijui dada yangu kama ni mtaalam. Sasa hapa ndiyo kuna shida hapa, Mheshimiwa Waziri mje mtujibu wataalam wanasema nini, *research* yao inasema nini na kama inafaa watuambie inafaa na kama haifai tuambiwe haifai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nataka niseme ndani ya Bunge hili, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kuwa mzalendo kwa kutaka kufufua viwanda vya nchi yetu lakini kuongeza viwanda...

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Muda wake huyu ni mdogo sana na nafikiri unamaliza sasa hivi.

MHE. KHALFAN H. AESHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa nia njema ya kutaka kufufua na kuanzisha viwanda. Mimi niseme kiwanda hiki ni cha Tanzania, tunaomba Serikali iweze kuboresha ...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Bashe ajiandae Mheshimiwa Chenge.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi nataka niseme mambo machache sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka niwaombe Waheshimiwa Wabunge, bajeti hii tutumie Kanuni ya 69 tuirudishe ili Wizara ya Kilimo na Wizara ya Fedha zikakae kuweza kuja na bajeti ambayo inagusa maisha ya watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitumie takwimu hizi. Tumeandaa bajeti ya shilingi trilioni 32, shilingi trilioni 12 ni fedha za maendeleo. Sekta ya kilimo inachangia *almost 30%* ya *GDP* ya nchi yetu, *development budget* ya sekta ya kilimo ni shilingi bilioni 94 ambayo ni sawasawa na *almost 0.8* ya *total budget* ya maendeleo, kweli? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta inayochangia *almost* 30% ndiyo inatengewa chini ya asiliamia moja ya bajeti nzima ya maendeleo. Sekta ambayo inaajiri kati ya asilimia 60 mpaka 70 ya Watanzania ndiyo inatengewa chini ya asilimia moja ya bajeti ya maendeleo. Sekta ambayo ina-*supply* asilimia 70 ya viwanda vyetu inatengewa chini ya asilimia moja ya bajeti ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la kusikitisha sekta hii imeendelea kuonewa katika nchi hii kwa muda mrefu na siyo sahihi. Sisi Wabunge, hasa wa Chama cha Mapinduzi, tuna wajibu wa kumlinda mkulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shinyanga, Tabora, Kigoma, Mwanza, Simiyu, Katavi, Mara, Rukwa na Ruvuma, huku kuna mkulima na mfugaji.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa hamna taarifa sasa hivi, tuna *time* mbaya hii, kaa chini. *(Kicheko)*

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, mikoa hii ndiyo inayolima mahindi, pamba, ndiyo yenye ng'ombe na samaki, halafu ndiyo watu tunaowatesa, *it is unfair.* Nadhani ni vizuri sisi viongozi wa nchi hii tukatambua hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Uislam Mwenyezi Mungu amemuumba mwanadamu kuwa Khalifa, kuwa kiongozi wa viumbe vingine. Mwenyezi Mungu kampa mwanadamu utu na akili ili aweze kuwatendea wema wengine, leo nyavu zinachomwa, leo mifugo ya nchi hii wafugaji wamekuwa wakimbizi, leo wakulima wa nchi hii wanaonewa, tunam-*sacrifice* huyo bwana aliyekaa hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikupe mfano mdogo, ili mkulima aweze kulima mahindi heka moja anahitaji *input* zifuatazo; trekta kulima mara mbili anatumia shilingi 90,000; *harrow* atatumia shilingi 35,000; kupanda atatumia shilingi 30,000; kupalilia atatumia shilingi 60,000 *in total;* ili aweze kupanda mahindi anahitaji mfuko wa jumla ya kilo nane ambayo atatumia shilingi 45,000; bado ataweka mbolea ya kupanda na kukuzia, *in total* anatumia shilingi 550,000. Leo mahindi ni shilingi 150 kwa kilo. *Cost per unit* ya *production* yake ni shilingi 500, *are we realistic?* Turudisheni hii bajeti. *This is not healthy for our country. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Tizeba hana *problem* kaomba *60 billion shillings* kwa ajili ya *inputs* ya tumbaku. Tumbaku mwaka jana tumeteseka wananchi wa Mkoa wa Tabora. Leo tumeletewa pamba mtu anaitwa *galagaja, galagaja* kule usukumani ni *middle man,* huu ushirika ulioletwa kwenye pamba hauna mtaji. Ziara ya kwanza ya kiongozi wa ushirika, mmoja alienda Kishapu anauliza eti inakuwaje wafanyakzi wa *SHIRECU* hawalipwi mshahara, ninyi *SHIRECU* mna shamba? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri turudishe bajeti hii na mambo yafuatayo yafanyike. *NFRA* apewe fedha aliyoomba. Suala la pili, kusiweko na *condition* kusafirisha... *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Chenge.

MHE. ANDREW J. CHENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. Nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Naibu Waziri wake Mheshimiwa Dkt. Mwanjelwa na timu ya Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe unafahamu kama tuna Wizara ambayo ina idadi kubwa ya wasomi ni Wizara ya Kilimo. Waheshimiwa Wabunge huo ndiyo ukweli, hizi changamoto naziona na mmezisema vizuri sana, upande wa bajeti mmeisema vizuri sana, sasa sisi ni Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nadhani badala ya kwenda kwa anachopendekeza Mheshimiwa Bashe, tuangalie kanuni zetu. Kanuni ya 105 inatoa fursa zile siku za mwisho baada ya mjadala wa Wizara zote Serikali na Kamati ya Bajeti wafanye majadiliano eneo hili la kilimo liwe miongoni mwa maeneo ambayo tunadhani yaangaliwe. Nadhani tukienda hivyo, tutakuwa tunaenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, mmesema vizuri maana tunaiona *development budget* ya Wizara hii inaenda chini lakini hotuba ya Waziri ina maeneo mengi mazuri sana, sina muda wa kuyasema lakini eneo la umwagiliaji, nchi hii kwenye mabonde lakini tukienda kwa sera yetu na mikakati yetu angalau tuelekee katika kupata hekta milioni moja ambazo tumejiwekea, sasa hii imekuwa ni ngonjera tu. *There is a big disconect* kati ya Wizara ya Fedha, Wizara ya Umwagiliaji na Wizara ya Kilimo katika mikakati yetu lakini tukienda kwa pamoja tutafanya vizuri. Kuna maeneo mengi ya nchi hii ambayo ni kukinga maji tu ya mvua haya Mwenyezi Mungu anatupa, kuyakinga na kuyatumia kwa shughuli za umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda niongelee kuhusu pamba. Mimi nimekulia kwenye zao hili la pamba na *Victoria Federation* ilikuwa inafahamika, Afrika nzima walikuwa wanakuja kujifunza Tanzania. Sitaki kurudi kwenye historia, tulivuruga sisi wenyewe lakini nasema hivi mimi kama kiongozi wa Bariadi sitakubali utaratibu unaopendekezwa na Serikali wa kulazimisha ushirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamba kwetu ni siasa kali, pamba ni uchumi, pamba ni hali yetu ya maisha. Ushirika ni kitu kizuri sana ndiyo nimeanza nalo, tulikuwanao, tulipambana na Wahindi na Waganda ndiyo tukaanzisha shughuli zetu, lakini haikuwa suala tu la kulima na kuuza pamba, uchambuzi wa pamba, zile *ginneries* zote zilikuwa za wakulima. Sasa huwezi ukanidanganya mimi pamba nikuletee eti kutoka kwenye *AMCOS* halafu iende kwa mtu *private,* ulishasikia ni ushirika huo? Hapana hiyo... *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Chenge.

MHE. ANDREW J. CHENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja lakini siyo kwa hoja hiyo. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, muda wetu wa mchana umekwisha. Nina tangazo, Mheshimiwa Shally Joseph Raymond, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Mtakatifu Thomas Moore, Bunge, anawatangazia kuwa leo tarehe 16 Mei, 2018 kutakuwa na Ibada ya misa kwa Wakristo Wakatoliki mara baada ya kuahirisha Bunge saa 7.00 mchana katika Ukumbi wa Pius Msekwa, ghorofa ya pili. Aidha, Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa.

Waheshimiwa Wabunge, wachangiaji wetu wa leo jioni tunaanza na Mheshimiwa Susan Kiwanga, Mheshimiwa Gimbi Masaba, Mheshimiwa Kunti Majala, Mheshimiwa Boniventura Kiswaga na Mheshimiwa Margaret Sitta.

Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00.

(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)

MWENYEKITI: Tukae. Katibu.

NDG. RUTH MAKUNGU - KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwakawa Fedha 2018/2018 – Wizara ya Kilimo

(Majadiliano yanaendelea)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, mchana nilitaja majina ya wachangiaji wetu wa jioni, nianze na Mheshimiwa Susan Kiwanga, Mheshimiwa Gimbi Masaba na Mheshimiwa Kunti Majala.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niseme tu ahsante sana kwa kunipa hii nafasi adimu ili na mimi nichangie kwa dakika tano katika Wizara hii ya

Kilimo ukizingatia mimi ni mtoto wa mkulima na hapa nilipo nimekulia kwenye kilimo na maisha yangu yote yapo kwenye kilimo. Uzuri zaidi katika Wilaya yangu ya Kilombero, Jimbo ambalo naliongoza mimi la Mlimba karibu asilimia 99 sisi ni wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana kuna haja ya kusema kwamba kilimo hiki ambacho sisi tunahangaika kwa majembe ya mkono, wengine *power tiller,* kwenye matope, barabara hamna, mbegu, panya tunapambana nao viwavijeshi na Maafisa wa Ugani hakuna yaani tunahangaika tu kama kuku wa kienyeji. Serikali imeshindwa kabisa angalau kuonyesha kumkomboa huyu mkulima siyo kwa maneno tu kwa vitendo kwa kutoa ajira nyingi kwa Maafisa Ugani hasa kwenye maeneo ambayo tunalima. Unaposema tu kilimo ndiyo uti wa mgongo karibu asilimia 80 ya Watanzania ni wakulima lakini asilimia 100 ya Watanzania tunatumia mazao ya kilimo halafu kilimo chenyewe kinakuwa *alfu lela ulela* kwa kweli inasikitisha sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema inasikitisha? Pamoja na kilimo hiki kuachwa kinahangaika chenyewe lakini katika pato la Taifa kinachangia asilimia 31 lakini leo katika bajeti ya kilimo haki ya Mungu inatia huruma, hivi kwa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi katika kipindi hiki cha kupanda nilihangaika sana kwenye Wizara ya Kilimo, kwa Waziri kwa Naibu Waziri, panya walivyovamia kwenye mazao, watu wamepanda mara ya kwanza panya wamekula, mara ya pili wamekula, mbegu wanahangaika lakini kwenda Wizarani hawana bajeti. Nilitegemea kwenye bajeti hii kuwepo na bajeti kabisa ya dharura kwa sababu wadudu wengine waharibifu wanatokea bila taarifa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunaomba bajeti ya dharura au maalum kwa ajili ya majanga kama haya katika suala la kilimo, hapo ndio mtakuwa mmeenzi kilimo kuliko kuacha watu wanahangaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kibaya zaidi sisi kule tunalima mpunga, kokoa, ufuta, mbaazi kule kila kitu kinakubali hata binadamu ukimpanda kule anaota Mlimba, Wilaya ya Kilombero. Cha kushangaza pamoja na mambo yote haya kwamba tunalima wenyewe mpunga mwaka jana soko likawa kubwa kweli kweli, Tanzania nzima wakaja Ifakara. Bei ya mchele na mpunga ikapanda kwa sababu pumba ni mali chakula cha mifugo, pumba tunachomea matofali yaani hakuna kitu kinachotupwa katika mpunga, lakini ikafikia mahali bei ilivyopanda tukaambiwa soko limefungwa hakuna tena kupeleka mazao nje, ninyi vipi kwani mlitugea ninyi mitaji? Kwa nini mnatuonea wenzenu? Barabara mbovu, tunahangaika tunalima wenyewe halafu mnafunga masoko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli naomba mipango hii ya Serikali ya kufunga masoko ya nje au kufunga mipaka naomba msitufanyie tu sisi wakulima. Mtuone kwamba na sisi tunastahili kuuza mazao yetu nje, siyo lazima tuuze hapa hapa Tanzania. Kwa sababu sisi Wilaya ya Kilombero hitaji letu sisi ni tani 130, tunazalisha tani 530 ziada ni tani 400 sasa mnataka tuzipeleke wapi? Kwa hiyo, ni vema sasa mkatuona kwamba na sisi tunastahili kupata maisha, kusomesha watoto, kujenga nyumba bora, kuchangia shule, elimu, hospitali tunajenga wenyewe majengo. Kwa hiyo, tunategemea tukilima, tukipata pesa ndiyo tunaenda kuchangia hizo huduma za jamii. Sasa mnavyotuacha hivi tunahangaika wenyewe huduma za jamii tutachangiaje na Serikali imesema wazi wananchi watajenga maboma Serikali ndiyo itakuja kumalizia. Sasa tunajengaje maboma kama hatuna kipato? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ushirika, hili nalo ni janga la Taifa kwa sababu hawa viongozi waliopo katika ushirika ndiyo walioua ushirika, leo zinaundwa timu kwenda kuhangaika na madeni halafu wanashirikisha viongozi hao hao. Mimi nataka nijue Serikali imechukua hatua gani kabla hatujaenda kwenye ushirika kwa wale viongozi walioua ushirika ambao wapo. Siyo mnakimbilia tu kuunda ushirika wakati wale walioharibu ushirika hamuwachukulii hatua.

Hiyo itakuwa ngumu sana mtu kujiunga katika ushirika na mtagombana na mtawafunga wengi kama mnapitisha maagizo ya namna hiyo huko chini, hayatatekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachokiomba bajeti ya kilimo iongezeke na ishuke chini watu waajiriwe, tupate wataalam watusaidie katika masuala ya kilimo na masoko yawe wazi mkulima awe na uwezo wa kuuza mahali popote. Kama mnataka kudhibiti masoko basi muwe na kilimo maalum, Serikali itoe hela kwa wakulima mseme mazao haya tumetoa pesa na mbolea bure kwa wakulima kwa hiyo hayo lazima tuyauze ndani lakini aliyehangaika mwenyewe, muacheni akauze mahali popote, tutakuwa tumemstawisha huyo mkulima. *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Gimbi Masaba ajiandae Mheshimiwa Kunti Majala.

MHE. GIMBI D. MASABA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa fursa ya kuchangia Wizara hii ya Kilimo. Wizara hii ni muhimu sana hususani kwa sisi Wabunge ambao tunatoka kwa waathirika wakubwa wa kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siko mbali na wale waliozungumzia bei ya pamba. Kama umesikiliza Wabunge wengi wanazungumzia bei ya pamba, mwaka jana tuliuzia shilingi 1,200 na mwaka huu ni shilingi 1,100. Ikumbukwe kwamba wakati tunauza pamba shilingi 1,200 bei ya nondo ilikuwa ni shilingi 9,000 leo tunauza pamba shilingi 1,100 bei ya nondo ni shilingi 22,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kuonesha namna ambavyo mkulima huyu anaendelea kudidimizwa kana kwamba analima kwa ajili ya chakula cha dagaa. Sisi tulitamani kwamba wakulima wanaolima zao la pamba lengo lao ni kubadilisha maisha ikiwa ni pamoja na kujenga

nyumba nzuri. Cha kushangaza Serikali ndiyo imekuwa muumini mkubwa wa kuhakikisha kwamba wakulima hawasongi mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niungane pia na Wabunge waliosema kwamba suala la ushirika halina tija yoyote kwa wakulima. Serikali imetangaza kufufua ushirika lakini haina mtaji wowote wa kuendesha ushirika. Wakati Waziri Mkuu amekwenda Mwanza alikutana na wafanyabiashara, masikitiko yangu ni kwamba nilitarajia badala ya kukutana na wafanyabiashara angekutana na wakulima wenyewe ambao ndiyo wahanga wakubwa wa tatizo hili la kilimo cha pamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetangaza ushirika, mnaagiza kwamba yale mashirika yanayonunua pamba eti ndiyo yapeleke fedha kwenye huo ushirika halafu ndiyo yanunulie pamba za makampuni yale yanayonunua pamba, hili ni jambo ambalo halikubaliki. Wakati tunazungumzia historia ya kuua ushirika maana yake ni kwamba walioua ushirika hawajachukuliwa hatua yoyote ile, lakini leo mnataka tena kuchukua fedha za wafanyabiashara wa haya makampuni wanaonunua pamba maana yake ni kwamba muwaangamize hawa wafanyabiashara kwa lengo la kuua mitaji yao, hii haikubaliki hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Bunge lililopita tulipitisha hapa kwamba msimu wa pamba uanze tarehe 1 na ndivyo ilivyokuwa, lakini mpaka hivi ninavyozungumza hakuna pamba yoyote iliyoanza kununuliwa. Hainunuliwi kwa sababu ya hili suala la ushirika la kutaka kupeleka fedha kwenye ushirika ili waweze kununua hizo pamba sasa wafanyabiashara wamegoma kupeleka fedha zao. Nachotaka kusema sasa, Serikali kama inataka suala la ushirika liendelee pelekeni fedha zenu ili muendelee kununua kwa njia ya ushirika na siyo fedha za makampuni yaliyoko kule Mkoani Simiyu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe masikitiko yangu, kuna watu wamechangia hapa kuhusu zao la mihogo na kuna

taarifa kwamba Serikali hii imeingia mkataba na Wachina kwa ajili ya kupeleka mihogo lakini utashangaa hakuna sehemu kwenye hiki kitabu cha Waziri pameandikwa kitu kinaitwa muhogo. Ukitoka hapo nje kuna watu wamekuja kwa ajili ya kutetea kilimo cha muhogo. Hii ni aibu ndugu zangu kwamba watu wametoka mbali kwa ajili ya kuja kutetea zao lao la mihogo, halafu halimo hata kwenye kitabu hiki, ni mambo ya kusikitisha sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe kwamba kama Serikali inataka suala la ushirika liendelee pelekeni fedha zenu kuliko kutumia fedha za wakulima na kitendo cha kuwagombanisha makampuni ya pamba na wakulima kwamba wasionane nao na badala yake wakauze kwenye ushirika hilo halikubaliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Kunti na wajiandae Mheshimiwa Kiswaga na Mheshimiwa Margaret Sitta.

MHE. KUNTI Y. MAJALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa nafasi. Mimi naamini kuwa kila mtu anapofanya kazi anatakiwa anapopata ujira wake autumie bila ya mtu yeyote kumuingilia katika kipato chake. Wafanyakazi wa nchi hii wanafanya kazi na wanalipwa mshahara hakuna Serikali yoyote ya nchi hii inayokwenda kumpangia matumizi mfanyakazi yule ya mshahara wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini wakulima wanalima kwa shida, kwa taabu wanapovuna mazao yao mnataka kuwapangia namna ya kuyatumia mazao yao? Nimwombe Mheshimiwa Waziri akija hapa, pamoja na kwamba zigo hili tunamtwisha lakini yeye ndiye mwenye dhamana na Wizara hii, aje atuambie hivi ni kwa nini wakulima hawa ambao hamuwapi mbegu, wananunua mbegu kwa shida ambazo bei zake ni aghali, pembejeo mnachelewesha na wengine kwa mfano huku Dodoma sisi pembejeo za Serikali hatuzijui kabisa, hamuwasaidii kitu

chochote kile lakini mnataka kuwapangia namna ya kutumia mazao yao pale wanapokuwa wamevuna? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala zima la mbegu za mahindi; kilo mbili ya mbegu ya mahindi inauzwa shilingi 14,000. Mwananchi huyu anapanda mbegu ile ya kilo mbili kwa shilingi 14,000, leo ndani ya Mkoa wa Dodoma, Wilayani kwangu Chemba wakulima wale wanauza debe la mahindi shilingi 2,500. Mbegu kanunua kilo mbili Sh.14,000 lakini debe la mahindi anauza shilingi 2,500. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wakulima tunachowataka ni nini? Yaani hii shilingi 2,500 anayouza hata nusu kilo ya dagaa hana uwezo wa kununua ili aweze kula. Mtu huyu anatakiwa kuuza madebe mawili apate shilingi 5,000 aende akanunue kilo moja ya sukari aweze kunywa chai ama uji na familia yake. Hiki kitu hakikubaliki na Mheshimiwa Waziri ukija mimi nitaomba unisaidie tu, umejipangaje na Wizara yako kuhusiana na upatikanaji wa mbegu ambazo zitapatikana kwa urahisi na kwa gharama ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la pili kuhusiana na migogoro ya ardhi. Tumeona migogoro mingi ya ardhi inayotatuliwa leo ni upande wa maliasili tu. Wakulima hawa pamoja na shida kubwa wanayoipata ya kulima chakula na sisi Wabunge tunakula chakula cha wakulima hao lakini mahali pa kulima nako pia imekuwa ni changamoto. Migogoro ya wakulima watu hao wanakufa kifo huku wakiwa wanajiona wao wenyewe wanakufa na kitanzi chao. Hawana watu wa kuwapigia kelele kwenye migogoro na wakisema wanaonekana ni wakorofi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka Mheshimiwa Waziri akija aniambie suala la migogoro ya ardhi ya wakulima nini mkakati wake kwenye bajeti hii ya fedha ya 2018/2019 ili wananchi wetu wakulima hawa ambao wanafanya kazi kubwa ya kutafuta chakula kwa ajili ya Taifa letu tuweze kuona namna gani migogoro hiyo inakwenda kutatulika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri akija naomba wakulima wangu wa Wilaya ya Chemba, eneo la Sekii pamoja na Champanda nataka aje aniambie mgogoro huu baina ya *WMA* ya Makame (Kiteto) na wananchi hawa kwenye vijiji hivi hatma yao ni nini? Wananchi hawa wameendelea kunyanyasika, mashamba yale ni ya kwao, *Makame WMA* wameenda kurudisha mpaka nyuma, matokeo yake watu wetu wanaenda kufyekewa mazao, si sawa sana. Mheshimiwa Waziri akija naomba anisaidie huu mgogoro unakwenda kuishaje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee suala zima la madeni ya mbolea, wameongea Wabunge wengi. Siku za nyuma huko mwaka 2014 na kurudi nyuma, watu hawa pamoja na kuwa walikuwa wanafuja hizo nyaraka na kadhalika lakini walikuwa wanalipwa. Leo ni mwaka wa nne watu hawa hawajalipwa mnadai kwamba mnafanya uhakiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2016 mlituambia mnahakiki, mwaka 2017 mnahakiki, leo mnafanya nini? Mtaendelea kuhakiki mpaka lini? Hivi kwa Serikali na vyombo vyake vyote mlivyonavyo mmeshindwa kubaini nani anastahili kulipwa na nani hastahili kulipwa? Mheshimiwa Waziri akija tunaomba... *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Kiswaga, ajiandae Mheshimiwa Margaret Sitta.

MHE. KISWAGA B. DESTERY: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na kesi ya miti, miti inalalamika inakatwa, tunamalizwa, tunamalizwa, mwisho wake ikakaa kikao ikabaini kwamba nani anatumaliza ni shoka. Baadae wakasema shoka hili nani analileta ni mpini. Mpini si ni sisi humu tuliomo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna tatizo Wabunge wanalalamika, wananchi wanalalamika pamba kuuzwa kwenye ushirika. Kwa hiyo, wananchi wamegundua wanaopeleka hili jambo kwenye ushirika ni akina nani, ni viongozi tuliowatuma kwa maana ya sisi Wabunge pamoja na Serikali. Maana yake ni nini? Badala ya kufika mahali tukaona kwamba tunapaswa kuwatetea wananchi lakini hatuwatetei. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ushirika Wabunge wamelalamika wasikilizeni, viongozi wa ushirika waliochaguliwa si wale tuliokuwa tunawatarajia. Wahasibu waliochaguliwa ni wale waliotumia rushwa kupita. Maana yake ni nini? Maana yake wanakwenda kuwaibia wakulima pamoja na wanunuzi wa pamba, hili jambo halikubaliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikataba iliyoko kule ni ya kukopa wakulima kwamba washirika wakusanye pamba halafu ipelekwe kiwandani, baada ya kupimwa kiwandani ndipo mkulima alipwe, siku ngapi hizo? Kwa nini tuliweka soko huria? Tuliweka soko huria kwa sababu wananchi wetu waliteseka, hili jambo haliwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri tukaliangalia upya, wananchi wanalalamika sana na sisi ndiyo viongozi na sisi ndiyo watu wa kuwasemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niishauri sana Serikali kwamba tumechelewa kwa sababu washirika waliokwenda kuchaguliwa wamechaguliwa na bodi ya watu wachache, watu saba/kumi wale washirika wangeweza kuchaguliwa na mkutano wa hadhara tungepata watu wanaostahili. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hili jambo tungelifanya mwakani halafu sasa tukaruhusu mfumo wa soko huria ukafanya kazi. Mtawapa shida ma-*DC*, mtawapa shida Wakuu wa Mikoa, hakuna kazi watakayokuwa wanaifanya bali kulinda tu wezi wa ushirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu katika mkokotoo wa soko ni kweli bei iko hivyo, lakini makato yameongezwa. Tunapokwenda kuulipa ushirika shilingi 45 halafu shilingi 33 inabaki kwenye *AMCOS*, shilingi 12 inakwenda ushirika *(union),* hivi tunawasaidia wakulima? Kwa nini hata hiyo shilingi 12 tusiiache kwenye kijiji? Kama kijiji kimeuza kilo 800,000 sawa na shilingi 9,600,000 hizo zitanunua madawati, zitajenga zahanati ili watu waone *impact* kweli hata ya kurudisha ushirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashauri, jambo hili tunalipeleka kwa kweli wananchi hawako tayari, wananchi hawa hatujawashirikisha, jambo hili limetoka juu halijashirikisha wananchi. Naomba tushauri tubaki na soko huria kama ilivyokuwa mwaka jana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumzia uwezo wa ushirika, kama kituo kitanunua kilo 40,000 kwa siku tunazungumza shilingi ngapi? Tunazungumza shilingi 44,000,000 kwenye kituo kimoja; je, fedha hizo zina ulinzi na ni vituo vingapi, tuna polisi wangapi wa kulinda fedha hizo? Tunapeleka maafa kwa wakulima na benki, hili jambo linapaswa litazamwe upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tuliingia kwenye soko huria? Tuliingia kwenye soko huria baada ya Vyama vya Ushirika kushindwa. Hivi vyama kama nilivyotangulia kusema mwanzo vimejigeuza kuwa vyama ambavyo hata Waziri Mkuu hukuhitaji hivyo, Waziri Mkuu ulihitaji *AMCOS* ziundwe kutokana na wakulima wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa washirika tunaokueleza Mheshimiwa Waziri Mkuu wengine, hawana hata shamba wala pamba, sasa mtu anakwenda kumnunulia mwingine ambaye hata zao hilo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo msipoangalia Mheshimiwa Waziri na Serikali, wapo viongozi/watendaji wanashauri vibaya, wanataka ku-*sabotage* Serikali na hili litakuja litugharimu sisi kama wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia kwenye mkokotoo; kwenye mkokotoo ni sahihi lakini ile shilingi 100 ingepungua. Mwaka jana tulikuwa na shilingi 30 ya kuendeleza zao la pamba, inakuwaje tunaweka mara nne/tuna-*double* mara nne kwa nini tusiende kwenye shilingi 60? Hii shilingi 60 tumeijaribu tukaona haiwezi kulipa madeni? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana Serikali iliangalie hili, ione ili angalau tukokotoe vizuri tumuongeze mkulima ili angalu mkulima mwaka kesho aweze kulima vizuri kama ambavyo wameitikia mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanalalamika mahindi hapa, mahindi haya bila kuweka utaratibu mwaka huu yataoza. Ni vizuri Serikali ikafungua mipaka ikaachana na suala la vibali ili watu waweze kusafirisha nje ya nchi waweze kuuza haya mahindi na mahindi haya yakiuzwa ndio uchumi wenyewe unaozunguka... *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango mzuri sana, Mheshimiwa Margaret Sitta.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nichangie hoja iliyopo mezani. Nichukue nafasi hii pia kuwashukuru wapiga kura wa Urambo na wakati huo nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Kilimo hii ni ngumu, kwa kweli nichukue nafasi hii kuwapa pole Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Makatibu Wakuu wawili pamoja na watendaji wote kwa kazi ngumu wanayoifaya, lakini wasikate tamaa, waendelee kufuatilia ili hatimaye wafanye kazi nzuri kwa manufaa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kipekee kwa kazi nzuri

aliyoifanya Mkoani Tabora alipokwenda kushughulikia changamoto za tumbaku, ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mambo aliyafanya Mheshimiwa Waziri Mkuu pia ni kuteua Bodi mpya ya Tumbaku ambayo imeanza vizuri, nawatakia kila la kheri na hasa kwa vile wameongeza ndani yake wajumbe wenye uwezo na uzoefu wa zao hili la tumbaku, nawatakia kila la kheri. Pia nichukue nafasi hii kuiomba Serikali ikamilishe uteuzi wa Mwenyekiti ili bodi iweze kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nachukua nafasi hii kumuuliza Mheshimiwa Waziri na Wizara nzima kwa ujumla, hivi kweli ina kalenda ya kilimo kwa mikoa yote ya Tanzania? Kama ina kalenda ya lini mvua zinaanza mkoa gani, wakati gani pembejeo zinatakiwa; iweje wakulima waanze kulima baadae washtukie hawana mbolea, inakuwaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kitu ambacho kinawasaidia wakulima wapate mazao mazuri ni kuwa na pembejeo hususan mbolea kwa wakati, lakini inasikitisha pale ambapo wakulima wamelima lakini hakuna mbolea unaambiwa zitakuja wiki ijayo na mazao yanaharibika pale ambapo hayapati pembejeo kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha atuambie hivi kweli wanafanya kazi kwa kufuatana na kalenda ya misimu mbalimbali ya mvua katika mikoa kwa sababu mikoa inatofautiana ili tuache usumbufu wa wakulima kulima bila kuwa na matumaini ya kuwa na pembejeo yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kukumbusha Wizara kwamba katika mazao ambayo yamekuwa na matatizo hapa Tanzania moja wapo ni tumbaku; wakisahau kwamba tumbaku inaiingizia nchi hii fedha za kigeni zaidi ya asilimia 40. Sasa kama zao linaingiza zaidi ya asilimia 40 ya fedha za kigeni, iweje lisipewe

kipaumbele ili nchi yetu iendelee kupata fedha za kigeni? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kwa sababu ukiangalia sana changamoto hizi si kwamba tunazizungumzia leo kwa mara ya kwanza, tumezungumzia kila wakata hasa hata mimi mwenye kama Mbunge wa Jimbo la Urambo nimekuwa nikilizungumzia suala la tumbaku na pembejeo kila ninapopata nafasi ya kuongea humu Bungeni. Sasa iweje zile changamoto bado ziendelee pamoja na jitihada kubwa ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na Serikali kwa ujumla?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano tumbaku tofauti na mazao mengine, tumbaku inatakiwa mbolea iwe imefika kabla ya mwezi wa saba. Je, Serikali inatuhakikishia kwamba mbolea inayotumika na tumbaku hasa *NPK* itakuwa imefika nchini hapa na kupatikana kwa wingi kabla ya mwezi wa saba? Kwa sababu ndipo ambapo wanaanza kuandaa mabedi *(seed beds)* kwa ajili ya kupanda mbegu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi ningeomba hili suala Mheshimiwa Waziri husika alizungumzie pia anapo-*wind-up,* kweli wakulima wa tumbaku wanahakikishiwa kwamba kuna mbolea ya *NPK* tayari nchini mwezi wa saba karibu unafika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumekuwa na tatizo kubwa sana la pembejeo hasa *NPK* ambayo inategemewa sana na wakulima wa tumbaku. Kwa sasa hivi bei ya tumbaku inatofautiana kwa sababu ya utaratibu wa uingizaji wa mbolea nchini. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kutuhakikishia kwamba kama wamefanya utaratibu wa *bulk procurement* kwa ajili ya mbolea za mahindi, hawawezi kufanya utaratibu huo huo pia kwa ajili ya zao la tumbaku ili wakulima wapate tumbaku nyingi kwa wakati mmoja lakini pia iondoe tofauti ya mbolea inayojitokeza kutokana na manunuzi ya mbolea kutoka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala ambalo tumekuwa tukiliongelea sana Mheshimiwa Waziri anajua, msimu uliopita

sasa hivi wa zao la tumbaku tumepata shida sana wakulima wa tumbaku kutokana na tumbaku nyingi kushindwa kuuzwa, na hii imetokana na uhaba wa masoko. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kutuhakikishia sisi wakulima wa tumbaku kwamba ameweka utaratibu mpaka sasa wa kupata wanunuzi wangapi ili waingie nchini wasaidie kuinua bei ya tumbaku? Kwa sababu panapokuwa na wanunuzi wengi kunakuwa na ushindani.

Je, Mheshimiwa Waziri utakuja utuambie hatua ambazo tayari Serikali imeshachukua, hata kwa kutumia Waheshimiwa Mabalozi waliopo nchi za mbali ili kupata wanunuzi ili kuwe na ushindani katika kuuza tumbaku yetu nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la masoko ni la muhimu sana ukiangalia adhabu waliyopata wakulima wa tumbaku mwaka huu. Kwa vyovyote mkulima anapolima kitu cha kwanza anachoangalia ni soko, sasa anapokuwa na uhakika wa soko ndipo analima vizuri ili aweze kujiendeleza yeye mwenyewe kibinafsi lakini pia kusaidia nchi yetu kuingiza fedha za kigeni kutoka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala muhimu sana la Bodi ya Tumbaku, kweli Bodi ya Tumbaku ipo lakini nasikitika kusema kwamba bado haijawezeshwa kufanya kazi vizuri, maana yake ni kwamba kupata fedha za kutosha... *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango mzuri wa tumbaku. Sasa namwita Mheshimiwa Monko, ajiandae Mheshimiwa Fatma Toufiq.

MHE. JUSTIN J. MONKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana...

MWENYEKITI: Dakika tano.

MHE. JUSTIN J. MONKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia katika wizara hii muhimu kabisa ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri anaonesha kabisa kwamba asilimia 65.5 ya wananchi wa Tanzania wanashughulika na kilimo. Ukiangalia katika bajeti ambayo inaombwa na Wizara hii ni ndogo sana ukilinganisha na idadi ya Watanzania hawa. Watanzania hawa ndio ambao tumewaita katika hotuba hii kwamba ni maskini sana. Watanzania hawa ndio ambao wamekuwa wakihangaika kwa muda mrefu na kwa wakati wote huu tumekuwa tukiwatengea fedha kidogo kama ambavyo imeoneshwa katika takwimu. Nisingependa kurejea katika takwimu zilizopo kwa sababu ya muda ambao nimeupata katika kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wetu wa Singida na hususan Jimbo la Singida Kaskazini sisi ni wakulima wa vitunguu na alizeti. Katika taarifa ya Kamati mtaona kwamba nchi yetu inatumia fedha zaidi ya shilingi bilioni 413 kila mwaka katika kuagiza mafuta, lakini hatujaweka mkazo katika zao la alizeti ambalo linalimwa na wananchi wa Mkoa wa Singida na maeneo mengine. Ni kwa nini Serikali imeendelea kutoa fedha za kuagiza mafuta ghafi kwa asilimia 70 badala ya kuwekeza katika kilimo cha alizeti ili wananchi waweze kupata ajira? Kilimo ndicho kinachoajiri idadi kubwa ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais amepita katika maeneo mengi akisema yeye ni Rais wa wanyonge, wanyonge wa Tanzania hii wapo katika sekta ya kilimo huko vijijini. Ukienda katika majimbo yale ya vijijini zaidi ya asilimia 90 ya wananchi hawa wanategemea kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunahitaji kuwekeza sana katika kilimo ili kuweza kuwakomboa wananchi hawa ambao wamekuwa wanashinda kwa muda mrefu na kwa kweli hawapati fedha za kuweza kuendesha

maisha yao, wameendelea kuwa maskini kwa muda mrefu kwa miaka mingi tangu tumepata uhuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme ukuaji wa sekta ya kilimo ni mdogo sana kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake. Mpaka sasa ni asilimia 3.1; hatuzuiliwi kwenda kwenye asilimia sita kama ukuaji wa uchumi ulivyo, tunahitaji kuwekeza fedha katika sekta hii. Ukiangalia... *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante, dakika tano ni ndogo kwa mchango mzuri, Mheshimiwa Toufiq ajiandae Mheshimiwa Mipata.

MHE. JUSTIN J. MONKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

MHE. FATMA H. TOUFIQ: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa na mimi nichengie japo kwa dakika tano katika hoja iliyopo mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi niungane na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote kwa kuandaa hotuba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba nijielekeze moja kwa moja kwenye zao la biashara katika Mkoa wa Dodoma ambalo ni zao la zabibu. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri hakuna katika ukurasa wowote ambako amebainisha kwamba wanatoa kipaumbele gani katika kuendeleza zao la zabibu katika Mkoa wa Dodoma na hii inafahamika kabisa kwamba ni miongoni mwa mazao ambalo linaweza likawakomboa wananchi wa Dodoma katika suala zima la umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitaomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha labda anieleze mkakati wa Serikali ni upi wa kuhakikisha kwamba zao hili linaweza likawekewa mkakati maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna mbegu za kutosha kwa ajili ya zabibu, lakini sambamba na hilo mbegu za zabibu zinapatikana katika Kituo cha Makutupora. Kituo hiki bado hakina taasisi ya utafiti, kwa hiyo, hata baadhi ya magonjwa ya zabibu hayajulikani. Kwa hiyo, nilikuwa naomba niishauri Serikali yangu tukufu kwamba iione umuhimu wa kuanzisha kituo cha utafiti wa zao la zabibu ili kusudi kuweza kufahamu magonjwa na jinsi gani ya kuweza kupata suluhu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 38 amezungumzia kuhusu Sheria ya Zana za Kilimo. Naomba tu nihamasishe kwamba Serikali imechelewa kuleta sheria hii, hivyo basi hebu ifanye haraka kwani hizi zana za kilimo kwa kweli kuna baadhi ambazo hazikuwa katika ubora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie pia kuhusu suala zima la alizeti. Mkoa wa Dodoma ni miongoni mwa mikoa ambayo mvua zake ni chache kwa hiyo mtawanyiko wa mvua ni kidogo. Kwa hiyo, zao la alizeti pia linastahimili katika Mkoa wa Dodoma. *(Makofi)*

Sambamba na hilo kuna changamoto nyingi, mbegu hazitoshelezi na wakulima wengi wanatumia mbegu ambazo wanakuwa wamezizalisha katika kipindi kilichopita. Kwa hiyo, nilikuwa naomba tu nitoe shime kwa Serikali yangu ione ni jinsi gani itaweka utaratibu wa kuhakikisha kwamba mbegu za alizeti zinapatikana kwa wakati na zilizo bora ili kusudi tuweze kupata hizo mbegu bora na hatimaye wakulima wetu waweze kupata mazao yenye tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti ...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante...

MHE. FATMA H. TAOFIQ: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge kuna jambo mahsusi ndani ya Bunge leo, Mbunge wa Jimbo la Kongwa ambaye ni Spika wa Bunge yupo ndani ya nyumba, Mheshimiwa Spika karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Mipata, ajiandae Mheshimiwa Adadi.

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kunipa nafasi. Kulingana na muda niende moja kwa moja kwenye hoja. Nitazungumzia hoja chache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo cha mahindi, Mkoa wa Rukwa unalima mazao mengi na hali ya hewa inakubali kuzalisha mazao mengi lakini mahindi yanalimwa kwa asilimia 43 ya mazao yote yanayolimwa pale na ardhi yote. Ndio kusema kwamba kilimo cha mahindi kwa Mkoa wa Rukwa ndiyo maendeleo yao kwa kila kitu kielimu, afya, watoto kwenda shule na kila kitu, lakini sasa tunaanza kukwama kutokana na kilimo kutokwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kilimo hiki kinakwama kwenda vizuri kwa sababu ya mipango mimi niseme mibovu ya kuendeleza kilimo, haiwekwi vizuri. Sasa tunaanza kuona mwaka hadi mwaka hali inakuwa inabadilika, lazima tusimame tupaze sauti. Wakulima sasa wanangamizwa na ndiyo hao wanakaa kijijini ndiyo wanatuchagua na kutuweka kwenye madaraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali ibadilike, mtazamo wa kilimo sasa si sawa hata kidogo. Kuna mawakala wamehudumia kilimo, si sawa kufikiria kwamba wote walikuwa wezi na kwamba kazi waliyoifanya haina maana, siyo sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie muda mfupi huu kuwasilisha kilio cha wakulima wa Vijiji vya Kasu, Kisula, Milundikwa na Malongwe. Wakulima hawa hawana shughuli nyingine ya kufanya kutokana na uamuzi wa Serikali wa kutwaa maeneo ya jeshi, wamekosa ardhi kabisa. Nitatumia muda mwingi kulisemea hili na leo nashukuru nimefanikiwa kumuona Waziri Mkuu nikamfikishia, najua limefika Serikalini, Serikali najua inasikia. Kwa huruma ya Serikali naomba jambo hili lizingatiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo ni muhimu sana, leteni mbolea; Minjingu sisi hatuitaki, Minjingu haitakiwi, anayesema Minjingu fanyeni utafiti. Basi kama mnaitaka iwekeeni *subsidy,* muilete kwenye soko halafu wananchi waende kwa kupenda au kwa ubora wake na si kwa kulazimisha. Minjingu katika Mkoa wa Rukwa ni kitu ambacho hakitakiwi na hakizalishi vizuri, labda sehemu nyingine ambayo wameweka wakaleta utaratibu mzuri zaidi, wakafanye utafiti, kwa utafiti uliopo sasa hivi haina matokeo mazuri na mimi ni mkulima ninayesema hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaweza ikatoboreshea Minjingu lakini ituwahakikishie iweke *subsidy* kidogo, iwekwe kwenye soko ilete ushindani na mbolea halafu baada ya miaka miwili, mitatu wananchi wataamua wenyewe sio kuwala... *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mipata, Mheshimiwa Adadi jiandae Waziri wa Maji.

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB: Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nashukuru sana kupata nafasi hii ya kuchangia kwenye hoja hii ya kilimo ambayo ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposema kilimo kipewe kipaumbele ni muhimu sana, na ningeshauri kwamba kipaumbele hiki kiende sambamba na ujezni wa viwanda,

tuwe wabunifu kwenye mambo mbalimbali yaweze kuweza kukuza kilimo chetu ili kumuondoa mkulima kulima na jembe. Sasa twende kwenye ubunifu wa ulimaji ambao ni wa kisasa, ulimaji ambao ni wa umwagiliaji, ambao utaleta manufaa makubwa kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa sana kuishauri Serikali kwamba kuna mifano mingi ya nchi nyingi, hili suala la mbolea, suala la mbegu, hebu Serikali ijiangalie, itoe mbegu bure, itoe mbolea bure. Tutakapotoa hivyo, kuna mifano ya nchi jirani ambayo imewahi kufanya hivyo, kwa hiyo nafikiri tutakapotoa hivi vitu bure na baadae tunakuja kuwachaji wakulima kwenye faida ambayo watapata baada ya kuuza hayo mazao yao. Nafikiri ni muhimu tuchague baadhi ya mazao ambayo tunaona kwaba yanaweza kuwa na manufaa kwa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kule Tanga, Amani, tunalima sana chai, kuna kiwanda kimoja cha *EUTCO,* wanalima sana chai, lakini wana tatizo moja ambalo nimeshawahi kumwambia Mheshimiwa Waziri, kwamba hawa watu wanalima chai, wanatakiwa wa-*brand,* wanatakiwa wa-*pack,* wanatakiwa wauze, lakini hawaruhusiwi, wao wanalima baadaye wanaambiwa kwamba baada ya kuchakata wakauze mnadani kule Mombasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunawapa faida hawa watu wa Mombasa, watu wa Kenya, kwa nini hayo mambo tusiyafanye hapahapa nchini? Hawa watu wako tayari kabisa kufungua kiwanda, na ndiyo maana tunataka kwamba tuweke viwanda kwenye hii nchi viwe vingi. Sasa hivi vikwazo ambavyo vinawekwa hapa, naomba Mheshimiwa Waziri uliangalie sana hili, hii ni mara ya pili nakwambia, naomba uliondoe, waruhusiwe hawa watu, wachakate, wa-*brand* na wauze hapa hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni katani, naona vipaumbele vingi vinapewa kwenye korosho na pamba, lakini katani sasa hivi ina bei kubwa sana kwenye Soko la

Dunia, lakini haipewi kipaumbele na sielewi ni kwa nini kwa sababu mashamba yametaifishwa lakini hakuna kiongozi ambaye anakuja kushawishi kuweza kusema kwamba tulime katani. Sasa naomba kabisa kwamba suala la katani lipewe kipaumbele, kwa sababu katani yenyewe si kamba tu, ina mambo mengi pale kwenye ule mti. Huwezi kutupa katani, inatengeneza mpaka umeme; kwa hiyo naomba kabisa kwamba Mheshimiwa Waziri suala hili la katani lipewe kipaumbele cha hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri sana na ninaunga mkono Kamati ambayo imeshauri kwamba Mheshimiwa Spika na uzuri yuko hapa, atengeneze Kamati ya Bunge ambayo inaweza kushauri hili suala la kilimo, vinginevyo hatuelewi tunakwenda wapi, mbele, nyuma, bajeti inazidi kuteremka. Sasa itakapo...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango mzuri.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. MARY D. MURO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali iweke kipaumbele juu ya ulipaji wa mawakala na kuwaokoa na udhalilishaji unaofanywa na mabenki. Nashauri Serikali kuhakikisha haizuii uuzaji wa mazao ya kilimo bali itoe maelekezo ya kuhifadhi baadhi ya chakula ili kutoangukia kwenye njaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishauri Serikali kuongeza fedha za utafiti wa vituo vyetu, kwa mfano Vituo vya Utafiti vya Mlingano, Ukiriguru na Naliendele ili itoe matokeo yatakayoleta ufanisi katika kilimo. Pia niishauri Serikali kuhakikisha inaangalia zaidi katika suala zima la ushirika nchini kwani hakuna watumishi wa kutosha tangu

walipostaafisha watumishi kwa manufaa ya umma hawakuajiri watumishi wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishauri Serikali kuangalia umwagiliaji kwenye mashamba yetu, kwenye mito yetu mfano Mwalimu Nyerere alianzisha shamba la mpunga Ruvu ambalo sasa hivi linapimwa viwanja tu na umwagiliaji uko mahututi. Niishauri Serikali kufufua mashamba haya badala ya kufanya maji haya kupotelea baharini.

MHE. JANETH M. MASABURI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwapongeza Waziri wa Kilimo, Naibu Waziri wa Kilimo, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote walioshiriki katika kutenda na kusimamia shughuli zote zinazohusika na kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo, kuna changamoto ambazo zinatakiwa kupatiwa ufumbuzi wa haraka ili kukidhi mahitaji ya Watanzania kwa kuzalisha mazao ya chakula na biashara kwa kupunguza uagizaji wa mafuta ya kula na sukari kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iwapo nchi yetu itazalisha mazao ya mbegu za mafuta ya kula na sukari kwa kiwango kikubwa, kwa Serikali kuwekeza kwenye kilimo cha miwa na mbegu za mafuta kuongeza mashamba na kushiriki. Jeshi la Magereza, Jeshi la Kujenga Taifa na wawekezaji kutoka nje ya nchi na Watanzania wenyewe kwa kuweka mazingira mazuri ya kilimo, kuweka miundombinu ya umwagiliaji kama kuvuna maji ya mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kushirikisha nguvu kazi ya vyombo vya ulinzi itasaidia vijana wetu kushiriki kikamilifu katika kuzalisha mazao mbalimbali na pia itasaidia vijana kupata ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazao makuu ambayo ni ya kiuchumi hapa nchini yanapaswa kuwekewa mkakati wa kudumu na endelevu kwa kuweka misingi imara. Kilimo cha kisasa cha umwagiliaji hakikwepeki katika zama za sasa.

Kilimo kiendane na dhana ya Tanzania ya viwanda kwa vitendo, kila Wizara inahusika na kushabihiana na Tanzania ya viwanda.

MHE. RISALA S. KABONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia hoja hii ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda haviwezi kuwa endelevu kama hakutakuwa na malighafi ambazo kimsingi zinatokana na kilimo. Waziri atakubaliana na mimi kwamba bila kuwa na mapinduzi ya kilimo ndoto ya Tanzania ya viwanda haitafanikiwa. Nasema hivi kwa sababu kilimo chetu bado ni duni sana kuweza kuzalisha malighafi za kulisha viwanda hivyo vinavyokusudiwa kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu zao la mbaazi, zao hili uzalishaji wake umeongezeka sana ambapo wakulima walizalisha tani milioni 2.3 za mbaazi mwaka 2016. Naiomba Serikali iendelee kuangalia kwa jicho la ukaribu soko la mbaazi ili wakulima hawa wasiendelee kupata hasara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mafuta, ninaamini kuwa wananchi wengi wanaelewa kuhusu utumiaji wa mafuta ya mbegu. Ninashauri Serikali itoe mikopo kwa wakulima ili waweze kuzalisha kilimo cha mbegu za mafuta na mafuta yatosheleze nchi nzima, sambamba na upatikanaji wa mashine kwa bei nafuu za kukamulia mafuta ili wakulima waweze kuuza mafuta na kupata faida kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri pia Serikali iendelee ku-*support* zao la *apples* katika Mkoa wa Njombe. Mwaka jana nilizungumzia suala hili naomba nilisemee tena kwa kuwa tumekuwa tunatumia sana *apples* kutoka Afrika ya Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya kilimo iangaliwe kwa jicho la karibu ili kusaidia wakulima wetu hasa kuwafikia kutoa elimu ya mbegu bora na kilimo chenye tija.

MHE. RUTH H. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kupata nafasi hii kuchangia hoja iliyopo mezani. Pamoja na kwamba kilimo ndicho kinachotoa ajira kubwa kwa Tanzania, bado bajeti inayotengwa kwa eneo hili ni ndogo sana. Hivyo ili kuleta mapinduzi ya kilimo mambo yafuatayo yazingatiwe:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itenge bajeti ya kutosha, Maafisa Ugani wapewe motisha kama pikipiki na watawanywe kwenye vijiji vyote, wakipewa malengo ambayo yatatumika kupima utendaji wao wa kazi. Uwepo mfumo unaoainisha kila Afisa Ugani anahudumia idadi gani ya wakulima wawe na majadala kwa kila mkulima na kufuatilia maendeleo yao, kama ilivyo kwa madaktari kwa uwiano wa daktari mmoja kwa wagonjwa10,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwepo uhusiano wa karibu kati ya Wizara ya Kilimo inayotoa sera na kusimamia kilimo, taasisi za mafunzo kama *SUA* na taasisi zingine za utafiti. Tafiti bora kwa mazao zifikishwe sasa kwa wakulima kwa mafunzo na mashamba darasa. Nchi zilizofanikiwa kwenye mapinduzi ya kijani, Serikali kupitia Wizara iligharamia mafunzo ya wakulima kwenye taasisi za utafiti ili kuhakikisha wakulima wanajifunza mbinu mpya za kilimo cha mazao mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mafunzo mashamba darasa huanzishwa kwenye vijiji ikisimamiwa na Maafisa Ugani, mashamba haya ndiyo hutumika kusambaza teknolojia ya uzalishaji kwa makundi mengi ya wakulima wadogo wadogo. Ni muhimu hii Wizara ya Kilimo ikapata msimamo wa Wizara ya Viwanda kujua ili viwanda gani vinavyozungumziwa ili Wizara ya Kilimo ijikite kwenye kilimo cha mazao ambayo yatahitajika kwenye viwanda vinavyoanzishwa. Uratibu wa Wizara zinazohusiana ni muhimu kuepuka mkanganyiko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. ALFREDINA A. KAHIGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, namkushukuru Mheshimiwa Waziri wa Kilimo pamoja na

Naibu wako kwa hotuba yenu nzuri, napongeza Kamati ya Kilimo kwa maoni yao. Naomba Serikali iyafanyie kazi maoni haya na ushauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Mkoa wa Kagera tuna kilio cha mnyauko wa migomba na ni wa miaka mingi sasa. Ni tatizo gani Serikali imeshindwa kumaliza tatizo hili? Naomba itusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wa miwa *(outgrowers)* katika kiwanda cha *Kagera Sugar* wanauza miwa yao kwa mwekezaji, wanalipwa baada ya miezi mitatu, je, kuna uwezekano wa kumshauri mwenye kiwanda ili awalipe ndani ya wiki mbili ili kunusuru mashamba yao yasiharibike? Mkulima anamkopesha mwekezaji miezi mitatu miwa yake, kumbuka hawekewi riba yoyote, Mheshimiwa Waziri wasaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nawatakia kazi njema Mungu awasaidie katika kazi zenu.

MHE. ZAINAB M. AMIR: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Mhandishi Dkt. Charles John Tizeba (Mbunge), pamoja na Naibu wako Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa (Mbunge) kwa kazi nzuri mnayoifanya katika Wizara hii ya Kilimo. Naishauri Serikali iongeze idadi ya wataalam mabwana shamba na mabibi shamba ili wawasaidie kutoa elimu ya kutosha kwa wakulima wetu ili waweze kulima kilimo cha kisasa na chenye tija kwa wakulima na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali itoe mbolea na madawa kwa wakati ili iwasaidie wakulima kuweza kuitumia kwa wakati na kuweza kupata mazao bora na mengi kwa chakula na biashara. Serikali iwaruhusu wakulima waweze kuuza mazao nje ya nchi kwa kuzingatia taratibu zilizowekwa na nchi. Naishauri Serikali iwasaidie na kuwawezesha wakulima walime mazao ambayo yatatumika kama malighafi katika viwanda vyetu na kuepuka kuagiza malighafi za viwanda vyetu kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali iendeleze kilimo cha umwagiliaji katika Mikoa yote ya Tanzania ili kuweza kupata mazao mengi bila kutegemea mvua ambayo kwa wakati mwingine haina uhakika kutokana na mabadiliko ya tabianchi. Naishauri Serikali skimu iliyopo Wami Dakawa iboreshwe ili kuweza kupata mpunga mwingi kwa kuboresha miundombinu yake ambayo ni ya muda mrefu. Pia kuongeza eneo kutoka hekari zilizopo 2,000 hadi 5,000 ili kuweza kuwapa fursa baadhi ya wakulima wapate eneo linalotumia kilimo cha umwagiliaji badala ya kutegemea mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali iwashirikishe wakulima katika upangaji wa bei ya mazao na siyo Serikali kutoa bei elekezi kwa wakulima ambayo wakati mwingine haina tija kwa wakulima kulingana na gharama walizotumia katika kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho namuomba Mwenyezi Mungu Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wako awape afya njema na umri mrefu ili muweze kuwatumikia Watanzania.

MHE. LATHIFAH H. CHANDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kati ya tatizo kubwa na sugu linalofanya uzalishaji wa korosho katika Mikoa ya Kusini ni uzee wa miti iliyopo. Kama ilivyo katika mazao mengine kama miembe, michungwa, parachichi, limao na mengine mengi ni wakulima wachache sana wanazalisha mazao hayo kibiashara wanatumia miche au miti ya zamani ya kiasili. Wengi wanatumia ya kisasa *(cross breed)* ili kuweza kupata mti bora wenye uwezo mkubwa wa kuhimili magonjwa kutoa mazao mengi na kuweza kuzaa ndani ya muda mfupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mpango gani ili kuhakikisha kwamba wakulima wa korosho wanapanda kwa wingi miche ya kisasa ya mikorosho inayozozalishwa nchini ukizingatia kwa muda mrefu zao la korosho limekuwa likishika namba mbili nyuma ya tumbaku katika mazao yanayoliingizia Taifa pesa nyingi pamoja na pesa za kigeni,

kuna mashamba ambayo yameteuliwa kuzalisha miche ya mikorosho ya kisasa, mashamba hayo yapo Mkoa wa Tanga, Pwani na maeneo machache ya Mkoa wa Lindi na Mtwara. Serikali ina mpango gani wa kuinua uzalishaji wa mashamba haya ili miche inayozalishwa iweze kuwafikia wakulima wengi zaidi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine ni ufisadi uliokithiri, wawakilishi wa wanunuzi huhongwa katika minada badala ya kuwa upande wa wakulima wanakuwa upande wa wanunuzi pamoja na viongozi wa vyama vya msingi. Hii hupelekea wote kwa pamoja kushirikiana katika kumkandamiza mkulima na kumfanya mnunuzi anaeshinda kununua sio anayetoa bei ya kumnufaisha mkulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine lipo katika mfumo na mlolongo mzima wa malipo kuwa mlolongo mrefu sana kupelekea pesa kuchelewa kumfikia mkulima na kupelekea wakulima waone bora kuuza korosho kwa njia ya kangoma kuliko kupeleka korosho zao kwenye utaratibu wa stakabadhi ghalani. Malipo hupitia *process* ambazo ni *manual* na taratibu za kibenki kuchukua muda mrefu kiasi cha kwamba hadi pesa inamfikia mkulima inakua tayari imeshuka kwa mfumo thamani. Serikali ijitahidi kuhakikisha kuwa mfumo huo unafupishwa ili kuweza kutoa nafasi kwa mkulima kupata pesa zake kwa wakati na kufanya maandalizi ya msimu unaofuata mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuzungumzia suala la utawala mbovu katika Wizara ya Kilimo. Wafanyakazi wengi wamesimamishwa kwa muda hadi kufika mwaka mmoja na zaidi bila kupewa nafasi ya kusikilizwa wala kuchunguzwa jambo ambalo liko kinyume na taratibu za kisheria. Wengine walisimamishwa kwa kosa la kile tunachoita kutekeleza majukumu yao ya kazi mfano, *TPRA* ambao walileta taarifa kuwa mbolea iliyoingizwa nchini ilikuwa mbovu, iliamuliwa kwamba mbolea ikakaguliwe na Mkemia Mkuu ambaye alithibitisha kuwa mbolea haina matatizo lakini katika hali ya kushangaza mbolea hiyo hiyo ilipoingia kwa ajili ya matumizi ikaonekana na ikathibitika kuwa mbovu. Sasa

hao waliosimamishwa baada ya Mkemia Mkuu kuthibitisha kuwa mbolea ni nzima kwa nini baadae ilipothibitika kuwa kweli mbolea mbovu kwa nini hawajarudishwa kazini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni mfano mmoja tu lakini wafanyakazi wa vitengo mbalimbali wamesimamishwa kwa kipindi kirefu bila kujua hatma yao. Huu ni utawala mbovu ambapo haki za wafanyakazi hazisimamiwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa napenda kuzungumza juu ya makampuni na mawakala kuna madai ya mwaka 2014/2015, 2015/2016 hali kadhalika, lakini cha kushangaza kila siku Wizara inafanya ukaguzi na uhakiki wa madai hayo. Ifike wakati sasa watu walipwe madai yao. Wizara itueleza ni lini watalipwa madai yao.

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kuweza kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya kilimo Tanzania, leo ni miaka 57 baada ya uhuru bado Tanzania kilimo kimekuwa cha kusuasua na kimejaa siasa na misamiati kibao. Kwa kifupi bado nchi yetu haijawa *serious* na kilimo kwa kuwa bado wakulima asilimia 70 wanategemea jembe la mkono na asilimia tatu wanatumia wanyama kazi na asilimia tatu ndiyo wanaotumia zana za kisasa za kilimo kama matrekta na mitambo mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo chetu tumekiingiza kwenye siasa na misamiati ya maneno badala ya vitendo. Yapo maneno siasa ni kilimo, kilimo cha bega kwa bega, kilimo cha kufa na kupona, kilimo cha ushirika, kilimo ni uti wa mgongo wa Taifa letu, kilimo ni uhai na kilimo kwanza. Je, nchi jirani wanayo hii misamiati katika kilimo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kudharauliwa kwa bajeti ya Wizara ya Kilimo, pungufu asilimia 23. Bajeti ya mwaka 2017/2018 ilipelekwa asilimia 18 na bila shaka itapungua hadi asilimia tatu, hii ni hatari, hatujui kipaumbele ni kipi na kipi

kisubiri, kuna mambo namna tatu, moja umuhimu haraka sana, mbili muhimu lakini siyo haraka, tatu muhimu kawaida. Bajeti ya Kilimo ni asilimia 0.52 ya Bajeti Kuu, namtaka Waziri atakapokuja katika *winding up* atueleze vipaumbele katika Wizara yake. Bajeti haitoshi ni bado tunasema kilimo ni uti wa mgongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kizungumkuti cha mawakala, bajeti ya mwaka 2015/2016 ilikuwa shilingi 35 bilioni na deni wanalosema wanadai ni shilingi bilioni 67. Maswali ya kujiuliza Waziri uje na majibu ama shilingi halali yangu kuishika. Kwa nini shilingi bilioni 67 inatoka wapi?, kwa nini vocha zilizidi hata bajeti iliyotengwa ni vocha za thamani gani zilirudi kutoka Mikoa yote? Kwa nini zilitengenezwa vocha nyingi zaidi ya bajeti iliyotengwa, ni fedha shilingi ngapi zilitumika kutengeneza vocha hizo? Baada ya vocha kurudi deni halisi ni shilingi ngapi? Je, Serikali ipo tayari kuwasikiliza mawakala ili watoe hesabu halisi? Hakuna ofisi iliyovunjwa na vocha kuibiwa kwanini kuna tofauti ya deni ya shilingi bilioni 35 na shilingi bilioni 67? Waziri uje na majibu sahihi na uchunguzi ufanywe na Serikali ili kubaini waliohusika na hatua zichukuliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyama vya ushirika ni matatizo kwa wakulima. Zamani miaka ya 1950 – 1960 vyama vya ushirika kama *KNCU* - Kilimanjaro na *KNCU* - Kagera, Nyanza na Tanga - *TARECU*, vyama hivi viliwasaidia wakulima kwa kukata shilingi moja hadi mbili na kisha waliwalipia ada wanafunzi ambao leo ni madaktari, wachumi, maprofesa, *engineers, pilots* lakini pia bado vyama vya ushirika viliwasaidia wakulima katika kuendeleza kilimo, leo vyama vya ushirika kazi kubwa ni kuwaibia, kuwadhulumu na kuwatapeli wakulima mazao yao na bahati mbaya mnaihusisha Ilani ya CCM.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda cha mbolea Tanga - Tanzania *Fertilizer Company (TFC).* Tanga ilikuwa ni mji wa viwanda, miongoni mwao ilikuwa ni Kiwanda cha Mbolea. Kiwanda kilifanyiwa hujuma na kikafa kwa maksudi ili pafanyike biashara ya kuagiza mbolea kama *urea, sulphur/*

DAP bei juu, kisha eti kikajengwa Minjingu lakini vifungashio *made in Kenya.* Wakati Kiwanda cha Mbolea Tanga kinafanya kazi hakijauliwa kwa makusudi tatizo la mbolea halikuwepo na wala *issue* ya mbolea ilikuwa haijadiliwi Bungeni kwa ghadhabu na hasira kama ilivyo leo. Tujiulize tatizo nini na liko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania kwa jina la Mwenyezi Mungu bila ya kuimarisha na kuboresha kilimo kinachotoa *raw materials* za viwanda tutabaki na hadithi za paukwa pakawa hapo zamani za kale, bajeti ya kilimo ni asilimia 18 kwa mwaka 2018, nashauri Serikali iongeze bajeti kwa mwaka 2018/2019 angalau ifikie asilimia 35 kwa kuwa kilimo kinaajiri Watanzania asilimia 75 angalau kilimo kitaimarika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wakulima kukosa masoko; Tanga ni wazalishaji wakubwa wa zao la muhogo katika Kata za Kirare, Mzizima, Tongoni, Pongwe na Kiomoni lakini tatizo kubwa ni soko la uhakika kiasi kikubwa cha muhogo hutegemea soko la Tanga Mjini na Dar es Salaam. Masoko hayatoshelezi na kusababisha muhogo kuporomoka bei, zimekuwepo tetesi kuwa Wachina wanahitaji muhogo, *Tanzania Chamber of Commerce* iko katika mazungumzo ili kujua kwa mwaka China itahitaji tani ngapi kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri, Waziri wa Kilimo wakati wa majibu ni vyema akaeleza ukweli na uthibitisho wa taarifa hii ili kuweza kuwatoa shaka wakulima wa muhogo wa Tanga na Tanzania kwa ujumla. Masoko ya mazao mengi yamekuwa mashakani na mazao hayo ni mbaazi, mtama, miwa, machungwa, mahindi, ufuta na kadhalika. Serikali iwe na mipango ya muda mrefu ya utafutaji wa masoko, Serikali ifuate mfano wa nchi za India, Brazil, Rwanda, Burundi na Uganda kutafuta masoko ya mazao ya wakulima wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mikopo kwa wakulima katika mabenki; mikopo katika mabenki ya nchi yetu ni haki kwa kila Mtanzania atakayekamilisha taratibu zilizopo. Serikali ilianzisha hatimiliki za kimila na moja ya

manufaa ya hati hizi ni wakulima kuweza kuzitumia katika mabenki na kuweza kupata mikopo, kitu cha kushangaza wananchi wengi waliotaka kuzitumia hatimiliki za kimila kutaka mikopo katika benki za *NMB, NBC* na *CRDB*. Hati hizi hazitambuliki na wakulima wanashindwa kuelewa kati ya mabenki na Serikali nani ni mkweli au nani ni muongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri kwa Serikali, isiwadanganye wakulima inawakatisha tamaa, wakulima wamejitahidi kupata hatimiliki za kimila lakini hazina maana yoyote. Serikali itafute njia mbadala kuwawezesha wakulima wa Tanzania kuweza kupata mikopo katika mabenki yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kilimo cha Mkonge Tanga. Tanga imefahamika na kupata umaarufu katika Afrika Mashariki, Afrika na dunia kutokana na zao la mkonge kuanzia katika miaka 1886, zao hili lililetwa na Wagiriki na Wajerumani, Serikali ya *United Kingdom*, walikuja kuliboresha na kuliimarisha kwa kuwa walipata kodi kubwa katika mkonge. Mkonge katika Tanzania upo katika Mikoa ya Tanga, Kilimanjaro na Lindi. Mkoa wa Tanga pekee ulikuwa na mashamba 72 yaliyoajiri wafanyakazi 40,000 na vibarua 32,000. Serikali baada ya kuimarisha mashamba ya mkonge iliamua kuzibinafsisha Mamlaka ya Mkonge *(Tanzania Sisal Authority)* na hapo ndipo mkonge ulipoanza kufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati njema sana dunia imeamua kutumia bidhaa za mikonge kwa kuwa mkonge hauchafui mazingira, lakini mkonge katika Tanzania haupo mikononi mwa Serikali, mamlaka na udhibiti ipo kwenye taasisi na watu binafsi ambao hawawezi kuendesha mkonge. Nashauri Serikali iamue kwa makusudi kulifanyia kazi na kulithamini zao la mkonge kama inavyofanya kwa mazao ya korosho na pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho Maafisa Ugani wasikae ofisini waende mashambani.

MHE. ZAINABU N. MWAMWINDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba nianze kwa kumshukuru

Mungu aliyeniwezesha kutoa mchango wangu katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Waziri wa Kilimo, Naibu Waziri pamoja na watendaji wote katika Wizara hii kwa kutekeleza vema majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe kuishauri Serikali kwa jicho la huruma imtazame mkulima wa zao la mahindi. Mkulima huyu ameteseka sana, amelima kwa taabu lakini anapofika kuuza mahindi yake anapatiwa masharti na kuzuiwa kujitafutia masoko likiwemo la kufanya mipaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie katika mambo mawili yanayohusu Wizara hii ya Kilimo kuhusu zao la pareto. Inafahamaika kuwa Tanzania ni miongoni mwa nchi tatu duniani zinazozalisha asilimia 90 ya zao la pareto. Kilimo cha zao hili katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini mwa Tanzania kimeweza kuwa mkombozi kwa wananchi kiuchumi na kukuza pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Wizara isimamie kwa ukaribu ustawi wa zao hili katika Mikoa inayolima na hasa kufanya tafiti mpya zitakazobainisha maeneo mapya ya uzalishaji na kuongeza uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante.

MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Namtumbo na mimi mwakilishi wao tunaiunga mkono hii hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kwa niaba ya wananchi wa Namtumbo kukuomba radhi kwa kauli ya kiongozi wetu wa Wilaya aliyedai eti Mheshimiwa Waziri wa Kilimo pamoja na sisi viongozi wa Wilaya ya Namtumbo wa Chama na Serikali tunawadhulumu wakulima wa tumbaku kwa kuwakopesha mbolea kwa bei ya juu tofauti na iliyotangazwa na Serikali na kwa kuwacheleweshea mbolea

hiyo. Tumempuuza kwa sababu najua kabisa na wala hataki kujua utaratibu wa msimu wa kilimo cha Tumbaku ulivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri ili aelewe vizuri tatizo tulilonalo kiongozi wetu huyo wa Wilaya alitembelea mashamba ya mpunga yanayolimwa na wakazi wa Kata ya Mchomono na alipoona mpunga ulivyostawi akadhani ni magugu na akatoa amri magugu hayo yateketezwe kwa kutumia kemikali ya kuunguza magugu iliyotolewa na *NGO* ya *PAMS Foundation* ya Wajerumani na Wajerumani hao walitoa dawa husika na ikanyunyiziwa kwenye mashamba ya wakulima hao wa mpunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi hao hawajui wataishije kufuatia tendo hilo la kiongozi wetu Luckiness Adrian Amlina, *DC* wa Namtumbo. Nikuombe utumie nafasi yako kumjulisha Mheshimiwa Rais atuondolee adha hii ili wananchi wa Namtumbo waendelee kuishi kwa kutegemea mavuno ya mashamba yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Mheshimiwa Dkt. Charles Tizeba, Waziri wa Kilimo tunashukuru kwa kutuwezesha kumpata mnunuzi wa tumbaku ya Moshi, Kampuni ya *Premier Leaf Tanzania Limited*. Ulitoa kibali kwa kampuni hiyo kusafirisha *green leaf* nje ya nchi kwa miaka miwili kwa masharti kuwa katika kipindi hicho wajiandae kuchakata tumbaku nchini na maandalizi wameanza kwa kushirikiana na *SONAMCU* kufufua kiwanda cha kusindika tumbaku cha Songea. Ungekosa kutoa kibali kile kampuni hiyo haingeingia mkataba wa kununua tumbaku Namtumbo na Songea na hivyo kutuwezesha kulima tumbaku mwaka huu na miaka itakayofuata na hivyo kufufua zao hilo la kibiashara na la muda mrefu huko nyuma. Mwezi ujao tu pesa zitaingia Namtumbo kupitia kufufuliwa kwa zao hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mheshimiwa Waziri udumu kuhudumu katika Wizara hii. Amina!

MHE. SILAFU J. MAUFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni pana inayohusika na idadi kubwa ya wananchi

wanaoshiriki kwa upatikanaji wa chakula na kibiashara katika uchumi wa wananchi hao. Kutokana na uzito wa Wizara hii, sina budi kutoa shukrani za dhati na pongezi kwao Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote wa kada mbalimbali kwa kazi nzito waifanyayo kuhudumia wananchi, pamoja na uchache wa bajeti yao na bado Wizara ya Fedha inawasilisha kwa fedha za miradi ya maendeleo kwa asilimia 18 kwa fedha zilizoidhinishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni hatari kwa watekelezaji na wasimamizi wa kilimo chetu nchini. Hivyo, Fungu 43 kwa mwaka 2017/2018 ya tengeo la shilingi 150,253,000,000 na kupelekewa shilingi 27,231,305,232.69 ambayo ni 18%. Tunaomba kwa mwaka 2018/2019 fungu hili liweze kutekelezewa kwa angalau 65% kama sio 75% kutokana na shilingi 162,224,814,000 ili tuweze kuboresha zaidi maendeleo ya kilimo chetu nchini na kuweza kuongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuendelea kusubiri mvua za msimu ambazo zinaendelea kupungua na kutokukidhi haja ya kuivisha baadhi ya mazao kwenye baadhi ya maeneo hapa nchini na kurudiarudia kila mwaka na wananchi wa maeneo hayo kupata shida ya upatikanaji wa chakula, kwani kinakuwa kwa gharama kubwa na wengine kushindwa kukipata na kuwasababishia kubadili utaratibu wa kutumia chakula kwa mlo mmoja kwa siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inafahamu maeneo hayo, lakini urasimu wa utekelezaji kwa wataalam wetu wa kuchukua muda mrefu wa utafiti wa kufanyia kazi kwa wakati bado maeneo hayo hayana mavuno mazuri. Wataalam waweke mikakati ya makusudi ya kukabiliana na uharibifu wa hali ya hewa kwa kujikita zaidi kwenye kilimo cha umwagiliaji kwa kuhakikisha maji ya mvua yanavunwa, tusikubali maji haya yakapotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano Bonde la Rukwa linapokea maji mengi kutoka Ufipa ya Juu na kwenda moja kwa moja Ziwa Rukwa na kujaza udongo na kusababisha ziwa kujaa udongo na kina chake kupungua na maji

kupotea. Maji hayo yakingwe kwenye mabwawa kadhaa yatasaidia kilimo cha umwagiliaji, maji ya kutumiwa na wananchi, mifugo na viwanda vidogovidogo na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala zima la ushirika kwa sasa wananchi wengi na ambao wanaumia na utekelezaji wa viongozi waliotangulia kutokutenda haki, hasa kipindi cha hapa kati, kunawakatisha tamaa kwa kuendelea na suala la kuendelea na ushirika. Ushauri ni bora sasa ukafanyika kwa kina uchambuzi wa viongozi wetu ndani ya ushirika kwa kila eneo hapa nchini, ikibidi tupate viongozi tofauti kabisa. Ushirika tulionao tuone utaratibu wa kuunda muundo tofauti na tulionao ambao hauna usimamizi na ukaguzi wa karibu na chombo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kushukuru kwa jitihada zote zinazoendelea kwa kuendeleza kilimo, lakini bado uchelewesho wa mbolea na pembejeo kwenye maeneo kwa kuzingatia na msimu wao kuanza. Nashauri pembejeo na mbolea uwepo utaratibu wa kuwa ni bidhaa zinazokuwepo ndani ya maduka yetu mwaka mzima. Kwa kuwa ni mwanzo, tunaomba Wizara kutoa maombi Serikalini ya kusogeza huduma hiyo angalau kwenye kuunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

MHE. MARY P. CHATANDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hotuba ya bajeti ya Waziri wa Kilimo na maoni ya Kamati. Kilimo ni uti wa mgongo, kauli hii haiendani na utekelezaji kutokana na changamoto zifuatazo;

Kwanza, kutopewa kipaumbele kwenye bajeti kwa kutengewa fedha kidogo zisizoweza kukidhi uhitaji wa utekelezaji wa yale yanayopaswa kutekelezwa.

Pili, kutopewa fedha yote iliyotengwa pamoja na uchache wake kunachangia kukwamisha Wizara hii kutekeleza majukumu yake na tatu, kutokuwa na Maafisa Ugani wa kutosha huko vijijini ambao wangeweza

kuwasaidia wakulima kulima/kupanda mbegu bora/kupalilia na kuvuna mazao kwa lengo la kujiinua kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, vyuo vya utafiti kutopewa fedha za kutosha kufanya utafiti wa mbegu ili wakulima waweze kupanda mbegu bora na yenye kuwawezesha kuvuna mazao ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, uwepo wa migogoro ya ardhi kunachangia kwa asilimia 50 kati ya wakulima na wafugaji kukwamisha juhudi za wakulima kujipatia mazao ya kutosha kutokana na wafugaji kulisha mifugo kwenye mazao yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuishauri Serikali kama ifuatavyo:-

Kwanza, Serikali ina mpango mzuri wa nchi yetu kuwa ya viwanda na kilimo ndicho kitakachotoa malighafi zitakazolisha viwanda hivyo. Ni vema bajeti ya kilimo iangaliwe upya na kupewa kipaumbele cha juu ili Wizara iweze kutekeleza majukumu yake vizuri na Tanzania ya viwanda itawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, bajeti wanayotengewa wapewe yote kulingana na umuhimu wa majukumu yao yatakayowezesha na kuandaa Tanzania ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, Serikali itoe ajira za wagani maeneo /vijiji ambavyo hawana watumishi wa fani hii waweze kupelekwa na kuwawezesha vitendea kazi, ili waweze kutenda majukumu yao kikamilifu. Vyuo vya utafiti viwe na bajeti ya kutosha ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Ardhi, Maliasili na Utalii wakamilishe kuondoa migogoro ya wakulima na wafugaji ili wananchi hawa kila mmoja waweze kuishi kwa amani na shughuli za uzalishaji ziweze kufanyika kwa uhakika zaidi. Naomba kuwasilisha.

MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI: Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za maendeleo zinazotolewa na Hazina zimekuwa zikipungua kila mwaka na kusabaisha madhara kwa Watanzania 70% wanaotegemea rasilimali ardhi kwa shughuli za kilimo. Ushauri; Wizara ijipange ili kuhakikisha inatengewa fedha za kutosheleza ili kufanikisha malengo yake. Wizara iunde *strategic team* ili kufanya tathmini na kuja na mikakati mahususi ya kuiwezesha kutengewa na kupatiwa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo haijaweka mikakati ya wazi ya kufungamanisha sekta ya kilimo na sekta ya viwanda, wakati ni dhahiri malighafi *(raw materials)* nyingi za viwanda husika zinategemea *products* za kilimo. Ushauri; Wizara ya Kilimo iweke wazi uhusiano wake na sekta ya viwanda, hii pia italeta chachu ya kutengewa bajeti halisia, itasaidia ku-*justfy* umuhimu wa sekta ya kilimo katika kukuza na kuimarisha viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu pembejeo; kuna changamoto nyingi sana katika eneo hili, maeneo mengi nchini yamekuwa na kilio cha kukosa mbolea ama kutopata kabisa ama kuja kwa kuchelewa sana. Mbolea zimekuwa za ubora hafifu maeneo mengi, hususan ya vijijini kwa sababu za miundombinu mibaya ya barabara mbolea imekuwa ya bei ya juu sana. Sekta hii imekosa mfumo thabiti wa kuuzia pembejeo zisizo na ubora kwenye soko. Mfumo wa sasa wa *bulk procurement* kwenye mbolea umeongeza changamoto kwenye biashara ya mbolea. Ushauri, Wizara ijitathmini kwa upya na kuja na *solution* ya kudumu katika kuwezesha/ kuboresha mfumo mzima wa upatikanaji na usambazaji wa mbolea nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna upungufu mkubwa wa rasilimali watu katika sekta ya kilimo (wataalam na maafisa ugani) ambao wameajiriwa na wachache waliopo wanafanya kazi katika mazingira magumu (ukosefu wa vitendea kazi). Ushauri, Wizara ije na *document* inayoonesha ni wataalam wangapi wanaohitajika na katika maeneo gani

na kufikisha suala hili katika taasisi/Wizara husika ili lipatiwe ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mapungufu makubwa sana ya udhibiti wa mazao baada ya kuvuna *(post harvest losses),* hali hii husababishwa na idadi ndogo sana ya maghala nchini, kwa sasa kuna takribani maghala 1,200 wakati kuna vijiji 13,000. Hali na hadhi/teknolojia zinazotumiwa wakati wa kuvuna na kusindika mazao ni duni sana. Hali hii husababisha upotevu mkubwa wa mavuno, takribani 20% ya mazao hupotea baada ya mavuno. Ushauri; Wizara ijipange kimkakati na hata kushirikisha *private sector* kuhakikisha angalau kila kijiji/kata kinakuwa na ghala la kisasa linaloendana na mazao husika yanayolimwa katika eneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kilimo sio kipaumbele kwa Serikali (rejea kitabu cha mpango cha sasa). Basi ni bora Wizara ikajitathmini kwa ujumla wake ili Wizara hii muhimu na nyeti ikawa *more visible.*

MHE. MBARAKA K. DAU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa fursa hii. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao la nazi linapotea kwa kasi kubwa na nimepitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri sijaona mikakati yoyote ya kufufua zao hili ambalo ni muhimu sana maeneo ya mwambao wa Pwani hususan Kisiwa cha Mafia, mkoani Pwani. Ninamuomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kujibu hoja anieleze mipango kupitia utafiti ili kunusuru zao hili la nazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kituo cha utafiti wa kilimo kilichopo Mikocheni kina hali mbaya sana kifedha na Wizara bado haipeleki fedha ambazo kwa kiasi kikubwa itaokoa zao la nazi ambalo linazidi kupotea kutokana na minazi ya zamani kuanza kuzeeka na hakuna mipango mbadala ya kupanda miche ya kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo cha mwani kinacholimwa zaidi Kisiwani Mafia hakijapewa kipaumbele chochote katika bajeti hii. Miongoni mwa changamoto za kilimo hiki ni soko, mpaka sasa wananchi wa Mafia wamezalisha mwani mwingi na umerundikana katika maghala, changamoto nyingine ni vifaa duni wanavyotumia wananchi. Nimuombe Mheshimiwa Waziri awape zana za kisasa wananchi wa Mafia, hususani Kisiwa cha Jibondo ambao uchumi wao umeporomoka sana kutokana na katazo la kuvua wanategemea kilimo hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna changamoto ya taaluma ya kisasa, tunaomba Serikali itupatie wataalam wa kuendesha mafunzo ya ukulima wa kisasa wa mwani. Ninashukuru na ninaunga mono hoja.

MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na tatizo la mbolea kwa Wilaya ya Ludewa. Mbolea ya kupandia inachelewa kufika kwa wakulima na matokeo yake uzalishaji wake unakuwa hafifu na pia mbolea hiyo inauzwa kwa bei kubwa mno tofauti na bei elekezi iliyotolewa na Serikali. Serikali ije na mfumo madhubuti wa upelekaji kwa wakulima mbolea inayohitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu masoko ya mazao, wakulima wa Tanzania wanazalisha mazao kwa wingi mno na hasa pale Serikali inapotoa hamasa kwa wakulima kufanya hivyo. Serikali ichukue hatua ya utafutaji masoko kwa wakulima wetu hasa masoko ya nje mazao kama mahindi, maharage, viazi na kadhalika. Wakulima wetu wasaidie kutafuta masoko kwani kutofanya hivyo kuna shusha morari kwa wakulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ukulima kwa kanda *(zone)* Tanzania ina maeneo mengi ya ukulima wa mazao mbalimbali katika maeneo mbalimbali nchini, sasa tuanze mkakati wa kulima mazao kutokana na hali ya hewa husika katika maeneo husika. Mfano kuwepo na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kama *center* ya uzalishaji wa mazao ya chakula

na kuwepo na mpango mahsusi ambao utaleta kilimo cha tija. Pia yawepo maeneo mahsusi ya kilimo cha miwa kwa ajili ya kuondoa tatizo la sukari, pia maeneo mengine (kanda) kwa ajili ya alizeti, karanga, mawese ili kuondoa tatizo la mafuta ya kula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila eneo likipewa zao maalum na jitihada ziwekwe ili kila kanda ifanye jitihada za ukuzaji wa mazao mbalimbali. Kilimo cha namna hii kikipewa kipaumbele tutajinasua na upungufu wa chakula na pia kutoa malighafi kwa ajili ya viwanda vyetu ili kuongeza thamani mazao ya wakulima. Kilimo kiki-*link* na viwanda vyetu, lengo la Serikali ya viwanda litafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalishaji wa mbegu, Serikali iweke nguvu za kutosha katika utengenezaji wa mbegu za mazao. Mbegu imekuwa changamoto kubwa, ifike mahali ziwepo *center's* za utengenezaji mbolea hasa za kitafiti kutokana na ardhi mbegu hizo zinaenda kufanyiwa kazi.

MHE. HASNA S. K. MWILIMA: Mheshiwa Mwenyekiti, naomba nichangie Wizara hii muhimu sana na ndiyo uti wa mgongo wa Taifa kwani ni zaidi ya asilimia 80 ya Watanzania ni wakulima na ndiyo wanapata kipato chao. Wizara hii inategemewa sana tumaini la viwanda vya Tanzania vinavyotarajia kupata malighafi za kuendeshea viwanda vyao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pembejeo imekuwa ni tatizo kubwa sana kuna mikoa yenye misimu miwili na mikoa yenye msimu mmoja. Lakini sote tunatambua kuwa wakulima wengi wanaanza kuandaa mashamba mwisho wa mwezi wa nane au mwazo wa mwezi wa tisa. Lakini pembejeo hadi wakulima wamemaliza mashamba na mazao yameanza kuota hakuna pembejeo iliyopelekwa. Niombe Serikali chonde chonde tupelekeeni pembejeo kwa wakati ili wakulima wapate pembejeo za kupandia na kukuzia kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mbegu za ruzuku, huko nyuma tulikuwa na utaratibu wa kutoa mbegu za

ruzuku mfano, mahindi, mpunga alizeti, choroko, kunde na kadhalika. Leo hii mbegu hizo za ruzuku hazipatikani, niombe sana kwa Mheshimiwa Rais anataka viwanda vya mafuta vya ndani kwa nini sasa tutoe ruzuku msimu wa 2018/2019 kwa mbegu zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, alizeti, ufuta, michikichi, michikichi, niombe Serikali kwa kuwa Malaysia ilikuja kuchukua miche ya michikichi kutoka Kigoma. Kwa nini Serikali sasa isiombe Serikali ya Malaysia irudishe mbegu, miche ya michikichi ili basi na wakulima wa Mkoa wa Kigoma wanufaike na mbegu hizo kutoka Malaysia. Sambamba na hilo, tunaweza pia kuchukua mbegu za michikichi kutoka Burundi ili basi tuwe na aina tatu za aina ya michikichi ya kutoka Naliendele, Burundi, Malaysia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa na tatizo kubwa sana kwenye zao la tumbaku kwa wakulima wa Tarafa ya Nguruka, Kata ya Basanga, Itebila, Mganza na Nguruka, mfano kucheleweshwa, kutokana kwa makisio ya uzalishaji wa kilo na makampuni waliyoingia mkataba na wakulima, kwa mujibu wa sheria ya makisio yanatoka mwezi wa tatu na mwezi wa nne, hadi leo bado tunasikia makisio hayo ya kutoka mwezi wa Septemba, 2018. Kwa kuchelewesha makisio hayo kutasababisha mambo yafuatayo:-

Kwanza, kuchelewa kuagiza pembejeo, makisio hayo kutolewa mapema ndiyo benki wanajua wamekopesha wakulima kiasi gani, kwa kuchelewa kuna sababisha mkulima kulima chini ya kiwango cha makisio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la masoko, wakulima wamelima mazao mengi, mahindi, maharage, mbaazi mpunga na kadhalika. Tatizo kubwa ni soko, tuombe Serikali iwaruhusu wakulima kuuza mazao yao nje. Tanzania iko kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa nini sasa wakulima wasiruhusiwe kuuza mazao nje ya nchi hususani ndani ya nchi ndani ya nchi za Shirikisho la Afrika Mashariki. Kitendo cha kuwazuia wananchi kuuza mazao yao nje ni kosa kubwa wakulima hawa wanasomesha watoto wao, watoto

hawapewi pesa wakati na Serikali mmekataza mazao yasiuzwe nje ya nchi hii ni tatizo kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho niombe kumshauri Mheshimiwa Waziri sisi Wabunge wa Majimbo ndiyo wawakilishi wao, anapofanya ziara kwenye majimbo yetu tunapomtafuta tunahitaji kumpa changamoto zaidi za wakulima wetu, sasa anaacha kutupa taarifa za ziara zake ndani ya majimbo na kuacha kuwasiliana na sisi, matokeo yake anasema ya kwake na kupokea changamoto chache, changamoto kubwa za wananchi walio wengi hazipokei, tunaomba sana, atambue umuhimu wa Wabunge wenzake wa Majimbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. EDWARD F. MWALONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Njombe Mjini sasa wamepata zao la parachichi ambalo wananchi wamelipokea vizuri sana kila mwananchi sasa anashughulika na kilimo hiki. Wananchi hawa wa Jimbo la Njombe Mjini wanahitaji msaada kidogo sana wa Serikali, katika upatikanaji na usambazaji wa miche bora. Zao hili limepata soko kubwa sana nje ya nchi na hii itasaidia sana nchi yetu kuongeza pato la fedha za kigeni. Katika mauzo ya zao la parachichi nyenzo muhimu sana ni *pack house (cold storage)* ambazo mkulima hana uwezo wa kujenga na wanunuzi hawawezi kujenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali iangalie hili na inipe maelezo kwa niaba ya wakulima wa parachichi wa Jimbo la Njombe Mjini ni kwa namna gani inaweza kusaidia hili, Wizara iunde timu ya wataalam kusimamia kuendeleza zao la parachichi na kupima vihatarishi vyake ili tuweze kusaidia zaidi utaratibu wa masoko na mauzo kwa manufaa ya wakulima na nchi kupata fedha za kigeni.

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nnianze na masoko ya mazao. Kama tunavyojua wananchi zaidi ya asilimia 80 wanaishi vijijini na kule ndipo wakulima wa mazao tofauti walipo. Kwa mfano mkulima wa mahindi

anajitahidi analima, palizi, vibarua, dawa na kuvuna kwa kutumia fedha zake. Lakini Serikali inaweka bei elekezi ya kuuza mahindi na kwa sasa hivi bei ya mahindi imeshuka hadi shilingi 30,000 kwa gunia, isitoshe kama tujuavyo mahindi ya kisasa huwezi kuhifadhi bila dawa na ukitaka kuhifadhi bila dawa ni kutumia ma-*tank* ambayo ni ghali sana kuanzia magunia 100 tani ni shilingi milioni tatu mpaka shilingi milioni 2.8; sasa kwa kukatishwa tamaa huku mkulima anaweza kununua hiyo *storage?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamekuwepo na mazao kama nyanya na matunda mbalimbali, kwa nini Serikali (Wizara ya Kilimo na Wizara ya Viwanda) visiwawezeshe wakulima kupata viwanda vidogo vidogo vya kusindika mazao kule kule vijijini halafu wanavipeleke kwenye viwanda vya kati?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo Gairo kuna wakulima wengi sana wa nyanya wangeweza kusindika na nyanya na kupeleka kwenye Kiwanda cha *Tomato Sauce* kilichopo Iringa cha DABAGA, pia kuna kiwanda kinachoitwa DASH kipo Iringa lakini hakina malighafi ya kutosha na hii pia baadhi ya nyanya hazikidhi viwango, kuna haja ya wataalam (Maafisa Ugani) waende wakatoe elimu kwa wakulima na kuwashauri kuhusu mbegu bora na dawa zipi za kutumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo cha ndizi ni kati ya zao kubwa sana linalokubali katika mikoa ya Kilimanjaro, Kagera, Mbeya, Morogoro na kadhalika, lakini zao hili Serikali halijalichukulia kama zao linaloweza kutuingizia fedha za kigeni. Zao hili la ndizi kwa nchi kama Uganda wamekuwa waki-*export* kwenda nchi za Ulaya na zinauzwa kwa bei ya juu sana *peace* tano tu za ndizi ni sawa na *pound* za Uingereza tatu sawa na shilingi 9,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri sasa Serikali kutoa elimu pia jinsi ya ku-*pack* ili tuweze ku-*export* zao hili. Tukitumia Balozi zetu kwenye Kitengo cha Biashara watafute masoko kule ndio kazi yao. Hili liende sambamba na matunda kama parachichi, maembe na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhaba wa pembejeo na ukosefu wa mbegu bora hili limekuwa ni tatizo sasa. Kila hotuba ya bajeti tumekuwa tukiulizia suala hili na yote haya yanasababishwa kwa nchi kushindwa kuzalisha mbegu na viwanda vya pembejeo. Ushauri tunaweza kushirikisha jeshi, wafungwa kwa kutumia wataalam tukazalisha mbegu zetu na zenye ubora, Serikali iwajali wakulima.

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na mkakati wa zao la michikichi Mkoa wa Kigoma. Mwezi Februari, 2017 Serikali ya Mkoa wa Kigoma kupitia kikao cha *RCC* ilipitisha mpango wa kuendeleza zao la michikichi. Mpango huu ulikuwa na shabaha ya kuongeza uzalishaji wa mafuta ya mawese nchini mpaka tani 400,000 kw mwaka kwa kulima hekta 100,000 za michikichi katika Wilaya tatu za Mkoa wa Kigoma. Mpango huu ungewezesha kufunguliwa kwa viwanda vya kati nane vya kusindika mawese na mazao ya mawese na mazao na kutengeneza ajira 6,400. Mpango huu ungewezesha familia 100,000 kulima michikichi kwa kila familia hekta moja(ekari 2.5) na kuongeza kipato cha familia kwa jumla ya shilingi za Kitanzania 13,000,000 kwa mwaka na hivyo kuwaondolea kwenye umaskini watu 600,000 na kuwafikisha kwenye kipato cha kati ndani ya miaka mitatu tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango huu pia ungewezesha Tanzania kutoagiza tena mafuta ghafi kutoka Malaysia na Indonesia na kuokoa shilingi dola milioni 294 (shilingi bilioni 646) ambazo Tanzania hutumia kila mwaka kuagiza mafuta hayo. Ukijumlisha uzalishaji wa alizeti na mawese nchini, mpango huu ungewezesha Tanzania kujitoshereza kwa mafuta ya kula na ziada nje ili kupata fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa mpango huu unahitaji dola milioni 45 tu na Benki ya Maendeleo ya Afrika ina *facility* hiyo ya uzalishaji wa mafuta ghafi ambapo Mkoa wa Kigoma uliomba Serikali iombe huko ili kupata mbegu, kutoa mafunzo ya ugani na kuandaa sheria ndogo za

Mahakama za Serikali za Mitaa kuwezesha mkakati hu kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Kilimo haijachukua hatua yoyote katika kusaidia Mkoa wa Kigoma kutekeleza Mpango huu, hata barua kutoka Ofisi ya Rais, Mkoa wa Kigoma haijajibiwa na Wizara na Waziri wa Kilimo na Chakula hajakanyaga Mkoa wa Kigoma tangu aanze kazi licha ya kuwa ndiyo Mkoa pekee nchini haujawahi kupewa msaada wa chakula tangu dunia iumbwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naisihi Serikali iusaidie Mkoa wa Kigoma kutekeleza mkakati wa michikichi kupitia mpango wa kuendeleza zao la mchikichi ili nchi ipone kutoka kwenye kuagiza mawese na mafuta ya kuzalisha sabuni ambayo ni *by product* ya michikichi kupitia mafuta ya mise.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri Wizara za Fedha, Kilimo na Viwanda zikae na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kigoma ili kuweka mkakati wa utekelezaji wa mpango huu ili ifikapo mwaka 2022 Tanzania iwe muuzaji *(net exporter)* wa mafuta ya kula badala ya kuwa muagizaji *(net importer).* Ahsante sana.

MHE. JOSHUA S. NASSARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza kwa yale mliyofanikiwa ndani ya Wizara lakini pia nawapa pole kwa yale ambayo yamekwama kwa namna moja ama nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *one thing,* wananchi kwenye maeneo ya milimani waliokuwa wanalima zao haramu la bangi kama zao la biashara na hivi ndivyo ambavyo wameweza kusomesha watoto na kujikimu kimaisha. Serikali kupitia Bodi ya Pareto waliahidi kuanzisha zao hili kama zao mbadala na iliahidiwa kuwa elimu ingetolewa na miche ingetolewa mapema mara tu mvua za masika zitakapoanza. Mvua zilianza mwanzoni na katikati ya mwezi Machi lakini mpaka mwezi wa nne bado hakukuwa na lolote. Tafadhali naomba kauli ya Wizara katika hili ukizingatia kilimo cha bangi kilikuwa kwa sababu za kibiashara hususan kwenye

nchi jirani na walikuwa wakitegemea kilimo hiki kwa *livelihood* yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *otherwise, all the best.*

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wa tumbaku wanapitia kipindi kigumu sana kuhusu masoko na bei ya zao hili. Najua kuwa Serikali inafanya kila njia kuwasaidia wakulima katika hili. Pamoja na hayo wawakilishi wa wakulima wa tumbaku Kusini mwa Ikweta walikaa Lilongwe nchini Malawi na kutoa azimio la pamoja lenye maslahi ya kuwalinda wakulima. Serikali italeta azimio hilo Bungeni lini ili Bunge liweze kuridhia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sana Serikali ifanye haraka kuleta azimio hilo Bungeni. Naunga mkono hoja.

MHE. JOSEPH L. HAULE: Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe nichangie kidogo kwenye Wizara hii nyeti ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mawakala wa pembejeo, Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa maelezo Bungeni kuwa wanafanya uhakiki wa mawakala wanaopaswa na kustahili kulipwa. Je, hili suala limefikia wapi na lini mawakala hawa wa pembejeo watalipwa stahiki zao maana wengi wamefilisika na wengi wanakufa maskini huku haki zao zikiwa mikononi kwa Serikali.

MHE. ANATROPIA L. THEONEST: Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa dawa za kuua wadudu ni changamoto hasa vijijini, dawa hizi pia zitolewe kama ruzuku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa pembejeo za kilimo kama mbolea katika Wilaya hasa Wilaya ya Kyerwa bado ni changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *power tiller* zitolewe wa mkopo katika vikundi na walipe kidogo kidogo kwa wakati tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uimarishaji wa masoko ya mazao ya wakulima hasa yale yanayooza kama nyanya, matunda na kadhalika. Wananchi wamezidi kupata hasara kwa kuwa haya mazao yanakuwa hayatunzwi muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuendeleza zao la maua *(hot culture)*. Hii ndiyo namna kuu tutakayoweza kupata pesa ya kigeni na soko lake liko tayari hasa nchi za Ulaya kama wafanyavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo kubwa la mnyauko katika zao la mgomba (Wilaya ya Kyerwa). Ni kiwango gani Wizara imejipanga kusaidia wakulima hawa kutokomeza tatizo. Sambamba na hilo wananchi wanaokutwa na migomba iliyo nyauka wamekuwa wanatozwa *fine.* Hii ni sawa na kuweka chumvi kwenye kidonda.

MHE. BENARDETHA K. MUSHASHU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri kwa kazi nzuri mnayoifanya kwenye kilimo na ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo ni muhimu sana katika kuleta maendeleo ya Mtanzania. Huwezi kuleta maendeleo ya Tanzania kama wakulima ambao ni asilimia 70 watakuwa wamekosa kuendelezwa/wameachwa nyuma. Kwa sasa kilimo kinacholimwa hakina tija, bado wanatumia zana duni kama jembe la mkono, hawalimi kitalaam, wanalima kilimo cha kujikimu siyo kilimo cha biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji tuwe na Maafisa Ugani ili waweze kuwaelimisha/kushauri wakulima.Kuna upungufu mkubwa sana wa maafisa ugani. Mkoa wa Kagera tuna upungufu wa Maafisa Ugani takribani 500 lakini wako ngazi ya kata. Kata moja ina vijiji vitatu mpaka sita, hana vitendea kazi hana hata pikipiki, atawazungukia vipi wakulima? Napendekeza waajiriwe Maafisa Ugani kwenye ngazi ya kila kijiji. Hawa wakitosheleza wakafanya kazi yao ya ugani, tutainua kilimo, tutapata malighafi ya viwanda katika uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei ya kahawa ni mbaya sana, kilo moja inauzwa kwa shilingi 1,000. Mbuni ukiupanda utatumia miaka miwili mpaka mitatu kuanza kuzaa kahawa. Zikianza kuzaa unaulea mbuni kwa mwaka mzima ukipalilia, ukiweka mbolea, unapulizia dawa unaishia kupata shilingi 1,000 tu kwa kilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu mkulima wa kahawa ameendelea kuwa maskini kwa sababu ya bei ndogo ya kahawa. Amekata tamaa ya kuendelea kulima kahawa. Serikali imependekeza kuondoa tozo 21 zifutwe. Nawaunga mkono hoja kwa hili lakini ili haya yasibakie kwenye makaratasi tu, baada ya bajeti hii. Wawakilishi wa wananchi (Wabunge) kutoka maeneo yanayolima kahawa tukutane na watalaam, tupitie mpango mkakati wa kupandisha bei ya kahawa kiukweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndizi kwa mtu wa Kagera ni zao la chakula, ni zao la biashara ya migomba imeshambuliwa na ugonjwa mbaya wa mnyauko, ni janga. Wakulima wanashauriwa mgomba ukigundulika una mnyauko, anaambiwa kata/ng'oa/zika. Matokeo yake mashamba yamebaki yakiwa wazi/matupu.Migomba imeisha sababu ya kung'olewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo miche ya migomba isiyoshambuliwa na mnyauko. Kwa kiasi kikubwa wanategemea maabara ya Arusha ni mbali sana na Kagera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kagera kuna Kituo cha Utafiti cha Maruku ambao wanao watalaam lakini hawana maabara kubwa, wanategemea Arusha. Naomba ili kumsaidia mkulima wa Kagera kumuondolea umaskini zitolewe fedha nyingi za kutosha, ili Kituo cha Utafiti cha Maruku waweke maabara kubwa. Wazalishe *tissue*, *culture*. Miche safi isiyo na vimelea vya mnyauko isambazwe kwa wakulima wengi waondokane na gonjwa baya la mnyauko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. QAMBALO W. QULWI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ushirika bado unakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo ubadhirifu wa mali za vyama vya ushirika uliofanywa na baadhi ya viongozi na wanachama wasio waaminifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *Ayalabe SACCOS* Wilayani Karatu, fedha za ushirika zilifujwa miaka zaidi ya sita iliyopita na hadi sasa hakuna majibu. Waliohusika kupoteza fedha hizo wanafahamika maana fedha zilitoka benki ya *TIB* na kuingia kwenye *account* zao. Hapa wezi si wako wazi lakini kwa kuwa wezi wana mtandao ndani ya Wizara bado wameendelea kulindwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanachama wa *SACCOS* hii pamoja na viongozi wa Wilaya wamelalamikia sana na *SACCOS* hii kwamba imeendelea kudorora na wananchi wanakosa imani kabisa na vyama vya ushirika. Leo hii Serikali inajitahidi kufufua ushirika lakini wananchi hawaelewi kutokana na mifano hii mibaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mrajisi wa Vyama vya Ushirika anatuhumiwa sana na wanachama wa *Ayalabe SACCOS* kama ndiye anayewalinda wezi hao. Najua jambo hili liko mezani kwa Naibu Waziri wa Wizara hii. Niishauri Wizara ilifanyie kazi tatizo hili ili haki itendeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo ardhi nzuri na hali ya hewa nzuri kwa zao la alizeti. Hatuna kabisa sababu ya kuagiza mafuta nje wakati tungeweza kulima wenyewe na kuwasaidia wananchi wetu. Serikali iwapatie wananchi mbegu bora ya alizeti.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote kwa kuandaa hotuba na kuleta hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makampuni ya tumbaku Mkoa wa Tabora yanaendelea kupunguza makadirio/makisio ya tumbaku kila mwaka. Msimu wa mwaka 2017/2018 makisio yalishuka kutoka tani 13 hadi tani 10, na msimu huu

wa mwaka 2018/2019 zipo dalili za makisio kushuka zaidi wakati wakulima wameshakopa benki, wakapata pembejeo na sasa wanakosa soko kwa kukosa makisio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali/Waziri inasaidiaje wakulima wa tumbaku inayoendelea kuvunwa wakati hawana uhakika wa soko?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeelezea juu ya kununua mbolea kwa pamoja na kusambaza kwa bei ya ruzuku. Pamoja na kuja na mfumo huu, bado tatizo la upatikanaji wa mbolea kwa wakati na kwa bei elekezi na ya kutosha ni tatizo kubwa sana. Serikali itueleze ni mfumo gani umewekwa kwenye Wilaya zetu wa kuhakikisha mbolea hii ya ruzuku inawafikia wakulima na kwa wakati kwa bei elekezi na ya kutosha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2017/2018, tumbaku ya Kaliua zaidi ya tani milioni tano zimeuzwa kwa bei ya makinikia, USD 0.073 hadi 0.070 baada ya bei elekezi ya USD 2 hadi 2.5. Wakulima wengi wamebakiwa na madeni makubwa ya benki na taasisi za fedha. Wengi wao wameshindwa kuingia kwenye kilimo cha tumbaku na wana hali mbaya. Tunaiomba Serikali iwasaidie wakulima hawa ili waweze kunyanyuka tena na kuingia kwenye kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali mwaka jana iliruhusu chini ya tani wanunuzi wa mazao chini ya tani moja wasilipe kodi, hili limekuwa ni tatizo na pia kunyima mapato Halmashauri za Wilaya zinazotegemea kilimo na mazao kama chanzo cha mapato. Wanunuzi wanasafirisha gunia 10 mpaka 15 bila kulipa ushuru hivyo wanabeba kidogo kidogo ili wasilipe ushuru. Serikali mnasaidiaje Halmashauri za Wilaya kupata mapato kupitia ushuru wa mazao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kila Mkoa kuna mazao ya kimkakati ya biashara ambayo ndiyo yaliyosaidia kuinua uchumi wa mikoa hiyo. Mazao mengi yaliyotegemewa yamedorora na mengine hayalimwi kabisa kwa kukosa msukumo wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kahawa-Kilimanjaro, kokoa-Mbeya, minazi-Pwani, korosho-Kusini, ndizi-Bukoba, zabibu-Dodoma, tumbaku-Tabora, mawese-Kigoma na kadhalika. Serikali itupe maelezo ni mikakati gani ya uhakika kuhakikisha maeneo haya yanayotegemewa kuinua uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo kandarasi waliongia mkataba na Serikali kwa ajili ya kujenga ma-*godown* kwa ajili ya mazao, wengine hawajalipwa tangu mwaka 2016. Wapo waliojenga ma-*godown* saba tangu mwaka 2016 mpaka leo hawajalipwa na wanadai kwa miaka yote bila kulipwa. Pia mawakala wa kusambaza pembejeo za kilimo hawalipwi kwa wakati. Serikali ilieleze Bunge mpango wa kulipa madeni yote ya kandarasi waliokopwa miaka mingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna kilimo cha uhakika bila ushirika wenye nguvu. Serikali iweke utaratibu endelevu wa kukagua Vyama vya Ushirika *(AMCOS)* mara kwa mara ikiwezekana kila robo ya mwaka. Waziri apewe taarifa za ukaguzi wa ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, mafunzo yatolewe kwa uongozi wa ushirika ili waongoze *AMCOS*/ushirika kwa ufanisi na uaminifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imejipangaje kuongeza uzalishaji wa mazao kwa kuhakikisha tunaongeza hekta za umwagiliaji kufikia hata hekta milioni moja kwa mwaka 2020? Tangu mwaka 2013 mpaka leo hata nusu hatujafika. Kilimo chetu kwa asilimia zaidi ya 80 tunategemea mvua. Kuna mabadiliko ya tabianchi, mvua hazieleweki. Serikali itueleze inajipangaje kwenye sekta ya umwagiliaji na kuwasaidia wakulima kuelekea uchumi wa viwanda?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu masoko, Serikali inahamasisha wananchi walime, wanaingia benki wanachukua mikopo, wanaweka nyumba zao *bond,* wakizalisha hakuna masoko. Ili kupata masoko ya uhakika, tunahitaji wataalam ambao watatembea duniani kuangalia fursa za masoko kwa mazao ya aina mbalimbali. Kuna

mpango gani wa haraka kuhakikisha mazao ya mahindi, karanga pamoja na mbaazi ambayo yamekosa soko yanapata masoko.

MHE. MUHAMMED AMOUR MUHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenye - Enzi – Mungu, mwingi wa rehema kwa kuniwezesha kuchangia hapa hoja iliyopo mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ninapenda nikupongeze wewe mwenyewe kwa namna unavyosimamia Bunge hili kwa umakini mkubwa sana. Ninaomba nizungumzie mambo yafutayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mazao ya mahindi na mbaazi, msimu huu mazao haya yamepatikana kwa kiasi kikubwa, ni hawa wakulima wetu wamelima kwa ajili ya mahitaji tofauti kama kujikimu, kusomesha, kutibu watoto, kujenga na kadhalika, hivyo inakuwaje wananchi wanazuiliwa kuuza mazao yao nje ya nchi? Si jukumu lao wananchi kuhakikisha kwamba nchi ina chakula cha kutosha, huu ni wajibu wa Serikali. Hivi sasa mbaazi zinauzwa shilingi 100 hadi 150 kwa kilo moja, wapi tunakwenda? Mahindi nayo hayana soko, hayatakiwi. Ni vyema Serikali ikafikiri zaidi kuhusu suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuje kwenye zao la kahawa, ni vyema tungeongeza nguvu kwenye zao hili, tulikuwa tukipata fedha za kigeni. Ni vyema Serikali ingesimamia kwa umakini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ya kuweka pembejeo na mawakala, mawakala wa pembejeo wametiwa umaskini na Serikali bado imekaa kimya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu korosho, mpaka sasa hatujawa na soko la uhakika la korosho. Ni vyema Serikali ingehangaika ili kuhakikisha kwamba tunapata masoko ya uhakika kwa wakulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kusimamia wakulima, ni vyema Serikali ikasimamia kwa umakini mkubwa kuhusu wakulima, si waachiwe walime tu. Ni vyema wakasimamiwa ili waweze kulima na tija iwe kubwa zaidi, matumizi ya ardhi kuhusiana na kilimo bado yako chini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema Serikali ikahangaika kutafuta masoko ya kuuzia bidhaa zetu ndani na nje ya nchi yetu. Wakulima wamekuwa wanavuna mazao yao kwa wingi ila hawana pa kuyauza, yanawaozea mikononi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si vyema Serikali kubaki na maneno tu. Watu wanaumia, hawana pa kuuza mazao yao. Ni hatari, yanawaozea mikononi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwa maandishi. Kwanza niipongeze kazi nzuri inayofanywa na Waziri, Mheshimiwa Dkt. Tizeba na Naibu wake Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa ya kuiongoza Wizara ya Kilimo kwa umahiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri, Wizara iongeze kasi katika kuhimiza uwezeshaji wa kuzalisha *high nutritional value crops* kama mboga na matunda kwa ajili ya kuimarisha lishe ya jamii. Viazi lishe vyenye *vitamin 'A'* kwa wingi, mbegu yake inatafutwa na wananchi wengi lakini haipatikani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Wizara iwezeshe uzalishaji wa mbegu za viazi lishe ili iweze kupatikana kwa wingi, wananchi waipande na kutumia viazi hivi ili kuimarisha lishe zao. Inasikitisha na kushangaza kuona mboga mboga kama karoti, nyanya na pilipili hoho zinaingia nchini kutoka nchi jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iielekeze Idara za Mipango Miji katika Halmashauri zetu ili Halmashauri ziweze

kutenga maeneo ya kutosha katika miji na vijiji kwa ajili ya *urban farming* ili wakulima na hasa vikundi vya vijana, waweze kulima mboga na matunda ambayo yatawezesha upatikanaji wa malighafi kwa viwanda vidogo mijini na vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maafisa Ugani wahimizwe kwenda kwa wakulima badala ya kubaki ofisini. Wakatoe elimu ya mbinu za kilimo bora, jinsi ya kupambana na visumbufu vya mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. TUNZA I. MALAPO: Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la wakulima wa korosho kuuza korosho zao katika minada tangu mwezi Novemba, 2017 mpaka leo hawajalipwa fedha zao linasababisha wakulima hawa kukosa fedha kwa ajili ya kujikimu, kusomesha watoto wao na pia kuandaa mashamba kwa wakati kwa ajili ya msimu wa mwaka huu. Je, Serikali imeshindwa kulisimamia suala hili ili wakulima hawa wapate fedha zao kwa wakati kwa ajili ya kutatua shida zao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukosefu wa mbegu bora za mazao mbalimbali unasababisha wakulima kupata mavuno kidogo ikilinganishwa na nguvu inayotumika kulima kwa sababu tu ya kukosa mbegu bora. Pia hata zikipatikana basi bei inakuwa kubwa sana ambayo mkulima wa kawaida anashindwa kumudu kununua. Ni upi mkakati wa Serikali wa kuhakikisha wakulima wa mazao mbalimbali hapa nchini wanapata mbegu bora kwa ajili ya kufanya kilimo chenye tija?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kilimo cha umwagiliaji kinaleta tija? Mfano katika Mkoa wa Mtwara kuna bonde kubwa katika Kata ya Kitere, Mtwara Vijijini ambalo kama lingetumiwa vizuri lingesaidia uzalishaji wa kutosha wa zao la mpunga na kuwawezesha wananchi kujipatia chakula na kipato. Pia bonde hilo lingewezesha kulima mboga mboga kwa ajili ya biashara na matumizi mengine ya kifamilia. Ni nini mkakati wa Wizara

utakaoleta tija kwa wakazi wa Mkoa wa Mtwara wenye mabonde yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji, kama vile Kitere, Mahurunga na Ruvuma?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupata ufafanuzi juu ya madeni yanayodaiwa na mawakala waliosambaza pembejeo za kilimo, kwa sababu kuna kauli zinazochanganya kutoka upande wa Serikali na mawakala, nani ni mkweli? Mawakala wanasema wanadai madai halali wakati Serikali inasema mawakala waongo. Je, Serikali imebaini nini baada ya kufanya uhakiki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini Serikali imeshindwa kutoa bure pembejeo ya zao la korosho, ikizingatiwa kwamba zao hili linachangia pato la Taifa hili la Tanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo la wakulima wa korosho kucheleweshewa malipo yao yaliyopitia benki, kwa hiyo nashauri Serikali kuzitaka benki kuwalipa wakulima mara moja pindi tu wanunuzi wanapolipa hela za wakulima.

MHE. JOYCE J. MUKYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia pia katika Wizara ya Kilimo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, masoko bado ni changamoto kubwa kwa wakulima hapa Tanzania. Tanzania imezidi kuwa nyuma katika udhibiti wa masoko ya mazao ya kilimo kutokana na masharti magumu ya usafirishaji nje ya nchi. Hata katika taarifa ya Benki ya Dunia *(WB)* nchi yetu inaonekana ipo nafasi ya 56 kati ya nchi 62. Hii inasababishwa na ugumu wa kupata vibali vya kusafirishia mazao hayo nje ya nchi hii. Kwa Tanzania inachukua hadi siku zaidi ya 20 ili kukamilisha tararibu zilizopo ili kuweza kupata vibali wakati kiutaratibu kwa nchi zilizizopo Kusini mwa Jangwa la Sahara zinahitajika siku si zaidi ya sita kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naishauri Serikali ikazane kupunguza vikwazo kwenye upatikanaji wa vibali vya kusafirishia mazao nje ya nchi ili wakulima wa Tanzania

pia waweze kufaidika na sekta hii ya kilimo. Uchumi wa Tanzania utatengemaa zaidi kama sekta ya kilimo itakuwa nzuri. Tukumbuke wakazi wengi wa Tanzania wanaishi vijijini na huko ndiko msingi wa kilimo ulipo. Wakulima wengi wanalima na kuishi vijijini, lakini cha kushangaza huko ndiko kuna matatizo kila siku. Kama uchumi kupitia kilimo ungekuwa mzuri hata maisha ya wananchi waishio vijijini yangekuwa na ahueni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalishaji wa mazao ya mbegu za kilimo nchini bado ni changamoto kubwa. Nasema hivyo kwa sababu Serikali imetumia pesa nyingi sana kufanya uzalishaji huu lakini wakulima wengi hawana taarifa au hawajapata elimu ya kutosha kuhusiana na mbegu hizi ambazo nyingi sifa yake kubwa ni kuhimili ukame na kuzalisha mavuno mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Wizara ya Kilimo kutoa elimu ya kutosha kwa wakulima wa Tanzania ili mbegu hizi ziweze kutumika na hatimaye kuongeza kipato pamoja na mavuno mengi ya mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo makubwa ya ardhi yanamilikiwa na wakewezaji wachache, hii ni kwa ajili ya wakulima wadogo wengi kukosa kipato cha kutosha cha kumiliki ardhi na hivyo kukosa ardhi ya kutosha ya kufanya kilimo. Ugawaji wa ardhi umekuwa ukifanyika bila kumilikisha wenyeji wa maeneo husika na kusababisha tatizo kubwa la migogoro ya ardhi ambavyo hata Serikali imeshindwa kutatua katika sehemu nyingi hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kuhusisha wenyeji wa maeneo husika wakati wa kumilikisha na kununua ardhi ili kutoa haki kwa kila mtu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na tatizo kubwa katika utoaji wa mikopo nchini, wakulima wadogo wadogo wamekuwa wakikosa fursa ya kupata mikopo katika taasisi mbalimbali za kifedha ili waweze kuwekeza kwenye kilimo,

na hii inatokana na wananchi wengi kutokuwa na hatimiliki ya ardhi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri na kuisisitiza Serikali kupeleka mikopo kwa wakulima wadogo hasa wa maeneo ya vijijini ambako ndiko wakulima wengi walipo.

MHE. CATHERINE N. RUGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya kilimo mwaka 2018/2019 Serikali ya CCM haina dhamira ya dhati kuendeleza kilimo na haina mpango wa kuwasaidia wakulima. Lengo la MKUKUTA lilikuwa kwamba sekta ya kilimo ikue kwa asilimia sita mpaka asilimia nane kwa mwaka kwa miaka 10 mfululizo ili Watanzania wa vijijini waondokane na umaskini. Hata hivyo hali halisi ni kuwa kati ya mwaka 2011 – 2015 sekta ya kilimo ilikuwa ni wastani wa asilimia 3.4 kwa mwaka. Mwaka 2016 na 2017 miaka miwili ya Serikali ya Awamu ya Tano kilimo kilikua kwa asilimia 19 mwaka 2016 na 2017 ni asilimia 1.3.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalishaji wa mazao yote makuu isipokuwa korosho umeshuka katika mwaka 2016/2017; kahawa uzalishaji umeshuka kutoka tani 760,000 mwaka 2015 mpaka tani 48,000 mwaka 2017; pamba imeshuka kutoka tani 50,000 mwaka 2015 mpaka tani 48,000 mwaka 2017; tumbaku imeshuka kutoka tani 87,000 mwaka 2015 mpaka tani 61,000 mwaka 2017 na chai imeshuka kutoka tani 33,000 mpaka tani 27,000 mwaka 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata mazao ya chakula; wakati mahindi uzalishaji umeongezeka kutoka tani milioni 6.1 mwaka 2016 mpaka tani milioni 6.6 mwaka 2017, bei ya mahindi imeporomoka sana kufuatia Serikali kuzuia mahindi kuuzwa nje ya nchi na Serikali yenyewe kutonunua mahindi kwa ajili ya ghala la Taifa. Hii ni kwa sababu *NFRA* haikuwepewa fedha za kununua mahindi na hivyo Serikali kuwapa umaskini wananchi na wafanyabiashara wa mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya Wizara ya Kilimo imezidi kushuka, kwa mfano mwaka 2017/2018 pesa zilizoidhinishwa na Bunge zilikuwa shilingi bilioni 221.10. Mwaka

2018/2019 Wizara inaomba kuidhinishiwa na Bunge shilingi bilioni 170.27, hii ni pungufu ya asilimia 23 kulingana na bajeti ya mwaka jana. Hii sio sawa ukizingatia umuhimu wa sekta hii ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kushauri mambo yafuatayo:-

Moja, kwa ajili ya kujenga uchumi shirikishi ni muhimu kufanya jitihada za makusudi kuhakikisha kwamba kilimo chetu kinaanza kuchangia vya kutosha katika ukuaji wa uchumi. Serikali iweke shabaha ya kufuatilia ukuaji wa asilimia nane wa sekta ya kilimo.

Mbili, Serikali lazima itambue kuwa kilimo ndiyo shughuli kuu ya kutokomeza umaskini. Shughuli za kilimo ziendeshwe na wananchi wenyewe kwa kuwawezesha kumiliki ardhi, kuongeza tija na kupata mitaji.

Tatu, Serikali itunge *stable fiscal regime* katika sekta ya kilimo na kuhakikisha kwamba mkulima anabaki na sehemu kubwa ya mapato baada ya mavuno ya mazao yake.

Nne Serikali iunde mamlaka ya kilimo itakayosimamia sekta ya kilimo na kutekeleza mikakati yote ya maendeleo ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano na mwisho, Serikali ihusike kikamilifu kwenye uhifadhi wa mazao kupitia soko la bidhaa *(commodities exchange)* ambao utashirikisha vyama vya wakulima na hivyo kufuta *middle men*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

MHE. RASHID ALI ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu sekta ya kilimo inabebea asilimia 65.5 ya Watanzania ni lazima Wizara itoe kipaumbele ili kutoa au kupunguza umaskini kwa wakulima na kuongeza pato kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukuaji wa kilimo hauridhishi hata kidogo, inasikitisha tangu tupate uhuru mwaka 1961 huu ni mwaka wa 57 bado kilimo kinasuasua. Ili kupunguza umaskini ilikuwa ni lazima kilimo kikue kuanzia asilimia 8 hadi 10 hadi sasa. Huu ni mwaka wa 57 kilimo kinakua kwa asilimia 2.7 hadi 3.0. Ni lini tutapunguza umaskini wakulima wetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, uelekezaji katika kilimo, Serikali bado haijaamua na kuonesha nia ya kupunguza umaskini kwa wakulima; bajeti inapungua kila uchao. Inasikitisha kuona nchi kama Rwanda imewekeza jumla ya dola bilioni 32 na Tanzania kushindwa kufanya uwekezaji wa kuwapunguzia wahusika umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tuwe na tahadhari na umakini mkubwa katika kilimo. Jambo la kwanza ni lazima kuwa na watafiti wa kutosha kuwa na vyombo vya kilimo kama *tractor* na *power tillers,* kutumia ardhi kitaalam; kwa mfano tunazo hekta 1,955,270 zinazohitajika kulimwa. Hata hivyo jambo la kusikitisha ni hekta 13,915 zimelimwa na *tractors* na *power tillers.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko hekta 3,404,494, hizi zinalimwa na wanyama na hekta 8,560,517 zinalimwa kwa jembe la mkono. Kwa takwimu hizi ni wazi kwamba Wizara ya Kilimo haijajiandaa kwa ajili ya kupunguza umaskini kwa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhuru wa wakulima, wakulima lazima wapewe uhuru wa kuuza mazao yao yote. Kama Serikali wanahitaji basi iweke mazingira ya soko la ndani ili wakulima waweze kuuza mazao yao na kupata faida.

MHE. MUSSA R. SIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Wizara kwa hotuba iliyoeleza uhalisia na changamoto zinanojitokeza katika kukamilisha utekelezaji wa miradi. Naiomba Serikali ifuate yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, iongeze bajeti ya kilimo hasa kwenye miradi ya maendeleo kwa sababu bajeti iliyopo ni

ndogo kulinganishwa na ya mwaka 2017/2018. Mazao yote ya kibiashara yapatiwe masoko ndani na nje ili kukidhi mahitaji ya wakulima na kuinua uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na uhaba wa pembejeo na mbegu bora, kwa mfano zao la alizeti. Tunaiomba Serikali kuhakikisha inaondoa uhaba huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna uhaba mkubwa wa maafisa ugani pamoja na vitendea kazi. Tunaiomba Serikali iajiri na kuleta vitendea kazi.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na nia njema ya Serikali kumekuwa na changamoto nyingi sana kwenye sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye zao la korosho kuna maswali ambayo bado hayajapata majibu. Kuna mkakati gani wa Serikali wa kuhakikisha uzalishaji wa korosho unaongezeka? Hivi mwisho kabisa wa matumizi ya *sulphur* ni nini? Kwa nini utafiti ulifanyika taratibu magonjwa mengine ya korosho tukatumia viatilifu vingine ili kuweza kuongeza uzalishaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa za kampeni za *hammers* kuhujumu usambazaji wa *sulphur* liko kila mara, lakini bado hao hao ndio wanapewa *tender* kila mwaka ya kusambaza viatilifu. Hujuma za msimu uliopita zilitosha kampuni hii isipewe kazi hiyo na wahusika wachukuliwe hatua.

Mheshimiwa Mwwenyekiti, kuhusu suala la malipo ya wakulima, kuna tatizo kubwa sana juu ya malipo ya wakulima juu ya kupokelea pesa zao benki. Bado wananchi hawa wanatakiwa kupewa elimu ya kutosha. Suala lingine ni ucheleweshwaji wa malipo kwa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusimamie sana wanunuzi ili wawalipe wakulima mapema, itasaidia kuepukana na hujuma ya kangamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa ni kuhusu soko na uuzaji wa ufuta. Kuna mkanganyiko mkubwa sana juu ya biashara hii. Tunataka kushauri kwamba suala la ufuta kuingizwa kwenye stakabadhi ghalani litaleta usumbufu mkubwa sana. Unyaufu sio suala la kufumbia macho kabisa litaleta shida kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufuta ni zao ambalo lina nyauka kwa haraka sana, suala hili linahitaji utafiti mkubwa sana.

MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimpongeze Waziri pamoja na timu yake yote kwa kazi nzuri wanayoifanya pamoja na hotuba iliyojaa matumaini ya kuendeleza wakulima na hatimaye kuvuna mazao yenye tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kahawa ni zao kuu la biashara ambalo linaingiza pesa za kigeni, lakini zao hili sasa hivi ni zao ambalo haliangaliwi wala halina tija tena. Hivyo basi niishauri Serikali yangu ipeleke miche ya kutosha ya kahawa ili kuweza kufufua zao hili na pia zipelekwe pembejeo pamoja na zana zote zinazohitajika katika kilimo hicho. Pamoja na hayo Serikali ihakikishe inawapa miche bure kuisimamia kwa karibu. Pia Serikali inatakiwa itafute masoko ili mkulima huyu aweze kupata bei nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unavyojua zao la kahawa lina hatua nyingi, mpaka kufikia kuvuna na kuuza inakuwa imegharimu pesa nyingi. Kwa hiyo, bila kutafuta soko zuri wakulima hawa watakata tamaa na kuacha kabisa kulima zao hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Lushoto ilikuwa inatoa zaidi ya tani 300,000 lakini zao hili limeshuka. Kwa sasa huwezi kupata hata tani 50 kwa msimu na bado uzalishaji unazidi kushuka. Yote haya yanasababishwa na kushuka kwa bei ya zao hilo na wakulima kuacha kahawa ife yenyewe mashambani. Pia mibuni mingi ni ya zamani kwa hiyo imezeeka na kufa na kuzaa mazao kidogo sana. Hivyo basi

kuna uhitaji mkubwa sana wa kupeleka miche ya kutosha katika Wilaya ya Lushoto ili kufufua zao hili ambalo ndilo mkombozi wa wananchi wa Lushoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Lushoto ni Wilaya ya wakulima wa mboga mboga na matunda na katika Halmashauri ya Lushoto mapato mengi yanatoka huko. Hivyo basi ipo haja kubwa ya kuwaangalia wakulima hawa ili nao waweze kupata pembejeo au kuwapunguzia bei ya dawa kwani wakulima wananunua dawa kwa bei ya juu sana na ukizingatia magonjwa ya mboga mboga yanaongezeka kila kukicha hasa huu ugonjwa wa *kantangaze* unasumbua sana wakulima hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili mkulima aweze kulima kwa uhakika kama Ilani ya Chama chetu inavyosema, kwamba kilimo ndio uti wa mgongo, ni lazima tuwaandalie wakulima wetu mazingira ya kila hitaji.

Kwanza, lazima kujengwe mabwawa ya kutosha kila kijiji ili waweze kulima kilimo cha umwagiliaji; pili, lazima wapate zana za kilimo kwa wakati; tatu, pia lazima watengenezewe miundombinu ya barabara ili wasafirishe mazao yao kwa wakati na nne, kuwapatia pembejeo za wakati. Yakizingatiwa yote haya naamini yatatimiza ndoto yetu ya kuelekea kwenye uchumi wa viwanda na viwanda vyetu kupata malighafi katika mazao yetu haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala la kurudisha vyama vya ushirika. Hili suala litakuwa ni gumu sana kusimamia kwani ushirika hawa ndio waliotufikisha hapa tulipo na ushirika hawa wana madeni makubwa sana na imefikia hatua benki zimefilisi baadhi ya mali za vyama hivyo. Leo hii mnataka ndio wanunue mazao ya kulima, hili ni suala ambalo wakulima wamelikataa, kuuza mazao yao katika vyama hivyo. Suala hili lingewezekana kama Serikali ingejenga imani kwanza kwa wakulima na kwa kutoa elimu mpaka hapo wananchi watakapoelewa. Lakini zaidi ya hapo naamini zoezi hili halitafanikiwa na Serikali itazidi kupoteza fedha bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kilimo cha katani katika Mkoa wa Tanga, zao hili la katani ni zao ambalo kwa sasa lina soko zuri, lakini lina changamoto nyingi. Hivyo basi niiombe Serikali iliangalie zao la katani kwa jicho la huruma kwani zao hili tayari lipo vizuri sasa na litaingiza fedha za kigeni, pamoja na soko la ndani lipo kwa kufufua viwanda vyetu vya magunia, kwa hiyo, Serikali ipeleke vifaa vya kilimo katika zao hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishauri Serikali iunde vikundi vya vijana na kuviwezesha mitaji na kuwawekea miundombinu wezeshi ili vijana hawa waweze kulima katika vikundi. Hii itatoa fursa ya vijana kujiajiri na kuacha kukaa vijiweni. Pamoja na hayo niishauri Serikali ianzishe benki za kilimo katika kila mkoa kwani hii itarahisisha wakulima wetu kupata mikopo kwa wakati na bila kwenda mbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi mvua za kwanza ni za kupandia. Hivyo basi naomba Serikali iwe inawafikishia wakulima mbolea ya kupandia mapema kabla ya mvua za mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo mawakala waliofanya kazi ya kusambazia wakulima mbolea na mpaka sasa hawajalipwa pesa yao. Kwa vile Serikali ilishafanya uhakiki, kwa vyovyote ilishabaini ukweli uko wapi. Hivyo, naomba wale waliofanya kazi kwa uaminifu waweze kulipwa na wale waliodanganya wasilipwe, wengi wanapoteza maisha yao kwa sababu ya kudaiwa na mabenki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno haya, naomba kuunga mkono hoja.

MHE. YOSEPHER F. KOMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii inachangia zaidi ya asilimia 30 ya pato la Taifa na inaajiri zaidi ya asilimia 65 ya Watanzania na inachangia asilimia 65 ya malighafi viwandani. Cha kushangaza ni

asilimia 0.52 ya bajeti kuu ya Serikali na imekuwa ikishuka kila mwaka wa bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mbunge wa Mkoa wa Tanga na Mkoa wa Tanga tunalima mazao mbalimbali lakini mazao makuu ni mahindi, mihogo, machungwa, viungo na michikichi. Naomba Waziri atakapokuja atoe maelezo katika mambo yafuatayo:-

(i) Zao la machungwa limeingiliwa na wadudu. Wakulima wanalima kwa gharama kubwa, mfano mzuri wakulima wa Wilaya ya Muheza wanauza machungwa kwa bei ya hasara ya shilingi 40. Je, Waziri ana mkakati gani wa kusimamia soko la machungwa na dawa kwa ajili ya magonjwa yanayokumba zao hili?

(ii) Zao la minazi (Pangani) linasumbuliwa na wadudu, hivyo kufanya wakulima kupata hasara sokoni na mazao kukosa ubora unaotakiwa sokoni.

(iii) Katika Mkoa wa Tanga, Serikali ya Mkoa na Wilaya zake tulikubaliana kuwezesha wakulima wa zao la mihogo. Je, Serikali ina mkakati gani kuandaa soko kwa wakulima hawa pindi inapofika kipindi cha mavuno? Je, ni mpango gani wameuandaa kuhusu dawa ili kunusuru zao hili?

(iv) Zao la michikichi Tanga (Muheza), Kata ya Magoroto kuna *estate* kubwa ya shamba la michikichi lakini shamba hili halina faida kwa wakulima na viwanda vya kukamulia vimekufa. Je, Serikali ina mkakati gani wa kufufua zao la michikichi ili kukabiliana na upungufu wa mafuta ya kupikia nchini, hasa kuhamasisha wakulima wadogo wadogo kuendelea kulima michikichi na kufufua kiwanda?

(v) Chuo cha Kilimo cha Utafiti Mlingano kilikuwa mkombozi mkubwa kwa wakulima wa Mkoa wa Tanga na Tanzania kwa ujumla. Chuo hiki kimesahaulika, wakulima wanapambana na magonjwa kwenye mazao mbalimbali hasa michungwa, viungo, mihogo na michikichi. Naomba

Waziri aje atuambie mpango mkakati wa Wizara katika chuo hiki hasa wataalam na vitendea kazi.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni muhimu kwa maisha ya watu na kiuchumi pia, na ndiyo Wizara inayoweza kutupeleka kwenye nchi ya viwanda kwa upatikanaji wa malighafi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ipeleke fedha za kutosha ili kuiwezesha Wizara hii kufikia uchumi wa kati. Ili Watanzania waweze kuishi na wawe na afya bora lazima wale chakula kinachozalishwa nchini na wakulima waishio vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na wakulima hao kulima kwa bidii bila hata msaada wa kitaalam, inafika mahali Serikali inamuwekea masharti mkulima huyo namna ya kuuza mazao yake. Huu utaratibu haukubaliki na unakandamiza mkulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi tuliyonayo ni kubwa na inafaa kwa kilimo, lakini ni kwa nini Serikali haiandai mipango bora ya kutumia ardhi hiyo kuzalisha mazao ambayo yatasababisha nchi kuuza nje ya nchi. Matokeo yake Serikali inafunga mipaka kwa mazao kama mpunga, mahindi, kahawa na kadhalika na kumzidishia umaskini mkulima mdogo kwa kushindwa kuuza mazao yake na kusababisha mazao hayo kuharibikia kwenye maghala ya kienyeji. Serikali iwe na huruma kwa wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Mlimba ni eneo la kilimo, wananchi wanalima mazao ya biashara na chakula ambayo ni mpunga, mahindi, ufuta, ndizi, kokoa, alizeti, miti na pia ni eneo la *SAGCOT* lakini barabara za vijijini na barabara kuu hazipitiki kwa mwaka mzima na kusababisha mazao hayo kununuliwa kwa bei ya chini na kumuongezea umaskini mkulima. Nashauri Wizara ione haja ya kuwezesha jimbo hilo kupata pesa za kujenga masoko ya kisasa ili kupata urahisi wa kuuza mazao hayo kwa bei zinazokubalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushirika umeleta taharuki kwa wananchi wa Tanzania hususan Wilaya ya Kilombero. Viongozi wengi takribani asilimia 95 ya viongozi wa vyama hivyo wamefanya ubadhirifu wa fedha na mali za ushirika. Matokeo yake sasa eti wameunda timu ya kukusanya madeni matokeo yake, wanatoza tozo watu na viongozi walioua ushiriki ndiyo wanaoshirikiana nao. Ushahidi upo na viongozi hao walioua ushirika wapo, lakini hawajachukuliwa hatua yoyote. Hili halikubaliki kabisa.

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia hoja hii na naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo inabidi kipewe kipaumbele sambamba na ujenzi wa viwanda. Wizara inabidi iendelee kubuni mipango ya kisanyansi kama tunataka tutoke katika jembe la mkono, kwa mfano, kilimo cha umwagiliaji, mabwawa na visima viimarishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao la chai ni moja ya mazao ambayo sisi Amani – Muheza linalimwa kwa kiwango kikubwa. Makampuni yanayolima chai Amani ni *EUTCO* lakini wana tatizo kubwa, wanalima chai hawaruhusiwi ku-*pack,* ku-*brand* na kuuza. Wanachokifanya ni kuchakata na kwenda mnadani Mombasa kutafuta soko. Kwa nini twende mnadani nje ya nchi? Kwa nini msiruhusu hawa wenye uwezo ku-*pack,* ku-*brand* na kuuza nchini na nje Mombasa, Kenya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanga tunalima katani kwa kiwango kikubwa sana lakini zao hili halijapewa umuhimu wa kipekee ili kuweza kusaidia ulimaji wa zao hili na uuzaji wake ambao kwa sasa soko lake ni zuri kwenye soko la dunia. Aidha, tuna kiwanda cha pamba ambacho kinanunua katani kwa wingi lakini hawana soko kubwa ndani na nje ya nchi. Mipango ifanywe ili kuzuia bidhaa kutoka nje, kukuza soko na kufanya wananchi waweze kulima sana katani. Kampuni hii ya *Katani Limited* imeingia mikataba na wakulima wadogo wadogo kulima katani na kuwauzia wao kwa bei ndogo. Mikataba hii wananchi wanaumizwa, iangaliwe vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ingeangalia utaratibu wa kutoa mbegu na mbolea bure kwa wananchi. Nimeona mfano kwenye nchi moja jirani ambapo wananchi walivuna mahindi mengi hadi wakaamua kuwauzia *WFP/ WHO.* Sio lazima Serikali itoe kwa nchi nzima, ingechagua baadhi ya mikoa michache kwa majaribio. Aidha, mikopo ya zana za kilimo itolewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kulima pamba kwa wingi hapa nchini tatizo kubwa lililoko ni ubora *(quality)* ya pamba yetu bado iko chini ukilinganisha na nchi zingine ambapo *grades* za pamba zao ziko juu. Nashauri tuangalie uwezekano wa kuona tutawasaidia namna gani wakulima wetu kuweza kulima pamba yenye ubora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasifu sana mradi wa Mkulazi. Mradi huu ingawa sijafanikiwa kuuona lakini ni mradi wa mfano. Tuwe na miradi mingi kama hii itatuvusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Wizara ijipange na kuona itasaidia namna gani kuzuia panya wakubwa Mkoani Tanga ambapo walikula mahindi yote. Tafadhali angalieni namna ya kusaidia.

MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia katika hotuba ya Waziri wa Kilimo. Watanzania wote tunakubaliana kwamba zaidi ya asilimia 60 ya wananchi hupata ajira zao kupitia sekta ya kilimo. Pia tunakubaliana kwamba sekta hii hutoa chakula chote cha wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kusikitisha ni kwamba kilimo hapa nchini kinachukuliwa kama cha kujikimu tu na wala hakuna mpango mkakati wa kuonesha kwamba kilimo chetu kimejiandaa kufanya biashara ya kuhakikisha tunauza mazao kwa wingi nchi za nje ili kuongeza fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kilimo chetu kinategemea mvua kwa kiasi kikubwa. Katika ukurasa wa

saba wa hotuba ya Waziri ameonesha kuwa mwaka 2016/2017 uzalishaji ulipungua kutokana na uhaba wa mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna dhamira ya kufanya kilimo cha umwagiliaji, Wizara itafanikiwaje kama Idara ya Umwagiliaji bado iko chini ya Wizara ya Maji? Nashauri Waziri alete pendekezo Bungeni kusema kwamba Idara ya Umwagiliaji ihamishiwe Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Same Mashariki lina mito mingi na ardhi zaidi ya hekta 300,000 ambazo zinafaa kwa kilimo cha umwagiliaji. Nimeomba Wizara ya Maji tusaidiwe miundombinu ya umwagiliaji. Ni mwaka wa tatu huu maji ya mito yote yanaenda baharini na Wizara haikujali hata kujibu kama wana mpango gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Kilimo amesema kuwa mazao ya kilimo huchangia asilimia 65 ya malighafi yanayohitajika viwandani. Je, kumekuwa na mkakati gani kati ya Wizara hizi mbili kuona jinsi zitakavyoshirikiana ili kuhakikisha ni viwanda gani vitawekwa mikoa gani ili kuwe na hakika ya uzalishaji wa mazao hayo kutosheleza mahitaji ya kiwanda tarajiwa? Kwa mfano, Wilaya ya Same imechagua zao la tangawizi kuwa ndilo litatumiwa kuanzisha kiwanda kikubwa cha kuchakata tangawizi. Pia kuna tarajio la kutoa tangawizi nyingi ili kiwanda kiweze kuzalisha kwa soko la nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la wazi ni kwamba tangawizi inahitaji maji mengi sana. Tatizo ni kwamba hakuna miundombinu ya umwagiliaji ya kutosheleza kupanua kilimo hicho. Wakati *LAPF* wanawekeza kujenga kiwanda kikubwa na kuweka mashine za kisasa, je, malighafi za kutosha zitapatikanaje wakati hakuna miundombinu ya umwagiliaji? Naomba Waziri wa Kilimo aeleze kwamba kilimo kitakuwaje bila umwagiliaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo la Maafisa Ugani kwamba huko vijijini na kwenye kata hawasaidii wakulima. Waziri akihitimisha hotuba yake aeleze jinsi Wizara yake

itakavyoweza kufanya kazi na TAMISEMI ili kuwaondoa Maafisa Ugani ambao hawana tija na kisha kuajiri na kusimamia utendaji kazi wa hawa Maafisa Ugani kwenye vijiji, kata na kwenye wilaya. Ahsante.

MHE. KIZA H. MAYEYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na kuniwezesha kuchangia leo hii kwa maandishi. Napenda kuanza kuchangia kwa kusema hakuna asiyefahamu kwamba kilimo ni uti wa mgongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yoyote duniani ambayo imefanikiwa, kilimo kinapewa kipaumbele kwa asilimia kubwa. Kilimo ndiyo tegemeo la wananchi wengi kwa asilimia 99. Wengi wetu tumefanikiwa hapa leo kwa ajili ya kilimo, wazazi wetu wanategema kilimo, maisha yao yanaongozwa na kilimo lakini leo kilimo hakithaminiwi kabisa kwani changamoto ni nyingi sana, wakulima wanapata shida sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima hawanufaiki kabisa na kilimo kutokana na kwamba mkulima analima, anatumia pesa na muda mwingi lakini anapovuna bei zinakuwa ndogo na hazimlipi kabisa ukilinganisha na gharama alizotumia. Leo Mkoa wa Kigoma wakulima wanalima kahawa, kwanza wanatumia gharama na muda mwingi ila anapokuja kuuza anauza kwa bei ndogo. Hii ni changamoto kubwa sana. Serikali iwasaidie sana wakulima kuuza mazao yao kwa bei nzuri lakini pia kuwatafutia masoko ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mbolea kutofika kwa wakati, mbolea zimekuwa zikichelewa, hazifiki kwa wakati. Wananchi wanateseka sana kwani mbolea zinafika mkulima anavuna. Hivi kweli hapa mnawasaidia wakulima au mnawakomesha? Leo wakulima wa korosho wanalia kwa kukosa *sulphur* kwa wakati. Niombe sana Serikali suala la mbolea liangaliwe kwa makini, wakulima imefika mahali wanakata tamaa katika mfumo mzima wa kilimo, wanaona bora wasilime lakini kilimo ndiyo tegemeo lao na msaada,

wanategemea kusomesha watoto, kupata afya nzuri kupitia kilimo lakini wakulima wamepoteza matumaini kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viuatilifu vya kuua wadudu. Mazao mengi yanaharibiwa sana na wadudu kama viwavi jeshi, wakulima wanapata hasara kubwa sana. Mtu analima hekta 30 za mahindi lakini anapata hasara ya hekta 10, zinaharibiwa na wadudu. Naomba sana Serikali iwasaidie wakulima dawa za kuuwa wadudu. Watu wanajiua kwa kupoteza pesa, mtu analima hekta 50 anapata hasara kubwa, mazao hayazai, wadudu wanakula. Nchi za jirani zetu Barani Afrika mpaka sasa wametenga pesa kwa ajili ya kukabiliana na wadudu hawa waharibifu kama viwavi jeshi. Niombe sana Serikali itenge pesa sasa za kuhakikisha inawasaidia wakulima katika kupambana na wadudu waharibifu, wakulima wagawiwe dawa za kuulia wadudu na kuzuia. Hii itasaidia sana kupata mazao vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu migogoro ya ardhi na vyanzo vya maji, kumekuwa na migogoro mingi inayotokea katika maeneo mengi. Watu wanauana kwa kugombania ardhi. Niombe sana Serikali isimamie na kuwasaidia ardhi ya kutosha ili kuondoa maafa na migogoro ambayo inazidi siku hadi siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kigoma migogoro ya wakulima kugombania ardhi ni mingi sana katika vijiji vya Kasulu, Pamila, Manyovu na Kibondo. Wananchi wa Kasulu wanazuiwa kulima katika eneo la Kagerankanda wakati wananchi wamelima miaka mingi na ni eneo ambalo wanalitegemea na hata Mheshimiwa Rais alipopita aliwaahidi wananchi kutumia eneo lile lakini wanakuja viongozi wanatoa matamko yao na wanakwenda kinyume na kauli ya Rais. Niombe sana Serikali iwaachie wananchi hawa eneo hili waendelee kulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia kubwa ya wananchi wa Kigoma hasa Wilaya ya Kigoma Vijijini wanategemea zao la michikichi lakini zao hili limesahaulika kabisa na linaonekana kama halina thamani. Wenzetu wa Malaysia

walikuja kuchukua mbegu kwetu, wamelipa thamani zao hili na sasa ni nchi inayosambaza mafuta duniani. Kwa hiyo, Tanzania tulifanye zao hili kama zao la biashara ukizingatia tunaenda katika nchi ya viwanda, kwa nini tusiwe watengenezaji wakubwa wa mafuta kwani katika michikichi tunapata mafuta mazuri sana kwa afya ya mawese, mise lakini pia kupitia mafuta haya tunapata sabuni nzuri sana za gwanjwi. Naomba Serikali iwapatie wananchi wa Kigoma mbegu bora za michikichi kwani kampuni inayouza miche hii inauza mche mmoja kwa shilingi 5,500, wananchi hawana uwezo wa kununua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana kuiambia Serikali kilimo ndiyo kila kitu, wananchi wanategemea sana kilimo. Kama kweli tunataka nchi ya viwanda basi lazima Wizara ya Kilimo ipewe kipaumbele, bajeti iwekwe kubwa wananchi wamekata tamaa kabisa na kilimo.

MHE. TASKA R. MBOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Tizeba, Waziri wa Kilimo na Naibu wake Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuendeleza kilimo nchini Tanzania. Niende moja kwa moja kwenye Mkoa wangu wa Katavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Katavi ni mkoa ambao unazalisha mazao ya chakula na biashara. Sisi Katavi ni miongoni mwa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini inayolisha Tanzania, *the big six* ambayo ni Katavi, Rukwa, Songwe, Mbeya, Iringa na Ruvuma. Katavi hatuna njaa, tunalima mazao ya kilimo cha biashara na chakula. Mazao hayo ni mahindi, mpunga, alizeti, karanga, pamba, korosho na nyuki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Katavi tumekuwa tukilima zao la biashara la tumbaku kwa muda mrefu sana, ni zao linalotegemewa kwa biashara, lakini zao hilo limekuwa likiwaumiza sana wakulima, afya zao zinaharibika maana tumbaku inashuruba sana kuanzia ulimaji wake, kukausha, mpaka kuuza, kote kuna kazi ya kutumia nguvu. Mkulima anapokuwa amevuna anakuwa ameumia sana. Pia katika uuzaji wa zao la tumbaku kuna shida maana kuna utaratibu

wa kupangiwa kilo za tumbaku za kuuza na kila mwaka kilo wanazopangiwa kuuza zinapungua. Hii inawapa shida wakulima, wanapata hasara maana wanachopangiwa kinapungua kila mwaka hivyo basi lipo hitaji la kuongeza zao la biashara Katavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilo za tumbaku walizopewa ni kama ifuatavyo:-

(i) Season 2014/2015 walipewa kilo 11,910,459.

(ii) Season 2015/2016 walipewa kilo 8,445,786.

(iii) Season 2016/2017 walipewa kilo 12,099,742. Tumbaku iliyozidi imevunwa ni kilo 2,711,709.

(iv) Season 2017/2018 ambayo inakaribia kununuliwa, makadirio ni kilo 7,452,562.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahitaji ya Mkoa wa Katavi ni kama ifuatavyo:-

(i) Tunaomba mtuongezee Maafisa Ugani kwa sababu Mkoa wa Katavi asilimia 80 ya mkoa mzima hakuna maafisa hawa. Hivyo, tunaomba tumepewa Maafisa Ugani kila kijiji.

(ii) Maafisa Ugani waliopo ambao ni wachache wapewe mafunzo kuhusu mazao mapya ya pamba na korosho ambayo yameletwa Mkoani Katavi. Kwa sasa hivi Maafisa Ugani waliopo hawana ujuzi wa zao la pamba na korosho.

(iii) Mfumo wa soko wa zao la pamba haujawekwa vizuri maana wakulima wanatakiwa wawauzie vyama vya ushirika. Pia wakulima wa Katavi hawana uelewa wa zao hili la pamba.

(iv) Serikali iruhusu mapema kuuza mahindi nje, sio wasubiri mpaka mahindi yaharibike.

(v) Mkoa wa Katavi tunaomba mbegu za korosho kwa wingi ili wakulima waweze kulima kwa wingi.

(vi) Tunaomba Bodi ya Korosho ituletee mbegu ya korosho Mkoani Katavi.

(vii) Miundombinu ya biashara ni mibovu inafanya wafanyabiashara wanunue mazao kwa wakulima kwa bei ndogo sana.

MHE. SUSANNE P. MASELLE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitekeleza au kukiboresha kilimo unagusa maisha ya mwananchi wa kawaida kabisa. Takwimu zinaonesha kuwa kilimo kinaajiri kati ya 70% hadi 75% ya Watanzania na kinachangia 20% hadi 28% ya pato la Taifa. Kwa nini sekta inayoajiri watu zaidi ya nusu ya ajira na inayochangia kwa kiasi kikubwa pato la Taifa inapuuzwa na kupangiwa bajeti ndogo ukilinganisha na umuhimu wake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ije hapa ituambie kwa nini haitekelezi Azimio la Maputo kuhusu kilimo na usalama wa chakula ambapo ilitakiwa kutenga 10% ya bajeti ya Serikali kila mwaka kwa ajili ya kilimo. Pesa hii ingesaidia sana katika kutatua changamoto nyingi ambazo zinaikumba sekta hii ya kilimo na kukuza uchumi wa wakulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wa pamba wanazidi kukata tamaa kwa sababu pamoja na kazi kubwa wanayofanya wanaishia kupata hasara tu kuanzia maandalizi ya kilimo, kwenye mavuno na hadi kwenye mauzo. Wanakabiliwa na matatizo ya mbegu ambazo hazioti na wameuziwa na mawakala waliopitishwa na Bodi ya Pamba. Hivyo, inawalazimu kununua mbegu mara mbili na kuwafanya wapishane na misimu. Mbali na mbegu mbovu, wanakumbana na dawa ambazo haziui wadudu, wanunuzi wadanganyifu wanaochezea mizani ili kupata faida kubwa, pembejeo kuchelewa kufika na kupishana na msimu wa kilimo na kilimo cha kutegemea msimu huku kukiwa na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wa pamba wa Mwanza na maeneo mengine takribani mikoa 17 inayolima zao hili wanateseka sana na kuona zao hili kama halina faida kwao. Ni wakati sasa wa Serikali kutatua changamoto hizi ili wakulima hawa wafaidike na hili zao lao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali iwafutie madeni wakulima wanaodaiwa kwa muda mrefu yanayohusu pembejeo na huduma za ugani hasa mbolea, viuatilifu na mbegu. Madeni haya ambayo yanaongezeka kila mwaka yanawafanya wanalima huku wakiwa na mzigo wa kulipa madeni kila mwaka, matokeo yake hawapati kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iwapatie ruzuku wakulima kama mataifa makubwa duniani wanavyowapatia ruzuku wakulima wake. Kwa nini hapa tunaacha wakulima kuwa ni watu wa kuhangaika wenyewe? Tuanze na wakulima wa pamba, tuwasamehe madeni yao na wapewe ruzuku ili sasa turudishe hadhi ya maisha ya wakulima wa pamba ambao walitufanya tukasifika duniani na watu kuendesha maisha vizuri kabisa ikiwemo kujenga makazi bora na kusomesha watoto wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo cha umwagiliaji kipindi hiki ni muhimu sana kutokana na mabadiliko ya tabianchi ambayo yanasumbua sana kutabiri misimu ya masika, vuli, kipupwe au ukame. Ni nini mikakati ya Serikali kibajeti hasa kwa maeneo ambayo wananchi wameshaonesha utayari kwa vyanzo au uwezo kidogo walionao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo cha umwagiliaji kinaweza kabisa kuliokoa Taifa na mahitaji ya chakula, kuongeza pato la Taifa na kuboresha maisha ya wananchi. Nini mikakati ya Serikali hasa kulitumia Ziwa Victoria kama wafanyavyo wenzetu wa Misri ambao kilimo cha umwagiliaji kwa kutumia Mto Nile kutokana na Ziwa Victoria ndio uti wa mgongo wa uchumi wa Taifa hilo? Ni hatua gani Serikali inachukua pamoja na ushirikiano wa Serikali na sekta binafsi

katika kuwekeza katika shughuli za kilimo, uzalishaji na usindikaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwanza ina rasilimali kubwa sana ya maji huku 53.25% ya eneo la mkoa likiwa katika Ziwa Victoria. Ni kwa mantiki hiyo kilimo cha umwagiliaji kinaweza kufanywa kutegemea maji ya ziwa hilo, pamoja na mabonde ya mito yanayopeleka maji katika ziwa hilo. Eneo linalofaa kwa kilimo cha umwagiliaji katika Mkoa wa Mwanza ni takribani hekta 39,411 lakini mpaka sasa ni hekta 1,429 (sawa na 3.93%) ndizo zinazotumika kwa kilimo cha umwagiliaji. Serikali iweke mikakati madhubuti kuongeza idadi za hekta ili wananchi wanufaike na hiki kilimo cha umwagiliaji.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na kumpongeza Mheshimiwa Waziri Dkt. John Tizeba, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa, Makatibu Wakuu na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri. Nampongeza pia Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa ziara zake nyingi zilizoleta tija kwa ajili ya kilimo chetu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia 75 ya wananchi wanaishi vijijini na asilimia 65 ni wakulima na wanategemea kilimo, lakini bado Serikali haijaweza kuwa na mkakati wa kumsaidia mkulima. Yapo mambo ambayo ningeomba kupata ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Kilimo ilianzishwa ili kuweza kumsaidia mkulima mtaji kwa sababu wakulima hawakopesheki. Pamoja na benki hii kuwa Dar es Salaam, bado Serikali haijaweza kuweka pesa ya kutosha kwa ajili ya kukopeshwa wakulima. Kwa ushauri wangu benki hii makao makuu yahamie Dodoma, lakini kuwepo na matawi kila kanda ili wananchi waweze kuwafikia kwa urahisi. Ushauri wangu ni kwamba Serikali iongeze mtaji katika benki hiyo ili ibebe jukumu la kutoa mikopo kwa wakulima wengi na yenye riba nafuu ili kilimo kiwe na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu pesa ya utafiti 1% ya bajeti, ni lini Serikali itatenga pesa ya kutosha kwa ajili ya

watafiti ili wataalam wetu waweze kufanya tafiti mbalimbali hasa za mbegu, mbolea hata waweze kupima udongo wa maeneo mbalimbali ili wakulima wetu walime kilimo chenye tija na cha uhakika kuliko sasa hivi ambapo mkulima analima kilimo cha kubahatisha, hana uhakika na kilimo chake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo huu unadhihirisha kukosekana kwa dhamira ya dhati ya uwekezaji katika miradi ya kilimo na kikwazo katika ukuaji wa kilimo na kupunguza umasikini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maafisa Ugani wanafanya kazi gani katika maeneo yao? Mbona wakulima wetu hawana elimu ya kutosha ya kilimo ya kueleweshwa kuhusu mbegu bora, utumiaji wa mbolea na matumizi ya ardhi kwa ujumla? Ni kwa nini yasianzishwe mashamba darasa katika maeneo mbalimbali kwa ajili ya kusaidia kuwapatia elimu wakulima wetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu alipofanya ziara Iringa alitueleza kuwa *NSSF* wameamua kufufua kinu cha kusaga mahindi cha Iringa *(National Milling)* kwa ajili ya kuleta tija kwa wakulima wetu wa Mkoa wa Iringa. Sasa je, huo mpango bado upo? Sababu kinu hiki kilikuwa kinaleta ajira, pia ni soko hata kwa wakulima wetu la mahindi. Wakulima nchini hasa wa Mkoa wa Iringa wanapata shida sana kwa sababu upatikanaji wa mbolea katika maeneo mbalimbali haukidhi mahitaji ya wakulima nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia zipo changamoto nyingi sana zikiwemo za wasambazaji mbolea kwamba hawazingatii kabisa bei elekezi za Serikali na kusababisha bei ya mbolea kuwa kubwa sana, mbolea haifiki kwa wakati, hawazingatii msimu unaanza lini na kadhalika. Ni kwa nini Serikali isiangalie uwezekano wa kuondoa tozo katika mbolea ili bei ya mbolea ipungue?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali izingatie ushauri wa Kamati. Kamati imeshauri mambo mengi sana

ambayo kama yakizingatiwa yanaweza kusaidia wakulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Tanzania tumekuwa na kilimo cha kubahatisha na wakulima wengi wanategemea kilimo cha mvua na msimu wake hautabiriki, ni lini Serikali itaanzisha Bima ya Kilimo ili wakulima waweze kukopesheka kuliko ilivyo sasa mkulima hakopesheki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. JUMA OTHMAN HIJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia katika hotuba ya Waziri wa Kilimo. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo pamoja na watendaji wake wote kwa kuandika na kuiwakilisha hotuba hii kwa ufanisi mkubwa. Katika kuchangia hotuba hii ya kilimo, napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Wizara kwa juhudi zake inayochukua kuimarisha na kuhamasisha wakulima wa nchi hii. Wakulima wa nchi hii wameendelea kuonesha juhudi zao katika kilimo cha mazao tofauti hasa yale mazao ya biashara. Juhudi hizi zimeonekana kudorora kutokana na upatikanaji wa masoko ya kuuza mazao hayo. Wakulima wamekuwa wakilundika mazao yao katika maghala kwa muda mrefu jambo linalopelekea kuvunja moyo kwa kiasi fulani. Hivyo nachukua fursa hii kuiomba Serikali kupitia Wizara hii kulichukulia suala hili la kuwatafutia masoko ya uhakika wakulima wetu ili wawe na uhakika wa kuuza mazao yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu kupitia Wizara ya Kilimo inachukua juhudi ya kutafuta namna ya kuboresha kilimo kwa kuwatafutia wakulima wetu zana za kilimo. Nachukua nafasi hii kuipongeza Wizara kwa jambo hili zuri. Imeonekana kuwa jambo hili lina tatizo la wakulima wetu kutomudu kununua zana hizo za kilimo hasa matrekta. Hii ni kutokana na bei kubwa ya ununuzi wa matrekta. Wakulima wa nchi hii, idadi kubwa ni wakulima wa kipato cha chini/

kati kiasi ambacho uwezo wao ni mdogo sana. Hivyo naiomba Serikali kupitia Wizara ya Kilimo kuangalia utaratibu mzuri wa kuwawezesha wakulima kupata zana hizi kwa kuwapunguzia bei au kuwakopesha kwa masharti nafuu wakulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. ENG. RAMO M. MAKANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana timu nzima ya Wizara ikiongozwa na Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu kwa kazi nzuri mnayoendelea kuitekeleza Wizarani ili sekta ya kilimo iendelee kuwa miongoni mwa sekta kiongozi katika kuchangia uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa zinaonesha kuwa kuna uhaba wa Maafisa Ugani kwa viwango vikubwa. Ni vema kwanza Serikali ikaandaa kanzidata *(database)* ili kujua idadi na ujuzi walionao wale wachache waliopo kwa madhumuni ya kuandaa mkakati kutatua tatizo, *skills* maalum kwa maeneo maalum, idadi kulingana na mahitaji ya kila eneo, kipaumbele kwa maeneo yenye umuhimu kimkakati; kwa mfano katika uzalishaji wa mahindi *the big four regions,* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifano ya uhaba mkubwa wa Maafisa Ugani (Sera ya Afisa mmoja kila kijiji), katika hotuba ya bajeti ukurasa 47 Mkoa mzima wa Kagera, licha ya kuwa mkoa wenye shughuli kubwa na nyingi za kilimo, inao Maafisa Ugani 548 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Tunduru yenye mahitaji ya Maafisa Ugani 227 inao 72 tu, sawa na asilimia 32. Hali hii inasababisha changamoto nyingi kama wakulima kutojua viuatilifu sahihi, viwango na matumizi sahihi. Pia aina za udongo katika maeneo na mazao yanayofaa kustawishwa na kadhalika. Wananchi wengi wanapata mavuno wanayodhani ni mengi katika eneo la ukubwa ambao wangezalisha zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu viwanda, Wilaya ya Tunduru imefikia uzalishaji wa tani 20,000 za korosho mwaka 2017/2018. Wilaya ina kiwanda kimoja tu cha kubangua korosho chenye uwezo wa kubangua tani 3400 tu sawa na asilimia 17 tu. Ili kuendana na mkakati wa Kitaifa wa uchumi wa viwanda na ili kuongeza thamani na kuongeza pato kwa mkulima, Halmashauri na Taifa kwa ujumla, lengo (ndoto) ni kubangua korosho zote. Ili tufikie katika lengo la ubanguaji kwa asilimia 100 au karibu na hiyo, tunahitaji viwanda vingi zaidi kama ilivyo kwa nchi kama ya India wanaofanya vizuri. Viwanda hivi ni vidogo na vya kati vyenye wamiliki wa uwezo mdogo hadi wa kati. Viwanda hivyo vinahitaji malighafi, lakini ununuzi wa korosho ghafi unasimamiwa na Sheria ya Tasnia ya Korosho. Kanuni zake na Mwongozo Na. 1 wa mwaka 2017/2018 wa mauzo ya korosho. Sheria, Kanuni na Mwongozo huo siyo rafiki kwa utekelezaji wa hitaji hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali itathmini kwa kina jambo hili.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna uhitaji mkubwa wa sukari na mafuta hapa nchini. Kinachohitajika ni kutengeneza mazingira bora ya kuzalisha miwa na *oil seed* (alizeti, ufuta na kadhalika). Naamini Serikali ikifanya kazi kwa pamoja kati ya Wizara za Kilimo, Wizara ya Viwanda na Wizara ya Fedha, kwa mfano, Brazil imefanikiwa kutokana na kuwekeza katika viwanda vidogo na vya kati, hii ni kwa sababu kuwekeza katika viwanda vikubwa inahitaji fedha nyingi lakini pia huchukua muda mrefu mpaka hata miaka mitano na ndiyo maana Wizara inayo kila sababu kutengeneza mazingira ya kuibua maeneo yanayofaa kwa kilimo cha miwa na uwekezaji wa viwanda vya sukari. Tujifunze kutoka Brazil, *potential* ipo kubwa na ya wazi. *The same can be applied* kwenye suala la mafuta ya kula. Ninaamini hata kwa kushirikiana na Wizara ya Ulinzi (JKT) tunaweza kuibua maeneo yanayofaa kulima *oil seeds* (alizeti) na kadhalika ili kuwa na malighafi ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini Wizara ya Kilimo iki-*take lead,* Taifa hili litapiga hatua na dhana hii ya uchumi

wa viwanda itakuwa ya vitendo na yenye kuleta tija. Pamoja na mchango huu, naambatanisha nakala yenye kuonesha maeneo *potential* kwa uwekezaji wa kilimo cha miwa na uzalishaji sukari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachangiaji wengi wamesema sana kuhusu mbolea. Ushauri wangu ni kwamba hiyo inayoitwa ruzuku, afadhali fedha yake ingetumika kufanya *distribution,* kwa maana kuwa isaidie ku-*cover* gharama za usafirishaji. Hii ni kwa sababu wakulima wanachohitaji ni mbolea kuwafikia kwa wakati. Suala la bei kwao siyo *issue* sana, *issue* ni mbolea iwafikie kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maeneo mengi nchini ambayo tunaweza kujenga viwanda vidogo na vya kati (tani 10,000 mpaka tani 30,000 kwa mwaka). Kila mkoa una maeneo kama haya, kwa mfano, Kilosa tani 10,000; Manyara tani 10,000; Mara tani 30,000; Ruvuma tani 10,000; Dodoma – Chamwino tani 10,000; Kigoma – Bonde la Malagarasi tani 30,000; Pwani – Rufiji tani 30,000 na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uendelezaji wa viwanda vidogo unachukua muda mfupi, kama miezi minane hadi kumi. Gharama zake ni za chini USD milioni tatu hadi USD milioni 10 ukilinganisha na vile vikubwa USD milioni 100 hadi USD milioni 300 ambavyo huchukua miaka miwili mpaka mitano. Viwanda vidogo viko karibu na wananchi. Bei ya sukari yake ni nafuu kutokana na gharama kuwa chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri za Wilaya husika zinaweza kuingia ubia na wawekezaji wazalendo katika maeneo yao na miradi hii inaweza kuingizia mapato Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MHE. DKT. MARY M. NAGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru na kumpongeza Waziri na Serikali kwa bidii. Naomba leo nianze kwa kuongea suala la masoko ya mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima ndio wanaopinda migongo yao kulima mashambani na wanabeba gharama zote za kilimo. Hawakubaliani na wasingependa kukutana na pingamizi lolote la kuuza mazao yao ambapo wamepata masoko hata kama ni nje ya nchi, badala yake wanataka wasaidiwe ipasavyo. Jukumu la kuona Taifa lina uhakika na usalama wa chakula siyo la mkulima mmoja mmoja zaidi ya wao kulima kwa tija. Uamuzi wa Serikali wa kuwafungia mipaka wananchi kuuza mazao yao, matokeo yake ni Zambia kunyang'anya masoko ya asili nje ya mipaka (nchi jirani). Wakulima wa Hanang wamepata hasara kubwa na kukosa mitaji ya kulima msimu huu kwa kushindwa kuuza mazao yao. Walishindwa kununua pembejeo zao kutokana na bei ya juu pamoja na bei elekezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kuamua kujenga maghala makubwa yenye uwezo wa kuhifadhi angalau tani 500,000. Jitihada hizo zikutane na *NFRA* kuongezwa fedha za kununulia nafaka ya akiba kuhakikisha usalama wa chakula na matumizi bora ya maghala. Napenda kuomba Serikali ipunguze kodi na tozo katika mifuko maalum ya kuhifadhi mazao ili bei ya kununua iwe nafuu. Hatua hii itapunguza upotevu wa mazao ndani ya maghala yaliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuuliza utekelezaji wa *commodity exchange* umepotelea wapi toka sheria kupitishwa? Utekelezaji wa *commodity exchange* unategemewa kuwa ufumbuzi wa kudumu wa kuwapatia wakulima soko la mazao lililo muhimu. Tungependa kuona Serikali ikiweka mazingira mazuri katika kushiriki sekta binafsi katika sekta hii kikamilifu. Hii ni kwa sababu sekta binafsi ina uwezo mkubwa wa kuwekeza katika sekta hii ikiwa sekta binafsi itawekewa mazingira mazuri hasa yanayohusiana na sera za kikodi na udhibiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ninalotaka kuongea ni ukuaji wa sekta ya kilimo kutoka 6% mwaka 2004/2005 hadi 2.1% mwaka 2016/2017. Ukichunguza sababu kubwa ni kupungua kwa bajeti iliyotengwa na kutolewa kila

mwaka katika miaka iliyofuata. Naiomba Serikali iwe inaongezea sekta ya kilimo bajeti hadi kufikia 10% ya bajeti yote kwa mujibu wa Azimio la Malaba na Maputo. Ikiwa azimio hili likitekelezwa, litavutia sekta binafsi kuwekeza zaidi katika kilimo. Uwekezaji wa ziada utaongeza uzalishaji wa mazao na tija ambao utanufaisha Taifa kwa usalama na uhakika wa chakula, upatikanaji wa malighafi kwa ajili ya viwanda, ongezeko la mauzo ya nje ya mazao ya kilimo na ongezeko la mapato ya Serikali kupitia kodi na ushuru. Matokeo ya manufaa niliyotaja hapo juu ni kuongeza kasi ya azma ya Taifa kufikia uchumi wa viwanda na mapato ya kati ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa ni vigumu kufikisha bajeti ya kulima 10% ya bajeti ya Taifa tuondoe tozo zote kwenye pembejeo zote, zana zote za kilimo na uchakataji wa mazao ya kilimo. Hii itasaidia kupunguza gharama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kuongeza bajeti iliyotengwa kutoka shilingi 162,224,814,000 mwaka 2017/2018 mpaka shilingi 214,815,759,000 katika bajeti hii tunayoijadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhakiki wa mawakala ni jambo muhimu, lakini tunataka matokeo ya uhakiki ili wale wanaostahili wapate kulipwa na wasiostahili wachukuliwe hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushirika ni muhimu kwa wakulima lakini uliingiliwa na mchwa na kuingiza hofu kubwa kwa wakulima. Tuwauwe mchwa na kuupanga ushirika vizuri kabla ya kupitisha fedha za wakulima katika ushirika.

MHE. NURU A. BAFADHILI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuchangia machache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo tunacholima Watanzania siyo chenye tija. Wakulima wengi wanalima kwa mazoea, siyo kama biashara ya kuwapatia kipato.

Mheshiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Tanga kuna Kituo cha Utafiti cha Kilimo kilichopo Mlingano Wilaya ya Muheza. Kutokana na kituo hiki, wakulima hawapati msaada wowote kutokana utafiti wa udongo wa mazao yanayostahili kulimwa katika eneo hilo. Ombi, kwa nini Mheshimiwa Waziri asihamasishe umuhimu wa kupima udongo na kuelewa aina ya mazao yanayoweza kustawi katika maeneo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mikoa ya Pwani ni maarufu kwa kilimo cha minazi. Minazi ikivunwa ina manufaa sana. Mafuta ya nazi ni mazuri sana, hayana lehemu. Mheshimiwa Waziri atueleze, ni lini Tanga kutaanzishwa kiwanda cha kutengeneza mafuta kutokana na nazi zinazovunwa Tanga, Pangani, Mkinga na Muheza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ya 1960 sekta binafsi waliweza kutengeneza kiwanda cha kukamua mafuta ya nazi. Kiwanda hiki kilikuwa katika Jiji la Tanga. Mafuta yaliyozalishwa hapo yaliitwa *Nicolin*. Wananchi walitumia mafuta hayo kupikia vyakula mbalimbali na wala hayakuleta madhara kwa walaji. Tunaomba Serikali itujengee kiwanda cha kusindika mafuta ya nazi.

MHE. ESTER A. MAHAWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumshukuru Mungu kwa ulinzi, nguvu na afya aliyonijalia mimi na Wabunge wenzengu wote humu ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia zaidi ya 65 ya wananchi wa Tanzania ni wakulima. Ni kweli kwamba kaulimbiu yetu ni kufikisha nchi yetu kwenye uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025 na ili kufika huko tunakotaka kwenda ni lazima tufufue viwanda vyetu. Mazao ya kilimo ndiyo malighafi ya kufanya viwanda vyetu vizalishe, vitoe ajira, vituletee fedha za kigeni na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu sasa Wizara ya Kilimo ilikuwa haipewi kipaumbele kabisa, pamoja na kuwa ndiyo Wizara pekee ambayo ina uwezo mkubwa wa kuondoa umaskini wa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatambua kwa dhati ya moyo wangu juhudi kubwa ya Serikali yetu ya Awamu ya Tano chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, ninatambua nia ya dhati ya Mawaziri wa Kilimo ya kuleta mapinduzi ya kilimo, lakini ifike mahali watalaam wa Wizara hii wafikiri njia bora na sahihi ya kumkomboa mkulima huyu maskini anayevunja shamba kwa mikono yake, anayepanda, kupalilia na kuvuna mazao yake kwa gharama na jasho jingi, ni kwa namna gani kazi yake hiyo itamlipa? Kwani wakati akilima hakusaidiwa na mtu wala Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa wafanyakazi wa nchi hii wanapopokea mishahara yao baada ya kufanya kazi kwa mwezi mzima, ni kwa nini mkulima huyu abebe gharama zake mwenyewe halafu baadae apangiwe wapi akauze?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa kilimo cha mahindi kimeshamiri sana hapa nchini, mbali na kuwa zao la chakula, lakini sasa hivi zao hili limekuwa la kibiashara, pia na wananchi wengi wanalima kama zao la biashara. Mwaka 2017 Serikali ilipofunga mipaka ili mahindi yasiuzwe nje, wakulima wengi wamepata hasara kubwa sana. Mahindi mengi yameoza na yaliyobaki yanauzwa kwa debe moja shilingi 5,000, gunia ni shilingi 25,000. Kumbuka mbegu ya mahindi kilogramu mbili ni shilingi 12,000, weka gharama za kilimo, palizi na kuvuna. Kwa heka moja mkulima anapoteza zaidi ya shilingi 600,000, lakini leo anauza mahindi kwa debe shilingi 5,000 kuna tija gani hapo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mkulima huyu aliyelima mbaazi na bado mbaazi inakosa soko huko India, mkulima huyu amelemewa.

Naomba Serikali ione ni kwa namna gani sasa mkulima huyu atasaidika. Suala la pamba kuuzwa kwenye ushirika nalo ni janga lingine. Ninaomba sana Serikali yangu iangalie kwa upya jambo hili na ikiwezekana ijipe muda kidogo wa kufanya utafiti ili kujiridhisha vilivyo ili hatimaye tusije kutukamuumiza tena mkulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema ukweli bajeti iliyotengwa mwaka 2017/2018 yenyewe ilikuwa ndogo lakini kinachouma zaidi ni kiasi kidogo sana kilichopelekwa. Kama kweli tunataka kutoka hapa tulipo kiuchumi, ni lazima tuwekeze vya kutosha katika kilimo chenye kuleta tija hasa kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi zote zilizoendelea katika uchumi wa kilimo, wamewekeza zaidi katika kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni na mpaka sasa bado mvua kubwa zinaendelea kuleta mafuriko makubwa na maafa, lakini inashangaza sana kuona kuwa hatuwekezi kwenye utengenezaji wa mabwawa ili maji hayo yaweze kutumika katika kilimo cha umwagiliaji. Pamoja na kwamba hii siyo njia pekee, tunahitaji kuchimba visima virefu ili kutekeleza azma hiyo. Naishauri Serikali, Wizara ya Maji ifanye kazi sambamba na Wizara ya Kilimo ili uwekezaji huo wa kilimo cha umwagiliaji, kiweze kufanikiwa ili tupate malighafi ya kutosha ya viwanda vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wengi waliomaliza vyuo va kazi na Vyuo Vikuu hawana ajira. Nashauri Serikali itenge maeneo yanayofaa kwa kilimo, vijana hawa wakopeshwe zana kama matrekta na kadhalika ili waweze kujiajiri kwenye kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kusema nashukuru sana. Naunga mkono hoja.

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasita kuunga mkono hoja Wizara hii ya Kilimo kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaona juhudi za kuimarisha kilimo hata kidogo hasa wakulima ambao ndio wapiga kura wa nchi hii, hawajasaidiwa vya kutosha. Mbolea haipatikani kwa wakati, bei yake haieleweki, wala masoko ya mazao hayapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mbolea nashauri Serikali itumie waagizaji wa pamoja *(bulk procurement system)* lakini waagizaji watakiwe kwenye masharti wafikishe mbolea kwenye mikoa ya uzalishaji na kwa kiwango cha mahitaji, usambazaji uanzie pale Makao Makuu ya Mikoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri mbolea ya Minjingu isilazimishwe kwa wakulima, ifanyiwe utafiti na Serikali iiwekee ruzuku ndogo ili wananchi waitumie miaka miwili au mitatu, wakiipenda wataendelea kuitumia. Mbolea nyingine kama *DAP* iendelee kuwepo kwenye soko.

Aidha, mawakala walioisadia Serikali kutoa pembejeo wasidhulumiwe, wapewe kile kitakachoonekana ni haki yao. Siyo sahihi kuona kuwa mawakala wote ni wezi na hawapaswi kulipwa. Mbolea ije kwa wakati, Mkoa wa Rukwa leta mbolea mwezi Agosti mpaka Septemba. Mbegu ziwe za viwango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu masoko, wakulima wa Nkasi Kusini wanalima kwa gharama zisizolingana na soko la mahindi kwa sasa. Inakatisha tamaa. Mfumo wa *commodity exchange system* inaonekana unafanya vizuri. Nashauri *NFRA* inunue mahindi hata kwa kutengeneza siasa na hawa wakulima, ni muhimu sana. Hawa ndio waliotuamini na kutuweka madarakani. Sasa mambo yao hakuna hata moja lenye nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muujiza gani utafanyika kuinua uchumi wa viwanda huku umeacha kilimo nyuma? Hii siyo sawa kabisa, Serikali ishughulikie mambo ya wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi ambao ni wakulima wa vijiji vya Kasu, Kisura, Milundikwa na Malongwe wamenyang'anywa mashamba waliyopewa kwa utaratibu wa kawaida na sasa hawana mahali pa kulima. Zaidi ya watu 4000 wameathirika kwa jambo hili, hawaendi kulima maana wao ni wakulima na sasa watashindwa kusomesha watoto, kujenga nyumba bora, kupata matibabu bora, kuvaa nguo nzuri na kupata chakula cha afya. Serikali iangalie hili jambo.

MHE. DEVOTHA M. MINJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia kwa maandishi, kwanza ni kuhusu pembejeo za kilimo. Wizara imeshindwa kusimamia utaratibu wa ugawaji pembejeo za wakulima kwa wakati badala yake imekuwa kilio na kupata pembejeo za kilimo kwa kuchelewa ikizingatiwa kuwa wakulima wengi hawana uwezo wa kumudu gharama kubwa za mbolea na wanategemea mbolea ya ruzuku ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ikiri wazi kuwa mfumo wake wa kupatia wananchi mboleo ume-*fail* na watafute mbinu nyingine ya kufikisha mbolea hizo kwa wakulima kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masoko ya uhakika wa mazao bado. Bado kuna changamoto, Serikali imekazana kudhibiti uuzwaji wa mahindi nje ya nchi huku Serikali ikishindwa kuwa na mfumo mbadala wa kusaidia wananchi wake kuuza mazao yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazao ya mahindi yameharibika, wananchi wamepata hasara ikiwemo Mkoa wa Morogoro. Serikali imewaweka wananchi katika mazingira magumu sana wengine kupata hasara. Cha kushangaza, mahindi kutoka Zambia yanapita Tanzania na yanaenda Kenya kuuzwa, hiyo siyo sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madai ya mawakala wa pembejeo za kilimo ambao wamefanya kazi ya kupeleka huduma kwa wakulima mpaka sasa hayajalipwa. Hii ni aibu na uonevu kwa wakulima. Serikali iliahidi kupitia madai yote na kubaini madai hewa na halali, mpaka sasa hamna majibu. Tatizo hili kama Serikali haitatenda haki kwa mawakala halali, hii itaendelea kujenga chuki kati ya Mawakala na Serikali yao. Ni vyema Serikali ikapitia upya madai hayo na kutoa haki kwa mawakala.

MHE. ZUBEDA H. SAKURU: Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya kilimo ni sekta ya muhimu sana katika ukuaji wa uchumi hasa katika mapinduzi ya viwanda. Ni ajabu sana

kuona kuwa hakuna msisitizo mkubwa kwa sekta ya kilimo hasa ukizingatia kuwa hata mapinduzi makubwa ya viwanda duniani yaliyotanguliwa kwanza na mapinduzi ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya kilimo ni sekta muhimu, siyo katika uzalishaji wa malighafi, bali pia katika kutoa ajira hasa ukizingatia kuwa vijana ni wengi kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012 ambayo imeweka wazi kuwa zaidi ya asilimia 52 ya idadi ya watu ni vijana. Hivyo Serikali ilitakiwa kutenga bajeti yake siyo tu kutekeleza sera yake ya viwanda, bali pia kuweka mkazo katika sekta ambayo inatatua changamoto za ukosefu wa ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado zipo changamoto kubwa ambazo zina athari kubwa na za moja kwa moja kwa sekta ya kilimo na ukuaji wake hasa miundombinu. Nchi yetu ina changamoto ya kijiografia. Kwa mfano, Mkoa wa Ruvuma una changamoto kubwa ya miundombinu hasa kwa Wilaya ya Mbinga, Nyasa, Namtumbo, Tunduru na hivyo kuleta changamoto ya masoko hasa kipindi cha masika. Hivyo Wizara hii inatakiwa kuweka mkakati wa pamoja na sekta ya miundombinu ili kuwezesha ukuaji wake na kuendeleza wananchi kiuchumi. Je, ukakasi wa kuweka miradi ya pamoja kukuza sekta hii muhimu unatoka wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kuwa Mkoa wa Ruvuma ni mojawapo ya mikoa yenye kuzalisha kwa wingi mazao ya kibiashara na chakula. Hivyo tulitegemea iwe mojawapo ya mikoa yenye ukuaji mzuri wa kiuchumi, lakini hali ni tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Serikali kutoa majibu kuwa mbaazi ni nzuri kwa chakula, leo mwananchi wa Tunduru aliyewekeza kwenye mbaazi akitegemea soko la dunia, anadhihakiwa vipi kwa soko la mbaazi kushushwa na kauli za kisiasa? Ipo haja ya Wizara ya Kilimo kuwanasua wakulima hasa wanaotegemea jembe la mkono kwa kuwaunganisha na masoko na siyo kuwafanyia dhihaka pale wanapozalisha ziada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha kuona kuwa Wana Ruvuma wanazalisha mazao ya kibishara na chakula lakini hawanufaiki na kilimo. Upo usemi unaosema kuwa mtaji wa maskini ni nguvu zake mwenyewe. Je, nguvu kiasi gani itumike ili Mtanzania aweze kunufaika na kilimo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo jambo linatakiwa kutazamwa kwa jicho la ziada ili kunusuru wakulima, nalo ni soko la mahindi. Nia njema ya Serikali iko wapi ikiwa *NFRA* haipewi fedha za kutosha na hivyo kupelekea kununua sehemu ndogo tu ya mahindi yaliyozalishwa nchi nzima?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Ruvuma ambao kwa sehemu kubwa wakulima wamelima mahindi kiasi cha kuwa na ziada lakini kutokana na uwezo mdogo wa *NFRA*, leo mkulima anabaki na ziada ikumuozea shambani bila kuwa na uhakika wa soko. Hata kama Serikali inasema itajenga maghala kuhifadhi ziada *(surplus),* bado bei ya soko la mahindi haiwezi kumpa mkulima wa mahindi uwezo wa kurejesha gharama za uzalishaji wa bidhaa hiyo muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa *NFRA* imeshindwa kununua mahindi, kuna ugumu gani wa Serikali kutoa kibali kwa wananchi kuuza mahindi kwa kuwa *NFRA* inanunua inachoweza kuhifadhi (ikiwemo kuwauzia *WFP* na *private traders*) lakini bado kiasi cha mahindi yaliyovunwa inabaki mikononi mwa mkulima na kuleta hasara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili mkulima wa mahindi anufaike, ni aidha Serikali iongeze bajeti ya *NFRA* iweze kununua mahindi kwa bei nzuri ama/na kuamua kutoa uhuru kwa mkulima aliyezalisha ziada auze kwa bei ya soko la nje ambalo kwake ni nguvu yake mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. Siungi mkono hoja.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji kwa dakika kumi, ajiandae Waziri wa Fedha naye kwa dakika kumi.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda nimshukuru sana Mwenyezi Mungu, lakini nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri anayoifanya katika kuwaletea maendeleo Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee nitumie nafasi hii kumpongeza Waziri wa Wizara hii pamoja na Naibu wake kwa kazi nzuri wanayoifanya, wamekuwa wakizunguka maeneo mbalimbali ya nchi yetu katika kuhakikisha wanatatua changamoto mbalimbali zinazohusiana na wakulima. Pongezi za kipekee katika nia yao ya dhati kabisa kuondoa tozo zaidi ya 21 katika kuhakikisha zinawaondolea kero wananchi hawa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua kabisa nchi yetu asilimia kubwa ya Watanzania wanaishi vijijini na wanategemea kilimo na kilimo chenyewe ni cha kudra za Mwenyezi Mungu kwa maana ya mvua, lakini Wizara yetu imejipanga vizuri sana katika kuhakikisha na kujua namna ya kuweza kumtoa Mtanzania, lazima tuwekeze katika kilimo cha umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumebainisha eneo ambalo linafaa kwa kilimo cha umwagiliaji katika nchi yetu ni hekta milioni 29,000.4, lakini mpango wa Serikali mpaka itakapofika mwaka 2025 tuwe angalau tuna hekta milioni moja, na moja ya mipango ambayo tumeipanga tumeshafanya mapitio ya miradi yote kuona changamoto. Tumeona kuna miradi mingi ya umwagiliaji lakini haijakamilika, lakini bado uzalishaji wake unakuwa wa msimu mmoja. Tumeshajipanga, baadhi ya miradi ya umwagiliaji sasa hivi inafanya vizuri na imekuwa ikilima zaidi ya msimu mmoja, kama Mradi wa *Lower Moshi,* Madibila – Mbarali pamoja na Dakawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru Serikali kwa kutenga fedha zaidi ya shilingi bilioni 29 ambayo imewekeza katika suala zima la kilimo cha umwagiliaji. Nataka nilihakikishie Bunge lako Tukufu, sisi kama viongozi wa Wizara

tutasimamia fedha hizi katika kuhakikisha tunajenga miundombinu ya maji ili hatimaye miradi hii ya umwagiliaji iweze kuwa na tija. Kwa sababu tunapozungumzia uchumi wa viwanda ni lazima tuwe na kilimo cha umwagiliaji kitakachoweza kutuzalishia mazao ya kutosha na yenye msimu wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo sisi kama Wizara tumejipanga vizuri, na tunaahidi kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo katika kuhakikisha tunawekeza katika kilimo cha umwagiliaji ili mwishowe uchumi wa viwanda uweze kukamilika. Kubwa niwaombe san Waheshimiwa Wabunge tuipe ushirikiano wa dhati kabisa Wizara hii ya Kilimo kwa sababu watendaji wanafanya kazi nzuri sana, na sisi kama Wizara ya Maji tutawapa ushirikiano wa dhati katika kujenga na kuunda miundombinu hii ya umwagiliaji katika kuhakikisha azma ya Mheshimiwa Rais ya uchumi wa viwanda inatimilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine katika bajeti hii tumeona nia ya dhati kabisa ya Serikali kuhusu ujenzi wa Bwawa la Kidunda. Bwawa hili litatumika katika suala zima la maji, lakini pia tutakuwa na kilimo cha umwagiliaji. Hii ni nia njema kabisa ya Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. John Pombe Magufuli, katika uwekezaji wa kilimo cha umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, ajiandae TAMISEMI.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumshukuru Mungu kwa kutufikisha hatua hii.

Pia nichukue fursa hii kuwapongeza Mawaziri wa Wizara hii, Mheshimiwa Waziri, Dkt. Tizeba, pamoja na Naibu wake, kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wakiifanya ndani ya Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie kwa kusema machache katika mambo yaliyoonekana yako ndani ya Wizara yetu ya Fedha. Nianze na jambo la kwanza kabisa kusema kwamba kama Wizara ya Fedha tunatambua umuhimu wa Wizara ya Kilimo kwenye ukuaji wa uchumi wa taifa letu na tumekuwa tukiipa kipaumbele cha kutosha kabisa Wizara hii ya Kilimo kama ambavyo bajeti yetu imeonesha, kwa dhati kabisa tunatambua mchango wake na tutaendelea kuwekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirejee tu kusema Waheshimiwa Wabunge, jambo la msingi tunalotakiwa kuelewa; katika mchakato wa kibajeti na katika *theory* ya uchumi ambayo ni ya kawaida kabisa, tunatambua mahitaji yako mengi kuliko rasilimali *(resources)* tulizonazo. Tukilitambua jambo hili tutaweza kwenda sambamba na bajeti ambayo Serikali imependekeza, la msingi tuweke nguvu kwenda kwenye utekelezaji wa bajeti tuliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niende *specific* kwenye hoja, nayo ilisema ni asilimia kumi, *Maputo Declaration* au *Malabo Declaration* kwamba Serikali ifike huko. Nimeanza kusema kuwa *resources* ziko chache kuliko mahitaji tuliyonayo. Sote kwa pamoja tuko hapa tumeanza kupitisha bajeti hizi, tulianza na bajeti ya afya tukasema iongezwe, bajeti ya maji iongezwe, lakini la msingi tukubali tu kwamba Serikali inatambua umuhimu na inawapa kipaumbele cha uzito wa juu sana wakulima wetu wa taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili tunafahamu kabisa kuwekeza katika sekta ya kilimo ni jambo la kwanza, lakini pia uhalisia uliopo. Sekta ya kilimo ni nani wawekezaji? Wawekezaji kwenye sekta ya kilimo ni wawekezaji binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siamini sana kama Mheshimiwa Dkt. Tizeba ana mashamba ya kupeleka pesa moja kwa moja. Tunachokifanya kama Serikali kuiwezesha sekta hii ni kuziwezesha sekta nyingine ambazo zinafanya kazi pamoja na sekta hii ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge tunasema Serikali ya vitu badala ya Serikali ya watu, si sahihi hata kidogo. Niliwahi kusema ndani ya Bunge lako tukufu kwamba barabara zetu zimewezesha sasa hivi chakula kinaweza kutembea kwenye mkoa unaozalisha kwenda kwenye mkoa ambao hauzalishi, na ndiyo maana limesemwa pia hili, kwamba tunazuia kuuza mahindi nje, na Mheshimiwa Waziri atalisemea vizuri ili ku-*control* mfumuko wa bei, hapana, mfumuko wa bei una-*attributes* zake ambazo zinachangia kwenye mfumuko wa bei, chakula ni sehemu moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwa nini chakula ndani ya Tanzania kinachangia kwa kiwango kikubwa, ni kwa sababu Taifa letu limeweza kufunguka kwa miundombinu ambayo Serikali ya Chama cha Mapinduzi imewekeza kwa kiwango kikubwa. Unaweza ukasafiri kutoka Mbeya ukafika Arusha ndani ya siku moja kwa sababu ya miundombinu. Kwa hiyo, twende tu kwa pamoja tuelewe uchumi unafanya vipi kazi ili tuweze kwenda wote kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yetu ya Kilimo ilisema kuhusu uwekezaji kwenye Benki yetu ya Kilimo *(TADB).* Tulianza kuwekeza shilingi bilioni 60 na mpaka sasa hivi niwapongeze uongozi wa Benki ya *TADB,* katika shilingi bilioni sitini waliyokuwa nayo, sasa hivi wana shilingi 66,785,790,000 wameweza kuongeza kiwango hiki katika utendaji wao wa kazi. Vilevile kama Serikali pia hatukuiacha wazi, tumechukua mkopokutoka *TADB* na kuonesha tunathamini wakulima wetu, bilioni mia mbili na sita zote tumezipeleka kwenye benki yetu ya kilimo. Dhamira ni ileile moja, kuwawezesha wakulima wa Tanzania ili waweze kufikiwa na benki yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kama ambavyo nimekuwa nikiliambia Bunge lako tukufu kwamba Benki ya Kilimo inajiandaa mwezi huu wa tano inafungua tawi hapa Dodoma, mwezi wa sita inakwenda kufungua tawi Mbeya, mwezi wa tisa inafungua tawi Mwanza. Dhamira yetu ni ya dhati, kuwafikia wakulima wetu kule walipo ili waweze kupata huduma hii. Pia katika benki zinazofanya kazi na

wakulima ni Benki yetu ya Kilimo. Popote mkulima alipo akishaonesha *interest* anahitaji mkopo anatembelewa kule alipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kengele imegongwa, naomba nilisemee jambo moja, nalo ni kuhusu Bodi ya Korosho na pesa ambazo zipo. Ni sahihi, pesa ipo na Serikali iko tayari kuitoa lakini lazima tukubali itolewe kwa mfumo upi na inakwenda kufanya nini, hilo ni jambo la msingi sana. Tunalalamika hapa kuhusu utendaji mbovu wa watendaji wetu, lazima tusimame imara wote kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetoa shilingi bilioni kumi kwa sababu tumejiridhisha zinakwenda kufanya kazi ya Bodi ya Korosho, zilizobaki kama Wizara tunaendelea kuzihakiki, na kwa sababu tulishawapa Bodi ya Korosho mwongozo wa nini cha kufanya, wametuletea mahitaji yao na sisi tunaendelea kuhakiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwape mfano tu ndugu zangu umuhimu wa hiki ambacho Serikali yetu inafanya, umuhimu wake ni huu, katika maombi tuliyoyapokea kutoka Bodi ya Korosho, nichukulie kipengele kimoja cha pesa za utafiti. Katika pesa za utafiti walikuwa wameomba shilingi bilioni 7.2, katika shilingi bilioni 7.2 kwa ajili ya utafiti, ndani ya pesa hizi kulikuwa na pesa ambazo haziendi kufanya kazi ya utafiti, sasa ni jambo la ajabu kusema kwamba Serikali tuachie, tupeleke tu kwa sababu sheria inatuelekeza hivyo. Tumepewa dhamana ya kuangalia pesa za nchi yetu. Mfano wa hizi shilingi bilioni 7.2 maombi yalikuwepo na shilingi bilioni 2.8 zinazokwenda kuwalipa *honorarium* watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo dhamira ya pesa ya utafiti kutumia shilingi bilioni 2.8 kwenda kuwalipa *honoraria* watumishi, lazima tumeaminiwa na Serikali yetu kusimamia rasilimali fedha ya taifa letu. Tujiridhishe, hii *honorarium* inayoenda kulipwa, kila mtumishi kwa *honorarium* hii anakwenda kulipwa shilingi milioni 19 kwa mwaka kwa ajili ya *honorarium* tu, hapana, tujiridhsihe anakwenda kufanya kazi gani ya ziada inayomuwezesha kulipwa. Tulianza kubana

matumizi na mafanikio ya kubana matumizi tunayaona kwenye maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme jambo moja nalo ni kuhusu malipo ya watu wa pembejeo. Waheshimiwa Wabunge wamesema vizuri sana; mchanganyiko wanaousema wao ndio ambao Serikali tuliupata, na ili kuondokana nao nani kaiibiwa Serikali katika maombi haya? Vyombo vya uchunguzi vipo kazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waheshimiwa Wabunge, sisi kama wasimamizi wa rasilimali za taifa hili tusimame wote kwa pamoja. Vyombo vya uchunguzi vifanye kazi yao. Mheshimiwa Kunti, vyombo vya uchunguzi ni muhimu sana, kama ni watumishi wa Serikali waweze kujulikana nani aliongeza sifuri kwenye shilingi milioni 20 ikawa shilingi bilioni mbili, lazima tuweze kukubaliana na hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, TAKUKURU ikijiridhisha, tukipata taarifa yao, Serikali iko tayari. Pesa si tatizo kwa Serikali ya Awamu ya Tano, tutatoa pesa tutawalipa wote ambao wanaidai Serikali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa wa TAMISEMI.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPH G. KAKUNDA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kwamba Awamu ya Pili ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo itaendelea kutekelezwa chini ya uratibu wa mipango shirikishi ya maendeleo ya sekta ya kilimo katika Halmashauri zetu n Na kwa kweli utaratibu huu utakuwa mzuri zaidi na utafanikiwa zaidi kama watu wetu watakuwa wamejitolea kusimamia vizuri kwa mujibu wa taratibu na sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo ndipo tunapoagiza na tayari Serikali imeshawaagiza watumishi hasa Maafisa Ugani na Maafisa Kilimo, wahakikishe kwamba mipango ya maendeleo ya sekta ya kilimo katika Halmashauri zetu lazima itekelezwe kwa umakini na weledi wa hali ya juu. Na tunawaamini, watumishi ambao walikuwa wamezoea kuweka kambi katika makao makuu ya Halmashauri hawawatembelei wakulima, Serikali imeshatoa maelekezo kupitia Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba lazima wawatembelee wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hii kama tutaendelea kuona kwamba kuna uzembe kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wengi wamelalamika hapa, tutaanza kuchukua hatua kali, kwa sababu maelekezo haya ya Serikali ni halali. Lazima wakulima wapate haki yao ya kupata elimu ambayo inatoka kwa watu ambao wameajiriwa na Serikali, na hawa ni pamoja na maafisa walioko katika Halmashauri, Kata na katika Vijiji, lazima wafanye kazi zao. Utaratibu wa kusubiri posho, kwamba lazima kuwe na posho ndiyo mtu akafanye kazi yake ambayo ameajiriwa kuifanya, tumeshaupiga marufuku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kupata kilimo bora kama hakuna elimu bora ya kilimo, na ndiyo maana tunawasisitiza hawa jamaa waweze kufanya kazi yao ambayo wameajiriwa kuifanya, hii ni pamoja na Maafisa Ushirika. Maafisa Ushirika wameshaelekezwa kwamba lazima Maafisa Ushirika wahakikishe wanafanya mapitio ya vyama vya ushirika vya msingi vilivyopo katika maeneo yao kuona utendaji wa vyama vya ushirika kama ni mzuri. Ili kama utendaji wao ni mbovu waweze kuvifuta na kuvisajili upya vyama ambavyo vitawasaidia wakulima. Hayo ni maelekezo halali ya Serikali na sisi tutaendelea kuyasimamia na kuyafuatilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maafisa Ugani wameshaelekezwa wafanye mazoezi ya kuwatambua wakulima wote na mahitaji yao ya pembejeo ili Serikali ifanye

maandalizi mazuri na mapema ya pembejeo, kwa hiyo hilo nalo tutaendelea kulifuatilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nadhani nisiseme sana kwa sababu mwenye sekta mwenyewe yuko hapa, wale watu ambao wako chini ya TAMISEMI waipatepate huko waliko, wajue kwamba sisi tuko macho tutaendelea kuwafuatilia kuhakikisha kwamba uzembe wa aina yoyote hautavumiliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante, Naibu Waziri Kilimo dakika 20.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba niseme kabisa kwamba ninaunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ninamshukuru sana Jehova kwa kunifanya hivi nilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili kwa sababu hii ni mara yangu ya kwanza kwenye hotuba hii, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mbeba maono wa Taifa hili, kwa imani yake kwangu na kuniteua ili nihudumu kwenye Serikali yake ya Awamu ya Tano katika nafasi ya Naibu Waziri, Wizara ya Kilimo. Naomba kumhakikishia Mheshimiwa Rais kuwa naendelea kumuomba Mungu azidi kunipa macho ya rohoni na kamwe nisimuangushe yeye na Taifa letu kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa napenda niwashukuru ndugu na wanafamilia yangu, hususani watoto wangu, marafiki zangu wapendwa *Joseph and David* kwa kuniombea na watumishi wa Mungu wote kuniinua mbele za Bwana katika kutekeleza majukumu yangu haya mapya. Aidha, napenda kuwashukuru wapiga kura wangu, Umoja wa Wanawake wa Chama cha Mapinduzi Mkoa wa Mbeya

ambao wapo mahali hapa ukumbini na ninapenda kuwathibitishia kuwa ni ahsante, tuko pamoja na *A luta continua. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kumshukuru Waziri wangu Mheshimiwa *Engineer* Dkt. Charles Tizeba, Mbunge, kwa ushirikiano na miongozo anayonipa katika kutimiza majukumu yangu kwenye utumishi wangu wa kila siku kama Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuwashukuru watendaji Wakuu wa Wizara *Engineer* Mathew Mtigumwe - Katibu Mkuu Kilimo; Dkt. Thomas Kashililah, Naibu Katibu Mkuu, Watendaji wote katika Wizara, Taasisi na Mashirika yaliyo chini ya Wizara kwa ushirikiano wao katika kufanikisha uwasilishaji wa hotuba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia nikushukuru wewe na Wabunge wenzangu wote kwa ushirikiano na ushauri mwema ambao mmekuwa mkinipa na kunitia moyo, pia bila kumsahau Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, Mungu awabariki nyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia hoja kwa kutoa ufafanuzi wa baadhi ya hoja zilizochangiwa na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza naomba nitoe ufafanuzi wa baadhi ya Wabunge kuhusu *TANECU.* Kama inavyofahamika kwamba *TANECU* ina vyama vya ushirika vya mazao kwa maana ya *AMCOS* vipatavyo 186 vinavyojumuisha *AMCOS* za Wilaya ya Newala na Tandahimba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nilieleze Bunge lako tukufu kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu alifanya ziara Wilaya na nilipata maombi ya kuigawa *TANECU* kutokana na ukubwa wa chama hicho. Aidha, msingi mwingine wa kuigawa *TANECU* ni ukweli kuwa viongozi wa chama hicho

walihusishwa na ubadhilifu na uzembe. Hali hiyo ilibainika pia baada ya uchunguzi uliokuwa umefanywa na tume iliyoundwa na Mkuu wa Mkoa wa Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo Serikali kuanzia leo inaagiza kuwa Chama Kikuu cha *TANECU* kigawanywe ili kukinusuru chama hicho na pia katika kuimarisha ushirika. Kutokana na hatua hiyo Newala itabaki kuwa na *AMCOS* 53 na Tandahimba itakuwa na *AMCOS* 133 na Serikali inasisitiza kabisa kwamba utekelezaji wa maamuzi haya ufanyike kabla ya msimu huu kuanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali inatoa maelekezo kwa Wakuu wa Wilaya wote nchini na Wakuu wa Mikoa wote nchini kwa kushirikiana na Maafisa Ushirika wa Wilaya na Warajisi Wasaidizi wa Mikoa kusimamia mwenendo wa ushirika kwa ukaribu na kuwa ikidhihirika kuwepo uzembe wa aina yoyote katika utekelezaji wa maagizo hayo basi hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao. Ikumbuke kabisa kuwa kwamba katika utelezaji wa suala hilo Serikali haipo tayari kabisa kulipa madeni yoyote ya nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili naomba nifafanue hoja chache za Kamati na mengine Waziri wangu atayatolea ufafanuzi kwa mapana.

Katika hizo hoja za Kamati walisema kwamba hakuna bajeti ya maendeleo iliyotengwa kwa Tume ya Maendeleo ya Ushirika. Naomba niwaeleze Wabunge wenzangu kwamba baada ya kukamilika kwa programu ya mageuzi na *modernization* ya ushirika ile ya mwaka 2015 kwa maana ya *Cooperative Reform and Modernization Program*, Wizara imekuwa ikiandaa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili *(ASDP II)* ambapo kuna miradi kadhaa ya kuendeleza ushirika ambayo itaratibiwa na kusimamiwa na tume ya maendeleo ya ushirika lile Fungu 24.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Wizara inaiongoza Tume ya Maendeleo ya Ushirika kuandika maandiko mapya ya miradi na kuyasajili katika Wizara ya Fedha na Mipango.

Kuanzia mwaka ule wa 2019/2020 tunatarajia Tume hii ya Maendeleo itaweza kujisimamia yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, Kamati imeshauri Serikali kuchukua hatua kwa mawakala waothibitika kuwa ni wadanganyifu pamoja na maafisa wa Serikali walioshiriki kwenye udanganyifu huu. Naomba nilieleze Bunge lako tukufu kwamba katika zile hatua za awali watumishi wa Serikali wote waliohusika wameshakamatwa pamoja na vile vyombo vya dola vimeshawakamata na wamechukuliwa hatua kali sana. Kuhusu mawakala hawa uhakiki unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo Kamati imeishauri ni kwamba ni vyema midada ya zao la kahawa ikaongeza ili kuwa na wigo wa kutosha na hivyo kuwezesha upatikaji wa soko la uhakika. Naomba nilieleze Bunge lako tukufu kwamba kwa sasa minada ya kahawa inafanyika mara moja kwa wiki Mjini Moshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kahawa ikishakuwa tayari kwa mauzo katika maeneo ya uzalishaji nchini hutoa sampuli na kupelekwa Moshi kwa ajili ya mauzo kwa ushindani. Suala la kuongeza minada halileti tija kwa kuwa litaongeza gharama za uendeshaji na kupunguza ushindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya nimeongea kwa ufupi sana ili nisigongewe kengele, lakini Mheshimiwa Waziri wangu ataeleza kwa mapana na marefu na naomba niseme tena, naunga mkono hoja, ahsanteni sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa mtoa hoja.

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kusimamia mjadala huu na kunipa fursa ya kuhitimisha hoja niliyoitoa jana asubuhi kwa kutoa maelezo kuhusu masuala mbalimbali yaliyojitokeza na yaliyozungumzwa na Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kutoa maelezo kuhusu hoja hizo ni vyema niwatambue Wabunge wote waliochangia kwa maandishi na kwa kuongea. Jumla ya Waheshimiwa Wabunge 117 wamechangia hoja hii, kati yao Wabunge 62 wamechangia kwa kuzungumza na Wabunge 54 wamechangia kwa maandishi. *(Makofi)*

Niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yenu ya maandishi na kwa kuzungumza na kimsingi mmetoa hoja nzuri sana zenye malengo ya kuimarisha utelezaji wa majuku katika Wizara yangu. Hii inaonesha ni namna gani Wabunge wako tayari kutoa michango yao ya kimawazo kwa ajili ya kuendeleza sekta muhimu ya kilimo hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, michango iliyotolewa ni mingi sana. Ni ukweli pia kwamba muda niliopewa hauwezi kukidhi kujibu hoja zote zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, naomba mtambue kwamba michango yote iliyotolewa ninaithamini sana na Serikali kwa ujumla kama mlivyosikia inaithamini sana na tutaifanyia kazi kwa umakini ili kuendeleza sekta hii ya kilimo. Majibu ya hoja zote yataandaliwa kimaandishi na Waheshimiwa Wabunge mtapatiwa kabla Bunge hili halijahitimishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kujibu hoja jumla zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Nianze na hoja za Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeishauri Serikali kuongeza bajeti ya kilimo. Ni kweli bajeti ya kilimo kama bajeti za Wizara zingine nyingi hazitoshi. Ukipewa *unconstrained budget* ni matrilioni ya pesa kwa kila bajeti, lakini kwa sababu ya *resource envelope* yetu tuliyonayo bajeti zetu karibu Wizara zote Waheshimiwa Wabunge zinaminywa, ndiyo maana kila Wizara imewekewa ukomo wa bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Wizara ya Kilimo haitekelezi majukumu ya kilimo yote yenyewe peke yake. Muundo wa Serikali yetu Waheshimiwa Wabunge

umegawanya kilimo kitekelezwe katika Wizara nyingine kadhaa. TAMISEMI ndio watekelezaji wa shughuli za kilimo kwa asilimia 80 kwa sabau miradi yote ya wananchi ya kilimo iko katika mipango ya maendeleo ya kilimo ya Halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kilimo kwa muundo wa Serikali yetu Waheshimiwa Wabunge kinatekelezwa na Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Shughuli yote ya umwagiliaji; na nimewasikia humu Waheshimiwa Wabunge mkisema kwamba kilimo cha uhakika ni kile cha umwagiliaji na mimi nakiri, lakini kwa muundo wa Serikali yetu shughuli hiyo ya umwagiliaji inasimamiwa na Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Tuna suala la masoko kwa mazao ya kilimo, ni sehemu ya shughuli za kilimo, hili nalo halisimamiwi na Wizara ya Kilimo, linasimamiwa na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mambo ya maghala, mambo ya *marketing* ya masoko hili na lenyewe limewekwa kwenye Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, mamlaka ya maghala nchini iko Wizara ya Viwanda Biashara na Uwekezaji, hata wale wanaosimamia minada ya korosho hawako chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna shughuli zingine zinatekelezwa moja kwa moja chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Miradi ya kujenga uwezo inatekelezwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Tulikuwa na programu kubwa tu Waheshimiwa Wabunge ya *MIVARF* mnafahamu, hii imesimamiwa chini ya Ofisi ya Waziri, Uratibu na Sera, wamejenga barabara, masoko, wameweka viwanda vidogo vidogo vya kusindika. Yote haya ni sehemu ya kilimo cha nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wizara hii kimsingi ina mambo mawili makubwa, sera ya kilimo na uratibu wa kilimo chenyewe. Katika uratibu kuna mambo ya *research,* kuna mambo ya *back stopping* yaani kutoa msaada wa kiufundi pale unapohitajika. Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge hili jambo la kwamba hela iliyopelekwa kwenye kilimo ni kidogo sana, ndiyo ni kidogo wala hilo si jambo la

kubishania, lakini pia lazima tukumbuke kwamba kilimo hiki hiki tunachokizungumza kinasimamiwa pia na Wizara nyingine za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kwenye jambo la Malabo au *The Maputo Declaration.* Azimio la Maputo linazungumzia kilimo kwa tafsiri ya *FAO,* halizungumzii kilimo kwa tafsiri ya Wizara moja ya Serikali hii, linazungumzia kilimo kwa tafsiri ya Shirika la Chakula Duniani yaani kilimo kwa tafsiri ya *FAO* ni kilimo cha mazao, kilimo uvuvi, kilimo mifugo, kilimo ushirika na kilimo misitu. Sasa ukichanganyna haya mambo matano unaona kwamba hilo tunalolisema asimilia kumi, asilimia sita au kumi kuelekea asimilia kumi halipo *zoomed* yaani siyo la kilimo mazao peke yake na ushirika ambalo linasimamiwa na Wizara yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Waheshimiwa Waheshimiwa Wabunge tunawendelea kukokotoa, na nadhani Waziri wa Fedha atakapokuwa anahitimisha, atakapokuja na bajeti ataonesha sasa maeneo yote haya niliyoyataja yatakuwa yamewekewa au yametengewa kiasi gani cha fedha na hapo ndipo tutatazama sasa kwa tafsiri hiyo pana ya kilimo ni kwamba tumeelekeza kule fedha kiasi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo mazao na ushirika peke yake, haiwezi ikatengewa asilimia kumi ya bajeti Waheshimiwa Wabunge hapana, kilimo kinachojumuisha mifugo, uvuvi, ushirika, misitu na mazao hicho ndicho Malabo au *The Maputo Declaration* kinachohitaji kitengewe angalau tufike kwenye asilimia kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia imeishauri Serikali kuongeza kasi ya kutekeleza kwa vitendo azma yake ya kuzalisha mbolea hapa nchini na kujenga viwanda. Ni kweli hili wala siyo suala la kubishana, huu ushauri wa Kamati tunaupokea moja kwa moja asilimia mia moja kwa sababu leo tunahangaika, mara vocha, mara *BPS,* mara sijui nini hii yote ni kwa sababu uzalishaji wa mbolea ndani ya nchi ni mdogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Taifa tungekuwa tunazalisha mbolea haya mambo ya bei tungekuwa tuna *fix* wenyewe kwa sababu ni kitu *product* inayozalishwa hapa ndani, haya mambo ya ifike wapi, siku gani tungekuwa tunafanya haraka tu, lakini kwa sababu uzalishaji wa mbolea ndani ya nchi ni wa chini kabisa ndiyo maana leo bado tuko katika tafrani hii ya mifumo ya namna gani tuwasaidie wakulima na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge ni rahisi sana nchi inayozalisha mbolea ndani ya nchi yake kuweka ruzuku kwenye hivyo viwanda vinavyozalisha hiyo mboela na mbolea ikawa rahisi au kuweka *resume* ya kodi ambayo inawezesha mbolea kuwa ya bei ya chini kuliko mbolea unayoagiza kutoka nje. Mbolea unayoagiza kutoka ni lazima uingie kwenye mfuko uchukue kule fedha ya kigeni uagize mbolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejaribu ruzuku na vocha, Waheshimiwa Wabunge ninyi wenyewe ni mashahidi, nilikuwa naongea na Mheshimiwa Flatei hapa ananiambia kule kwao utaraibu wa vocha ulikuwa ni miujiza, kijiji kizima wanasainishwa vocha halafu hata mfuko mmoja hauendi watu wanaenda *NMB* wanapiga pesa, kilimo hakibadiliki ingawa kwenye hesabu ya matumizi ya fedha inaonekana mbolea kubwa imepelekwa kule. Sasa hii yote ni matokeo kwa sabau wenyewe hatujawa na uzalishaji wetu wa ndani wa mbolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nifurahi tu kuwaambia kwamba ujenzi wa kiwanda cha mbolea kule Kilwa sasa angalau unatia matumaini. Yale mabishano na mazungumzo yaliyokuwapo kuhusu bei ya gesi itakuwa kiasi gani, wauzie bei kama mtumiaji wa nyumbani au wauziwe ile gesi kama malighafi, hilo jambo sasa limemazika na kwa hiyo hatua inayofuata ni wao kuanza ujenzi wa kiwanda. Hata hivyo kule Mtwara Kampuni nyingine pia ya Kijerumani na yenyewe kwa makubaliano hayo hayo taaraifa ya *tariff* gesi na wao wame-*commit* wataanza ujenzi wa kiwanda. Kiwanda chetu cha Minjingu pale Arusha kinazo sura mbili. Mwanzo walianza na

mbolea ambayo Waheshimiwa Wabunge wengi wameisema haikufanya vizuri na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwaambie watu hawa walijirekebisha wakafanya utafiti wamepeleka kwenye Taasisi za Utafiti (Seriani), kule utafiti umefanyika. Jambo moja lililopo mbolea ya Minjingu inabidi ufanye kwanza utafiti wa udogo kabla ya kwenda kuitumia. Hili jambo tunalitafutia na tumepata mwarobaini wake, tumepata msaada wa magari mawili yanayotembea na maabara ya kufanya *analysis ya* udongo. Haya magari tutayapata ndani miezi miwili ijayo, yatazunguka kijiji kwa kijiji nchini, yatapima udongo ule ni wa aina gani, na kwa hiyo *recommendation* ya aina gani ya mbolea inafaa kwa kijiji gani, inafaa kwa mkoa gani, wilaya gani, sasa habari hiyo tutakuwa nayo. Kwa hiyo mambo ya kupeleka *DAP* nchi nzima holela, kupeleka *UREA* nchi nzima holela, tutaachana nayo hivi karibuni, tutakuwa sasa tunajua kwa uhakika kwamba mbolea hii ukiipeleka Kanda ya Ziwa *acidity* kule iko kubwa sana haitafanya kazi. Hivyo kitu cha kufanya tuwashauri wananchi waweke chokaa *(lime)* kwanza ili tunapopeleka hii mbolea iwe na manufaa kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda tu niseme jambo moja hapa ndani ambalo Waheshimiwa Wabunge wengi wanaweza kuwa hawalifahamu. Matumizi ya mbolea niseme tu ya kukuzia *UREA* tunayotumia sasa hivi nchini hapa, hii mbolea ukiitumia katika maeneo ambako tindikali imekwishafikia ile wataalam wanaita *PH-5* unapoteza mavuno yako kwa asilimia 60.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Mkoa wa Njombe hata wakiongeza matumizi ya mbolea ya *UREA* mara mbili bado mavuno yao hayawezi kuongeza kwa asilimia 30 kwa sababu ardhi ya eneo lile kwa kiwango kikubwa tindikali iko ya juu sana kiasi kwamba mbolea ikiwekwa inatengeneza ukame usiokuwa asilia yaani ukame ambao ni *artificial,* mizizi hairefuki ya mazao kwenda chini kuchukua virutubisho. Kwa hiyo uzalishaji unakuwa wa chini hata kama matumizi ya mbolea yanakuwa yameongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo ndiyo maana tumekwenda kwenye hatua ya kutafuta haya magari. Mwaka 2017 mnafahamu watafiti wetu waliuwawa hapa Dodoma kwa sababu walikwenda wenyewe wenyewe tu vijijini wanachokonoa chokonoa udongo, wakatuhumiwa kwamba labda ni majambazi, wakapigwa wakachomwa moto. Sasa tumetafuta nyenzo *(mobile laboratory)* magari mawili yatazunguka nchini, yatapima udongo na kwa hivyo tutakuwa na uhakika wa aina ya mbolea na mahitaji ya wananchi kila eneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia imeshauri kuwa ni vyema ununuzi wa mbolea kwa pamoja ufanyike mara tatu au mara nne kwa mwaka kadri itakavyowezekana. Mimi nakubaliana na maoni haya ya kamati, lakini nitoe tu angalizo kwa sababu tumefanya hili jambo, tumeyaona mapungufu na changamoto zilizopo. Wakati ule tumewapitisha kwenye semina Waheshimiwa Wabunge tulisema kwamba bei ya mbolea kwenye Soko la Dunia inabadilika sana. Bei ya Mbolea kwenye Soko la Dunia jamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wahindi (India) na Brazil wanapoingia kwenye msimu wa kilimo mahitaji ya mblea duniani yanapanda, kwa hiyo na bei pia na yenyewe inapanda kwenye soko la dunia. Sasa tukitangaza zabuni yetu hapa katika kipindi hicho kwa vyovyote vile tutakwenda kukutana na bei kubwa. Halafu mwezi mmoja uliopita labda ulikuwa umewatangazia watu bei elekezi 47, unakwenda unakutana na bei kwenye *bulk* nyingine inayofuata inayokupeleka kwenye 55; sasa ile inakuwa inawachanganya watu. Wanaona kama vile mfumo huu haueleweki, kwa nini mwezi fulani bei ilikuwa hii, mwezi mwingine bei ilikuwa hii, hii sasa manufaa yako wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo tunachokifanya tunavizia pale ambako bei ya mbolea katika Soko la Dunia iko katika *minimum* kabisa ndipo sasa tumesema tunatangaza na tunanunua ya mwaka mzima ili ikishaingia mbolea inakuwa na bei moja mwaka mzima kuliko hii ya

kununua mara nyingi nyingi, tukinunua mara nyingi nyingi bei haitakuwa moja mwaka mzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, tunapoagiza kiwango kikubwa sana hata wauzaji wanapunguza bei, lakini tunapoagiza tani 29,000, tani 30,000, wauzaji wanaona hawa ni kama reja reja tu kwa hiyo wanatuuzia kwa bei ambayo ni ya rejareja. Kwa hiyo tunavyojipanga sasa hivi tunataka tutangaze zabuni na tunajua bei itashuka kwenye mwezi wa sita, itakuwa ndiyo iko chini kabisa duniani, tutaagiza hiyo mbolea itakayokuwa inatutosha mwaka mzima na tukishafanya hivyo Waheshimiwa Wabunge tatizo tutakalokutana nalo tu ni namna ya kuisambaza, kuifikisha vijijini na hili ndiyo tunajipanga nalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi hapa naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge suala la kuingiza nchini mbolea si tatizo. Tatizo tulilonalo changamoto kubwa ni namna ya kuisambaza, kuifikisha huko vijijini. Tumejiwekea mkakati na hili naomba *support* yenu kwamba tutatumia nyenzo na mamlaka zote za Serikali. Tunayo Kampuni ya Mbolea ya Serikali wana *warehouses* mikoa na wilaya zote, hawa tutawapelekea kwanza mbolea huko. Wafanyabiashara wanaoshiriki katika mfumo huu tumewawekea sharti jipya kwamba ili ushiriki kwenye kuagiza ile mbolea tani 200,000 au 300,000 lazima uwe na mtandao wa kugawanya mbolea kwa eneo la nchi lisilopungua asilimia 60 ili mmoja tu akichukua ile *amount* aliyo-*commit* kuuza tunajua kwamba *at least 60 percent* ya nchi atakuwa amefikisha mbolea, sasa wakiwa watatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na jambo lingine katika hii *issue* ya mbolea wafanyabiashara wamekuwa na tabia ya kupeleka mbolea maeneo yanayotumia mbolea maeneo yanayotumia mbolea kwa wingi tu, kule ambako matumizi ya mbolea ni kiodgo hawaendi kabisa. Ndiyo maana utakuta eneo kama Kakonko kwa rafiki yangu Mheshimiwa Bilago, akipeleka anapeleka tani moja na akifika kule anaipandisha bei sana kwa sababu anajua hiyo mbolea itakaa miezi nane au miezi tisa haijanunuliwa, *and that's a business sense,* wala

mtu wa namna hii huwezi ukamlaumu atakuwa na *storage charges,* atakuwa analipa walinzi, atakuwa analipa nani, sasa akiweka bei ya chini badaa ya miezi tisa mfuko ule utakuwa bado unauzika kwa elfu ngapi hiyo? Atapata hasara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunachokifanya, ili tumpe leseni ya kuwa muuzaji mkubwa wa mbolea, tutawalazimisha wawe pia na maeneo ya kuuzia mbolea kwenye maeneo hayo ya namna hiyo ili tusiwe na *pocket* yoyote nchini ambako eti mkulima akihitaji mbolea hawezi kupata. Kwa sababu atakuwa anauza mbolea nyingi kwenye maeneo ya matumizi makubwa, hiyo itakuwa inafidia hata kule anakouza mifuko 10 au 20 kwa mwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo Kamati imetushauri ni kwamba minada ya kahawa iongezwe, na sisi tunasema minada ya kahawa itaongezwa, lakini kwa sababu tumeanza *commodity exchange* sisi Serikali tulikuwa tunadhani kwamba kahawa yetu ianze kuuzwa kwenye *TMX,* ianze kuuzwa kwenye *commodity exchange. Infrastructure* ya kahawa ya kuuza kahawa kwa mnada iko tofauti kidogo na ile *flow* ya *commodity exchange.* Kwa hiyo nimeshaelekeza kwamba *TMX* waende wakakodi ile *facility* iliyopo pale Bodi ya Kahawa-Moshi ili wao wawe ndio wanafanyia hiyo *commodity marketing* pale pale kuanzia Moshi, lakini isiwe tena huu mnada wa kahawa kama tuliouzoea ambako niseme tu ukweli kateli zilikuwepo kule, watu wanapanga bei nje ya mnada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tukiwaingiza wakulima wa kahawa kwenye *commodity exchange* kahawa yao itakuwa inajulikana tu duniani huko. Niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge wanaotoka kwenye maeneo ya kahawa, kwamba kahawa ikishaanza kuuzwa kwenye *commodity exchange* habari hii ya ushirika ita-*collapse* tu yenyewe, yaani hakutakuwa na haja ya kutumia nguvu sana kuzungumza ushirika gani una nini, unakwenda kwa nani, No, kwa sababu suala lile ni la kimtandao wa dunia nzima kwa hivyo ushirika wamekwenda wao, imeenda *AMCOS* au

imeenda *union it doesn't real make a big difference,* watu watakwenda pale, kahawa yao itajulikana duniani kote, watauza, watagawana pesa, mambo yatakuwa mazuri.

Waheshimiwa Wabunge, sasa naomba hoja zingine za Kamati pia tutazijibu kwa maandishi. Naomba nizungumzie mambo ambayo yamezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge kwa hisia sana, naamini tukiwa na uelewa mzuri kwenye hili jambo na tukaweka *commitment* ya Serikali basi nina uhakika tutakwenda tu vizuri na Mungu atatusaidia.

Mheshimiwa mwenyekiti, nianze tu na hili jambo la soko la mahindi hapa nchini. Kwa kweli, naomba tu niwambie ukweli, mimi ni mkulima, naomba niwaambie huu ukweli kabisa yaani usiokuwa na mawenge mawenge, mimi nalima. Nalima mtama, nalima vitunguu na nalima mahindi. Hii adha na mimi inanipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Lwenge hapa jana alipochangia alisema tunalima wote na mtama umetushika. Wamo humu Waheshimiwa chungu mzima waliolima na wao hawajauza mpaka leo. Wako wakulima wa vitunguu Singida kwa Mheshimiwa Monko, wako wakulima wa vitunguu hapa Kilolo kwa Mheshimiwa Mwamoto, wanalima mwisho wa siku hakuna soko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu Waheshimiwa Wabunge mnisikilize vizuri kwa unyenyekevu sana nalisema hili jambo, *seasonality,* kilimo chetu ni cha kutegemea mvua kwa asilimia kubwa. Kilimo cha vitunguu kwa maeneo mengi huku nacho ni cha msimu, mvua ikiwa inanyesha huwezi kulima. Kwa hiyo, watu wanalima mvua hakuna au watu wanalima mvua ikiwa inanyesha. Kwa hiyo, watu wakiwa wanalima kwa pamoja si ndiyo? Watavuna kwa pamoja, mahitaji yanashuka, *the low of demand and supply* ina-*setting,* na kwa sababu hatuna miundombinu ya kutosha ya uhifadhi wa mavuno yetu tunajikuta tumeingia kwenye hasara, tunajikuta tumeingia kwenye kuuza kwa bei za kutupa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo kama tungekuwa na miundombinu mizuri ya kuhifadhi, natoa mfano tu wa nyanya, mwaka jana watu wamelima nyanya nyingi sana hapa Dumila, hakuna *storage facilities.* Sasa hivi wanalima Parachichi nyingi tu Njombe, hakuna *pack house.* Kwa hiyo wakulima hawa wakivuna, akiona mazao yake yanaelekea kuoza ndugu zangu atauza tu kwa bei ya hovyo hovyo. Si kwamba mimi Tizeba nafurahia haya mambo. Kwa hiyo, Serikali tunachokifanya tunajitahidi ku-*overcome* hii *situation,* tunajitahidi sana ku-*overcome* hii *situation.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti iliyotajwa hapa ni ya Serikali, bajeti iliyosomwa hapa ni ya Serikali, tofauti sana niseme kwa mfano na Wizara ya Afya ambao wadau wetu wa maendeleo wanapeleka fedha kwenye *basket*, si ndiyo? Sisi wadau wetu wameamua kwenda moja kwa moja ku-*address issues* kule. Tunayo programu na *ADB* ambayo itatengeneza *complex* ya kilimo kuanzia uzalishaji mpaka usindikaji na tayari timu ipo inafanya kazi, tumeshakubaliana na ndiyo maana Rais wa Benki ya Afrika alikuwa Tanzania hivi juzi, amefanya mazungumzo na Mheshimiwa Rais, wameshakubalaiana, timu ya wataalam nilikuwa nayo ofisi siku kabla ya jana, hili jambo tunaendelea nalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, habari hii ya watu kuzalisha nyanya, anauza tenga shilingi 2,000 au mwisho wa siku unapita anakwambia chukua na wewe kawapikie watoto wako si sawa. Kwa hiyo, lazima tutafute suluhisho la haya mambo, *one step* ni *Agro processing.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge benki zetu za biashara; *NMB, CRDB* na *Bank of Africa* tumekwishafanya mazungumzo, wamekubali watakuwa wanatoa pesa kila mwaka kwa ajili ya kuingiza fedha kwenye *value addition* yaani kwamba mkulima akishalima, wananchi wengine ambao hawalimi, wa-*takeover* kwenye huo mnyororo wa thamani wale *off takers* wapate pesa, wanunue, wapeleke kwa wasindikaji, wasindikaji wasindike, wapeleke kwenye masoko na bidhaa zetu zikisindikwa masoko yake yapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania leo, niwape mfano tu, juzi hapa ndani hapa *debate* kubwa kabisa ya mafuta ya kula, si ndiyo? Tunaagiza *crude palm oil* tani 600,000; lakini tuki-*process* mahindi tu kuyakamua na kupata *corn oil,* namshukuru sana Mheshimiwa Sokombi alilisema hili jambo. Tuki-*process corn oil* inaweza ikachukua nusu ya mahindi yanayolimwa hapa nchini na bado mafuta yake yasitoshe kwa matumizi hapa ndani. Kwa hiyo hizi benki zime-*commit* kwamba zitatoa fedha kwa Watanzania wanaotaka kufanya hiyo shughuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo wafugaji wanahangaika na mifugo, kwa nini hatuwi na *feed loads* tukatuma mahindi yaliyokamuliwa yakatolewa mafuta, tukachanganya na soya tukapata chakula cha mifugo kizuri tu kabisa? Tumeanzisha programu ya uzalishaji wa soya nchini, *Clinton Foundation* wanatusaidia lakini pia tumeweka kwenye mipango yetu kwamba tuta-*enhance* uzalishaji wa Soya nchini ili tuanzishe utengenezaji wa chakula cha mifugo. Inawezekana watu wale ambao wanasumbuka na mazao yao wakapata masoko ya ndani hapa hapa kwa kuongeza thamani na tukafanya vizuri tu sana katika suala la masoko.

Lakini jambo lingine la masoko Waheshimiwa Wabunge, ziko nchi ambazo tuko jirani nazo lakini kwa hali ilivyo katika nchi zao hawawezi kuzalisha. Burundi, Sudan ya Kusini, Kenya nusu ya nchi hawawezi kuzalisha, hawa tunataka sasa wawe ndiyo soko letu. Kwa hiyo, nilikuwa ninazungumza hapa kwamba taasisi zetu za Serikali na za watu binafsi zichangamkie hizi fursa. Bodi yetu ya nafaka na mazao mchanganyiko; mimi nachelea sana kusema kwamba *NFRA* ndiyo ita-*spearhead* suala la biashara ya mahindi, hapana, wale wana jukumu lao la kisheria la *strategic reserve.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge hili lilianzisha chombo kwa ajili ya shughuli hiyo ya biashara ya mazao. Kuna ule mkopo ambao niliwambiwa hapa ume-*stack,* hapana, mkopo ule utapatikana, hawajajidhatiti sana kwa hiyo huwezi kuwarushia bilioni mia moja. Hizo fedha walizopewa na *NSSF* watazipata, wataendeleza sasa shughuli ya kununua

na kuuza mazao. Tulichokifanya, tunataka tuwatume waende Sudan, si wao ndiyo kazi yao kufanya biashara ya mazao? Tunataka tuwatiume waende Sudan ya Kusini, waende huko Mauritius, huko liko soko la mbaazi, waende wakazungumze na Wahindi wa Mauritus wakubali kununua mbaazi yetu, hela wanapata, kwa hiyo, wakishapata hizi pesa waanze biashara. Kibaya ni kuwaanzishia pesa nyingi ambazo hawatakuwa na uwezo wa kuzitumia halafu waishie kupanga matumizi ya kuzimaliza. Kwa hiyo, tuombe tu kwamba suala la biashara ya nafaka, wenye *mandate* ya kisheria wapo na sisi mtusukume tu kuhakikisha kwamba wanafanya kweli hiyo biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi na mazao yao, nimesema katika hotuba yangu na inavyoelekea haikueleweka sawa sawa. Hakutakuwa na kizuizi kwa mtu yoyote kuuza mazao yake nje. *(Makofi)*

Narudia tena, hakutakuwa na kizuizi kwa mtu yoyote kuuza m azao yake nje. Angalizo tu, wakulima wasiuze kila kitu mpaka cha kula wenyewe, uzeni. Yale mambo ya mpakani pale mtakutana na Afisa *TRA* atakwambia una kiasi gani humu ili aweke *record* unatoka na nini basi, uzeni tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yale maeneo yanayofanya vibaya katika kuvuna chakula, kwa sababu Waheshimiwa Wabunge msisahau kwamba si kila sehemu ya nchi yetu wanavuna vizuri, yako maeneo Tanzania ambayo hayavuni vizuri na sisi kama Serikali hatuwezi kufumbia macho hilo jambo. Kuna mchangiaji mmoja amesema vizuri tu, suala la usalam wa chakula ni suala la usalama wa nchi. Ni vigumu sana Waheshimiwa Wabunge, hata kambi hii naomba mnielewe vizuri, ni vigumu sana kutawala watu au kuongoza taifa lenye watu wenye njaa, ni vigumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo *NFRA* itafanya hiyo shughuli ya kuhakikisha kwamba chakula cha dharura kinapatikana kwenye maeneo ambayo kisheria yatathibitika kwamba yanahitaji msaada wa chakula. Utaratibu

tulioweka ni kwamba wata-*maintain presence* kwenye maeneo hayo, kwa sababu gani; mazao yaliyonunuliwa mwaka juzi, *shelf life* yake ni miaka mitatu kwahiyo lazima yatoke whether kuna dharura au hakuna dharura. si ndiyo? Sasa yake yatakayokuwa yana-*approach shelf life* yake kwisha tutayapelekea tu kwenye maeneo haya ambapo uzalishaji wao sio mzuri ili wananchi waendele kununua kwa bei himilivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na huu ndio mpango ambao nadhani utatutoa hata kwenye haya mabishano, mahindi yaende nje, au yasiende nje, mahinda acha yaende, ngano acha iende, mchele acha uende, chochote, *as long as* hatutafikia hali kwamba sasa eti nchi haina chakula halafu tena, kama ndugu yangu Mheshimiwa Zuberi siku moja alivyosema kwamba nchi imebakiza chakula cha siku tatu. Hiyo ndio *situation* ambayo tutajitahidi tu kama Serikali tusifikie hapo. Hakuna namna tunaweza tukasema eti tumefanya fanya mambo leo tumefikia nchi tuna chakula cha nane au saba. Vinginevyo niwatoe hofu Waheshimiwa kwamba wananchi watakaozalisha wanaruhusa tu ya kupeleka chakula chao huko nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo limezungumzwa kwa hisia sana ni hili la uingizaji wa mbolea kwa pamoja. Nimeshalizungumza na kwa hivyo sitaki kulirudia tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo limezungumzwa na wachangiaji ni hili la pamba. Pamba ndugu zangu, kwanza niweke *clarification* ya moja kwa moja. Ushirika hawanunui pamba, kwa hiyo Mheshimiwa Kiswaga, Mheshimiwa Ndassa, Mheshimiwa Mashimba, Mheshimiwa Njalu na wengine wote wanaozungumza hili jambo kwa mtazamo huo niwafahamishe tu kwamba ushirika kwa sasa, *unless* wana hela zao wenyewe, maana yake sheria haiwazuii kununua, *unles* wana hela zao wenyewe lakini hawatanunua eti watanunua pamba kwa fedha ya wafanyabishara, hili jambo halipo. Hili jambo ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge halipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Ushirika ambayo Bunge hili limepitisha haizuii ushirika kununua pamba na ushirika umekuwa ukinunua pamba miaka yote Nyanza na *SHIRECU* ni washirika wale, lakini kwa msimu huu hawana fedha ya kununua pamba. Suala lililokuwa limezungumzwa hapa ni kwamba wawaweke pamoja wakulima wao na hili jambo Waheshimiwa Wabunge lilitokana na kilio cha wanunuzi wa pamba pia, walisema kwamba wanatumia gharama kubwa sana kuweka utitiri wa wale mawakala huko kwenye maeneo ya huko vijijini, wakaweka *figure* ya watumishi 22,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika kutafakari pamoja nao ikaonekana labda inawezekana watu katika ushirika wao waka-*aggregate* halafu ninyi mkaenda kununua. Lakini inavyoonekana imani bado haipo ya kuwapa washirika hawa pesa. Kwa hiyo kama nilivyosema kwenye taarifa yangu na vyombo vya habari, watu wa ushirika wawaache wanunuzi waende na hela zao, wakakae pale, wapime pamba wao waweke *record* kwamba wakulima wao wameuza kiasi gani, wawaandalie maghala, wakute pamba iko kwenye maghala wawakodishie nyumba kama zinakodishwa huko vijijini, wawatengenezee mazingira ambayo wanunuzi wetu hawatasumbuka kununua pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninachokisema niwaondoe wasiwasi Waheshimiwa Wabunge, kwamba hela italiwa, itaenda kufanya nini, *no,* hela haitaliwa. Serikali yote, kuanzia Wakuu wa Mikoa nchi nzima huko pamba inakolimwa, Wakuu wa Wilaya, Wakurungezi wa Halmashauri wanaochukua *cess* kutoka kwa wakulima hawa ni lazima wawepo huko pamba inakouzwa kujiridhisha kwamba utaratibu unakwenda ambako si mkulima au mfanyabiashara anayepata hasara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo tutalisimamia Waheshimiwa Wabunge, si kwamba ni kitu *impossible*, kinawezekana, tutawasimamia. Msitie mashaka sana na dhamira ya Serikali, tumesema tutasimamia tutawasimamia,

ushirika ule wa wizi ule hatuna namna ya kujiridhisha kwamba tumeukomesha kama hatuanzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tuna-*fear of the unknown*. Walishatuibia tunajua na namna walivyokuwa wanaiba, tukaja hapa Bungeni tukarekebisha sheria, sasa hivi wanafungwa. Zamani hakuna mtu alikuwa anaiba Nyanza anafungwa, sasa hivi jaribu kuchukua kitu cha Nyanza uone utakakoishia. Nimesikia hapa mchangiaji mmoja anasema huko *TANECU* sijui wapi wameiba pesa, wameiba pesa na watafungwa tu, si wameiba pesa? Imethibitika wameiba? Sheria tunayo mkono kwa nini tusiwapate hawa? Tutawapata watafungwa na kufilisiwa mali zao, ndicho kinakachofuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu mmoja Mkuu wa Mkoa wa Mara alisemaje, tunapenda kweli mtu ajaribu kuibia wakulima ili aone tutakachomfanyia. Hata mimi natamani nimpate mmoja atakayeenda kudokoa hela ya pamba aone, tumtoe mfano, kwani kuna tatizo gani kumtoa mfano? Tunamtoa mfano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyeiti, na jambo la pili kwenye pamba Waheshimiwa ni ile shilingi 100. Shilingi 100 ndugu zangu mtakumbuka tu Bunge lililopita hapa wakati wa kupulizia dawa Waheshimiwa Wabunge wote mnaotoka maeneo ya pamba mlikuwa mnadai viuatilifu vimechelewa, viuatilifu hakuna, jamani Wizara inafanyaje, pamba inakufa, pamba inakufa. Tumechukua hatua *extra ordinary* kupata hivyo viuatilifu, tumenunua chupa milioni saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya Serikali ilikuwa bilioni tatu kwa viuatilifu vya mazao yote. Pamba tu iliyozalishwa kwa wingi namna hii msimu huu ilikuwa inahitaji viuatilifu vya bilioni 30. Sasa tungejifunga kwenye bajeti ya Serikali leo tungekuwa na pamba ambayo tunazungumzia? Tumeenda tumezungumza na benki yetu ya kilimo imetoa *LC* kwa makampuni ya kuagiza dawa, wameagiza dawa hiyo ni *commitment* ya benki, imetoa pesa zake sasa italipwaje hiyo pesa? Bajeti ya Serikali ilikuwa shilingi bilioni tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunahitaji pesa kutoka kwa waliotumia hiyo dawa ili tuilipe benki iliyotukomboa. Nataka niipongeze sana Benki ya Kilimo, kwa hili wametusaidia kweli kweli. Kwa sababu wangejielekeza na wao kama benki ya biashara nyingine yoyote wakasema tunataka *collateral* tunataka nini..., leo pamba ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge tunayoizungumza isingekuwapo. Sasa tunataka pesa ya kuwalipa, Mheshimiwa Kiswaga shilingi 30 walikatwa wakulima mwaka jana ndiyo, makadirio ya zao ilikuwa ni tani laki moja, mwaka huu tumekwenda tani laki sita, mwaka kesho dhamira yetu ni tani milioni moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunaweza kweli tukatoka kwenye shilingi 30 ya kuhudumia tani 100,000 tukaenda kwenye shilingi 60 ya kuhudumia tani milioni moja. Tunahitaji fedha na tuwe nayo mapema ili kuwaandalia wakulima mazingira ya kulima. Hakuna itakayempendeza hapa ikifika mweziJanuari, mwaka kesho hakuna dawa ya pamba nchini, nani atafurahi wakulima? Wetu tunawafahamu kutoa fedha mfuko kwenda kununua bomba ni *issue*. Kwa hiyo, niwaombe tu Waheshimiwa Wabunge, 30 zitatumika kulipa deni na hizo bilioni 20 tutaziweka tena benki kama *cash cover* ili watukopeshe fedha nyingi zaidi...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri hiyo ni kengele ya pili lakini kutokana na somo muhimu unalolitoa Bungeni nakuongezea muda kidogo. (*Makofi*)

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge, wakulima wanaelewa sana dhamira ya Serikali. Naomba niwahakikishie, mimi nilikuwa Igunga wakati tunazindua msimu, Mheshimiwa Kafumu ni shahidi yangu. Tulipoeleza haya wananchi walipiga makofi kwa sababu wanakuwa na uhakika. Si wananchi wetu wote wanao uwezo wa kutunza

fedha kusubiria kuwekeza tena katika kilimo, lazima Serikali ichukue nafasi yake. Naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge hii hela haiendi kulipa madeni ya nyuma, sijui ya iliyokuwa mfuko wa pamba. Haiendi kulipa hayo, huko bado hatujaelewana nao nani alisababisha hayo madeni. Tunataka tumjue huyo alipeleka wapi hizo fedha. Kwa hiyo, hii pesa inakwenda kwenye hayo mambo matatu mbegu, dawa na mabomba, na kuna hela kidogo sana ambayo pia ni lazima tuipeleke kwa ajili ya watafiti wetu wa pale Ukiriguru. Vinginevyo hii hela inarudi kwa wakulima wenyewe kwa manufaa yao itasimamiwa na Bodi ya Pamba. Bodi ya Pamba ni chombo cha Serikali. Wanatumia fedha kwa kanuni za fedha za Serikali, akidokoa fedha tunaye. Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge niombe sana mniruhusu tu niendelee na hiki kilimo, mipango si mibaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo moja tu lingine labda ambalo kwa haraka haraka kwa ruhusa yako, naomba niwatoe hofu Wabunge wa eneo la kati hapa la nchi yetu. Ilisemekana kwamba korosho hapa haifai kulimwa na kadhalika. Watafiti wetu na tunao ushahidi, tulikuwa tumeomba mngeweza kuona kwenye *screen* pale jinsi korosho inavyostawi vizuri Mkoa huu wa Dodoma na Mkoa wa Singida. Korosho inastawi vizuri Kongwa kiasi kwamba inazaa mara mbili kwa mwaka. Hiyo ni korosho inayozalishwa huko Singida. Nimuombe tu mdogo wangu na swahiba wangu Mheshimiwa Ditopile anielewe tu kwamba mimi nina wataalamu waliobobea, *a center of excellency* ya korosho duniani iko Tanzania, dunia nzima wanakuja kujifunza kwetu korosho. Sasa tusiwakatishe tamaa watafiti wetu, wanafanya vizuri na nitumie nafasi hii kuwapongeza na kuwashukuru sana, wanachokifanya ndicho hicho wanachostahili kupongezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, korosho inastawi Singida, korosho inastawi Dodoma na hii tunawapa *option* wakulima wetu, wakilima mtama hali ya hewa ikawa mbaya wawe na pa kuangia, angalau kwenye korosho. Wakilima mahindi yakakauka wawe na angalau na kilo mia moja za kuuza waende sokoni wanunue mahindi. Tusiwaache tu kwamba

wakilima zao moja likashindikana basi wao ni watu wa kwenda kupiga hodi kwa Mkuu wa Wilaya kuomba pesa au kuomba mahindi ya msaada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Ahsante Waheshimiwa hoja imeungwa mkono na nikupongeze sana Mheshimiwa Waziri, umekuwa *man of substance* umefanya kazi nzuri sana. Sasa Mheshimiwa Tizeba wale waliofikiri unaondolewa sasa hivi wanalia naona. Katibu.

NDG. RUTH MAKUNGU- KATIBU MEZANI:

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 43 – Wizara ya Kilimo

Kif.1001- *Admin. and HR Management*.....Sh.6, 906,755,300/=

MWENYEKITI: Waheshimiwa nina majina ya vyama, Mheshimiwa Edwin Ngonyani, Mheshimiwa Nape.

MHE. NAPE M. NNAUYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka tu maelezo ya Serikali kwenye suala la pembejeo. Maelezo ya Serikali juu ya maboresho ya suala la pembejeo na hasa majibu yao juu ya suala la *export levy* kwa kweli hayaridhishi.

Kwa hiyo, nilikuwa natafuta maelezo ya ziada kutoka kwa Serikali na kama yataendelea kutoridhisha nitakamata shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wake hapa ni moja tu kwamba maelezo waliyoyatoa yanaonesha vikwazo vingi mno. Vikwazo hivi mpaka vitakapokwisha msimu utakuwa uko katikati na kwa hiyo, watachelewa na kwa kweli watakuwa wameua kabisa zao la korosho. Kwa hiyo, ombi langu hapa ni kwamba, kama Serikali wanayo maelezo ya ziada kuliko yale waliyoyotoa kama yanaweza kushawishi vinginevyo basi niondoke na shilingi yangu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa kwanza kabisa nimshukuru sana Mheshimiwa Ashatu Kijaji, Naibu Waziri wa Fedha kwa maelezo aliyoyatoa kuhusu jambo hili na kwa hivyo kwa upande huo wa fedha na namna ambavyo itatoka ikimpendeza ataongeza maelezo. Mimi nizungumzie tukiwa katika hali hiyo Wizara tumefanya nini, Serikali ili-*commit* kwanza shilingi bilioni kumi kwa ajili ya kuanza uagizaji wa *sulphur*. Kampuni ya Mbolea ya Taifa *(TFC)* wamekwishapewa hii pesa ile na kupewa *go ahead* ya matumizi ya hizi fedha waweze ku-*commit* na uingizaji wa *sulphur* na wameingia mkataba wa kuingiza *sulphur* tani 15,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tulizungumza mara ya mwisho na Gavana wa Benki Kuu na wakawa wamekubali wataandika *OC* moja kwa moja wao ili yule *supplier* aweze kuwaletea *sulphur TFC,* hiyo ni tani 15,000. Pia vyama vikuu vya ushirika waliruhusiwa na wao waiingie mikataba ya moja kwa moja na *supplier.* Kwa hiyo, Chama Kikuu cha Ushirika cha *TANECU* wakaingia mkataba na kampuni moja iwaletee *sulphur* ambayo inawatosha wanachama wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini yako maeneo ambayo wanazalisha korosho lakini hawana vyama vikubwa vyenye uwezo wa kuagiza *sulphur* vyenyewe hivi hivi. Kwa hiyo hivi ndivyo ambavyo *sulphur* itakayoagizwa na *TFC* itakwenda maeneo ya namna hiyo. Bodi ya Korosho pia imeingia mkataba na kampuni mbili zitakazoingiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanzo walikuwa wameingia mkataba na kampuni tatu, lakini kampuni moja baadae ikaonekana inasuasua na kwamba inaweza ikatuchelewesha, kwa hiyo tukavunja mkataba ule mkabata ili wale ambao wako *active* na tumeona *commitment* ya maana ya *shipping document* zao, wale tumewapa sasa ruhusa ya kuingiza *sulphur.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla katika *commitment* hizi *sulphur* kiasi cha tani 35,000 itaingizwa nchini. *Sulphur* hii tumeiwekea bei elekezi na tumewaambia *suppliers* wote baada ya ku-*scan* soko la *sulphur* huko inakotoka, kwamba asitokee mtu au chama cha ushirika wale wanao-*contract* wenyewe akatuingizia *sulphur* hapa nchini atakayoiuza zaidi ya shilingi 32,000 kwa mfuko wa kilo 50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka ninavyozungumza hapa *sulphur* iliyoingia nchini tani 7,680 kati ya *sulphur* hiyo tani 7,680 tani 1,320 tayari imeshagawanywa kwa wakulima na sasa hivi wiki hii tutaanza kugawanya *sulphur* kwenye maeneo yote yale ambayo maua tayari kwenye mikorosho yameanza kutoka kwa sababu hata korosho yenyewe sio kwamba maua yanatokea kwa korosho eneo lote linalolimwa korosho kwa hivyo kwa sababu tunajua zile *spots* ambazo...

MWENYEKITI: Uwe unasikiliza kengele lakini endelea kidogo. *(Kicheko)*

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tunafahamu yale maeneo ambayo wanatangulia kabisa hii tani 5000 na zaidi ambayo iko nchini hii tunam-*direct* wiki hii ianze kupelekwa maeneo hayo ili wakulima wasihangaike na kwa vyovyote vile bei haitavuka shilingi 32,000.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Nape.

MHE. NAPE M. NNAUYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru pamoja na maelezo ya Mheshimiwa Waziri ambayo ameyatoa upande mmoja na upande wa *export levy* amesema Wizara ya Fedha watatoa inaonekana wenzetu hawaelewi ukubwa na matatizo ya jambo hili.

Kwa hiyo, naomba kutoa hoja wenzangu ambao wameathirika na tatizo hili tulijadili pengine tuwasaidie wenzetu waelewe ukubwa wa tatizo ili watusaidie namna ya kulitatua. Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ghasia, Mheshimiwa Bwanausi, Mheshimiwa Ulega, Mheshimiwa Kangi, Mheshimiwa Mgumba, Mheshimiwa Ashatu, Mheshimiwa Masala, Mheshimiwa Mwambe, Mheshimiwa Katani na Mheshimiwa Chikambo. Mheshimiwa Khatib vipi upo? Haya Mheshimiwa Ghasia.

MHE. HAWA A. GHASIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba niunge mkono hoja kwa sababu kama ambavyo wametangulia kusema kupitia sheria ambazo zilitengenezwa na Bunge hili zao hili lilikuwa na chanzo chake cha *export levy* ambapo asilimia 65 inayopatikana inaenda kwenye mfuko wa kuendeleza zao la korosho na asilimia 35 inaenda katika Mfuko Mkuu na hii pesa tunayoizungumzia ni ya msimu wa mwaka 2016/2017 ambao mwaka 2017/2018 tutatumia kwa msimu huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tunavyozungumza tayari baadhi ya maeneo wameshaanza kupuliza na kwa utaratibu kama Serikali inatumia *export levy* wananchi wanalipa nusu ya bei na kwa kawaida tulipaswa kununua kama hiyo ni shilingi 32,000 maana yake shilingi 16,000. Sasa hivi Mheshimiwa Waziri anatoa maelekezo kwamba inunuliwe si zaidi ya shilingi 32,000 maana yake ile pesa ya *export levy* haina mchango hata kidogo kwa mkulima kwa sababu mkulima alikuwa anachangia nusu na Serikali inamchangia nusu. Lakini pesa hiyo ya *export levy* sio kwa pembejeo tu inatakiwa iende kwenye kituo cha *research* cha Naliendele, inatakiwa ikajenge maghala na inatakiwa pia

ikasaidie katika masuala mazima ya ugani na mpaka sasa hivi tunavyozungumza mikorosho imeshaanza kutoa maua na unapoanza kupuliza unapuliza mara tano kila baada ya siku 21. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Bwanausi.

MHE. JEROME D. BWANAUSI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi na mimi niunge mkono hoja ya Mheshimiwa Nape kwamba kwa kweli inaonekana Serikali haijawa makini katika kuhakikisha kwamba zao hili linaliendeleza. Tulifuatailia sana suala hili tangu mwanzo na tulishatoa angalizo kwa Serikali kwamba kama hamkulifanyia kazi jambo hili tutaliathiri kabisa zao la korosho na kwa mwenendo unavyoelekea ni kwamba hata huo upanuzi wa kupanua korosho kwa mikoa 18 hauna maana kama hizi fedha za *export levy* zitakuwa hazitolewi.

Kwa hiyo, naomba Serikali kwa kweli isiwe na kigugumizi katika kutoa fedha hizi na ni yale maeneo kama alivyosema Mheshimiwa Waziri ni kwamba hata hivi tumeshachelewa anasema wiki ijayo ndio tutapeleka *sulphur* kwenye maeneo ambayo maua tayari, kwa hiyo niiombe Serikali kuhakikisha kwamba inartoa *commitment* ya uhakika kwamba hizi fedha zipatikane.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwambe.

MHE. CECIL D. MWAMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaungana na Mheshimiwa Nape kwenye hili suala la pesa za *export levy* sina hakika sana, umaliziaji wake kwa sababu anaweza akarudisha shilingi kwa maana ya maslahi ya chama, lakini niseme kwamba wananchi wa Mkoa wa Mtwara, Mkoa wa Lindi hii ndio pesa ambayo kwa vyovyote ilikuwa inawasaidia kwa ajili ya kuendeleza zao la korosho na kuongeza mavuno. Tumeona hapa taarifa ya Mheshimiwa Waziri kwenye kitabu wanatarajia kuongeza mazao mpaka kufikia tani 311,000 msimu ujao kama mpaka sasa pesa hii haijawa *released* ambayo iko kisheria kabisa inatakiwa ifike ikawasaidie wale wakulima tunategemea nini?

Mheshimiwa Waziri sidhani kama mmefanya utafiti wa kutosha anasema wataanza kupeleka hii *sulphur* kwenye maeneo ambako tayari maua yanakaribia kuanza. Kuna maeneo mkoa wa Lindi, kuna maeneo mkoa wa Mtwara, kuna maeneo Wilaya ya Newala kule chini Mnavila hawa watu tayari wanatakiwa waanze kupata *sulphur* wameanza kuingiza *sulphur* kutokea Mozambique sasa ni lini Serikali itueleze waziwazi walete hiyo pesa iko kisheria, sio ombi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Katani.

MHE. KATANI A. KATANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na ndugu yangu pale Mheshimiwa Mwambe msije mkashika shilingi halafu ikawa mnatania kwenye jambo *serious* la korosho hili na tumepata kusema mara kadhaa...

MWENYEKITI: Kwanza futa hilo neno lako la kutania kuna mtu anatania kwenye Bunge hapa.

MHE. KATANI A. KATANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachojaribu kusema kwenye suala hili ya *export levy* hii fedha sio fedha ya kuomba kama tunavyoiomba, ni fedha ambayo inatengwa kisheria na imeshatolewa maelekezo yake namna ya matumizi na tunapozungumza leo hatuizungumzii hela la mwaka huu, tunazungumzia fedha jana nilitoa takwimu hapa kwamba shilingi bilioni 77 ya mwaka jana wakati nasema nilisema shilingi bilioni 77 ya mwaka jana ukiacha hii shilingi bilioni 116 ya mwaka huu. Sasa tunapozungumza jambo hili Waziri atuambie kabisa aidha, watuambie kwamba hii *export levy* sasa kwa sababu iko kwenye korosho tu kwenye mazao haya aidha ifutwe kwa sababu haimnufaishi mkulima kwa hali hii kwa sababu iko kwenye korosho tu sasa inapoonekana ...

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Mgumba.

MHE. OMARY T. MGUMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kunipa nafasi nichangie hoja hii na mimi naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Nape kwa sababu msingi wa

jambo hili la *export levy* lilitoka kwa wadau wenyewe wa korosho na lengo kubwa ilikuwa ni kuzuia korosho zisisafirishwe nje ya nchi zikiwa ghafi ili tubangue hapa ndani kwa ajili ya kutoa ajira na kuongeza fedha za kigeni. Lakini mpaka sasa hivi hizo hela tusiporudi kwa wadau wenyewe maana yake hata lile lengo la ubanguaji wa korosho kuwasaidia wabanguaji wa korosho ndani ya nchi utakuwa mdogo.

Kwa hiyo, mimi naungana na hoja ya Mheshimiwa Nape hizi pesa zirudi kwa wadau ingawa ziende kutumika kwa lengo lililokusudiwa ili tuweze kuwezesha viwanda vyetu vya ndani vya wabanguaji wadogo na wakubwa waweze kubangua kuongeza thamani na kuongeza ajira ndani ya wananchi wetu. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mpakate.

MHE. DAIMU I. MPAKATE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Nape kwa sababu *export levy* kama walivyozungumza wenzangu ipo kwa mujibu wa sheria na wakulima wetu tangu imeanzishwa sheria hii wakiwa wanahudumiwa kwa kupewa bei ya nusu mfuko kwa maana ya kwamba bei halisi kama walivyozungumza leo shilingi 32,000 ilitakiwa wakulimwa walipie shilingi 16,000 na wadau wenyewe kwa maana ya wakulima wanajua kwamba pesa hii ipo na bado inahitajika na pesa hii ndio ile ambayo inatumika hata kwenye utafiti. Sasa hivi tuna tatizo la unyaufu ni mikorosho mingi imekauka lakini watu wa Naliendele wanashindwa kufanya kazi yao ya utafiti kujua dawa watapataje kwa kukosa pesa hii. Kwa hiyo, tunaomba sana pesa hii lazima itoke kwa sababu sio hisani ni ya kwao waliamua wenyewe ili iweze kusaidia sekta ya korosho, ahsante.*(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Mpakate. Aha *sorry* Mheshimiwa Chikambo.

MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwanza namuomba Mheshimiwa Nape

aendelee kuing'ang'ania hii shilingi na sisi tutaendelea kumuunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba hili jambo liko kwa mujibu wa sheria kama walivyochangia Waheshimiwa Wabunge wenzangu na kwa kweli kwa kufanya hivyo hatukusudii kusaidia zao la korosho. Ukiangalia kwenye kitabu cha Waziri ukurasa wa 30 ameeleza upatikanaji wa *sulphur,* lakini amesema kwamba wanasubiri Bodi ya Korosho itatangaza bei, lakini sasa hivi anasema kwamba bei wameshaweka bei elekezi.

Kwa hiyo, maelekezo yake tu yanaonekana kwamba yanajichanganya kwa hiyo, namuunga mkono Mheshimiwa Nape na ninaomba hii shilingi tuiendelee kuing'ang'ania kwa maslahi ya wakulima wa korosho ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Masala.

MHE. HASSAN E. MASALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, pia naomba bila kupoteza muda nimuunge mkono kaka yangu ndugu yangu Bwana Nape. Mheshimiwa Nape nitakushangaa sana kama utaiachia hii shilingi ikiwezekana uondoke nayo kabisa mpaka pale tutakapohakikishiwa kurudishwa kwa hii fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii fedha ni jambo la kisheria ni jambo ambalo tumeshakubaliana leo miongoni mwa wakulima ambao wanaathirika ni pamoja na wakulima ambao mimi ninawawakilisha. Tuna mahitaji ya kupata tani zaidi ya 3000 za *sulphur* lakini mpaka sasa nazungumza wana tani 128 maana yake hii tunaenda kuua moja kwa moja uzalishaji wa zao la korosho kitu ambacho hakiwezi kukubalika. Lakini fedha hii inatumika kwenye ubanguaji, inatumika kwenye ujenzi wa maghala, inatumika kwenye utafiti na inatumika kwenye maeneo yote yanayohusu korosho. Mheshimiwa Nape endelea kuishikilia hii shilingi mpaka tutakapopata maelekezo ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Ulega.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza kabisa nimuunge mkono Mheshimiwa Waziri Dkt. Tizeba, naomba ku-*declare interest* na mimi ni mkulima wa korosho mimi na wapiga kura wangu wa Mkuranga ni wakulima wa korosho na jambo moja kubwa ambalo hapa nilitaka nimuombe kaka yangu Mheshimiwa Nape...

MWENYEKITI: Mheshimiwa *order please*.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, muda hauko pamoja nasi na ni ukweli kwamba korosho inataratibu yake na taratibu yake ya kwanza ni kuhakikisha inapata palizi ni pamoja na kupulizia *sulphur*. Kwa nini nasisitiza kwamba muda hauko pamoja nasi sasa hivi *Abbasi Export* pale Dar es Salaam anazo *sulphur* anauza kwa shilingi 32,000 ninahakika ya asilimia zaidi ya 100 nina uhakika kwamba *Abbasi Export* anazo *sulphur* anazoziuza kwa shilingi 32,000. Tutakapomzuia Dkt. Tizeba kwa kumchukulia shilingi yake maana yake ni kwamba mchakatio wa kuweza kupatikana salfa kwa ajili ya wakulima wetu utachelewa zaidi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Kangi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, (MUUNGANO NA MAZINGIRA): Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekaa Lindi na Mtwara miaka 14, najua uchungu walionao wakulima wa korosho lakini nataka niwahakikishie kwamba naunga mkono majibu ya Serikali.

Serikali anayoiongoza Mheshimiwa Dkt. Magufuli ni Serikali yenye macho inayoona, ni Serikali yenye pua inayonusa, ni Serikali ya masikio inayosikia na ndio maana amejipambanua kuhakikisha kwamba wanyonge ambao kundi kubwa ni wakulima anahakikisha kwamba wananufaika na kilimo ambacho wanakilima.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Nape nakuomba Serikali ya Mheshimiwa Magufuli sio ya kutilia mashaka aliyoyasema

Mheshimiwa Waziri kuhusiana na mchakato wote wa ununuzi wa *sulphur* mambo hayo yataenda kufanyika kwa hiyo usiwe na wasiwasi na ndio maana Mheshimiwa Nape umeamua kuwa mwanachama wa CCM ukijua kabisa CCM sio ya kutilia mashaka na umempigia kura Mheshimiwa Dkt. Magufuli ukijua kwamba sio wa kutilia mashaka. Kwa hiyo, naamnini kabisa kwamba hoja yako urudhishe tu shilingi ili Serikali ya Mheshimiwa Magufuli iweze kuwaletea *sulphur,* ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Dkt. Ashatu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru kwa kupata nafasi hii tena na naomba niseme naunga mkono hoja ya Mhesimiwa Waziri wa Kilimo kwamba nimuombe sana kaka na jirani yangu Mheshimiwa Nape kwamba aiachie shilingi ya Mheshimiwa Waziri ili haya ambayo tumepanga kuyafanya kama Serikali yaweze kuifanyika kwa muda muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo naweza kumthibitishia Mheshimiwa Nape ni kwamba Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Mheshimiwa Rais wetu inadhamira ya dhati ya kuhakikisha wakulima wote wa korosho wanapata pembejeo kwa muda muafaka kabisa nasema haya kwa sababu moja tu kumekuwa na malalamiko ya wakulima wenyewe kwamba hawafaidiki na pesa hizi za Bodi ya Korosho ndio maana Mheshimiwa Kangi ametangulia kusema Serikali ya Mhesimiwa Magufuli ni ya wanyonge ni ya wakulima ndio ikasema tusikilize malalamikao yao tufanye uhakiki na tathimini ni nini wanalalamika wakulima ili kila shilingi inayotolewa iende kwa wakulima kweli, nilitoa mfano mdogo tu katika pesa bilioni saba iliyoletwa na...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri ngoja kwanza.

Waheshimiwa Wabunge tuko katika *serious discussion* mmejenga hoja za msingi majibu yanatolewa hamtaki kusikiliza na wengine hapa wala hata korosho hawaijui. Kwa hiyo, msishabikie vitu kwenye vitu *serious,* kuna *serious*

discussion hapa na nitaanza kuwataja watu wasiohusika na korosho ambayo ndio mnashabikia huku Mheshimiwa Dkt. Ashatu endelea. *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hii kwa sababu ya hayo malalamiko ya wakulima Serikali ikaona ni muhimu kwenda kujiridhisha hiki kinachotendwa ni sahihi nimetoa mfano wakati nachangia hoja hii, katika bilioni saba zilizoletwa kwenye orodha kwa ajili ya utafiti bilioni 2.8 zinakwenda kulipa *honorarium* sasa kama Serikali tunajiuliza ni *honorarium* ya nani katika orodha hiyo iko pia posho ya shilingi 1.3 kuna *honorarium* kuna posho. Waheshimiwa Wabunge tujiridhishe hivi maana ya *honorarium* na posho maana yake ni nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika pesa hiyo ya utafiti kuna shilingi bilioni 1.35 kwa ajili ya uratibu sasa hebu tufikirie haya yote yana kwenda kweli kwa mkulima? Ndio maana tunasisitiza Serikali ya awamu ya tano ina dhamira ya dhati ya kuhakikisha mkulima anafaidika na pesa inayopatikana kwa jasho lako nimuombe sana Mheshimiwa Nape dhamira ya dhati ya Serikali yako unaitambua nikuombe mrejeshee Mheshimiwa Waziri shilingi yake ili tukafanye kazi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru ninaelewa *concern* za Wabunge wengi hapa na nimuombe kwanza kabisa mkwe wangu Mheshimiwa Nape arudishe shilingi ya Mheshimiwa Waziri ni kwa sababu gani? Ni kwamba sisi kama Serikali *commitment* ipo na Mheshimiwa Naibu wa Fedha sasa hivi ameshatoka kusema ni kwamba hiyo shilingi bilioni saba ambayo inazungumziwa tunatakiwa tuifanyie uhakiki na mchanganuo wa shilingi bilioni saba ukoje.

Lakini kwa maana hiyo naomba niseme tu kwamba sisi kama Wizara tumejiongeza na ndio maana tukasema tunahakikisha kwamba *sulphur* inapatikana kupitia kwenye

AMCOS zetu na vilevile kupitia katika Bodi ya Korosho. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge wote tuiunge mkono bajeti ya kilimo na turudishe mshahara wa Waziri kwa sababu Serikali ya Awamu ya Tano iko *fit* na ina jicho kali, ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa *Chief Whip.*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa iuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote tunajua suala zima la umuhimu wa kilimo kwenye mazao yote lakini katika eneo hili la zao la korosho kama ilivyojadiliwa na Waheshimiwa Wabunge wengi ni jambo la msingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema yafuatayo kwanza nimuombe sana Mheshimiwa Nape arudishe shilingi ya Mhesimiwa Waziri kwa sababu zifuatazo; sababu ya kwanza sisi kama Serikali kwa mujibu wa kanuni tulizopewa na Bunge lako tukufu Kanuni ya 105 kunapotokea jambo ambalo tunaona katika mjadala limeshindwa kutufikisha mahali...

MWENYEKITI. Mheshimiwa, hebu isome hiyo Kanuni ili Wabunge wapate kuifahamu

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti kama muda wako utaniruhusu niongee kidogo...

MWENYEKITI: Nimekuruhusu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, basi nitaomba niisome kanuni hiyo.

Kanuni ya 105 inasema kwamba baada ya Bunge kukamilisha mjadala wa makadirio ya Wizara zote, mjadala wa makadirio ni kama hivi tunavyoendelea na mjadala,

ndani ya siku sita kabla ya hotuba ya bajeti kusomwa Bungeni, Serikali kwa kushauriana na Kamati ya Bajeti itafanya majumuhisho kwa ajili ya kuzingatia hoja zilizojitokeza wakati wa kujadili wa utekelezaji wa bajeti za Wizara kwa mwaka wa fedha unaoisha na makadilio ya bajeti ya Wizara hizo kwa mwaka wa fedha unaoisha na makadirio ya mwaka wa fedha unaofuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimesimama hapa kumuomba Mheshimiwa Nape suala hili wote tumeshalisikia, Mheshimiwa Waziri ameshaeleza kazi inaendelea kwa sasa, Serikali imeshatoa hizo shilingi bilioni 10 lakini Waheshimiwa Wabunge wanasema ni lazima Serikali iendelee kuangalia kusudi jambo hilo liweze kufanyika na fedha ziendelee kutolewa kwa namna itakavyowezekana. *(Makofi)*

Kwa mujibu wa kanuni hii, nimuombe Mheshimiwa Nape aachie shilingi ya Waziri tupitishe bajeti leo na kama bado kuna hoja ya kuzungumza tunazo siku sita kati ya Serikali na Bunge kuendelea kujadiliana mambo mbalimbali ambayo yatakuwa yamejiri wakati huu wa bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimdhihirishie Mheshimiwa Nape nia ya Serikali ni njema, *commitment* yetu katika kuhakikisha tunaendeleza kilimo ni kubwa na hakuna mtu asiyejua kwamba Serikali hii imedhamiria kufanya mapinduzi makubwa ya maendeleo katika nchi yetu ya Tanzania. Namsihi sana Mheshimiwa Nape kanuni tunayo, lakini vilevile asikilize hayo yote ambayo tumeyasema kama Serikali arudishe hiyo shilingi ya Mheshimiwa Waziri na huko mbele tutapata nafasi ya kuendelea kujadiliana na mwisho wa siku tunaweza kutatua matatizo mengi tu katika sekta yetu ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

MWENYEKITI. Ahsante Mheshimiwa *Chief Whip.*

Waheshimiwa Wabunge Kanuni 105 ndio inavyosema, na inasema siku sita kabla ya hotuba ya bajeti. Sasa

nakuomba Mheshimiwa Nape siku sita kabla hotuba ya bajeti ni mbali kutokana na *sensitivity* ya hoja yako, nakuomba mrudishie Mheshimiwa Waziri shilingi yake na naiagiza..., wewe Mheshimiwa Paresso kuna korosho kwenu? *(Kicheko)*

Nakuomba Mheshimiwa Nape ntakupa nafasi nna uwezo wa kuifunga hoja sababu ndio kanuni inavyosema, siisubiri siku sita kabla ya bajeti naiagiza Kamati ya Bajeti kesho. Mkae na Nape, mgeni rasmi wa Kamati yenu ni Nape na Wabunge wote. Wabunge wote wanaohusika na jambo hili waende kwenye Kamati ya Bajeti kesho baada ya kipindi cha maswali. Mheshimiwa Nape. *(Kicheko/Makofi)*

MHE. NAPE M. NNAUYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa busara na kuona uzito wa jambo hili kwa sababu kwa kweli kuiachia shilingi hapa ilikuwa ni kuwasaliti wakulima wa korosho, lakini ninaamini kwamba kikao cha kesho na Kamati ya Bajeti hatutakwenda kufanya blaa blaa maana yake vinginevyo tutarudi hapa kushughulikiana, kwa sababu kwa kweli kwetu sisi korosho ndio siasa ya Kusini. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kwa imani yako wewe hayo mengine yote nimepata nayo taabu lakini kwa imani yangu kwako na kwa maelekezo yako *engineer* endelea na kazi yako.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Haonga.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana ninaomba hoja yangu inahusu masoko ya mazao kuwa chini, lakini nitajikita sana kwenye soko la mazao ya mahindi. Ninaomba tu kwamba kama majibu kama yatakuwa hayaridhishi kama yatakuwa ya ubabaishaji, nitashika shilingi ya Waziri.

MWENYEKITI: Mheshimiwa hebu tuwe na lugha ya Kibunge, nani anakubabaisha humu ndani?

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Kama majibu yatakuwa hayaridhishi.

MWENYEKITI: Sema kama majibu hayakuridhisha. Una maana hapa Kiti kina babaisha, Serikali inababaisha?

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana nimekuelewa, kama majibu yatakuwa hayaridhishi nitashika shilingi ya Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu wote kwamba zao la mahindi bei iko chini sana, karibu maeneo yote yanayolima mahindi kanda ya nyanda za juu kusini, Mkoa wa Songwe, Mkoa wa Mbeya, Mkoa wa Rukwa, Mkoa wa Ruvuma na maeneo mengine yote mahindi kwa kweli yako chini sana, ni kwa sababu ya uzembe wa Serikali wa kufunga mipaka.

MWENYEKITI. Mheshimiwa Haonga uzembe unatoka wapi? Hivi saa zingine mkikaa huko kama husemi maneno maneno unaonekana baba mshamba mshamba mpaka useme maneno uonekane wewe mjanja. Nitakukalisha!

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba wakati Waziri anajaribu kutoa majibu hapo alisema kwamba yako baadhi ya mambo yanayohusika kwenye Wizara ya Viwanda na Biashara. Ninachokijua ni kwamba Serikali ni moja, sasa kama Serikali ni moja ninaamini kwamba hamna jambo linaweza likafanyika bila Serikali kukaa pamoja na kujadiliana na Wizara hii ya Viwanda na Biashara naamini kwamba haipo Uganda ipo Tanzania. Ninaomba sasa majibu ya Serikali katika hili, je, *commitment* ya Serikali, wananchi wale waliolima mahindi na sasa yako kwenye ma-*godown* mengine, yako majumbani mwao je Serikali iko tayari kuyanunua mahindi hayo? Lakini pia Serikali haiwezi kutoa *commitment* nyengine hapa kwamba hawatafunga mipaka tena. Nashukuru sana.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nahitimisha hoja nilisema maneno haya kwamba hata mimi ni mkulima na kuna mazao yamenishika.

Kwa hiyo, suala la masoko ya mazao na sio zao la mahindi peke yake mazao mengi tu, lina tabia yake ambayo sio kwanza *predictable* kihivyo, lakini linaweza likapanda au likashuka *anytime* na ndio maana katika wakati fulani hapa nchini ulianzishwa utaratibu kwa watu waliokuwepo miaka ile sijui niwaite wahenga. *STARBUCKS* ilianzishwa kama *instrument* ya *price stabilization* yaani kwamba bei ikipomoloka sana ya zao kupelekea watu kupata hasara basi mfuko huo utumike ku-*compensate* wakulima ili waweze kuingia kwenye msimu unaofuata bila ya kuwa na hasara kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, soko la mahindi na pamoja na soko la mazao mengine yote kwa pamoja kwangu mimi na kwa Serikali kama unavyosema ni jambo pia ambalo ni la kipaumbele kwa sababu wakulima wasipouza *purchasing power* yao inashuka. *Purchasing power* yao ikishuka hawaendi madukani kununua bidhaa. Wasipoenda kununua bidhaa madukani *consumption Tax VAT* haitozwi, mapato ya Serikali yanashuka. Kwa hiyo, sio kwamba suala ambalo eti huku Serikalini halipewi umuhimu kwamba watu wauze mazao yao. Lakini *situations* ya wakati ule ilikuwa ngumu kidogo Zambia walikuwa wamefunga mipaka, nchi zingine wamefunga mipaka, mnaona! Lakini hili lisitufanye sasa tusiende mbele, nimekwisha *commit* hapa kwamba hatutakuwa tena na *export burn* ya mazao yetu. *(Makofi)*

MWENYEKITI. Mheshimiwa Haonga *commitment* imeshatolewa.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mazungumzo yangu ya awali niliomba *commitment* katika maeneo mawili kwamba moja suala la...

MWENYEKITI. Hoja yako inatakiwa iwe moja tu Mheshimiwa.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naona kama majibu hayajitoshelezi naomba kutoa

hoja ili Wabunge wenzangu muweze kuniunga mkono kwa maslahi mapana ya Watanzania ambao wanaishi maisha ya chini lakini mazao yao bado hayajanunuliwa hadi sasa. Naomba mniunge mkono Waheshimiwa Wabunge.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ryoba, Mheshimiwa Sophia, Mheshimiwa Aida, Aida tayari kaa chini. Mheshimiwa Sakaya, Mwambe tena, nafasi ndogo. Mheshimiwa Kunti, Mheshimiwa Chikambo, Chikambo nilishakuita wewe basi kaa chini huwezi kupata namba. Mheshimiwa Aeshi, kule nyuma nani kule? Mheshimiwa Bulembo, Mheshimiwa Mattar, Mheshimiwa Makamba, Mheshimiwa Kandege, Mheshimiwa Chumi, Mheshimiwa Nagu, Mheshimiwa Mlinga, Mheshimiwa Mlata, Mheshimiwa Mhagama, Mheshimiwa Subira na wewe umesimama? Umesimama au ulikuwa unajinyoosha? Wewe si mwenye hoja kaa tu. Haya Mheshimiwa Ryoba.

MHE. CHACHA R. MARWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitegemea kwamba hapa ndipo Serikali ya CCM ingekuja na majibu kwamba kwanini mahindi bei iko chini? Kila siku nasikiaga mnasema Serikali ya viwanda, kweli mnategemea kwamba tu-*exports* mahindi ndio bei ya mahindi iwe juu. Mimi nilitegemea viwanda sasa hapa ndio mngejenga viwanda vingi vya ku-*process* mahindi ili tuweze kuuza unga lakini hilo halifanyiki mahindi siku zote yako chini.

Kwa hiyo, niombe kwa sababu hii ni Serikali ya viwanda, tupewe *commitment* nini kinafanyika kuhusu ku-*process* mahindi. Ili mahindi yetu yawe na soko, sio kutegemea ku-*export* mahindi sijui kwenda wapi, tu-*process,* tuuze unga. Hapo ndio tutajua ya kwamba mko makini kama hamuwezi ku-*process* mahindi msitudanganye hamuwezi, mmeshindwa.

MWENYEKITI. Mheshimiwa Sophia.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga hoja ya ndugu yangu Haonga kwa sababu Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini hususani Mkoa wa Mbeya wakulima mwaka juzi walilima mahindi kwa wingi, kwa kutumia gharama zao wenyewe ilipofika wakati wa kuuza

neno ambalo Mheshimiwa Waziri Mkuu alilizungumza humu Bungeni la kuzuia mipaka ya watu kwenda kuuza nje ya nchi liliwafanya wakulima wabaki na yale mazao mpaka leo na wengine wameshindwa hata kupeleka watoto shule kwa kukosa soko la mahindi.

Ninaomba *commitment* ya Waziri tena azungumze ni lini na vipi atawasaidia wakulima wanapolima kwa gharama zao waweze kuuza na kupata faida? Ninaomba *commitment* ya Waziri Mkuu upo hapa uwasaidie wananchi wa Nyanda za Juu Kusini waweze kuuza mahindi kwa gharama wanazotaka, kwa soko wanalolitaka na kwa wakati wanaotaka bila ya kuingiliwa na Serikali. Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Aida.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Haonga kwa sababu mkulima anapata pembejeo kwa muda ambao sio muafaka, mkulima anapata shida zote hakuna mtu anayemsaidia na majibu ya Waziri tulitegemea angetuambia kwamba soko lipo au halipo, lakini na yeye amelalamika. Kwa maana hiyo wakulima wanaendelea kulalamika vilevile kama Waziri alivyolalamika. Tunategemea Serikali itatuambia hapa kwa kuwa yenyewe ndio ilizuia na leo mahindi yanaoza watuambie soko lipo wapi? Upande wa Afrika Mashariki hiyo fursa tunaitumiaje? Na naiomba Serikali wasiwe wanatoa matamko bila ya kuangalia muda ambao wanaweza kutoa wakati huo soko lilikuwepo kwa sasa hamna. Wao ndio wanunue kwa kuwa walizuia wao. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Sakaya.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, naomba mkono hoja ya Mheshimiwa Haonga, lipo tatizo kubwa sana kwa kweli na ni jukumu la Serikali kuwaambia wakulima wanawezaje kupata soko. Lakini Mheshimiwa Waziri kuja tena analalamika na yeye amekwama wakati tunawashawishi

wananchi walime wanakopa mabenki, wanakopa kwa taasisi za fedha, wanalima kwa shida leo tunawambia kwamba hakuna masoko tunatakiwa tuwapatie *solution*.

Kwa hiyo, Serikali ituambie sasa mahindi ambayo yapo Kaluwa debe ni shilingi 4,000 mpaka 5,000; gunia shilingi 25,000 mpaka 30,000 wakati wanadaiwa yananunuliwaje? Na sio kuleta malalamiko tena mahali hapa. Serikali iwaambie wakulima wa Tanzania tunapoenda kuwashawishi walime haya ambayo yapo kwenye maghala yanakwenda wapi? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Bulembo.

MHE. ABDALLAH M. BULEMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwanza kabisa naunga hoja ya Waziri, lakini hebu tuelewane na inawezekana wakati wa majibu tunakuwa hatuko tayari kwenye majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye majibu ya Waziri amesema hivi Bodi ya Mazao Mchanganyiko itapewa pesa itaenda kuangalia masoko nje ili wananchi watakapoweza kwenda kuuza mazao yao. Lakini la pili akasema hivi mipaka sasa ipo wazi watu waende wakauze mazao yao nje. Hoja imeshaisha, imeshakubali sasa Waziri akishaweka *commitment* hiyo tunataka tuweke *commitment* ya aina gani? Bwana Haonga wewe kubali tu pamoja uko *boarder*, *boarder* imesharuhusiwa kuanzia jioni ya leo peleka mahindi nje kwa sababu wewe ni wa kupeleka kule. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Aeshi.

MHE. KHALFAN H. AESHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpongeze na kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kuruhusu mahindi kwenda nje, hii ni hatua moja kubwa sana kila mbunge aliyeko hapa aliyetoka Nyanda za Juu Kusini alikuwa nalilia kilio kikubwa kwamba tupatiwe uhuru wa kuuza mahindi kokote tunapotaka. Serikali imesikiliza na imeturuhusu kuanzia leo mahindi tunauza kokote tunakotaka. Naomba niseme jambo dogo, soko la mahindi *automatically*

lenyewe kama itakuwa mipaka ipo wazi itjipandisha yenyewe moja kwa moja.

Kwa hiyo, niseme Serikali imeamua kununua mahindi na kama imeachia mipaka kuwa huru basi haya mahindi hatutawapa mzigo Serikali tutauza sisi kokote tunakotoka nasema niipongeze Serikali kwa hatua kubwa iliyochukua imesikia kilio cha wananchi na sisi tunaunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kwa mamlaka ya kiti naongeza nusu saa na mara nyingi tunapenda Wabunge wakati Serikali inajibu muwe *very attentive* ndani ya Bunge. Wakati Waziri anajibu kila mtu anashughuli yake, halafu unakuja na hisia kitu kinaku-*burn* kumbe jibu limeshatolewa. Mheshimiwa Kunti.

MHE KUNTI Y. MAJALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa na mimi fursa ya kuweza kuchangia hoja ya Mheshimiwa Haonga na naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Haonga. Wakati soko la mahindi likiwa bei iko vizuri wananchi wetu wangepata faida, Serikali ilizuia wananchi kuuza yale mahindi, leo soko limeporomoka ndio mnakuja mnatuambia Watanzania wakuze mahindi, hii sio sawa. Lakini pili mnakuja kutuambia eti leo sijui ndio mmetoka ndotoni kwamba mtatuma wataalam wenu waende wakatafute masoko. Wakati wako kwenye huo muda wa kutafuta masoko haya mahindi ambayo yapo mnachukua hatua gani? Tunachokitaka tunataka tujue sasa haya mahindi yaliyopo Serikali ina mkakati gani ya kuyanunua tena kwa bei ambayo itampa mkulima unafuu ama faida na sio biashara ya kutuletea...

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Mhagama.

MHE. JOSEPH K. MHAGAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kwa moja niseme *bravo* Mheshimiwa Waziri, hongera sana kwa kuthubutu kuondoa zuio la mahindi na mazao mingine mipakani. Ombi langu kwamba Bodi ya Mazao Mchanganyiko inapotafuta masoko iwajengee pia uwezo

wadau wa ndani ili waweze kuendana na taratibu zilizowekwa mipakani ili shughuli hii iweze endelevu. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante Waheshimiwa tunakwenda kwa Mheshimiwa Mattar.

MHE. MATTAR ALI SALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimtake kaka yangu Haonga amrejeshee Mheshimiwa Waziri shilingi. Mheshimiwa Waziri ameshakubali, ameshatoa *commitment* rasmi kwamba sasa mipaka iko huru, ameshasema Bodi yake ya Mazao Mchanganyiko iko tayari kwenda nje kuhakikisha mahindi haya yanapata masoko, mipaka yote imeshafunguliwa. Kaka yangu Mheshimiwa Haonga, nikuombe sana kwa kazi na makubaliano ambayo Mheshimiwa Waziri amekubali tumrejeshee shilingi aweze kufanya kazi. Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Chumi.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi naunga mkono hoja ya Serikali na niwaombe Waheshimiwa Wabunge jambo moja, hivi vitabu tunavyopewa tuvisome. Ukienda ukurasa wa 62 wa hiki kitabu unasema; "Ili kuboresha upatikanaji wa masoko ya mazao ya chakula hususan mahindi, Wizara imeondoa zuio la kuuza mazao hayo nje ya nchi." Kwa hiyo, hata kabla ya kushika shilingi, jibu liko humu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia Serikali katika maelezo yake imejieleza vizuri. Kwa hiyo, tunavyopewa hivi vitabu tuvisome ili kusudi tutumie muda wetu vizuri. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Nagu.

MHE. DKT. MARY M. NAGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi naungana na Wizara na Waziri kwa sababu kwa kweli umeondoa kizuizi chochote cha wakulima kuuza nje na zaidi ya hapo wanajenga maghala ya kuhakikisha uhakika na usalama wa chakula na wanaituma Bodi ya Mazao Mchanganyiko ikatafute masoko. Wananchi wa

Hanang ambao wakiuza mahindi nje kwenda Kenya, walishindwa lakini maamuzi haya ya Serikali yataisaidia sana Hanang yangu sasa kuendelea kuuza na waweze kupata mitaji ya kuongeza mashamba yao na tuwe na uhakika wa mahindi nchini ambayo ndiyo chakula kikuu cha wananchi wa Tanzania. Nakupongeza sana Waziri na turudishe shilingi Mheshimiwa Haonga, mwanangu rudisha shilingi ili Waziri akafanye hii kazi ambayo ameiahidi humu ndani. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mlata.

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana Mungu aliamua kukaa mbali na sisi kwa sababu yaani angekuwa karibu hata sijui ingekuwaje...

WABUNGE FULANI: Weweee!

MHE. MARTHA M. MLATA: ...maana hatuna shukurani, tunakuwa mara moto mara baridi, popo si popo, mnyama si mnyama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni, nchi ilikumbwa na njaa kwa sababu watu waliruhusiwa kuuza mahindi popote walipotaka. Watu wakauza, wakamaliza, wakaililia Serikali wakasema haitujali tunakufa na njaa. Serikali ikaamua kuweka vizuizi kwenye mipaka ili iweke utaratibu mzuri kwa ajili ya kuhifadhi chakula kwa ajili ya watu wake. Watu hawa wakaja wakalalamika. Leo Serikali imekuja imetaja kwenye kitabu hiki watu hawa bado wanalalamika.

Mheshimiwa Mwenyekiti,...

MWENYEKITI: Ahsante!

MHE. MARTHA M. MLATA: Ninaiunga Serikali mkono. Twendeni tu...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Makamba.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri Tizeba kwa tamko la Serikali la kwamba Serikali sasa imeruhusu mazao ya wakulima kuuzwa popote pale watakapoona inafaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Serikali ni kuongeza thamani ya mazao ya wakulima na kuwapatia bei nzuri na masoko popote na ndiyo maana ikaunda Bodi ya Mazao Mchanganyiko na hivi karibuni kama Mheshimiwa Waziri alivyosema, Bodi ya Mazao Mchanganyiko, imeshapatiwa shilingi bilioni tisa kutoka *NSSF* na fedha hizo zitatumika kwa mambo mawili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kununua mazao na kuyatafutia masoko nje ya Tanzania lakini vile vile kazi itakayofanyika ni kufufua vinu vya zamani vya *National Milling Company* hapa Dodoma – Kizota, Iringa na Mwanza na kwa kufufua vinu hivyo tutaongeza thamani ya mazao ya wakulima, badala ya kuuza mahindi, sasa sisi Wabunge wote tupiganie tuuze unga nje ya nchi ili wakulima wapate fedha nyingi na Taifa letu lipate fedha za kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nampongeza Waziri na Serikali imetambua sasa rasmi kwamba wakulima wanayo haki ya kuuza mazao yao popote wanapoona inafaa na popote watakapopata bei nzuri. Kwa hiyo, haina sababu ya kuzuia shilingi ili Waziri ashindwe kutekeleza jambo ambalo hilo hilo Mbunge analitaka.

Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge umruhusu Mheshimiwa Waziri achukue shilingi yake ili atekeleze lile lile ambalo unalitaka. Wabunge na Serikali tunataka kitu kimoja na ndiyo hicho ambacho Serikali imeazimia kukifanya. Kwa hiyo, nakuomba ndugu Haonga umrudishie shilingi Mheshimiwa Waziri ili aendelee kutekeleza yale ambayo anataka kuyatekeleza kwa manufaa ya wakulima.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti...

MWENYEKITI: Subiri Mheshimiwa, kuna Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje hapa kwanza. Huyu ndiye mwenye Diplomasia ya Uchumi, akisema huyu mambo yamekuwa sawasawa. *(Makofi)*

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nataka kuwahakikishia Wabunge kwamba kuna nchi tatu jirani zetu ambazo zina njaa kali, Sudan Kusini, Somalia na DRC wanahitaji mahindi na nchi ambayo ina uwezo wa kutoa mahindi sasa hivi ni Tanzania. *(Makofi*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Waziri kwa kutuhakikishia kwamba hakutakuwa na kizuizi tena cha kuuza mahindi. Shirika la Umoja wa Mataifa *(WFP)* liko tayari kununua mahindi karibu yote ambayo yanaweza kupatikana Tanzania ili kuikabili hali iliyopo huku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tumrudishie Waziri shilingi ili mchakato wa kuuza zao letu la mahindi kwa nchi jirani uanze haraka iwezekanavyo. Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante, mwenye dhamana ya Diplomasia ya Uchumi na sauti yake ni ya kiuchumi uchumi, ya ki-*foreign* umeisikia. Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe sana rafiki yangu Mheshimiwa Haonga anirudishie hii shilingi tufanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama anavyosema Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje, Shirika la *WFP (World Food Program)* hivi tunavyozungumza wamekwishaingia mkataba hapa na Wakala wa *NFRA* wa kununua tani 31,000 ya mahindi. Kwa hiyo, hili tu lenyewe tayari linaipa *NFRA* uwezo wa kurudi sokoni kwenda kuendelea kununua

mahindi. Juzi lilikuwepo tangazo Dodoma hapa kwamba wenye mahindi waende wakauze hapa *NFRA* na wako wanauza hata leo tunapozungumza na wana-*roll out* sasa hivi kwenda Nyanda za Juu Kusini, Sumbawanga, kuendelea kununua mahindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi hapa kwamba suala la *processing* nalo tunalifanyia kazi. Kupeleka mahindi tu nje ya nchi namna hii wakati mwingine tuna *export* ajira na mambo mengine. Kwa hiyo, yote mawili tunaenda nayo kutegemea na mahitaji ya soko. Soko kama linang'ang'ania wanataka mahindi *unprocessed* tutawapelekea kama tulivyofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kama tuna uwezo wa ku-*add value* na tukapeleka huko nje, tu-*add value,* tupeleke nje.

Mheshimiwa Ryoba, nimekusikiliza vizuri tu, sio kwamba tunabishana dhamira, lakini yuko mtu anataka mahindi kama mahindi, sasa huwezi kumlazimisha pia anunue unga, yeye hahitaji unga, anataka mahindi. Kwa hiyo wa hivyo tutawapa mahindi lakini wale wanaohitaji unga kwa kadri inavyowezekana tutawapa unga na kwa hivyo soko yaani kuanza kununua mchakato tayari uko unaendelea, wakala huu sio msimu wake kununua mahindi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, leo mwezi Mei, *NFRA* haijawahi kununua mahindi Tanzania lakini sasa hivi wananunua na hii yote ni katika kuhakikisha tu kwamba mahindi yaliyoko kwa wakulima yaendelee kuchukuliwa kwa sababu soko limepatikana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Haonga ukitaka maji ya kisima lazima..., lakini ukitaka kuuza mahindi hakuna lazima. Mheshimiwa Haonga.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewasikiliza wachangiaji wote na nawashukuru waliounga mkono hoja hii ya Haonga, wameunga hoja ya Watanzania,

hawajaunga hoja ya Haonga lakini pia wale wote ambao hawajaunga mkono hoja, pia Mungu anawaona ni wasaliti wa wakulima wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada sasa ya kuzungumza hayo, naomba kura ziamue kwa sababu naona *commitment* haipo kabisa, kura ziamue ajulikane msaliti ni nani na ni nani anawatetea wananchi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Sawa, nitawahoji kuhusu hoja ya Mheshimiwa Haonga.

(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)
(Hoja Iliamuliwa na Kukataliwa)

MWENYEKITI: Hawa ndiyo wanauza mahindi nje hawa! Mheshimiwa Sakaya. *(Kicheko)*

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, kwenye mchango wangu niliomba Mheshimiwa Waziri atusaidie namna gani mawakala wanaoidai Serikali kwa muda mrefu, mawakala wa pembejeo, lakini pia wako wakandarasi ambao wamejenga maghala ya vyakula lakini hawajalipwa kwa muda mrefu. Kwa Mkoa wa Tabora tu mawakala wanadai zaidi ya shilingi bilioni 2.4 na ni zaidi ya miaka mitatu hawajalipwa. Lakini hao hao tunawategemea pia wakaendelee kusambaza mbolea tena kwa wakati, kitu ambacho hakiwezekani.

Kwa hiyo tunaomba tu Serikali itupe *commitment,* ni lini mawakala hao watalipwa, mawakala wa pembejeo na maghala na pia wakandarasi ambao wamejenga muda mrefu na hawajalipwa, watalipwa lini ili waendelee kutoa huduma kwa wakati na kwa ufanisi. Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri *commitment* na wala haitaki shilingi yako, unayo mwenyewe.

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati akichangia hoja ya Wizara, Mheshimiwa Kijaji amesema

bayana kwamba suala la mawakala hawa linafanyiwa ukaguzi wa mwisho na wale ambao watathibitika hawakuwa na tatizo watalipwa pesa zao. Wale ambao watathibitika walijaribu au walifanya jambo ambalo halistahili kisheria basi sheria itachukua mkondo wake. Nadhani hiyo ndiyo *commitment* kwamba wale ambao wamefanya *clean business* watalipwa pesa yao, jambo lenyewe ni kubwa sana ndiyo tatizo! Jambo ni kubwa sana, hali-*involve* mawakala peke yao, lina *involve* taasisi za Serikali, watumishi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kwa upande wetu wa Serikali tumekwisha kuwachukuliwa hatua wale ambao na alijibu vizuri tu Mheshimiwa Naibu Waziri, wale walioko katika Serikali waliojihusisha na haya wamechukuliwa hatua. Sasa ni maelfu ya mawakala ndiyo walikuwa wanasambaza mbegu kule, sio jambo la siku mbili mtu anaweza akajiridhisha kwamba huyu hakuna jinai au kuna jinai, huyu yuko *clean* au hayuko *clean.* Tuzipe tu muda taasisi zetu zinazohusika, wafanye hii kazi yao vizuri ili baadae tena tusijekuwa kwaba alikuwepo fulani alionewa maana hilo nalo lipo. Tukienda kwa haraka watu mwishoni watalalamika wamenewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo nimuombe tu Mheshimiwa Sakaya nimuaminishe kwamba mtu yeyote ambaye alifanya biashara na Serikali, atalipwa pesa zake kama amefanya biashara halali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hili la maghala, haya maghala mengi yalikuwa yanajengwa kwa mkopo wa *ADB (African Development Bank)* bahati mbaya ile *facility* ili-*expire* kabla ya maghala mengi hayajakamilika, sasa hizo ni taratibu za kifedha na benki za kimataifa. Kwa hivyo sasa hivi tunachakata hili jambo, nimekwishafanya *appointment* na anayehusika huko *ADB* anakuja nchini ili tuone tunakamilishaje ujenzi wa hayo maghala na kwa maana hiyo *certificates* za wale ambao walikuwa wameana ujenzi wakati *facility* inakwisha zitalipwa maana wamenihakikishia kwamba hiyo fedha bado ipo, isipokuwa tu kwamba muda

wa kutumia fedha ile ndiyo ulikuwa umekwisha. Kwa hiyo, nikuombe Mheshimiwa uwe na amani kwamba haya mambo yote mawili yatafanyika kwa mujibu wa kanuni na sheria za nchi.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Hussein Bashe.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kama Waziri na Serikali haitatoa *real commitment* na hatutapata *solution* ya hili nitakaloongea nitadhamiria kushika shilingi na nitaomba Waheshimiwa Wabunge waniunge mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana tulifunga mipaka na kote duniani *best practice* ya *agro-business* Serikali nyingi duniani zimeanzisha kitu kinaitwa *price stabilization basket.* Leo wakulima wetu mazao yao yameanguka na kwa kuwa nimesikia Waziri wakati anafanya *wind up* kaongelea Bodi ya Mazao Mchanganyiko, sasa hivi mtu mwenye *funds* ambaye anaweza kwenda kununua mazao ya wakulima ni *NFRA* na wewe mwenyewe Waziri hapa na Waziri wa Mambo ya Nje amesema *NFRA* anawauzia watu kama *WFP.* Ningeomba *commitment* ya Serikali, fedha zilizotengwa za *NFRA* zitaongezwa angalau ziweze kununua tani 1,500,000 kutoka kwa wakulima wetu wa mazao ya mahindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu tunapotegemea bodi hii izunguke kwenda kutafuta masoko nje, mkulima anaendelea kubaki na mazao ya mwaka jana na ya mwaka huu ambayo yanaharibika na tukitegema *forces* za *demand and supply* sokoni wengine nao wanazalisha na jukumu la Serikali ni kumsaidia mkulima asipate hasara.

Kwa hiyo, ningeomba *commitment* ya Serikali na Wizara ya Fedha kwamba wataongeza fedha za *NFRA* ili iweze kununua mazao ya kutosha kutoka kwa wakulima wetu sasa hivi na kwa kuwa kuna Bodi ya Mazao mchanganyiko inatafuta masoko hizi taasisi mbili zifanye kazi kwa sababu hili ni jambo la dharura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nilitaka nipate *commitment* ya Serikali katika hili. Nashukuru.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri *commitment.*

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafahamu kabisa nia ya rafiki yangu Mheshimiwa Bashe, njema tu. Nia njema sana lakini pamoja na nia hiyo njema Mheshimiwa Bashe nakuomba ufahamu kwamba yako mambo ambayo nia yako hiyo haiwezekani ikatekelezeka kupitia *NFRA.*

Waheshimiwa Wabunge, leo tunapozungumza uwezo wa maghala ya *NFRA* ulikuwa tani 251,000. Sasa katika tani hizi 251,000 tunaezua ghala la Sumbawanga la tani 18,000. Kwa hiyo tunaliezua ili kulitengeneza upya, linavuja na kadhalika na mahindi yaliyoko pale miaka miwili iliyopita yaliharibika. Kwa hiyo, uwezekano *NFRA* ulionao kuhifadhi mahindi, hata kama ingepata pesa ya kununua hizo tani 200,000 leo hawana mahali pa kuyaweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu tulioanzisha ndiyo unatupeleka kwenye tani 501,000 na lengo letu mwaka 2025 tuwe kwenye tani 700,000. Leo tunapozungumza Mheshimiwa Bashe, *NFRA* wananunua, wanaendelea kununua mahindi! Mimi nadhani *this is a very serious commitment* kwamba tunanunua mahindi lakini hatuwezi kununua mahindi Mheshimiwa Bashe tukayaweke nje, yataharibika! Halafu tutaanza tena kutafutana, Tizeba umeliingizia Taifa hasara. Nataka nikwambie kuna watu wamepoteza kazi, sasa hivi fedha zipo, wanazo, wameuza hizo tani 31,000 wanazo pesa! Wanaendelea kununua. Kwa hiyo, nikuombe tu sana Mheshimiwa Bashe, wala usiamke kuomba kuungwa mkono. Nakuomba sana niachie tu hii shilingi sisi tuendelee kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya labda mimi nina tatizo sio msemaji sana, eeh! Inawezekana, lakini niruhusu nifanye kazi, ninaamini mwisho wa siku matendo yatazungumza zaidi kuliko maneno, nakuomba sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Bashe kwa uzito wa hoja yako na nafasi nzuri sana ya kuweza wewe ukai-*discuss* na Serikali na Kamati ya Bajeti, ili mpate kuelimishana vizuri. Nakuomba mrudishie Mheshimiwa Waziri shilingi yake na mwezi umeshatangazwa saa hizi kuna sala za *Tarawei* na sasa hivi naingia kwenye *guillotine.*

Kwa hiyo, hata muda huo wa kuanza kusimama na mahoja na kuungwa mkono utakuwa hakuna. Kwa hiyo, nakuomba tu mrudishie shilingi yake, ili kesho naiagiza Kamati ya Bajeti hoja yako hiyo na Wajumbe wengine muende mkakae na Kamati ya Bajeti na Serikali mpate muafaka wa maslahi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Bashe.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa umeagiza twende Kamati ya Bajeti na kwa kuwa tutakutana kwenye Kamati ya Bajeti na tusipoelewana niseme *in clear* na kwa sababu umesema mwezi umeandama, ni mwezi ambao sitakiwi kuwa mnafiki hata kidogo, nitarudi ndani ya Bunge hili kama hatutaelewana. *We can not allow* wakulima mazao yao yaoze kwa *inefficiency* ambayo hata Waziri amekiri. Ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Kifungu hiki kinaafikiwa?

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kif. 1002 – *Finance and Account*.....Sh.1,815,130,200/=
Kif. 1003 – *Policy and Planning* .....Sh.1,925,046,400/=
Kif. 1004 – *Agriculture Training Institute*.....Sh. 5,306,934,500/=
Kif. 1005 – *Internal Audit Unit* .....Sh. 440,072,500/=
Kif. 1006 – *Procurement Management Unit*...Sh. 698,855,200/=
Kif. 1007 – *Government Comm. Unit*.....Sh. 378,350,700/=
Kif. 1008 – *Legal Services Unit*.....Sh. 472,367,000/=
Kif. 1009 – *Mgt. Information Systems Unit*.....Sh. 460,373,200/=
Kif. 1010 – *Environmental Management* .....Sh. 371,245,200/=
Kif. 2001 – *Crop Development* .....Sh. 21,648,792,590/=

Kif. 2002 – *Agricultural Mechanization* .....Sh. 793,744,800/=
Kif. 2003 – *Agriculture Land use Planning and Mgt* .....Sh. 1,046,292,170/=
Kif. 2004 – *Plant Breeders' Unit*.....Sh. 161,103,080/=
Kif. 2005 – *Irrigation and Technical Services* 0
Kif. 3001 – *Research Development*.....Sh. 15,976,465,540/=
Kif. 5001 – *National Food Security* .....Sh. 5,703,769,620/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Fungu 24 - Tume ya Maendeleo ya Ushirika

Kif. 1001 – *Administration and HR Management Division*.....Sh. 2,743,583,500/=
Kif. 1002 – *Finance and Accounts Unit*.....Sh. 83,200,000/=
Kif. 1003 – *Planning Monitoring and Evaluation Unit* .....Sh. 96,200,000/=
Kif. 1004 – *Government Comm. Unit*.....Sh. 57,318,000/=
Kif. 1005 – *Legal Services Unit* .....Sh. 52,619,800/=
Kif. 1006 – *Procurement Management Unit*....Sh. 70,546,300/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

MWENYEKITI: Waheshimiwa tunaingia kwenye *guillotine.*

Fungu 24 - Tume ya Maendeleo ya Ushirika

Kif. 1007 – *Information Comm. Technology* ...Sh. 74,993,000/=
Kif. 1008 – *Internal Audit Unit* .....Sh. *36*,452,000/=
Kif. 1009 – *Research and Training Unit* .....Sh. 32,916,000/=
Kif. 4001 – *Cooperative Promo. & Coordination Section*.....Sh. 50,830,000/=
Kif. 4002 – *Cooperative Microfinance Section* Sh. 33,722,000/=
Kif. 4003 – *Regional Cooperative Offices*....Sh. 2,091,679,000/=
Kif. 4004 – *Cooperate Marketing and Investment Section*.....Sh. 57,748,000/=
Kif. 4005 – *Registration Service Section* .....Sh. 31,044,000/=

Kif. 4006 – *Inspection and Supervision Services Section* ..... Sh. 2,535,392,400/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 43 - Kilimo

Kif. 1003 – *Policy and Planning*.....Sh.19,684,795,800/=
Kif. 1004 – *Agriculture Training Institute* .....Sh. 8,500,000,000/=
Kif. 1009 – *Management Information Systems Unit*..... 0
Kif. 2001 – *Crop Development*.....Sh. 26,858,989,500/=
Kif. 2002 – *Agricultural Mechanization*.....0
Kif. 2003 – *Agriculture Land Use Planning and Management*.....Sh. 1,000,000,000/=
Kif. 3001 – *Research Development* .....Sh. 1,660,456,500/=
Kif. 5001 – *National Food Security*.....Sh. 40,415,274,200/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

(Bunge lilirudia)

MWENYEKITI: Tukae. Mtoa Hoja!

WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa Taarifa kwamba, Kamati ya Matumizi ya Bunge Zima imepitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo na taasisi zake, kifungu kwa kifungu kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Fungu 43 - Wizara ya Kilimo na Fungu 24 - Tume ya Maendeleo ya Ushirika na kuyapitisha bila babadiliko. Hivyo, basi naomba Bunge lako tukufu likubali na kuyapitisha makadirio hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Hoja imeungwa mkono, sasa nitawahoji kwamba Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

(Hoja Imetolewa Iamuliwe)
(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Makadirio na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 – Wizara ya Kilimo yalipitishwa na Bunge)

MBUNGE FULANI: ...ya Mheshimiwa Nape.

MWENYEKITI: Unajua heshima ni kitu cha bure sana Mheshimiwa Yussuf heshima ni kitu cha bure sana na si mara moja unafanya kitu kama hiki. Wewe mtu mzima na Bungeni uko miaka mingi humu.

Waheshimiwa Wabunge, bajeti ya Wizara ya Kilimo imepita, nakupongeza sana Mheshimiwa Waziri. Umefanya kazi nzuri sana wewe na Naibu wako na timu yako, wataalam, Katibu na Katibu Mkuu ambao wako kukusaidia, *you have done a very good job,* sivyo kama ilivyotegemewa, lakini umeweza kujibu hoja zote kwa uwezo mkubwa sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

(Saa 02.08 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Alhamisi, Tarehe 17 Mei, 2018 Saa Tatu Asubuhi)